

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 12 Mei, 2020

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Kamili Asubuhi)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tisa, Kikao cha leo ni cha Ishirini na Saba. Katibu.

#### NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:

#### HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani Na:-

#### NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

#### MHE. RITTA E. KABATI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 250

**Umuhimu wa Mafunzo na Mikopo kwa Vijana**

**MHE. GODBLESS J. LEMA aliuliza:-**

Machinga Complex haionekani kuwa suluhu ya matatizo ya ajira wala kuwa suluhu ya masoko kwa wafanyabiashara vijana:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka fedha *S/DO* kwa ajili ya mafunzo na mikopo kwa vijana ili kuishi maisha bora?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godbless J. Lema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhana ya Machinga Complex kama maeneo ya biashara yanapopatiwa miundombinu muhimu kama vile umeme, maji, barabara, majengo na kusimamiwa vizuri katika Halmashauri zetu zote nchini itasadia sana kutatua tatizo la ukosefu wa ajira hususan kwa vijana na kuwahakikishia maisha bora.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuwezesha mafunzo kwa vijana, Serikali imekuwa ikitenga shilingi bilioni 15 kila mwaka kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa vijana nchini.

Katika kipindi cha mwaka 2018/2019 hadi 2019/2020 vijana 80,013 wanawezeshwa kupata mafunzo ya ujuzi wa kujajiri na kuajiriwa. Vijana hao wanapatiwa mafunzo hayo kwa njia ya uanagenzi (*apprenticeship*), mafunzo ya uzoefu wa kazi (*internship*), kutambua na kurasi mishya ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi (*RPL*). *SIDO* ni mionganoni mwa Taasisi za Serikali zinazohusika katika utekelezaji wa programu hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mikopo kwa vijana, Serikali inatenga kiasi cha shilingi bilioni 1 kila mwaka kuititia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kuwezesha vijana kupata mikopo yenye masharti nafuu. Aidha, Halmashauri zote nchini zimekuwa zikitenga asilimia nne ya bajeti ya mapato yao ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, *SIDO* inaratibu na kusimamia Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Ujasiriamali (*NEDF*) ambao unalenga kuwawezesha wajasiriamali kupata mikopo yenye riba nafuu. Mkopaji anaweza kukopa kuanzia shilingi 500,000 hadi shilingi 5,000,000. Aidha, *SIDO* inasimamia na kuratibu Skimu ya Udhamini wa Mikopo kwa Biashara Ndogo na Kati (*SME*) kwa kushirikiana na *CRDB*. Mkopaji anaweza kukopa kuanzia shilingi 10,000,000 hadi shilingi 50,000,000 na anatakiwa kurejesha mkopo kuanzia miezi 6 hadi 36.

Na. 251

### **Hitaji la Barabara Kata ya Masukulu - Rungwe**

**MHE. SAUL H. AMON** aliuliza:-

Daraja la London linaunganisha Kata za Kisiba na Masukulu. Barabara inayopita kwenye Dalaja hilo imejengwa upande wa Kata ya Kisiba lakini upande wa Masukulu hakuna barabara ni pori tu:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara upande wa Kata ya Masukulu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imeidhinishiwa shilingi milioni 110 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum ya barabara inayounganisha upande wa Daraja la Landani na Kata ya Masukulu yenye urefu wa kilometra 5.11. Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 90 na umepangwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni 2020.

Na. 252

**Ukosefu wa Waganga Zahanati za Same- Magharibi**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta waganga, watumishi na vitendea kazi katika Zahanati za Same Magharibi ili zahanati hizo zianze kutoa huduma kwa wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuipatia Wilaya ya Same watumishi wa kada mbalimbali za afya ambapo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wilaya ya Same ilipokea watumishi 56 ambapo watumishi 13 walipangiwa zahanati zilizopo Jimbo la Same Magharibi. Mwaka wa fedha 2019/2020 Madaktari wawili wamepelekwa Wilaya ya Same ambapo 1 yupo Jimbo la Same Magharibi Hospitali ya Wilaya Same. Aidha, Mei, 2020 Halmashauri ya Wilaya ya Same

imepatiwa Madaktari wawili waliopangwa kwenye Vituo vya Afya Ndungu na Kisiwani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitendea kazi, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021 imeidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 32.5 ambazo zitatumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Serikali itaendelea kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Na. 253

**Wafungwa Waliopata Msamaha katika Sherehe za Muungano**

**MHE.YUSSUF HAJI KHAMIS** aliuliza:-

Ni utamaduni uliozoeleka kuwa katika Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano hutoa msamaha kwa wafungwa wanaokidhi vigezo:-

Je, ni wafungwa wangapi waliopata msamaha wa Rais Siku ya Sherehe za Maadhimisho ya Muungano tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni utaratibu uliozoeleka kuwa katika Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hutoa msamaha kwa wafungwa wenyewe vifungo mbalimbali wanaokidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mheshimiwa Rais John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu aingie madarakani mwezi Novemba, 2015

ametoa msamaha wa jumla ya wafungwa 17,227 katika Sherehe za Maadhimisho ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Idadi ya wafungwa waliopata msamaha katika maadhimisho yaliyofanyika kwa miaka mitano (5) imechanganuliwa kama inavyooneshwa katika jedwali hapo chini.

| NA               | MWAKA      | JUMLA YA WAFUNGWA | WAFUNGWA WALIOPUNGUZA | WAFUNGWA WALIOPADILISHWA ADHABU YA KIFO | WAFUNGWA WALIOACHILWA HURU |
|------------------|------------|-------------------|-----------------------|---|----------------------------|
| 1                | 26/04/2016 | 2,887             | 2,326                 | NIL                                     | 551                        |
| 2                | 26/04/2017 | 2,219             | NL                    | NIL                                     | 2,219                      |
| 3                | 26/04/2018 | 3,894             | 3,319                 | NIL                                     | 585                        |
| 4                | 26/04/2019 | 4,252             | 3,530                 | NIL                                     | 722                        |
| 5                | 26/04/2020 | 3,975             | 2,786                 | 256                                     | 933                        |
| <b>JUMLA KUU</b> |            | <b>17,227</b>     | <b>11,961</b>         | <b>256</b>                              | <b>5,010</b>               |

Na. 254

### **Nafasi za Masomo nje Nchi**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Kwa miaka mingi vijana wa Tanzania wamekuwa wakipata nafasi za masomo nje ya nchi:-

(a) Je, ni vijana wangapi wamepata nafasi za masomo nje ya nchi kwa mwaka 2015-2020?

(b) Je, ni vijana wangapi kutoka Zanzibar ambao wamebahatika kupata nafasi hizo?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis lenye vipengele vya (a) na (b), kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikipokea fursa mbalimbali za masomo kutoka nchi wahisani pamoja na mashirika rafiki. Fursa hizo zimekuwa zikitangazwa kuititia Tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar. Kwa kipindi cha mwaka 2015-2020, jumla ya Watanzania 1,772, wamenufaika na ufadhili wa masomo nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Spika, fursa za masomo kutoka kwa nchi wahisani huwa zinatolewa kwa Watanzania wote kwa vigezo vinavyowekwa na nchi au taasisi zinazotoa ufadhili na wanufaika huwa wanapatikana kwa ushindani bila kujali upande wanakotoka.

Mheshimiwa Spika, elimu ya juu ni suala la Muungano hivyo, uratibu na uchakataji wa *scholarship* kupendekeza wanufaika hufanyika kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.

Aidha, hatua zote muhimu ikiwa ni pamoja na kutoa matangazo katika tovuti za Wizara zote mbili, uchambuzi wa majina ya waombaji hufanywa na Kamati inayojumuisha pande mbili za Muungano. Kamati hiyo hupendekeza wanufaika wa *scholarship* hizo kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyotakiwa bila kujali eneo analotoka mwombaji.

Na. 255

**Kilometa Saba za Barabara Zilizofanyiwa Upembuzi  
Yakinifu - Ukerewe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Jimbo la Ukerewe lina jumla ya km 90 za barabara zinazohudumiwa na *TANROADS*, lakini ni km sita (6) pekee zilizojengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, km saba (7) za barabara zilishafanyiwa upembuzi yakinifu, michoro na makadirio.

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kipande hicho cha barabara kilichofanyiwa upembuzi yakinifu?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipande cha barabara chenye urefu wa kilometra 7 kilichoelezewa na Mheshimiwa Mbunge ni sehemu ya Mradi wa Barabara ya Nyamuswa - Bunda - Bulamba - Kisorya - Nansio - Rugezi (km 130.8) ambao upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika. Ujenzi wa barabara tajwa hapo juu unahusisha ujenzi wa daraja la kuunganisha Wilaya ya Bunda na Kisiwa cha Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, gharama ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ni kubwa ukilinganisha na uwezo wa Serikali kugharamia mahitaji mengine mengi ya kijamii kwa wakati mmoja. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali imepanga kujenga barabara hii kwa awamu bila kuathiri miradi mingine iliyopangwa kutekelezwa katika maeneo mengine ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa, Serikali inaendelea kujenga barabara hiyo ambapo sehemu ya Bulamba, Kisorya (km 51) ujenzi umefikia asilimia 82.5, sehemu ya Nyamuswa - Bunda - Bulamba (km 56) na mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami ulisainiwa tarehe 1 Aprili, 2020 na mkandarasi yupo kwenye hatua za maandalizi ya kuleta mitambo na wataalam. Sehemu iliyobaki inayoanza Rugezi - Nansio (km 12.8) inayohusisha km 7 alizozitaja Mheshimiwa Mbunge itajengwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

Na. 256

### **Mkakati wa Kukabiliana na Ajali za Majini**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na ajali za majini hasa katika maziwa?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Asha Abdallah Juma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua na inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha usalama wa vyombo vyaa usafiri majini ili kuzuia matukio ya ajali ambayo yana athari kubwa katika taifa letu. Athari hizo ni pamoja na kupungua kwa nguvukazi kwa sababu ya vifo na majeruhi kuongeza gharama za matibabu, uokozi, bima, uchunguzi na uendeshaji wa kesi na pia kukosekana kwa huduma za usafiri, upotevu wa mali na uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na ajali hizo za majini, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kutunga sheria, kanuni na miongozo kwa ajili ya kusimamia usalama wa vyombo vyaa majini ikiwa ni pamoja na kutunga sheria kuhusu Uwakala wa Meli na Kanuni zake;

(ii) Kuimarisha usimamizi na udhibiti kwa kuunda taasisi maalum ya udhibiti usalama wa vyombo vyaa majini (*Tanzania Shipping Agencies Corporation – TASAC*) ambayo imeanzishwa kwa Sheria ya Uwakala wa Meli (Na. 14 ya mwaka 2017);

(iii) Kuimarisha mafunzo na utoaji wa vyeti vyaa mabaharia wanaohudumu katika meli zilizoko Pwani ya Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu kwa kuhakikisha mafunzo

yanayotolewa yanakidhi viwango vya Kimataifa vya Shirika la Bahari Duniani (*IMO*) kuitia Mkataba wa Mafunzo na Utoaji Vyeti (*STCW 78*) ya mabaharia;

(iv) Kuimarisha ukaguzi na utoaji wa vyeti vya meli kwa kuwa na wakaguzi katika Mikoa yote yenye maji nchini kama vile Mara, Mwanza, Kagera, Geita, Kigoma, Sumbawanga, Ruvuma na Mbeya.

(v) Kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo inasaidia nchi kuweza kupata uzoefu na mafunzo ya udhibiti wa usalama wa vyombo vya majini; na

(vi) Kushiriki katika zoezi la kubaini maeneo yasiyo rasmi ambayo yamekuwa yakitumika na vyombo kuondoka au kufika. Zoezi hili lina lengo la kuyarasimisha maeneo yatakayobainika kuwa na umuhimu kijamii na kiuchumi ili kusimamia taratibu za uondokaji wa vyombo katika maeneo hayo.

Na. 257

**Kutowatoza Kodi Wastaifu Wanaofanya Biashara  
Ndogondogo**

**MHE. JORAM I. HONGOLI** aliuliza:-

Watumishi wa umma wanapostaafu hupewa mafao yao na wengi wao hutumia fedha hizo kuanzisha miradi midogo ya kilimo na biashara. Wastaifu hao hutozwa kodi na *TRA* kutohana na biashara hizo:-

Je, kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa kutowatoza kodi wastaifu ambao biashara zao hazizidi mtaji wa shilingi milioni 4?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 4 cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kinatoa msamaha wa kodi ya mapato kwa mfanyabiashara ambaye mapato ghafi yake ya mwaka hayazidi shilingi milioni nne (Sh.4,000,000). Hivyo, wafanyabiashara wadogo wadogo ambao mapato yao ghafi ya mwaka hayazidi shilingi milioni nne (Sh.4,000,000) wakiwemo wastaifu walioanzisha miradi midogo ya kilimo na biashara hawatowwi kodi ya mapato kama ilivyobainishwa kupitia aya namba 2, aya ndogo ya 3 ya Jedwali la Kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332.

Na. 258

### **Wavuvi Kutumia Nyavu Haramu Nchini**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, Serikali inajua ni kwa nini wavuvi wengi wanatumia nyavu haramu?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Aida Joseph Khenan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvu inafahamu baadhi ya sababu zinazowafanya wavuvi kutumia nyavu haramu. Miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na ukosefu wa elimu na uelewa kwa baadhi ya wavuvi kuhusu madhara ya uvuvi huo.

Mheshimiwa Spika, aidha, tabia za ubinafsi uliokithiri na tamaa kwa baadhi ya wavuvi ya kupata utajiri kwa muda mfupi bila kujali madhara yanayotokea kwenye rasilimali za uvuvi, mazingira na afya za walaji. Kutokana na hali hiyo, vitendo vya uvuvi haramu vimeendelea kuongezeka siku hadi siku hali inayoweza kupelekeea kupungua au kutoweka kwa rasilimali za uvuvi iwapo hatua za udhibiti zisingechukuliwa.

Mheshiwa Spika, katika kukabaliana na vitendo vya uvuvi haramu, Serikali imeendelea kuielimisha jamii kuhusu njia za uvuvi endelevu na madhara ya uvuvi haramu. Elimu hiyo imekuwa ikitolewa kwa njia mbalimbali ikiwemo redio, runinga, semina na maonesho mbalimbali yakiwemo maonesho ya Sabasaba, Nanenane na Siku ya Chakula Duniani.

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Wizara imeendesha vipindi 19 vya redio na vipindi 34 vya runinga na makala mbalimbali kuhusu uvuvi endelevu, ufugaji bora wa viumbe kwenye maji na uhifadhi wa mazingira. Vilevile, katika kipindi hicho jumla ya wananchi 43,104 waliemishwa kuhusu uvuvi endelevu, ufugaji bora wa viumbe kwenye maji na uhifadhi wa mazingira kupitia mafunzo rejaa pamoja na maonesho ya Sabasaba na Nanenane. Aidha, Wizara imeendelea kuendesha doria na operesheni mbalimbali ili kudhibiti uvuvi haramu ambapo zana mbalimbali za uvuvi haramu na vifaa vinavyosaidia uvuvi haramu zilifikamatwa.

Mheshimiwa Spika, zana na vifaa vilivyokamatwa kwa kipindi cha mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020 ni pamoja na nyavi za kokoro 808, Kamba za kokoro zenye urefu wa mita 149,071, nyavi za makila 15,911 zenye macho chini ya inchi 6 kwa uvuvi wa Ziwa Victoria, nyavi za makila 3,754 zillizounganishwa kwa kina, nyavi za makila 600 zenye macho chini ya inchi 3 kwa uvuvi wa maji mengine, nyavi za timba 2,571, nyavi za *ringnet* 204 zenye macho chini ya milimita 8, nyavi za kumbakumba/gizagiza 117, nyavi za dagaa 493 zenye macho chini ya milimita 8, vyandarua 22, ndoano 10,601, boti 72, mitumbwi 680, injini za boti 275, magari 8 na pikipiki 27.

Aidha, jumla ya kilo 28,450 za samaki wachanga zilikamatwa na kugawiwa katika vituo vya kulelela watoto yatima pamoja na wananchi wenye mahitaji maalum. Pia, kesi saba (7) zimefunguliwa Mahakamani.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali Wizara kwa  
Mwaka wa Fedha 2020/2021 – Wizara ya Kilimo**

**SPIKA:** Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hasunga, uwanja ni wako, una nusu saa, karibu sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowailishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji iliyochambua bajeti ya Wizara ya Kilimo (Fungu 43), Tume ya Umwagiliaji (Fungu 5) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (Fungu 24) mnamo tarehe 25 na 26 Machi, 2020 Jijini Dodoma, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuendelea kujalia nchi yetu amani, utulivu na mshikamamo na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano wa Bunge la Kumi na Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni mukutano wa mwisho katika uhai wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia kilimo ambalo ndilo tegemeo la Watanzania walio wengi.

Vilevile namshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanazofanya kusukuma maendeleo ya nchi hii ikiwemo sekta ya kilimo. Aidha, binafsi nawashukuru

viongozi wangu wote kwa maelekezo, ushauri na miongozo wanayonipatia ambayo imesaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, naomba kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 1 Aprili, 2020. Hotuba hiyo iligusa maeneo mengi ikiwemo sekta ya kilimo ambapo alisisitiza uimarishaji wa huduma za ugani, kilimo cha umwagiliaji, ushirika, upatikanaji wa pembejeo sahihi na miundombinu ya masoko. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Hussein Mohammed Bashe, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo na ndugu Jerald Kusaya kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu katika Wizara ya Kilimo na kuungana na viongozi wengine wa Wizara kusukuma kilimo hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe binafsi na Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyolismamia na kuliendesha Bunge letu tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kwa kazi nzuri walizofanya katika miaka hii mitano ya kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili. Nampongeza pia Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki kwa kuchaguliwa kujunga na Bunge lako tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020: Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Jimbo la Kibwakwe kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira; na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi kwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, Bunge lako Tukufu limewapoteza wawakilishi wenzetu wanne ambao ni Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wa Newala Vijijini, aliyefariki tarehe 15 Januari, 2020; Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, aliyefariki tarehe 20 mwezi Aprili mwaka 2020; Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, aliyefariki tarehe 29 Aprili; 2020; na Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustino Philip Mahiga, aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria na aliyefariki tarehe 1 Mei, 2020. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, Chama cha Mapinduzi, familia za marehemu, ndugu, jamaa na wananchi wa Majimbo ya Newala Vijijini na Sumve.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kwa ushirikiano na ushauri mzuri walioutoa katika kipindi chote cha mwaka 2019/2020 pamoja na kupitia taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2019/2020 na mpango wa bajeti ya Wizara ya Kilimo wa mwaka 2020/2021. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba ushauri wao umezingatiwa na tutaendelea kushirikiana na Kamati ili kuleta mageuzi ya kilimo na kufikia matarajio ya wananchi katika kufikia uchumi wa kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Vwawa kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Napenda kuwahimiza kuendelea kuniamini na kuiamini Serikali ya Awamu ya Tano na kwamba maendeleo ya Jimbo letu yanategemea sana kufanya kazi kwa pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa namna ya pekee nawapongeza sana Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe

kwa jinsi wanavyonisaidia katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya Wizara ya Kilimo. Vilevile, nawapongeza Katibu Mkuu, Ndugu Gerald Kusaya; Naibu Katibu Mkuu, Profesa Siza Tumbo; Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo; Wakuu wa Taasisi; Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano na kazi nzuri wanazoendelea kuzitekeleza ili kufanikisha malengo ya kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza tena Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa msukumo wa kuendeleza sekta ya kilimo. Aidha, katika hotuba yake aliyoitao tarehe 20 Novemba, 2015 akifungua rasmi Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma alisitisiza kutekeleza ahadi alizozitoa kwa wakulima kupitia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetelekeza ahadi hizo kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, Awamu ya II na kuwezesha kilimo kuchangia katika uchumi wa maendeleo ya Taifa letu hususani katika maeneo ya usalama wa chakula na lishe, ajira, upatikanaji wa malighafi za viwanda na kuchangia katika kupunguza umaskini na kuongeza kipato cha wakulima. Baadhi ya ahadi alizozitoa ni pamoja na kuimarisha huduma za ugani; upatikanaji na usambazaji wa pembejeo; dhana za kilimo za kisasa; masoko ya uhakika ya mazao; kuimarisha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya kilimo na kuondoa ushuru; kodi na tozo ambazo ni kero kwa ajili ya maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta ya kilimo katika uchumi. Kilimo kimeendelea kuwa ni mhimili mkubwa katika maendeleo ya uchumi wa Taifa letu. Katika kipindi cha miaka mitano, pato la Taifa linalotokana na kilimo kwa kutumia bei za mwaka 2015 limeongezeka kwa asilimia 17 kutoka shilingi triliioni 25.2 mwaka 2015 hadi shilingi triliioni 29.5 mwaka 2019. Vilevile, sekta imeendelea kutoa ajira kwa Watanzania kwa asilimia 58 kwa mwaka 2018, imechangia asilimia 28.2 ya pato la Taifa ambapo sekta ndogo ya mazao imechangia asilimia 16.2. Hii inatokana na kuongezeka kwa

uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwemo vyakula vinavyotokana na mazao ya kilimo. Aidha, kati ya mwaka 2018 na 2019, sekta ya kilimo imeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 5.2 ambapo sekta ndogo ya mazao imeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 5.8.

Mheshimiwa Spika, mapato na matumizi ya mwaka 2019/2020. Wizara ya Kilimo kupitia (Fungu 43), (Fungu 5) na (Fungu 24) iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi bilioni 253.86 ili kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 77.78 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 176.08 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Maelezo ya kina yanapatikana katika kitabu cha hotuba ambacho tumekiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, Homa Kali ya Mapafu. Mlipuko wa Ugonjwa wa Homa Kali ya Mapafu (*COVID-19*) unaosababishwa na virusi vya *Corona* imeathiri sekta mbalimbali za kiuchumi nchini ikiwemo sekta ndogo ya mazao. Tathmini imefanyika na kubaini kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2019/2020 haujaathirika kwa kuwa pembejeo ziliikuwa zimeshawasili hapa nchini. Aidha, katika kukabiliana na uhaba wa mbolea unaoweza kutokea kutokana na kuendelea kuwepo kwa tatizo la Ugonjwa huu wa Homa ya Mapafu, Wizara imeagiza (*TFRA*) kuhakikisha mbolea zote zinaagizwa mapema kipindi hiki kabla ya msimu ujao kuanza.

Mheshimiwa Spika, mazao ya asili ya biashara ambayo ni pamba, korosho na kahawa misimu yake ya mauzo imeisha mwezi Machi, 2020 na hivyo kutoathirika na ugonjwa huu. Aidha, kwa zao la tumbaku, wakulima wameshafunga mikataba na wanunuzi kwa ajili ya msimu wa mwaka 2020/2021 na hivyo kutokuathirika na ugonjwa huu wa *COVID-19*. Mazao ambayo yameonyesha dalili za kuathirika ni chai na mazao ya bustani ambapo masoko na usafirishaji wake nje ya nchi umeathirika sana. Vilevile ugonjwa wa *COVID-19* iwapo utaendelea kwa muda mrefu, unaweza ukaathiri soko la pamba, korosho, kahawa na mazao mengine yanayotegemea minada ya moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na ugonjwa huu, Serikali imepanga kununua tani laki tatu (300,000) za chakula kupitia *NFRA* lakini pia imepanga kuhakikisha sekta binafsi zinahifadhi kwenye maghala yao chakula cha kutosha. Zaidi ya hapo, tunakusudia kutumia Mfuko wa Soko la Bidhaa (*TMX*) kwa mazao ambayo hutegemea zaidi wanunuzi kutoka nje ya nchi kama vile zao la korosho, kahawa, pamba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi ya hapo, tunakusudia kutumia Balozi zetu zilizoko nje ya nchi kutafuta wanunuzi na masoko ya moja kwa moja ili kuingia mikataba katika kipindi hiki ili kuweza kufanya biashara ya mazao haya asilia. Hivyo, kwenye upande wa mazao ya chakula katika kipindi hiki cha ugonjwa ni fursa kubwa ambayo imejitokeza kwa sababu chakula kinaendelea kuhitajika mahali kwingine kwingi. Kwa hiyo, Watanzania watumie fursa hii sasa kuendelea na uzalishaji, kufaya kazi kwa bidii ili kuweza kuzuzia zile nchi zitakazohitaji chakula kwa wakati huu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2019/2020. Katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kutekeleza maeneo ya kipaumbele ya kuongeza uzalishaji na tija kwenye kilimo kwa kuimarishe upatikanaji wa pembejeo za kilimo; udhibiti wa visumbufu; matumizi ya dhana bora za kilimo na huduma za ugani; ujenzi na ukarabati wa miuondombinu ya umwagiliaji; ujenzi wa miuondombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo na masoko; kufanya utafiti wa kilimo na kuzalisha teknolojia kwa mazao ya mahindi, muhogo, ngano, michikichi, ufuta, alizeti, pamba, mpunga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Wizara ya Kilimo katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano. Katika kipindi cha miaka mine, Wizara imepata mafanikio makubwa katika maeneo ya usalama wa chakula na lishe; uzalishaji wa mazao makuu ya bishara; upatikanaji wa pembejeo za kilimo; viwanda vyta kuchakata mazao ya kilimo na masoko; utafiti; huduma za ugani na mafunzo; hifadhi ya mazao; uzalishaji wa mazao ya bustani; kuimarka kwa Bodi ya Nafaka na

Mazao Mchanganyiko; kuimarika kwa ushirika; kuimarika kwa kilimo cha umwagiliaji; ongezeko la ushiriki wa vijana katika kilimo; matumizi bora ya ardh; kuuhiha mifumo na sera za kilimo; na kuanzishwa kwa kanzidata ya wakulima na wadau mbalimbali wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, usalama wa chakula na lishe. Katika kipindi cha miaka minne, upatikanaji wa chakula umeendelea kuimarika na hivyo kuwezesha nchi yetu kujitosheleza kwa chakula kwa wastani wa asilimia 121 na kuwa na wastani wa ziada ya tani milioni 2.79. Aidha, katika mwaka 2019/2020, upatikanaji wa chakula umefikia tani milioni 16.2 ukilinganisha na mahitaji ya chakula ambayo ni tani milioni 13.8. Hivyo ziada ya chakula ilikuwa ni tani milioni 2.47 na kuwa na kiwango cha utoshelevu cha asilimia 118.

Mheshimiwa Spika, hali ya lishe nchini. Kulingana na taarifa ya mapitio ya kati yaani *midterm review* ya hali ya lishe nchini katika utekelezaji wa Mpango Jumuifu wa Kitaifa wa Lishe wa mwaka 2016 - 2021 uliofanyika mwaka 2019 unaonesha kuwa udumavu wa watoto chini ya miaka mitano (5) umepungua kutoka asilimia 34 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 32 mwaka 2018. Aidha, kiwango cha ukondefu kwa watoto chini ya miaka mitano (5) kitaifa kimeendelea kushuka kutoka asilimia 3.8 hadi asilimia 3.5 na pia upungufu wa damu kwa akina mama umepungua kutoka asilimia 44.7 hadi kufikia asilimia 28.7 kwa kipindi hicho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali ni kuhakikisha mazao mbalimbali ya chakula yenye virutubisho kwa wingi yanazalishwa yakiwemo viazi lishe na maharagwe yaliyoongezewa madini ya chuma na zinki. Utumiaji wa mazao hayo unachangia kupunguza tatizo la upungufu wa damu unaosababishwa na ukosefu wa madini chuma na tatizo la upungufu wa vitamini A hususani kwa akina mama walio katika umri wa kuzaa na watoto chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya biashara yakiwemo pamba, kahawa, chai, pareto, tumbaku, korosho, mkonge na miwa umeongezeka kutoka tani laki 796,502

mwaka 2015/2016 hadi jumla ya tani 1,144,631 kwa mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 43.7. Aidha, zao la miwa limeendelea kuongoza kwa uzalishaji likifuatiwa na korosho na pamba.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kipindi hicho cha miaka minne kiasi cha tani 1,613,000 za mazao ya kahawa, pamba, katani, chai, tumbaku na korosho kilizwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa dola za Marekani milioni 3,419.77 sawa na shilingi trillioni 6.9. Aidha, Wizara kuititia Bodi ya Tumbaku imeuza jumla ya tani 500 za tumbaku za daraja la chini yaani *reject* ambayo mapato yake yamesaidia sana kupunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima na kuwaongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, hii tumbaku ambayo tulikuwa tunazalisha kipindi cha nyuma ilikuwa inatupwa na inatakiwa ichomwe moto. Kwa mara ya kwanza mwaka huu tumeweza kuiiza na wakulima wameweza kupata fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa miwa na sukari nchini. Hadi kufikia Aprili, 2020 uzalishaji wa sukari ulifiki tani 298,948.61 sawa na asilimia 86 ya lengo la kuzalisha tani 345,296 za sukari. Hata hivyo, uzalishaji wa sukari ulikumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uchakavu wa mitambo ya viwanda, kuharibika kwa mitambo, mlipuko wa ugonjwa wa vindung'ata wa njano na mvua nyngi zinazoendelea kunyesha sehemu mbalimbali. Ili kukabiliana na upungufu huo, Serikali ilitoa kibali cha kuingiza tani 40,000 za sukari kutoka nje ya nchi kwa kampuni nne za Kagera Sugar, Mtibwa, Kilombero na *TPC* ya Moshi Machi, 2020.

Mheshimiwa Spika, kikao cha pamoja na wawakilishi wa wazalishaji, Serikali, *TRA* na Bodi ya Sukari kilichokaa chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa pamoja tulikubaliana kuwa bei ya sukari haitapanda kwa sababu gharama zilikuwa ziko chini. Hata hivyo, kumejitokeza mambo yafuatayo: Kuchelewa kuingia nchini kwa sukari kutokana na tatizo la *COVID-19*; na baadhi ya wanunuzi kuficha sukari nalo limekuwa ni tatizo sugu sana hasa wale ambaio sio waaminifu. Kutokana na hali hiyo, Wizara kuititia Bodi ya Sukari baada

ya kufanya uchambuzi wa kina na kwa kutumia Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sehemu ya Nne, kifungu E, kifungu cha 11A illichukua hatua ya kutangaza bei elekezi ya jumla na rejareja ya sukari katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kwa lengo la kukabiliana na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu.

Mheshimiwa Spika, labda nitoe kidogo tu kwa muhtasari lakini baadaye nitaweza kufafanua. Sasa hivi ni kweli kabisa katika maeneo mbalimbali kunaonekana kumekuwa na upungufu wa sukari. Hii inatokana kwamba meli nyingi ambazo zilikuwa zibebi huo mzigo na kuuleta zimekuwa zikifaulisha mzigo huo kwenye meli zingine. Kwa hiyo, mzigo hauji kadri inavyotakiwa, umekuwa ukija kwa kiwango kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nitoe tu takwimu kwa kifupi sana kwamba kuanzia tarehe 10 juzi mpaka leo, tani ambazo zimeshawasili na ziko bandarini na nyingine zimeshatolewa tayari mpaka sasa hivi ni 4,000. Tani ambazo ziko njiani ni karibu 21,000 ambazo zote zitaingia mwezi huu. Baadaye kwenye majumuisho, nitaweza kutoa ratiba lini tunategemea kwamba sukari hiyo itaweza kuingia.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tani 500 ambazo zinaingilia kule Kasumulo ambazo zimetoka South Africa ambazo zinakuja kwa malori, zimeshafika. Kwa hiyo, hatutegemei kuwa na upungufu wa sukari hapa nchini kwa sababu sukari iliyoipo inatosheleza.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya sukari kwa mwezi ni tani 35,000. Ndiyo maana Serikali ilipotoa kibali cha uingizaji wa tani 40,000 tuliamini kwamba inatosha kwa sababu viwanda ilitakiwa vianze uzalishaji kufikia mwezi huu wa Mei mwishoni. Bahati mbaya mvua bado zinaendelea kunyesha na ni kiwanda kimoja tu kimeonyesha dalili kwamba kinaweza kikaanza uzalishaji mwisho wa mwezi.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Watanzania kwamba kwa sukari iliyoingia na hatua zilizochukuliwa, sukari inatosha kabisa na hatuhitaji kuwa na upungufu wa sukari.

Labda tu niwaelekeze wenzangu wanaohusika wahakikishe hiyo sukari ambayo imeshafika wanaitoa na kusimamia usambazaji kwenda katika mikoa yote ambayo inahitaji sukari hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, tumekokotoa bei ya sukari inayotoka nje, mpaka inafika Dar es Salaam ni dola 350 mpaka nchi za mbali za Brazil ni dola 500. Ukkokotoa kwa hela ya Tanzania sukari haitakiwi kuzidi bei tulizozitangaza. Jana tumekaa chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na waagizaji wa sukari hasa hivi viwanda na waliohudhuria wametuahidi kabisa kwamba bei haitakiwi kupanda. Hivyo, sukari yote inayokuja itauzwa kwa bei zile ambazo tumezizoea.

Mheshimiwa Spika, mazao ya bustani. Katika kipindi cha miaka minne uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka kutoka tani 5,931,900 mwaka 2015/2016 hadi tani 6,556,103 kwa mwaka 2018/2019. Thamani ya mauzo ya mazao ya bustani yakiwemo mbogamboga na maua nje ya nchi yameongezeka toka Dola za Marekani milioni 412 kwa mwaka 2015 hadi Dola za Marekani milioni 779 kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, uwekezaji katika mazao ya bustani kuitia sekta binafsi chini ya mwamvuli wa TAHU umefikia Dola za Marekani milioni 30. Aidha, zao la parachichi limeonesha mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka minne ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 20,000 mwaka 2015 hadi tani 190,000 kwa mwaka 2018/2019. Mauzo yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 8.5 yamefanyika katika Soko la Ulaya na tumbahatika kuza parachichi letu katika nchi za Ufaransa, Uhlanzi na Uingereza.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa pembejeo. Katika kipindi cha miaka minne upatikanaji wa pembejeo bora umeongezeka kutoka tani 36,614 mwaka 2015 hadi tani 76,725 katika mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 110. Aidha, uzalishaji wa ndani wa mbegu bora umeongezeka

kutoka tani 20,604.97 mwaka 2015 hadi tani 69,173.17. Vilevile, uzalishaji wa miche umeongezeka kutoka tani 5,000,000 hadi tani 25,285,859 kwa mwaka 2019. Pamoja na mambo mengine, naomba ieleweke kwamba sasa hivi uzalishaji wa mbegu asilimia 93 ya mbegu zote zinazalishwa hapa nchini. Pia Serikali imeendelea kuimarisha maabara ya *TOSCI* na hivyo kupata Ithibati ya Kimataifa ya Uthibiti wa Ubora wa Mbegu ambayo sasa inatufanya nchi yetu tuweze kuuza mbegu mahali popote duniani.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mbolea. Wizara imeimarisha upatikanaji wa mbolea hapa nchini kwa kuanzisha mfumo wa ununuzi wa pamoja ambao umewezesha kuongezeka upatikanaji wa mbolea kutoka tani 302,482 kwa mwaka 2015/2016 hadi tani 633,197 kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, viuatilifu. Upatikanaji wa viuatilifu umeongezeka kutoka tani 4,111.5 mwaka 2015 hadi tani 16,869.10 kwa mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, mafanikio Wizara ya Kilimo ni mengi lakini mambo mengine ambayo tumeyafanya ni pamoja na uboreshaji wa mazingira na uanzishwaji wa viwanda. Naomba niliseme hili, katika kipindi cha mwaka 2015/2016, Serikali imefuta ushuru, tozo na ada 105 na kupunguza tozo nne (4) kati ya 146 zilizokuwa zinatozwu katika mazao mbalimbali ya kilimo hapa nchini. Hali hii imechochea sana uwekezaji wa sekta binafsi na hivyo kuwavutia wawekezaji wengi ambao mpaka sasa hivi wamewekeza trilioni 3.7 katika mnyororo mzima wa thamani.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa masoko ya kilimo. Tumeanzisha Kitengo cha Masoko ambacho kinaendelea kutafuta masoko. Pia tumeimarisha huduma za ugani na huduma za mafunzo ambapo TARI wameweza kugundua mbegu zaidi ya 124 na kati ya hizo, mbegu 35 zimegunduliwa na sekta binafsi. Pia tumefundisha Maafisa Ugani 7,530 na 6,146 wamehitimu katika vyuo binafsi 12 lakini 7,530 katika vyuo vya Serikali. Aidha, jumla ya Maafisa Ugani 902 na

wakulima 42,192 wamepatiwa mafunzo kuhusu kanuni bora na teknolojia mbalimbali za uzalishaji na masoko.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 nchi ilikuwa na jumla ya maghala 3,400 yenye uwezo wa kuhifadhi tani milioni 2.7 za mazao ya chakula. Ujenzi na ukarabati wa miundombini ya vihenge 57 na ghala 118 zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 203,000 na tani 100,700 mtawaliwa na hivyo kuongeza uwezo wa kuhifadhi kutoka tani milioni 2.7 mpaka tani milioni 3.07 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 11.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumefanya kazi ya kuimarisha ushirika, ambapo Vyama vya Ushirika vimeongezeka kutoka 7,394 mwaka 2015 hadi vyama 11,626 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 57. Vilevile idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka milioni 2.3 hadi wanachama milioni 5.8 sawa na ongezeko la asilimia 146.

Hata hivyo, Wizara imechukua hatua ya kuvifuta vyama 3,348 ambavyo vilibainika kuwa ni hewa na hivyo kubaki na jumla ya vyama vilivyo hai 8,611 kwenye daftari la Mrajisi wa Vyama. Katika kipindi hicho hicho, thamani ya mikopo iliyotolewa na Vyama vya Ushirika iliongezea kutoka shilingi milioni 899.2 hadi shilingi triliuni 1.5 mwezi Machi, 2020.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji. Eneo la Kilimo cha Umwagiliaji limeongeza kutoka hekta 461,326 kwa mwaka 2015/2016 hadi kufikia hekta 694,715 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 33. Aidha, tija ya uzalishaji katika skimu za umwagiliaji zinazoendelezwa imeongezeka kutoka wastani wa tani 1.8 mpaka tani 2 kwa mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa tani 4 mpaka tani 5 kwa hekta kwa zao la mpunga na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, pia tumeboresha mifumo ya vibali kwa njia ya kielektroniki. Tumeanzisha Mfumo wa Kanzidata ya Wakulima ambapo wakulima wote sasa tunawasajili katika kanzidata hiyo ili tuweze kuwatambua na tuweze kuwashudumia.

Vilevile tumeanzisha mfumo wa kuwasajili wadau mbalimbali waliopo katika mnyonyoro mzima wa thamani lakini tumeanzisha bima ya mazao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, malengo na bajeti ya mwaka, Wizara itaendelea kutekeleza maeneo 10 ya kipaumbele kupitia Fungu 43, Fungu 25 na Fungu 5 katika Idara, Vitengo, Tume na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Katika mwaka 2020/2021 Wizara imepanga kutekeleza malengo na shabaha zifuatazo:-

(i) Kuzalisha tani za chakula milioni kumi na nane...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, sasa uombe fedha.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kwanza kuwashukuru wadau na wakulima wote wa nchi hii ambao wameshiriki kwa namna moja ama nydingine kuzalisha. Pia niwashukuru wadau wa maendeleo, taasisi zote za kimataifa ambazo zimechangia sana kwenye kilimo.

Mheshimwia Spika, maombi ya fedha. Katika mwaka 2020/2021, Wizara inatarajia kukusanya shilingi milioni 5.7 kutokana na ada za ukaguzi za wa mazao yanayouzwa nje ya nchi na kuingizwa nchini.

Mheshimiwa Spika, fedha za mafungu. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.229,839,808,000 kupitia Fungu 43, Fungu 5 na Fungu 24 kama ambavyo zinajieleza katika kitabu ambacho nimekiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni [www.kilimo.go.tz](http://www.kilimo.go.tz).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MHESHIMIWA JAPHET  
NGAILONGA HASUNGA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA  
KILIMO KWA MWAKA 2020/2021 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1. UTANGULIZI**

- 1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji iliyochangua Bajeti ya Wizara ya Kilimo (Fungu 43), Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (Fungu 05) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (Fungu 24) mnamo tarehe 25 na 26 Machi, 2020 Jijini Dodoma, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.*
- 2. Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuendelea kuijalia nchi yetu amani, utilivu na mshikamano na kutuwezesha kushiriki katika mkutano huu wa Bunge la 19 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni mkutano wa mwisho katika uhai wa Bunge la 11.*
- 3. Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini kusimamia Kilimo ambacho ndio tegemeo la Watanzania walio wengi. Vilevile, niwashukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanayofanya kusukuma maendeleo ya nchi hii, ikiwemo Sekta ya Kilimo. Aidha, binafsi ninawashukuru viongozi wangu wote kwa maelekezo, ushauri na miongozo wanayonipatia ambayo imenisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa.*

4. *Mheshimiwa Spika*, kwa mara nyingine naomba kumpongeza Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 1 Aprili, 2020. Hotuba hiyo iligusa maeneo mengi ikiwemo Sekta ya Kilimo ambapo alisisitiza uimarishaji wa huduma za ugani, kilimo cha umwagiliaji, ushirika, upatikanaji wa pembejeo sahihi na miundombinu ya masoko. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Hussein Mohammed Bashe (Mb.) kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri na Ndugu Gerald M. Kusaya kuwa Katibu Mkuu katika Wizara ya Kilimo na kuungana na viongozi wengine wa wizara kusukuma kilimo hapa nchini.
5. *Mheshimiwa Spika*, naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, na Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.) pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyolismamia na kuliendesha Bunge letu tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa. Aidha, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kwa kazi nzuri waliyoifanya katika miaka hii mitano ya kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili. Nimpongeze pia Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu Mbunge wa Singida Mashariki kwa kuchaguliwa kujeungu na Bunge lako Tukufu.
6. *Mheshimiwa Spika*, naomba kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene Mbunge wa jimbo la Kibakwe kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu Mbunge wa jimbo la Ilala kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Mbunge wa Iramba Magharibi kuwa Waziri wa Katiba na Sheria.
7. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 Bunge lako Tukufu limewapoteza Wawakilishi wenzetu wanne ambao ni Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wa Newala Vijiji aliyefariki tarehe 15

Januari 2020, Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare Mbunge wa Viti Maalum aliyefariki tarehe 20 Aprili, 2020, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa Mbunge wa Sumve aliyefariki tarehe 29 Aprili, 2020 na Mheshimiwa Balozi Dkt Augustine Philip Mahiga (Mb) aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria aliyefariki tarehe 1 Mei, 2020. Nitumie fursa hii kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, Chama cha Mapinduzi, familia za marehemu, ndugu, jamaa na wananchi wa majimbo ya Newala Vijijini na Sumve.

*8. Mheshimiwa Spika*, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma Mbunge wa Viti Maalum kwa ushirikiano na ushauri mzuri walioutoa katika kipindi chote cha mwaka 2019/2020 pamoja na kuipitia taarifa ya utekelezaji mwaka 2019/2020 na Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2020/2021. Naomba kulihakikisha Bunge lako Tukufu kwamba, ushauri wao umezingatiwa na tutaendelea kushirikiana na Kamati ili kuleta mageuzi ya kilimo na kufikia matarajio ya wananchi katika kufikia uchumi wa kati.

*9. Mheshimiwa Spika*, natoa shukrani zangu za pekee kwa Wananchi wa Jimbo la Vwawa kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Napenda kuwahimiza kuendelea kuniamini na kuiamini Serikali ya Awamu ya Tano na kwamba maendeleo ya Jimbo letu yanategemea sana kufanya kazi kwa pamoja. Aidha kwa namna ya peke ninawapongeza sana Naibu Mawaziri Mh. Omary Tebeta Mgumba (Mb) na Hussein Mohamed Bashe (Mb) kwa jinsi wanavyonisaidia katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya wizara ya kilimo. Vile nawapongeza Katibu mkuu Ndugu Gelard Kusaya, Naibu katibu Mkuu. Prof. Siza Tumbo, Wakuu wa Taasisi, Bodi na wakala zilizo chini ya wizara na Watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano na kazi nzuri wanazoendeleza kuzitekeleza ili kufanikisha malengo ya kilimo nchini.

*Homa Kali ya Mapafu (COVID-19)*

*10. Mheshimiwa Spika, mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (COVID-19) umeathiri sekta mbalimbali za kiuchumi nchini ikiwemo sekta ndogo ya mazao. Wizara ya Kilimo imefanya tathmini na kubaini kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2019/2020 haujaathirika kwa kuwa pembejeo zimeshawasili nchini. Aidha, katika kukabiliana na uhaba wa mbolea unaoweza kutokea kutokana na kuendelea kuwepo kwa tatizo la COVID-19 Wizara itaruhusu mbolea kuingizwa nchini bila kufuata utaratibu wa uagizaji wa mbolea kwa pamoja (BPS), kwa mujibu wa kifungu cha 7(4) cha Kanuni za Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja (*Fertilizer Bulk Procurement Regulations, 2017*).*

*11. Mheshimiwa Spika, mazao ya asili ya biashara ambayo ni pamba, korosho na kahawa msimu yake ya mauzo imeishia Machi, 2020 na hivyo kutoathirika na ugonjwa huo. Aidha, kwa zao la tumbaku wakulima wameshafunga mikataba na wanunuzi kwa ajili ya msimu 2020/21. Mazao ambayo yameonesha dalili za kuathirika ni chai na mazao ya bustani ambayo masoko na usafirishaji wake nje ya nchi umeathirika. Vilevile, ugonjwa wa COVID-19 iwapo utaendelea kwa muda mrefu unaweza ukaathiri soko la pamba ambalo msimu wake wa mauzo unaanza mwezi Mei na upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa msimu wa 2020/2021 hususan mbolea na viuatilifi ambavyo vinaagizwa kutoka nje ya nchi.*

*12. Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitekeza kutokana na ugonjwa wa COVID-19, Wizara kuititia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) itanunua tani 65,000 kutokana na fedha zilizotengwa kwenye bajeti 2019/2020 Shilingi bilioni 15 na fedha za mapato ya ndani Shilingi bilioni 24 ili kufanya hifadhi ya chakula kuongezeka na kufikia tani 103,698.794 ambayo inajumuisha akiba ya tani 38,698.794. Mahitaji ya nafaka kwa mwezi kwa Watanzania wote ni wastani wa tani 750,000. Tukichukulia asilimia 20 ya watanzania ndiyo pekee watakaohitaji kununua chakula kwa asilimia 100 ambao mahitaji yao ya nafaka kwa mwezi yatakuwa tani 145,000. Kiasi hicho cha chakula ni kidogo*

endapo dharura ya mahitaji ya chakula yatatokea. Hivyo, katika kukabiliiana na upungufu huo, Wizara kupitia NFRA itanunua tani 435,000 zenye thamani ya Shilingi bilioni 217.5 ambazo zitatosheleza kwa miezi mitatu (3). Katika kufanikisha mpango huo, Wizara itafanya mazungumzo na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuwezesha NFRA kupata fedha hizo. Vilevile, kuanzia Julai, 2020 NFRA itanunua tani 300,000 kupitia bajeti iliyotengwa katika mwaka 2020/2021 pamoja na mapato ya Wakala. Hivyo kufanya jumla ya chakula kitakacho nunuliwa kuwa tani 735,000.

13. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizoko pembezoni mwa nchi, itaendelea kuimarisha udhibiti wa utoroshwaji wa chakula nje ya nchi kupitia njia zisizo rasmi; itaimarisha usafirishaji wa chakula kutoka kwenye mikoa yenyе ziada kwenda kwenye mikoa yenyе upungufu; itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha matumizi ya Soko la Bidhaa kwa mazao ambayo hutegemea zaidi wanunuzi kutoka nje ya nchi kama vile zao la korosho ili kuwezesha biashara kufanyika bila kikwazo chochote. Vilevile, Wizara inasisitiza wananchi kusindika na kufungasha mazao hususan ya mbogamboga na matunda ili kulinda ubora na kuongeza muda wa matumizi (Shelf life).

## **2. MCHANGO WA SEKTA YA KILIMO KATIKA UCHUMI**

14. *Mheshimiwa Spika*, kilimo kimeendelea kuwa ni mhimili muhimu katika maendeleo ya uchumi wa taifa letu. Katika kipindi cha miaka mitano, Pato la Taifa linalotokana na kilimo, kwa kutumia bei za Mwaka 2015 limeongezeka kwa asilimia 17 kutoka Shilingi trillioni 25.2 Mwaka 2015 hadi Shilingi trillioni 29.5 Mwaka 2019. Vilevile, sekta imeendelea kutoa ajira kwa Watanzania kwa asilimia 58 Mwaka 2018, imechangia asilimia 28.2 ya Pato la Taifa ambapo sekta ndogo ya mazao imechangia asilimia 16.2. Hii imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwemo vyakula vinavyotokana na mazao ya kilimo. Aidha, katika ya mwaka 2015 hadi 2019 sekta ya kilimo imeendelea kukua kwa wastani

wa asilimia 5.2 ambapo sekta ndogo ya mazao imeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 5.8.

### **3. UTEKELEZAJI WA MALENGO NA BAJETI KWA MWAKA 2019/2020**

15. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kutekeleza maeneo ya kipaumbele ya kuongeza uzalishaji na tija kwenye kilimo kwa kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, udhibiti wa visumbufu, matumizi ya zana bora za kilimo na huduma za ugani; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo na masoko; kufanya utafiti wa kilimo na kuzalisha teknolojia kwa mazao ya mahindi, muhogo, ngano, michikichi, ufuta, alizeti, pamba na mpunga.

16. *Mheshimiwa Spika*, maeneo mengine ya kipaumbele ni kuboresha maarifa na ujuzi kwa watafiti kupitia mafunzo ili kuwezesha utafiti kufanyika kwa weledi na tija; kuimarisha huduma za upimaji wa matabaka na ubora wa udongo kuendana na mahitaji ya mazao ya kilimo ki-ikolojia; kuimarisha vituo vya utafiti kwa kujenga miundombinu muhimu na kuongeza vitendea kazi vya utafiti; kutoa huduma za ushauri kuhusu utafiti, mafunzo na usambazaji taarifa za kilimo na sayansi shirikishi; kusajili na kuandaa kanzidata ya wakulima na kuimarisha ushirika.

#### **3.1 Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2019/2020**

##### **3.1.1 Makusanyo ya Maduhuli**

17. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020 Wizarailidhinishiwakukusanya Shilingi 3,487,515,000 kuititia Fungu 43 na 05. Kati ya fedha hizo, Shilingi 3,472,515,000 ni za Fungu 43 na Shilingi 15,000,000 ni za Fungu 05. Hadi kufikia Machi, 2020 makusanyo ya mapato yalikuwa Shilingi 2,748,993,668.78 sawa na asilimia 78.82 ya lengo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,619,905,800.28 ni za Fungu 43 na Shilingi 129,087,868.50 ni za Fungu 05.

### 3.1.2 Fedha Zilizoidhinishwa

18. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ya Kilimo kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya Shilingi bilioni 253.86 ili kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 77.78 ni kwa matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 176.08 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

19. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ya Kilimo (Fungu 43 imeidhinishiwa Shilingi bilioni 208.04 ambapo Shilingi bilioni 64.47 ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 143.58 ni fedha za maendeleo. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (Fungu 05) iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 37.49 ambapo Shilingi bilioni 4.99 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 32.50 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Tume ya Maendeleo ya Ushirika (Fungu 24) ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 8.33 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

## 4. MAFANIKIO YA WIZARA YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA SERIKALI YA AWAMU YA TANO

20. *Mheshimiwa Spika*, Awali ya yote nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa msukumo wa kuendeleza Sekta ya Kilimo. Aidha, katika Hotuba yake alioitoa tarehe 20 Novemba, 2015 akifungua rasmi Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Dodoma alisisitiza kutekeleza ahadi alizozitoa kwa wakulima kupitia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2015-2020. Wizara imetekeleza ahadi hizo kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) na kuwezesha kilimo kuchangia katika uchumi na maendeleo ya Taifa letu, hususan katika maeneo ya usalama wa chakula na lishe, ajira, upatikanaji wa malighafi za viwanda na kuchangia katika kupunguza umaskini na kuongeza kipato cha wakulima.

21. *Mheshimiwa Spika*, baadhi ya ahadi alizotoa ni pamoja na kuimarisha huduma za ugani, upatikanaji na usambazaji wa pembejeo, zana za kisasa za kilimo, masoko ya uhakika ya mazao, kuimarisha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya kilimo na kuondoa ushuru, kodi na tozo ambazo ni kero kwa ajili ya maendeleo ya kilimo.

*22. Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha miaka minne Wizara imepata mafanikio makubwa katika maeneo ya usalama wa chakula na lishe; uzalishaji wa mazao makuu ya biashara; upatikanaji wa pembejeo za kilimo; viwanda vyta kuchakata mazao ya kilimo na masoko; utafiti, huduma za ugani na mafunzo; hifadhi ya mazao; uzalishaji wa mazao ya bustani; kuimarika kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko; kuimarika kwa ushirika; kuimarika kwa kilimo cha umwagiliaji; ongezeko la ushiriki wa vijana katika kilimo; matumizi bora ya ardhi; kuhuisha mifumo na sera za kilimo na kuanzishwa kwa kanzidata ya wakulima.

#### **4.1 Usalama wa Chakula na Lishe**

*23. Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano (5) uzalishaji wa chakula umeendelea kuimarika na hivyo kuwezesha nchi yetu kujitosheleza kwa chakula kwa wastani wa asilimia 121 na kuwa na wastani wa ziada ya tani 2,798,700.60. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2019/2020 ni tani 13,819,863 zikiwemo tani 8,730,677 za mazao ya nafaka na tani 5,089,186 za mazao yasiyo nafaka. Pamoja na kushuka kwa uzalishaji wa chakula katika msimu wa 2018/2019, kumekuwa na ziada ya tani 2,473,774 za chakula, zikiwemo tani 166,152 za mazao ya nafaka na tani 2,307,621 za mazao yasiyo nafaka. Kwa kuzingatia kigezo cha upimaji wa kiwango cha utoshelevu (*Self Sufficiency Ratio-SSR*), mwaka 2019/2020 nchi imekuwa na kiwango cha utoshelevu cha asilimia 118. (Jedwali Na. 1.).

Jedwali Na. 1: Upatikanaji wa Chakula

| Mwaka     | Upatikanaji wa Chakula (tani) * | Mahitaji (tani) | Ziada (tani) | Utoshelevu (%) |
|-----------|---------------------------------|-----------------|--------------|----------------|
| 2015/2016 | 15,528,820                      | 12,946,123      | 2,582,697    | 120            |
| 2016/2017 | 16,172,841                      | 13,159,326      | 3,013,515    | 123            |
| 2017/2018 | 15,900,864                      | 13,300,034      | 2,600,831    | 120            |
| 2018/2019 | 16,891,974                      | 13,569,285      | 3,322,686    | 124            |
| 2019/2020 | 16,293,637                      | 13,819,863      | 2,473,774    | 118            |
| Jumla     | 80,788,136                      | 66,794,631      | 13,993,503   | Wastani 121    |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo, 2020; \*Upatikanaji wa chakula kwa mwaka husika ni sawa na uzalishaji wa mwaka uliopita*

24. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na uwepo wa ziada ya chakula kitaifa, Halmashauri 16 za Wilaya katika Mikoa tisa (9) nchini zilbainika kuwa na upungufu wa chakula na bei kubwa ya vyakula katika masoko hususan zao la mahindi. Kutokana na hali hiyo, Wizara kuititia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) iliua jumla ya tani 6,330 za chakula kwa bei nafuu zikiwemo tani 3,130 za unga wa mahindi na tani 3,200 za mahindi katika maeneo yenye uhitaji (Kiambatisho Na.1).
25. *Mheshimiwa Spika*, kulingana na taarifa ya mapitio ya kati (Mid Term Review) ya hali ya lishe nchini katika utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa lishe (NMNAP 2016-2021) yaliyofanyika mwaka 2019, inaonyesha kuwa udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano (5) umepungua kutoka asilimia 34 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 32 mwaka 2018. Aidha, Kiwango cha ukondefu kwa watoto chini ya miaka mitano (5) kitaifa kimeendelea kushuka kutoka asilimia 3.8 hadi asilimia 3.5 na pia upungufu wa damu kwa kina mama umepungua kutoka asilimi 44.7 hadi kufikia asilimia 28.7 kwa kipindi hicho.
26. *Mheshimiwa Spika*, hali hii imechangiwa na juhudzi za wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi za Serikali na Binafsi, Bodi za Mazao, Wakala za Serikali na Sekta Binafsi ambazo zimekuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mazao mbalimbali ya chakula na hasa yenye viinilishe kwa wingi yanazalishwa, yanahifadhiwa vizuri ili kulinda afya ya walaji, yanasindikwa kuzuia upotevu na hatimaye yanaandalisha na kutumiwa ipasavyo ili kumpatia mlaji afya bora. Aidha, Wizara kuititia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imezalisha aina (5) za mbegu za viazi vitamu vilivyoongezewa vitamin A maarufu kama "viazi lishe" na aina (2) za maharage yaliyoongezewa madini chuma na zinki.
27. *Mheshimiwa Spika*, Uzalishaji na utumiaji wa mazao haya umechangia kupunguza tatizo la upungufu wa damu unaosababishwa na ukosefu wa madini chuma na tatizo la upungufu wa vitamin A hususan kwa akina mama walio katika

umri wa kuzaa na watoto chini ya miaka mitano. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa lishe imeandaa Mwongozo wa Uongezaji wa Virutubisho Kibailolojia Katika Mazao, Mwongozo wa kilimo kinachozingatia lishe, Mwongozo wa Kukabiliana na Upotevu wa Mazao Baada ya kuvuna, Mwongozo wa kukabiliana na sumukuvu Katika Mazao na Mwongozo wa Uzalishaji wa Mazao ya Mbogamboga na Matunda.

28. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Chakula na Lishe Nchini na Shirika la Kimataifa la Lishe imeandaa Mwongozo wa Uzalishaji wa Mazao Yaliyoongezewa Virutubishi Kibailolojia (*Biofortification Guideline*) kwa lengo la kutoa mwongozo kwa wadau wote katika mnyororo wa thamani wa mazao hayo. Uzalishaji na matumizi ya Mazao hayo utasaidia katika kupunguza matatizo ya ukosefu wa vitamini kama vile vitamini A na madini kama vile Zinki na Chuma. Aidha, kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Wizara imeandaa Kitini cha Mafunzo ya Mkulima chenye madhumuni ya kuboresha lishe ya wanakaya kuititia kilimo. Kitini hiki kinalenga kumuelimisha mkulima namna lishe ya wanakaya, uhakika wa chakula na kipato cha wanakaya kinavyoweza kuboreshwa kuititia kilimo chenye tija.

#### **4.2 Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara**

29. *Mheshimiwa Spika*, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara yakiwemo pamba, kahawa, chai, pareto, tumbaku, korosho, m Konge na miwa umeongezeka kutoka jumla ya tani 796,502 mwaka 2015/2016 hadi jumla ya tani 1,144,631 Mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 43.7 (Jedwali Na. 2.).

## Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara (Tani)

| Zao     | 2015/2016 | 2016/2017 | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020*   | Jumla        |
|---------|-----------|-----------|-----------|-----------|--------------|--------------|
| Pamba   | 149,445   | 132,934   | 222,039   | 348,910   | 300,000      | 1,153,328    |
| Kahawa  | 60,921    | 48,329    | 45,245    | 68,147    | 55,979       | 278,621      |
| Chai    | 32,629    | 26,975    | 34,010    | 37,193    | 11,185       | 141,992      |
| Pareto  | 2,011     | 2,150     | 2,400     | 2,014     | 1,627        | 10,202       |
| Tumbaku | 60,691    | 58,639    | 50,522    | 70,824    | 70,087       | 310,763      |
| Korosho | 155,416   | 265,238   | 313,826   | 225,053   | 232,000      | 1,191,533    |
| Mkonge  | 42,314    | 36,533    | 40,635    | 33,271    | 35,552       | 188,305      |
| Sukari  | 293,075   | 330,843   | 303,752   | 359,219   | 298,948.61   | 1,585,837.61 |
| Jumla   | 796,502   | 901,641   | 1,012,429 | 1,144,631 | 1,005,378.61 | 4,860,581.61 |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo, 2020: \*Msimu wa mwaka 2019/2020 unaendelea (Matarajio)*

30. *Mheshimiwa Spika*, vilevile katika kipindi hicho cha Serikali ya Awamu ya Tano, kiasi cha tani 1,613,000 za mazao ya kahawa, pamba, katani, chai, tumbaku na korosho kiliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa jumla ya Dola za Marekani Milioni 3,419.77 sawa na Shilingi 6,910,698,469,300 (Jedwali Na. 3a.). Aidha, kiasi cha tani 212,156 za mazao hayo ya biashara chenye thamani ya Shilingi 866,100,000,000 kiliuzwa ndani ya nchi (Jedwali Na.3b). Pia, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku kwa mara ya kwanza imeuza jumla ya tani 500 za daraja la chini (Reject) ambayo mapato yake yamesaidia kupunguza gharama za uzalishaji kwa mkulima na kumuongezea kipato.

Jedwali Na. 3a: Mauzo ya Mazao ya Biashara Nje ya Nchi

| Zao     | Mauzo (Tani '000) |        |        |        | Jumla   | Thamari (Milioni USD) |       |       |        | Jumla    |
|---------|-------------------|--------|--------|--------|---------|-----------------------|-------|-------|--------|----------|
|         | 2015              | 2016   | 2017   | 2018   |         | 2015                  | 2016  | 2017  | 2018   |          |
| Kahawa  | 51.9              | 58.7   | 41.8   | 56.6   | 2090    | 1622                  | 153.7 | 126.3 | 147.94 | 590.14   |
| Pamba   | 29.1              | 33.0   | 25.3   | 47.4   | 134.8   | 302                   | 468   | 33.8  | 68.39  | 182.19   |
| Katani  | 152               | 8.6    | 17.0   | 20.3   | 61.1    | 265                   | 172   | 28.7  | 33.22  | 105.62   |
| Chai    | 27.5              | 26.3   | 27.5   | 26.9   | 1082    | 44.0                  | 44.8  | 49.1  | 45.95  | 183.85   |
| Tumbaku | 66.3              | 74.3   | 48.3   | 72.2   | 261.1   | 287.6                 | 339.2 | 195.5 | 270.3  | 1,092.90 |
| Korosho | 171.7             | 217.5  | 329.4  | 120.2  | 838.8   | 218.8                 | 320.2 | 529.6 | 196.47 | 1,265.07 |
| Jumla   | 361.70            | 418.40 | 489.30 | 343.60 | 1,613.0 | 769.3                 | 921.9 | 966.3 | 762.27 | 3,419.77 |

*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, 2020*

Jedwali Na. 3b: Mauzo ya Mazao ya Biashara Ndani ya Nchi (2015-2018)

*Chanzo: Wizara ya Kilimo, 2020*

#### 4.3 Mazao ya Bustani

31. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka kutoka tani 5,931,900 mwaka 2015/2016 hadi tani 6,556,102 mwaka 2018/2019. Thamani ya mauzo ya mazao ya bustani yakiwemo mboga na maua nje ya nchi yameongezeka toka

| Zao       | Dola za Marekani millioni 412 mwaka 2015 hadi Dola za |                 |                 |                 |                 |
|-----------|---|-----------------|-----------------|-----------------|-----------------|
|           | Mauzo<br>(mln.)                                       | Mauzo<br>(mln.) | Mauzo<br>(mln.) | Mauzo<br>(mln.) | Mauzo<br>(mln.) |
| 2015/16   | 2014  | 2017/18         | 2018/19         | 2015/16         | 2018/19         |
| Kikawanda | 2,959   | 2,587           | 2,418           | 5,160           | 5,931           |
| Pambaa    | 2,621   | 2,370           | 2,283           | 4,335           | 4,682           |
| Melati    | 2,785   | 3,800           | 3,710           | 3,823           | 3,709           |
| Ciba      | 3,523   | 4,287           | 4,170           | 4,162           | 4,082           |
| Jumla     | 10,093  | 11,701          | 11,761          | 15,235          | 16,702          |
| Kigogo    | 2,171.7   | 1,715.5         | 1,622.8         | 2,088.8         | 2,293.7         |
| Jumla     | 45,942  | 47,844          | 46,064          | 53,572          | 52,136          |

32. *Mheshimiwa Spika*, uzalishaji wa mazao ya bustani hususan mboga, matunda na viungo huchangiwa na asilimia 85 ya sekta isiyo rasmi ambayo ni ya wakulima wadogo ambaa ndio wanaozalisha na kuza mazao hayo katika masoko ya ndani. Katika kipindi cha miaka minne (4) Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi iliendele kutoa mafunzo ya uzalishaji na uongezaji thamani mazao hayo kama sehemu ya kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Mazao ya Bustani (National Horticultural Development Strategy 2012-2021). Aidha, ili kuwezesha wakulima hao kuwa katika mfumo rasmi Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imeendelea kutoa

mafunzo ya kilimo biashara kwa mfano kupitia Mradi wa TANSHEP.

33. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi hicho, uwekezaji katika mazao ya bustani kupitia Sekta Binafsi chini ya mwamvuli wa TAHA umefikia Dola za Marekani milioni 30. Ongezeko hilo limetokana na maboresho ya mifumo ya biashara ikiwemo ya usajili, uzalishaji na uagizaji wa pembejeo za uzalishaji wa mazao hayo pamoja na maboresho ya kisera, kodi na tozo ambayo yamepunguza gharama za uzalishaji, ufanyaji biashara na kuimarisha ushindani wa mazao hayo katika masoko ya kikanda na kimataifa. Uwekezaji katika tasnia hii umewezesha uanzishaji wa viwanda mbalimbali yya kusindika matunda na mboga (Kiambatisho Na. 3) pamoja na kuongezeka kwa mauzo nje ya nchi.

34. *Mheshimiwa Spika*, zao la parachichi ni miongoni mwa mazao ya bustani yanayochipukia na limeonesha mafanikio makubwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 20,000 Mwaka 2015 hadi kufikia tani 190,000 Mwaka 2018. Kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa zao hili, mauzo ya parachichi nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 3,279 Mwaka 2015 hadi tani 9,000 mwaka 2018. Mauzo hayo yenye thamani ya Dola za marekani Milioni 8.5 yamefanyika katika soko la Ulaya katika nchi za Ufaransa, Uhlanzi na Uingereza.

35. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na TAHA imetoa mafunzo kuhusu matumizi ya teknokojia na mbinu za kilimo bora cha mazao ya bustani kwa wakulima 150,000. Kutokana na mafunzo hayo, tija ya mazao ya kabichi imeongezeka kutoka tani 12 kwa ekari hadi tani 44 kwa ekari; nyanya kutoka tani 2.8 kwa ekari hadi tani 10 kwa ekari; vitunguu kutoka tani 3.4 kwa ekari hadi tani 13 kwa ekari; na nanasi kutoka tani 16 kwa ekari hadi tani 37 kwa ekari.

36. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hicho Wizara kwa kushirikiana na Tanzania Horticultural Association (TAHA)

imewezesha upatikanaji wa usafiri wa moja kwa moja wa mazao ya bustani kutoka Tanzania kwa kutumia ndege ya Shirika la Ndege la Ethiopia kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro badala ya kupitia uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta nchini Kenya. Ndege hiyo itakuwa inachukua mizigo wastani wa tani 55 kwa wiki. Hatua hiyo imesaidia kuwa na usafiri wa uhakika, kupunguza gharama za usafirishaji, kupunguza upotevu wa mazao kwa kupunguza muda wa usafirishaji na kuongeza fedha za kigeni.



*Waziri wa Kilimo Mhe Japhet Hasunga (Mb), Mkuu wa Mkoa wa Kilimajaro Mhe. Anna Mghwira na Afisa Mtendaji Mkuu wa TAHA Dkt. Jacqueline Mkindi pamoja na watendaji akiwemo Rubani wa ndege ya mizigo aina ya 787-Dreamliner mali ya Shirika la Ndege la Ethiopia wakiwa katika picha ya pamoja ndani ya ndege hiyo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimajaro (KIA) tarehe 17 Aprili 2020 baada ya kupakia shehena kubwa ya matunda aina ya parachichi uliokuwa ukitoka Arusha kwenda Bara la Ulaya.*



*Waziri wa Kilimo, Mhe. Japhet Hasunga (Mb) akipakia mizigo ya matunda aina ya parachichi kwenye ndege mara baada ya kuongoza mapokezi ya ndege ya mizigo aina ya 787-Dreamliner mali ya Shirika la ndege la Ethiopia katika uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimajaro (KIA) tarehe 17 Aprili, 2020. Kushoto kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Dkt. Anna Mghwira akishuhudia zoezi hilo.*

#### **4.4 Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo**

##### **4.4.1 Mbegu**

37. *Mheshimiwa Spika, katika kipindi Serikali ya Awamu ya Tano upatikanaji wa mbegu bora umeongezeka kutoka tani 36,614.28 mwaka 2015/2016 hadi tani 76,725.52 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 110. Aidha, uzalishaji wa ndani wa mbegu bora umeongezeka kutoka tani 20,604.97 mwaka 2015/2016 hadi tani 69,173.17 mwaka 2019/2020. Uzalishaji huo umepunguza uagizaji wa mbegu kutoka nje ya nchi kutoka tani 16,009.31 mwaka 2015/2016 hadi tani 7,552.35 mwaka 2019/2020 sawa na punguzo la asilimia 53 (Kiambatisho Na.4(a)). Vilevile, uzalishaji wa miche umeongezeka kutoka miche 5,000,000 mwaka 2015/16 hadi kufikia miche 25,285,859 mwaka 2019/20. Pamoja na mambo mengine, mafanikio hayo yametokana na kuongezeka kwa*

eneo la uzalishaji wa mbegu na miche kutoka hekta 10,887 hadi hekta 94,368. (Kiambatisho Na. 4 (b))



*Uzalishaji wa ndani wa mbegu bora umeongezeka. Hii ni mbegu bora ya mpunga aina ya TARI – RIC-1 iliyogunduliwa na Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Kilimo (TARI Katrin Ifakara)*

38. *Mheshimiwa Spika*, ongezeko hilo limechangiwa na kupunguzwa ama kufutwa kwa baadhi ya kodi na tozo katika uzalishaji wa mbegu bora pamoja na kuimarisha mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Binafsi. Mathalani, Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) umefanikiwa kuhamasisha kampuni binafsi za mbegu kuzalisha mbegu bora kupitia mashamba matano (5) ya Wakala. Vilevile, Wizara inaendelea kutoa mafunzo ya kuzalisha mbegu Daraja la Kuazimiwa Ubora (QDS) kwa wakulima wadogo.

39. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora Wizara imeimarisha maabara ya TOSCI na hivyo kupata Ithibati ya Shirika la Kimataifa la Uthibiti wa Ubora wa Mbegu (International Seeds Testing Association – ISTA) pamoja na kuijunga na Skimu za Mbegu za Shirika la Kimataifa (OECD Seed Schemes) ambayo itaiwezesha nchi kufanya biashara ya mbegu kimataifa.

40. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Kamati ya Taifa ya Mbegu imepitisha matumizi ya aina mpya 40 za mbegu bora za mazao ya mahindi (10), mpunga (2), ulezi (1), pamba (3), muhogo (9), alizeti (9) na viazi vitamu (6). Mbegu hizo zinatoa mavuno kwa wingi, zina ukinzani dhidi ya magonjwa na wadudu, zinahimili ukame na zinaza kwa muda mfupi (Kiambatisho Na. 5). Kati ya mbegu zilizoidhinishwa, TARI imegundua aina 22.

41. *Mheshimiwa Spika*, katika jitihada za kuongeza uzalishaji wa mbegu za mafuta nchini, hadi mwezi Machi, 2020 TARI kwa kushirikiana na FELISA, Ndugu Development Foundation na Yangu Macho imezalisha jumla ya mbegu 1,791,768 za michikichi na kuzisambaza kwa ASA, Magereza ya Kwitanga na llagala, JKT-Bulombola na Halmashauri sita (6) za Mkoa wa Kigoma kwa ajili ya kuzalisha miche na kusambaza kwa wakulima.

#### 4.4.2 Mbolea

42. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hicho Wizara imeimarisha upatikanaji wa mbolea nchini kwa kuanzisha mfumo wa ununuzi wa pamoa (*Bulk Procurement System - BPS*) ambao umewezesha kuongeza upatikanaji wa mbolea kutoka tani 302,482 mwaka 2015/2016 hadi 633,197 mwaka 2019/2020 (Kiambatisho Na. 6 (a)). Mfumo huo umewezesha wakulima kupata mbolea kwa wakati na bei nafuu. Aidha, idadi ya viwanda vinavyotengeneza mbolea na visaidizi vya mbolea (*fertilizer suppliment*) vimeonge zeka kutoka viwanda vinne (4) mwaka 2015 hadi viwanda 13 mwaka 2019. Kati ya viwanda hivyo, viwanda viwili (2) ni vya visaidizi na 11 ni vya mbolea.



*Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kumeenda sambamba na utoaji wa elimu sahihi kuhusu mahitaji ya virutubisho kwenye udongo katika maeneo tofauti ya Wakulima*

43. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 kiasi cha mbolea kilichopo nchini ni tani 203,219 sawa na asilimia 35 ya mahitaji ya mbolea ya tani 586,604 kwa mwaka 2019/2020 (Kiambatisho Na.6(b)). Aidha, kiasi cha tani 197,596 za mbolea zilitokana na mfumo wa BPS ambapo tani 103,340 (Urea tani 74,840, na DAP tani 28,500) ziliagizwa katika mwaka 2019/2020 na tani 94,256 ni bakaa ya mwaka 2018/2019. Kutokana na matumizi ya mfumo wa BPS, bei ya mbolea imepungua kati ya asilimia 6 na 17.

#### 4.4.3 Viuatilifu

44. *Mheshimiwa Spika*, Upatikanaji wa viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya milipuko kama vile panya, nzige, kweleakwelea na viwavijeshi vamizi umeongezeka kutoka tani 4,111.50 mwaka 2015 hadi tani 16,869.10 mwaka 2019. Hadi Machi 2020, tani 8,719.53 za viuatilifu zimeingizwa nchini. Kati ya hizo, tani 3,011.21 ni viuadudu (*insecticides*), tani 3,232.38 ni vizuiakuvu (*fungicides*), tani 2,314.654 ni viuagugu (*herbicides*) na tani 161.287 ni viuatilifu vya kudhibiti panya na minyoo. Vilevile, tani 5,693 za kizuiakuvu cha Salfa ya unga kwa ajili ya zao la Korosho na ekapaki 902,000 za viuadudu kwa ajili ya zao la pamba zimeingizwa nchini. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Pamba imeweza upatikanaji wa vinyunyizi (mabomba) 20,000 vyenye thamani ya Shilingi bilioni 1.6 na ekapaki milioni 8.2 zenye thamani ya Shilingi bilioni 41.

45. *Mheshimiwa Spika*, ili kudhibiti ubora wa Viuatilifu Wizara kupitia TPR limekagua wafanyabiashara 222 wakiwemo wauzaji, watengenezaji, wafukizaji na waagizaji kutoka mikoa ya Ruvuma (78), Mbeya (46), Dar es Salaam (55), Geita, Mwanza na Shinyanga (28) na Tanga (15). Aidha, TPRI imetua mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa wakulima, maafisa ugani na wauzaji 765 kutoka katika mikoa ya Kagera (52), Kigoma (144), Arusha (63), Ruvuma (55) na Iringa (85). Vilevile, mafunzo kuhusu mbinu bora za unyunyizaji wa viuatilifu yametolewa kwa wakulima na maafisa ugani 366 kutoka mikoa ya Simiyu (329), Kigoma (7) na Tabora (30). Ili kuongeza upatikanaji wa viuatilifu na kupunguza upotevu wa mazao wakati wa kuvuna na baada ya kuvuna, Wizara, kupitia TPRI imesajili viuatilifu vipyta 66.

*Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Mazao*

46. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka 2019/2020 Wizara imesambaza lita 22,628 za kiuatilifu aina ya Duduba katika mikoa 7 na lita 146.5 za *Methyl Eugnol* katika Mikoa nane (8) kwa ajili ya kudhibiti Viwavijeshi Vamizi na Nzi wa matunda. Vilevile, Wizara imesambaza tani 3,011.21 za viuadudu (*insecticides*), tani 3,232.38 za vizuiaku (fungicides), tani 2,314.654 za viuagugu (herbicides) na tani 161.287 za viuatilifu vingine kwa ajili ya kudhibiti panya na minyoo. Kati ya tani 161.287, kilo 59.5 zilitumika katika eneo la ekari 3,570 kudhibiti panya katika Wilaya za Musoma na Shinyanga. Aidha, Wizara imefanya savei ya nzige wekundu katika mbuga za mazalio za Ziwa Rukwa (Rukwa), Ikuu/Katavi (Katavi), Malagarasi (Kigoma/Tabora), Wembere (Tabora), Bahi (Dodoma) ambapo imebaini uwepo wa mazingira rafiki ya kuzaliana kwa nzige wekundu katika hekta 35,875. Lengo la hatua hiyo ilikuwa ni kudhibiti nzige ili wasiendelee kuzaliana.

47. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ilifanya ukaguzi wa mazao yanayoingizwa na kusafirishwa nje ya nchi ambapo tani 1,102,057.011 za mazao zilisafirishwa nje ya nchi; tani 12,795.75 ziliingizwa nchini na vyeti 7,572 vya usafi vilitolewa. Wizara pia, imetua mafunzo kwa wataalamu 20 wakiwemo wataalam wa afya ya mimea, watafiti na wadhibiti viwango

vya usalama wa chakula kuhusu athari na mbinu za udhibiti wa Sumukuvu kibaolojia.

#### **4.5 Zana za Kilimo**

*48. Mheshimiwa Spika*, matumizi ya zana bora za kilimo yameongezeka katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano ambapo matrekta makubwa na matrekta ya mkono yanayomilikiwa na wakulima yameongezeka kutoka 14,200 na 6,348 mwaka 2015 hadi 19,604 na 8,883 mwaka 2019, mtawalia (Kiambatisho Na. 7). Ongezeko hilo limechangia mabadiliko makubwa katika ukatuaji ambapo asilimia 20 ya maeneo yanalinwa kwa trekta, asilimia 27 wanyama kazi na asilimia 53 kwa jembe la mkono ikilinganishwa na mwaka 2015 ambapo asilimia 14 yalilimwa kwa trekta, asilimia 24 wanyama kazi na asilimia 62 jembe la mkono.

*49. Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020 Wizara kwa kushirikiana na *Taasisi* ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) imetoa mafunzo ya matumizi ya zana za kilimo kwa vijana 135 kutoka Mikoa ya Morogoro, Mbeya, Mwanza, Kilimanjaro, Tabora, Songea, Dodoma na Singida. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo ya Kilimo Hifadhi kwa wakulima 300 na maafisa ugani 15.

#### **4.6 Mikopo ya Pembejeo**

*50. Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za kilimo (AGITF) imetoa mikopo 93 yenye thamani ya Shilingi 836,359,000 ikiwemo tisa (9) ya mitambo ya mashambani, 80 ya Pembejeo, mmoja (1) wa Ukarabati, miwili (2) ya Miundombinu ya Kilimo na mmoja (1) wa fedha za kuendeshea shughuli za shamba (Kiambatisho Na. 8). Aidha, hadi Machi 2020, Shillingi 1,399,759,668 katи ya Shilingi 2,754,145,834 za mikopo zimerejeshwa, sawa na asilimia 51.

#### **4.7 Mazingira ya Uwekezaji na Uanzishaji wa Viwanda vya Kuchakata Mazao ya Kilimo**

*51. Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2015/16 hadi 2019/20, Serikali imefuta ushuru, tozo na ada 105 na

kupunguza tozo nne (4) kati ya 146 zilizokuwa zinatozwa katika mazao ya kilimo, pembejeo za kilimo na ushirika ambazo zimesaidia kumuondolea mkulima kero, kupunguza gharama za uzalishaji na kuchochaea uzalishaji na uwekezaji katika kilimo. Hatua hiyo imevutia Sekta Binafsi kuwekeza takribani Shilingi Triliioni 3.7 kwenye mnyororo wa thamani wa kuendeleza mazao ya chai, kahawa, mkonge, ngano, shayiri na mpunga. Aidha, ajira katika mnyororo wa thamani ya mazao ya kilimo zimeongezeka kutoka wastani wa ajira 3,880,262 Mwaka 2015/16 hadi kufikia wastani wa ajira 5,204,607 Mwaka 2018/19.

52. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imehamasisha ujenzi wa viwanda ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na kutengeneza ajira kwa watanzania. Katika kipindi cha miaka minne (4), jumla ya viwanda vipyta 189 vya kuchakata mazao vimeanzishwa. Aidha, viwanda vikubwa na vya katika vya kubangua korosho vimeongezeka kutoka 22 mwaka 2015/2016 hadi kufikia 31 mwaka 2019/2020. Viwanda tisa (9) vilivyoongezeka vina uwezo wa kubangua korosho tani 25,000 kwa mwaka na vimeanzishwa katika Mikoa ya Mtwara (6), Dar es Salaam (1) na Pwani (2). Aidha, vikundi vya kubangua korosho vimeongezeka kutoka 92 mwaka 2016 hadi 206 mwaka 2020.



*Viwanda vikubwa na vya katika vya kuongeza thamani mazao ya kilimo kama zao la korosho vimeongezeka*

53. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, katika kipindi hicho, viwanda vitatu (3) vya chai vimeanzishwa kikiwemo kiwanda cha chai cha *Kabambe Tea Factory* (Unilever) chenye uwezo wa kusindika majani mabichi ya chai tani 50 kwa siku. Kiwanda hicho cha *Unilever* kimewekeza mtaji wa Shilingi Billioni 17.8 na kinaajiri watu 250 hadi 300 kwa siku. Viwanda vingine viwili (2) ni pamoja na *Tropical Treasures Limited* kilichopo Kilimanjaro chenye uwezo wa kusindika kilo 1,000 za majani mabichi kwa siku na *Chai Collection Tanzania Limited* kinachochanganya na kufunga chai kwenye vikasha kwa ajili ya Hoteli kubwa na kinaajiri watu 15 hadi 20 kwa siku kutegemeana na uzalishaji.

54. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa zao la mkonge, viwanda vikubwa 11 vyenye uwezo wa kuchakata mkonge tani 7,193 kwa mwaka na viwanda vidogo 70 vyenye uwezo wa kuchakata mkonge tani 7,343.2 kwa mwaka vimeanzishwa na kuzalisha jumla ya ajira 37,907. Pia, Shilingi bilioni 160.8 zimewekezwa katika uzalishaji na uendelezaji wa viwanda vya kahawa. Vilevile, kiwanda cha *Murzah Wilmar Rice Millers* chenye uwezo wa kukoboa tani 600 za mpunga la viwanda Kihonda



aji wa viwanda vya mkonge  
amani ya mazao ya mkonge na  
bidhaa zinazotokana na zao hilo

#### **4.8 Upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya Kilimo**

55. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha miaka minne (4) Wizara, imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi. Katika kufikia azma hiyo, Wizara imeanzisha Kitengo cha Masoko (Agricultural Marketing Unit) katika Idara ya Maendeleo ya Mazao inayosimamia utafutaji wa masoko, kufanya tafiti za masoko na bei za mazao pamoja na kufuatilia mifumo ya uuzaaji wa mazao. Mafanikio ya kuanzishwa Kitengo hicho cha Masoko, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara imeanza kutoa mwenendo wa bei za mazao ya kilimo kwa wiki, mwezi na kila robo. Baadhi ya mazao hayo ni pamoja na mazao ya nafaka, mikunde, mboga na mazao ya biashara.

56. *Mheshimiwa Spika*, Wizara pia imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Serikali ya Japan kupitia mradi wa JICA kuwezesha na kuhamasisha wakulima wadogo wa mazao ya bustani na matunda kutafiti masoko ya mazao hayo kwa kutumia kauli mbiu isemayo "ANZIA SOKONI MALIZIA SHAMBANI KWA KIPATO ZAIDI". Elimu na hamasa hii imetolewa katika Mikoa ya Tanga, Arusha na Kilimanjaro na jumla ya kaya 4,080 zimenufaika. Vilevile, Wizara imeendelea kuwaunganisha wakulima na wanunuizi, wasindikaji, wafanyabiashara wa pembejeo, na wadau wengine katika mnyororo wa thamani kuwasiliana ili kukidhi haja ya soko husika. Pia, Wizara imeendelea kuzitumia Ofisi za Balozi zilizopo nchini na Balozi za Tanzania zilizopo nchi za nje kutafuta masoko ya mazao ya kilimo. Hatua hii imeonesha kuwa na mafanikio makubwa hususan kuongezeka kwa kampuni za ununuizi wa mazao mbalimbali.

57. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kunufaika na masoko ya nje yenye masharti nafuu ambayo hayana ukomo wa bidhaa wala ushuru wa forodha (Duty Free Quota Free - DFQF). Masoko hayo yapo katika nchi za, China, India, Japan, Uswisi, Norway, Uturuki, New Zealand, Iceland, Brazil, Morocco, Jamhuri ya Korea; Soko la Marekani kupitia mpango wa AGOA (African Growth Opportunity Act); Umoja wa Ulaya, EAC, na SADC.

*58. Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Sekta Binafsi imeimarisha matumizi ya mifumo ya masoko ikiwemo Soko la Bidhaa (TMX), Stakabadhi za Ghala, Minada na Kilimo cha Mkataba. Matokeo ya mifumo hiyo ni pamoja na kuvunganisha Vyama vya Ushirika 63 vinavyozalisha ufuta na kakao kuuza mazao yao kwa Mfumo wa Soko la Bidhaa. Vilevile, Wizara imewezesha na kusimamia Vyama 16 vya Ushirika vya wabanguaji wadogo wa korosho kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na kuuza tani 291,329.51 katika nchi za India, China na Vietnam.

*59. Mheshimiwa Spika*, matumizi ya mifumo hiyo imesaidia kuimarika kwa bei ya mazao ya kilimo, kwa mfano bei ya zao la ufuta imeongezeka kutoka Shilingi 1,500 kwa kilo mwaka 2015/2016 hadi kufikia Shilingi 3,500 kwa kilo mwaka 2019/2020; bei ya kakao kutoka Shilingi 3,200 mwaka 2015/2016 kwa kilo hadi Shilingi 5,000 kwa kilo mwaka 2019/2020; bei ya zao la korosho imeimarika kutoka wastani wa Shilingi 1,820 mwaka 2015/2016 kwa kilo hadi kufikia wastani wa Shilingi 3,000 kwa kilo mwaka 2019/2020; na bei ya singa za mkonge imeongezeka kutoka Shilingi 2,083 kwa kilo mwaka 2015/2016 hadi Shilingi 2,745 kwa kilo mwaka 2018/2019 kwa mauzo ya ndani ya nchi. Aidha, bei ya kahawa iliyokobolewa aina ya Arabika katika soko la ndani imeimarika zaidi kwa kuuzwa kwa Dola za Marekani 112 ikilinganishwa na bei ya Dola za Marekani 107.04 katika soko la Dunia kwa gunia la kilo 50 na bei ya kahawa aina ya Robusta ilimariika kwa kuuzwa kwa Dola za Marekani 87.13 katika soko la ndani ikilinganishwa na Dola za Marekani 73.90 katika soko la Dunia kwa gunia la kilo 50.

*60. Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na TMX imehamasisha mfumo huo kwa viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika na Wakulima 3,200 katika Halmashauri za Wilaya za Bukoba Vijijiini, Manispaa ya Bukoba, Misenyi, Karagwe, Kyerwa, Ngara, Biharamulo na Muleba. Aidha, TMX imeanza maandalizi ya kuuza korosho kuititia mfumo wa OTS-*Online Trading System* katika msimu wa mwaka 2020/2021 ambapo imetoe mafunzo kwa wadau wa

zao la korosho katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani, Ruvuma na Tanga.

61. *Mheshimiwa Spika*, hadi Machi 2020, CPB imeuza jumla ya tani 210,445.524 za korosho ghafi za msimu wa 2018/2019 ambapo tani 148,077.892 ziliuzwa kwa utaratibu wa Malipwani (FOB) na tani 62,367.632 ziliuzwa kwa utaratibu wa Malighalani (ex-warehouse). Thamani ya korosho zilizouzwa kwa utaratibu wa Malipwani ni Dola za Marekani 233,864,795.62 na zilizouzwa kwa utaratibu wa Malighalani ni Shilingi 3,246,739,000.

62. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuwalipa wakulima wa korosho ambapo hadi Februari, 2020 jumla ya Shilingi 702,526,848,192 imelipwa. Aidha, kiasi cha Shilingi 20,421,479,180 bado hazijalipwa kama inavyooneshwa katika (Kiambatisho Na. 9). Serikali inaendelea kuhakiki madai ya wakulima ambao hawajalipwa na zoezi hilo la uhakiki na malipo linatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2020.

63. *Mheshimiwa Spika*, Vilevile Serikali imeendelea kufanya tafiti za masoko kwa mazao ya biashara, chakula na mazao ya bustani kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kama TAHA. Aidha, tafiti hizi zimebaini kwamba Kilimo cha Mkataba ndicho chenye uhakika wa soko la mazao ya mkulima ambapo kwa sasa Wizara kwa kushirikiana na TAHA imejikita kutoa elimu kwa wakulima kuhusu Kilimo cha Mkataba. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Sekta binafsi imeendelea kufanya tafiti za masoko ya mazao mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa kutumia ofisi za Balozi zetu kupata uhakika wa masoko ya mazao ya kilimo.

#### **4.9 Utafiti, Huduma za Ugani na Mafunzo ya Kilimo**

64. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha shughuli za utafiti na ugunduzi wa kilimo, Serikali ilianzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kuititia Sheria ya Bunge Na. 10 ya Mwaka 2016 (*TARI's Act No. 10 of 2016*). Katika kipindi cha miaka minne (4), kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imegundua aina 124 za mbegu bora (Kiambatisho Na.10). Aidha, kati ya hizo Kampuni binafsi zimegundua aina 35 za mbegu bora za

mazao ya kilimo. Vilevile Wizara kupitia TARI imefanya utafiti wa kupima afya ya udongo na kuandaa ramani zinazoonesha mtawanyiko na viwango vya mboji (Organic carbon) pamoja na uchachu (pH) wa udongo katika Mikoa yote nchini. Viwango vya mboji na uchachu wa udongo ni viashiria vya uwepo au kutokuwepo katika udongo virutubisho vya aina ya Naitrojeni, Fosfori, Potasimu, Salfa, Kalsiam na Magnesiam. Virutubisho hivi ni muhimu katika uzalishaji wa mazao ya kilimo.

65. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia TARI imegundua aina 22 za mbegu bora za mazao. Kati ya hizo aina tisa (9) ni za muhogo, mbili (2) za alizeti, mbili (2) za mahindi, mbili (2) za mpunga, moja (1) ya ulezi na sita (6) za viazi vitamu. Mbegu za alizeti zina kiwango kikubwa cha mafuta ikilinganishwa na mbegu zilizopo, mbegu za viazi vitamu zina vilini lishe vya vitamin A. Aidha, mbegu za mpunga zinatoa mavuno kati ya tani 7.3 hadi 7.9 kwa hekta, mchele wake unanukia vizuri na kupikika kiurahisi, wakati mbegu za mahindi zinatoa mavuno kati ya tani saba (7) hadi 10 kwa hekta na zina ukinzani dhidi ya ugonjwa wa *Maize Streak* na *Turcium Blight virus*.

66. *Mheshimiwa Spika*, TARI imetathmini upokeaji wa teknolojia ya zao la viazilishe vinavyoongeza upatikanaji wa viinilishe vya vitamin A mwilini na kubaini kuwa upokeaji huo umeongezeka kutoka asilimia 10 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 36 mwaka 2019. Aidha, TARI imetoa mafunzo kuhusu matumizi ya *Paper tool fertilizer optimizerna fertilizer optimizer App* kwa ajili ya kugundua kiwango cha matumizi ya mbolea kwenye eneo husika kwa Maafisa ugani 97 katika Mkoa wa Mbeya. Vilevile, TARI imeendelea kushirikiana na Taasisi za ndani na nje ya nchi, Vyuo Vikuu na Mashirika mbalimbali ambapo imesaini Makubaliano ya Ushirikiano (MoUs) 23 yenye jumla ya Shilingi 11,987,842,280 kwa ajili ya masuala ya utafiti wa kilimo nchini.

67. *Mheshimiwa Spika*, TARI imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia na ubunifu ambapo ilishirikiana na vyombo vya habari kuandaa na kuonesha matokeo ya utafiti

kupitia vipindi 88 vya Runinga na 39 vya radio. Jumla ya makala 95 zimeandaliwa katika lugha ya Kiingereza na Kiswahili na kuchapishwa kwenye magazeti. Aidha, TORITA imekamilisha utafiti wa awali wa mbegu nne (4) za tumbaku (Yunan 85, Yunan 87, NC 102 na NC 297). Utafiti huo umeonyesha kuwa mbegu za tumbaku ya mvuke za Yunan 85 na Yunan 87 zinafanya vizuri kwenye udongo wa kichanga na kikungu wa kanda tatu za tumbaku (Kahama, Tabora na Chunya).

68. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia TaCRI imezalisha na kusambaza kwa wakulima jumla ya miche 3,692,780 na imegundua aina tatu (3) za mbegu bora za kahawa ya Arabika zinazostahimili ukame ambazo ni N39-3, N39-10 na TaCRI 3F. Pia, TaCRI imezindua Vitabu vya Kanuni za Kilimo Bora cha Kahawa ya Arabika na Robusta na Mtaala wa Mafunzo kwa Maafisa Ugani wa Zao la Kahawa.

69. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha huduma za ugani, Wizara kupitia Vyuo vyake 14 imetoa wataalam wa kilimo 7,530 kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada za kilimo katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2019. Vilevile, katika kipindi hicho Wizara ilihamasisha Sekta binafsi kuwekeza katika mafunzo ya kilimo ambapo wataalam 6,146 wamehitimu katika Vyuo binafsi 12 ngazi ya Astashahada na Stashahada za kilimo (Kiambatisho Na. 11.). Aidha, kupitia mradi wa ERPP na TANRICE 2 pamoja na mashirika ya FAO, HELVETAs na USAID, jumla ya maafisa ugani 902 na wakulima 42,192 wamepatiwa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora, teknolojia mbalimbali za uzalishaji, jinsia na masoko.

70. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeandaa Mkakati wa Miaka Mitano (5) wa kuimarisha Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo (MATIs) na Vituo vya Mafunzo kwa Wakulima (FTC) unaolenga kutatua changamoto zinazokabili vyuo na vituo hivyo zikiwemo uchakavu wa miundombinu, uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, uhaba wa vifaa vya usafiri, uhaba wa watumishi, mitaala kutokuhuishwa kwa muda mrefu na watumishi kutojengewa uwezo kwa muda mrefu. Mkakati huo

unatarajiwa kutumia jumla ya Shilingi 70,773,001,847 kwa ajili ya kutekeleza malengo hayo kwa kipindi cha 2020 – 2025.

71. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza Mkatikati huo, Wizara imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 19 ngazi ya Shahada ya Uzamili na wanne (4) ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Vyuo Vikuu vya hapa nchini. Pia, Wakufunzi wawili (2) wamejunga na mafunzo ya Shahada ya Uzamili nje ya nchi na wakufunzi 15 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi kwa ufadhilli wa JICA na USAID-*Feed the Future India Triangular Training Programme*.

72. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na SAGCOT pamoja na mradi wa STAWISHA imejenga Kituo Mahiri cha kuendeleza zao la viazi mviringo katika kituo cha utafiti cha Uyole Mbeya. Kupitia kituo hicho, wakulima wapatao 2,000 kutoka nyanda za juu kusini wamefundishwa kilimo bora cha viazi mviringo. Aidha, aina sita (6) za mbegu bora za viazi mviringo zimethibitishwa na tani 699 za mbegu za viazi zimezalishwa.

#### **4.10 Uwezo wa Kuhifadhi Mazao**

73. *Mheshimiwa Spika*, Mwaka 2015 nchi ilikuwa na jumla ya maghala 3,400 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,774,106 za mazao ya chakula. Wizara imeendelea kuimarisha uwezo wa kuhifadhi mazao kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya hifadhi ikiwa ni pamoja na vihenge 57 na ghala 118 yenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 203,000 na 100,700 mtawalia na hivyo kuongeza uwezo wa kuhifadhi kutoka tani 2,774,106 mwaka 2015/2016 hadi tani 3,077,806 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 11 (Kiambatisho Na. 12.).



*Upatikanaji na uhakika wa chakula unaenda sambamba na ujenzi wa maghala madogo na makubwa*

74. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuimarisha hifadhi ya tafifa ya chakula kwa lengo la kuimarisha usalama wa chakula nchini. Katika mwaka 2019/2020 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ulihifadhi jumla ya tani 71,177.78 zikiwemo tani 67,335.917 bakaa ya mwaka 2018/2019 na tani 3,841.863 za mahindi zilizonunuliwa mwaka 2019/2020. Hadi kufikia mwishoni mwa Mwezi Aprili, 2020 akiba ya chakula katika maghala ya wakala ni tani 38,698.794 (Kiambatisho Na. 13).

75. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara kuititia NFRA imeuza jumla ya tani 25,679.683 za mahindi ambapo tani 24,000 zenye thamani ya Dola za Marekani 10,080,000 zimeuzwa nchini Zimbabwe na tani 1,679.683 zimeuzwa ndani ya nchi. Kati ya tani 1,679.683 za mahindi yaliyouzwa ndani ya nchi, tani 519.983 zimeuzwa Wilaya ya Longido, tani 30 Wilaya ya Dodoma na tani 1,100 kwa Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro.

#### **4.11 Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko**

76. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, Wizara imefanya maboresho katika Taasisi ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) ambapo mafanikio mbalimbali yamepatikana. Mafanikio hayo ni

pamoja na kurejeshwa kwa mali za Serikali zilizokuwa zinamilikiwa na Shirika la Taifa la Usagishaji (National Milling Corporation – NMC) ambazo ziliikuwa chini ya watu binafsi. Mali zilizorejeshwa ni kinu cha usagishaji cha Arusha kilichokuwa kikiendeshwa na kampuni binafsi ya *Monaban Trading and Farming* pamoja na ghala la Kiteto lenye uwezo wa kuhifadhi tani 3,000. Pia, Bodi hiyo imefufua Kinu cha Iringa chenye uwezo wa kusaga tani 60 za mahindi kwa siku, kujenga kinu kipyä cha kusaga chenye uwezo wa kusaga tani 60 za nafaka kwa siku katika eneo la Kizota mkoani Dodoma pamoja na kusimika kiwanda cha kusindika tani 20 kwa siku za mbegu za alizeti. Hatua hiyo imewezesha Bodi kuongeza uwezo wa kusagisha nafaka kutoka tani 100 hadi 180 kwa siku katika viwanda vyake vilivyopo Iringa, Dodoma na Arusha.

77. *Mheshimiwa Spika*, Taasisi ya CPB imefanikisha zoezi la kununua korosho kwa wakulima tani 222,561.179 na kuuza Tani 211,753.27 za korosho ghafi kwa msimu wa 2018/2019 pamoja na kuuza tani 980 za korosho zilizobanguliwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Aidha, Bodi imenunua na kuuza tani 170,000 za mahindi, mtama, maharage na mchele katika masoko ya ndani ya nchi.

78. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imenunua tani 12,474.23 za mahindi kutoka kwa wakulima sawa na asilimia 89.1 ya lengo. Vilevile, Bodi imesindika tani 5,764.25 za mahindi na kuzalisha tani 4,899.61 za unga na tani 1,207.08 za pumba katika vinu vya Arusha, Dodoma na Iringa. Aidha, CPB imenunua tani 140.6 za alizeti kutoka kwa wakulima. Ili kuongeza uwezo wa kusindika, Bodi imefunga mashine mbili zenye uwezo wa kusindika tani 60 za mahindi kwa siku na tani 20 za alizeti kwa siku katika eneo la Kizota, Dodoma. Pia, bodi imeongeza wigo wa ununuzi wa mazao ambapo, hadi Februari, 2020 imenunua tani 29.273 za maharage.

*Ujenzi wa Ghala na Miundombinu ya kuhifadhi Mazao*  
79. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuimarisha uwezo wa kuhifadhi mazao kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa

chakula na masoko. Kupitia Mradi wa ERPP, Wizara inakamilisha ujenzi wa ghala tano (5) za kuhifadhi mpunga zenye uwezo wa kuhifadhi tani 6,700 katika Mkoa wa Morogoro. Hadi Machi 2020, ujenzi wa ghala hizo umefikia hatua zifuatazo; Msolwa Ujamaa (1,700 MT) asilimia 82, Njage (1,700 MT) asilimia 87, Mvumi (1,300 MT) asilimia 99, Kigugu (1,000 MT) asilimia 80 na Mbogo Komtonga (1,000 MT) asilimia 70.

80. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Wakala wa Taifa wa Kuhifadhi Chakula (NFRA) inakamilisha ujenzi wa ghala na vihenge vya kisasa kupitia Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi mazao. Hadi Aprili 2020, ujenzi umefikia asilimia 60.5 ya utekelezaji, ambapo katika maeneo ya Songea, Makambako, Mbozi, Dodoma na Shinyanga umefikia asilimia 79 na ujenzi katika maeneo ya Mpanda, Sumbawanga na Babati umefikia asilimla 59. Awamu ya kwanza ya mradi huu inatarajiwa kukamilika Agosti, 2020 ambapo Wakala utaongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka kutoka tani 251,000 za sasa hadi kufikia tani 501,000.



*Ujenzi wa vihenge vya kisasa (Silos) kwa ajili ya kuongeza uwezo wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuhifadhi chakula cha kutoka katika Kanda zote Saba umekamilika kwa zaidi ya asilimia 60.*

81. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Nchini (TANIPAC) wenyе lengo la kuimarisha ubora wa mazao ya chakula hususan mahindi na karanga ili kulinda afya ya jamii na kuchochea mauzo ya nje. Hadi Machi 2020, Wizara kupitia Mradi wa TANIPAC imeendelea kusanifu ghala 14 za kuhifadhi mahindi na karanga, ambapo ghala 12 zitajengwa Tanzania Bara na mbili zitajengwa Zanzibar. Aidha, Wizara imeingia mkataba na mshauri elekezi kwa ajili ya usanifu wa Karantini na Maabara ya Udhibiti wa Magonjwa ya Mimea Kibaioloja (*National Biological Control Laboratory*) itakayojengwa Kibaha Mkoa wa Pwani.
82. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na athari za sumukuvu ambayo taarifa za kitafiti zinaonesha kuwa inachangia katika magonjwa yasiyoambukiza hususan saratani ya ini pamoja na udumavu. Wizara kupitai Mradi wa TANIPAC Inashirikiana na Taasisi za TBS, VETA, SIDO, TARI kwa upande wa Tanzania bara, pamoja na Wizara ya Kilimo Zanzibar, ZFDA na ZARI kutoa elimu kwa umma kuhusu athari na udhibiti wa sumukuvu kupitia runinga, redio, magazeti, machapisho mbalimbali na maonesho mbalimbali ya Kitaifa. Hadi Machi 2020, wananchi 1,100 wamepata elimu hiyo kupitia mafunzo na maonesho.
- ### 83.12 Kuimarisha Ushirika
83. *Mheshimiwa Spika*, Ushirika umeendelea kuimarika ambapo Vyama vya Ushirika vimeongezeka kutoka 7,394 mwaka 2015 hadi 11,626 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 57. Vilevile, idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka 2,390,593 mwaka 2015 hadi 5,880,736 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 146. Hata hivyo, Wizara imechukua hatua ya kuvifuta jumla ya Vyama 3,348 vimeshindwa kukidhi masharti ya usajili wake na hivyo kubaki na jumla ya Vyama vya ushirika 8,611 kwenye daftari/rejista ya Vyama vya ushirika nchini.
84. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hicho, thamani ya mikopo inayotolewa na Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 899.2

mwaka 2015 hadi Shilingi triliuni 1.5 Mwezi Machi, 2020. Vilevile, thamani ya hisa, akiba na amana imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 654 Desemba, 2018 na kufikia Shilingi bilioni 819 Machi, 2020 sawa na ongezeko la asilimiaAidha, idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka viwanda 304 mwaka 2015 hadi viwanda 379 mwaka 2019.

85. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha kuwa vyama vya ushirika vinaimarika kiuchumi na kiutendaji, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti kwa kufanya kaguzi za mara kwa mara kwa Vyama vya Ushirika. Katika kipindi cha miezi sita kuanzia Julai hadi Desemba, 2019 Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini (COASCO), limefanya ukaguzi wa nje kwa vyama vya ushirika 3,160 kati ya hivyo vyama 69 vimepata hati inayoridhisha; vyama 1,545 vimepata hati yenye shaka; Vyama 330 vimepata hati isiyoridhisha na Vyama 1,216 vimepata hati mbaya.

#### **4.13   Urejeshaji wa Mali za Ushirika**

86. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Miaka minne, Serikali ya Awamu ya Tano imefanikiwa kurejesha mali zilizokuwa za Vyama Vikuu Vya Ushirika ikiwemo NCU (1984) Ltd cha Mwanza, SHIRECU (1984) Ltd cha Shinyanga, KNCU cha Mkoani Kilimanjaro na shirika lake tanzu la TCCco zilizouzwa kinyume na utaratibu. Jumla ya mali nane za NCU (1984) Limited na mali mbili (2) za SHIRECU (1984) Limited ambazo ni nyumba za makazi, maghala, viwanda na viwanja viliuzwa kinyume cha sheria na taratibu za manunuzi bila kuzingatia thamani halisi ya mali husika.

87. *Mheshimiwa Spika*, mali za NCU zilizorejeshwa katika kipindi hiki cha miaka minne ni kama ifuatavyo; Jengo la Usafirishaji (KAUMA) - Kiwanja Na. 242, Kitalu "T", barabara ya Stesheni, Mwanza; Kiwanda cha Ashok - viwanja Na. 14, 14a, na 16a eneo la viwanda Igogo pamoja na viwanja vyake, Mwanza; kiwanda cha Mkonge - viwanja Na. 41 na 79, eneo la Viwanda Igogo, Jijini Mwanza; Kiwanda cha New Era Oil Mill

- viwanja Na. 83 na 84 eneo la Viwanda Igogo, Mwanza; Ghala la Igogo lilitopo katika kiwanja Na. 104/1 Kitalu A, Mwanza; Nyumba iliyopo Kiwanja Na. 80 Kitalu D Isamilo, Mwanza; Nyumba iliyopo katika Kiwanja Na. 110 Kitalu D, Isamilo, Mwanza; Nyumba iliyopo katika Kiwanja Na. 89 Kitalu D, Isamilo, Mwanza.

*88. Mheshimiwa Spika*, Vilevile Serikali imerudisha mali mbili (2) za SHIRECU ambazo ni; Ghala lilitopo kwenye Kiwanja Na. 30, Kitalu C Kurasini, jijini Dar es salaam; na Nyumba iliyopo kwenye viwanja Na. 49 na 50 Kitalu BB Mchikichini, Ilala, Dar Es Salaam. Pia, mali za Kiwanda cha Kukoboa Kahawa cha Kilimanjaro (TCCco) zikiwemo Nyumba tatu (3) na Lori moja aina ya Fiat nazo zimerejeshwa. Aidha, jumla ya Shilingi. 500,000,000/= mali ya KNCU fedha iliyolipwa na kuzidishwa kwa makusudi kwa mwekezaji ambaye alipaswa kulipwa fidia baada ya shamba hilo kuuzwa, fedha hizo zimerejeshwa KNCU (1984) Ltd na kutumika kulipa madeni ya chama hicho.

#### **4.14 Kilimo cha Umwagiliaji**

*89. Mheshimiwa Spika*, Wizara kuitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 461,326 mwaka 2015/2016 hadi hekta 694,715 mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 33.6 (Kiambatisho Na. 14). Aidha, tija ya uzalishaji katika skimu za umwagiliaji zilizoendelezwa imeongezeka kutoka wastani wa tani 1.8 – 2.0 kwa hekta mwaka 2015/2016 hadi kufikia wastani wa tani 4.0 – 5.0 kwa hekta 2019/2020 kwa zao la mpunga; tani 1.5 kwa hekta mwaka 2015/2016 hadi tani 3.7- 5.0 kwa hekta mwaka 2019/2020 kwa zao la mahindi; tani 13 kwa hekta mwaka 2015/2016 hadi 26 kwa hekta mwaka 2019/2020 kwa hekta kwa zao la vitunguu na tani 5 kwa hekta mwaka 2015/2016 hadi tani 18 kwa hekta mwaka 2019/2020 kwa zao la nyanya.

*90. Mheshimiwa Spika*, mafanikio hayo yamechangiwa na kukamilika kwa miradi 179 iliyogharimu Shilingi 96,188,597,689.55. Kati ya miradi hiyo, miradi 56 inasubiri kuzinduliwa (Kiambatisho Na. 15). Miradi iliyokamilika ni

pamoja na mradi wa uboreshaji miundombinu ya skimu ya umwagiliaji ya Dakawa yenye ukubwa wa hekta 2,000 iliyogharimu Shilingi 21,156,050,278; Skimu 9 katika skimu 16 yenye ukubwa wa hekta 2,547 za Mradi wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo (SSIDP); ukarabati wa miradi 4 ya skimu za umwagiliaji yenye jumla ya ukubwa wa hekta 2,000 iliyogharimu Shilingi 1,166,220,000.



*Tija na uzalishaji kwenye kilimo cha mpunga imeongezeka kutokana na kuongezeka kwa eneo la kilimo cha umwagiliaji*

91. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara kuititia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea na ukarabati na uboreshaji wa miundombinu katika skimu 21 za umwagiliaji. Kati ya skimu hizo, skimu 16 ni kuititia mradi wa kuendeleza Skimu za Wakulima Wadogo (SSIDP) na skimu tano (5) ni kuititia mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Zao la Mpunga (ERPP). Kati ya skimu 16 za SSIDP, skimu tisa (9) zimekamilika ambazo ni Soko (hekta 285) – Moshi DC; Kituani Mwenzae (hekta 180) na Kwemugiriti (Hekta 250) – Lushoto DC; Katela Ntaba (hekta 250), - Busokelo DC; Ngongowele (hekta-250) na Nanganga (hekta 300) – Ruangwa DC; Mwalunili (Hekta 630) – Igunga DC na Ngage (Hekta 402) – Simajiro DC. Aidha, skimu saba za umwagiliaji (7) zimefikia wastani wa asilimia 78. Pia, ukarabati wa skimu 5 za mradi wa ERPP umefikia asilimia 51.



*Miundombinu ya umwagiliaji imeendelea kukarabatiwa.*

#### **4.15 Ushiriki wa Vijana Katika Kilimo**

92. *Mheshimiwa Spika*, Serikali inatekeleza Mkakati wa Taifa wa Vijana kushiriki *katika* Kilimo wa Miaka Mitano (5) (National Strategy for Youth Involvement in Agriculture – NSYIA) uliozinduliwa tarehe 27 Oktoba, 2016 Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuwavutia vijana kushiriki *katika* shughuli za kiuchumi kupitia sekta ya kilimo nchini. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu imetekeliza mkakati huo kupitia mradi wa teknolojia ya kitalu nyumba (Green House) *katika* halmashauri 81 *katika* mikoa 12 kwa kujenga vitalu nyumba 84 na kufikia vijana 8,700 ambapo Shilingi 3,138,000,000 zimetumika.

93. *Mheshimiwa Spika*, *katika* mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuhamasisha Ushiriki wa Vijana *katika* Kilimo ambapo imeratibu Makongamano ya Vijana *katika* Kanda sita (6) ambazo ni Njombe (Njombe, Ruvuma na Iringa); Songwe (Songwe, Mbeya, Rukwa na Katavi); Tabora (Tabora, Kigoma, Dodoma na Singida); Arusha (Arusha, Tanga, Manyara na Kilimanjaro); Mara (Mara, Simiyu na Mwanza) *na* Geita (Geita, Kagera na Shinyanga). Vijana 2,100 walishiriki na kujadili namna bora ya kutumia fursa zilizopo *katika* mnyororo wa thamani wa mazao na kubadilishana uzoefu wa shughuli za kilimo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-Ajira Kazi, OR-TAMISEMI imeandaa Mpango kazi wa Utekelezaji wa Maazimio yaliyofikiwa *katika* makongamano hayo.

94. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la SUGECO chini ya Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), imetoa mafunzo kwa vijana 1,000 kuhusu kilimo biashara, uzalishaji na ujasiriamali katika vituo atamizi vyta mikoa ya Morogoro na Pwani. Kati ya vijana hao, vijana 100 wamekwenda Israel na 87 wamekwenda Marekani kwa ajili ya kuongeza ujuzi zaidi. Baadhi ya vijana hao wameanzisha mashamba ya mazao ya bustani ikiwa ni pamoja na parachichi, vitunguu, nyanya na wengine wameanzisha maduka ya pembejeo.

#### **4.16 Matumizi Bora ya Ardhi**

95. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Halmashauri za Wilaya imepima mashamba ya wakulima wadogo wanaozunguka mashamba makubwa na Hati za hakimiliki za Kimila 2,381 zimetolewa kwa wakulima wanaozunguka mashamba ya Ngalimila, Lukulilo, Skimu ya umwagiliaji ya Msolwa Ujamaa, Mvumi na Mkulazi. Wizara pia, katika kipindi hicho imewezesha upatikanaji wa Hatimiliki katika mashamba makubwa ya uwekezaji ya Lukulilo, Rufiji, Bagamoyo Sugar na Mkulazi ambapo mashamba hayo tayari yameshapata wawekezaji.

96. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia za hifadhi ya udongo na maji mashambani ili kuzuia mmomonyoko wa udongo na kuifanya ardhi ya kilimo kuwa endelevu. Wizara kupitia Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria imetoa mafunzo ya utunzaji wa udongo na maji mashambani kwa takribani 5,724 ambaao katika kipindi hicho wanatumia teknolojia za kuhifadhi udongo na maji mashambani katika eneo la Hekari 2,426. Aidha mavuno ya pamba yameongezeka kutoka kilo 300 kwa ekari moja hadi kufikia kilo 1,200 kwa ekari moja katika maeneo hayo. Vilevile, Wizara imehifadhi takriban hekari 300.8 za lindimaji kati ya hizo Hekari 121.3 ziko kando ya ziwa na Hekari 179.5 ziko Duma. Pia, Wizara imetoa mafunzo ya teknolojia za hifadhi ya udongo na maji mashambani kwa wakulima 200 kutoka katika vijiji vya Choma, Tangeni, Kolelo na Lubasazi vilivyoko katika milima ya Ulugulu mkoani

Morogoro na wakulima 50 kutoka katika vijiji vya kata ya Amani mkoani Tanga.

97. *Mheshimiwa Spika*, katika jitihada za kuongeza uzalishaji wa mbegu za mafuta ili kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje, Wizara katika kipindi cha miaka mine (4) imeshirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakiki jumla ya mashamba 42 yaliyobatilishwa umiliki na Serikali katika mikoa ya Morogoro (17), Tanga (13) na Arusha na kubaini kuwa, mashamba 21 katи ya 42 yanafaa kwa kilimo cha zao la alizeti na hatua za umilikishaji zinaendelea.

98. *Mheshimiwa Spika*, Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Halmashauri za Wilaya imepima mashamba ya wakulima wadogo wanaozunguka mashamba makubwa na kuwapatia wamilliki Hati za Hakimilliki za Kimila 2,381. Hati hizo zimetolewa kwa wakulima wanaozunguka mashamba ya Ngamilila, Lukulilo, Skimu ya umwagiliaji ya Msolwa Ujamaa, Mvumi na Mkulazi.

#### **4.17 Mkakati wa Kudhibiti Upotevu wa Mazao**

99. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeandaa Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Upotevu wa Mazao ya Chakula Nchini wenye lengo la kupunguza upotevu wa mazao hayo kwa asilimia 50 ifikapo 2027/2028. Uanzishwaji wa Mkakati huu ni utekelezaji wa makubaliano na maazimio ya Kikanda na Kimataifa yanayolenga kuimarisha usalama wa chakula na lishe nchini. Mkakati huo wa Miaka 10 ulianza rasmi mwaka 2017/2018 na ulizinduliwa rasmi tarehe 1 Agosti, 2019 na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Nakala 2,542 za mkakati huo zimesambazwa kwa wadau na maafisa ugani katika mikoa kumi (10) ya Mwanza, Dar es Salaam, Simiyu, Geita, Shinyanga, Mara, Singida, Dodoma, Morogoro na Manyara.

#### **4.18 Kuhuisha Mifumo na Sera**

4.18.1 *Mfumo wa Vibali kwa Njia ya Kielektroniki (ATMIS)*

100. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeanzisha mfumo wa vibali kwa njia ya kielektroniki (ATMIS) unaolenga kutoa huduma

za utoaji vyeti vya usafi wa mazao ya mimea na vibali vya kuingiza na kuuza mazao nje ya nchi. Mfumo huo umepunguza muda wa kupata kibali kutoka siku saba (7) za awali hadi siku moja (1) kwa wafanyabiashara. Vilevile, umechangia kudhibiti mianya ya udanganyifu wa nyaraka na kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kutoka Shilingi 2,345,082,308.46 Julai, 2018 hadi Shilingi 2,619,905,800.28 Machi, 2020 sawa na ongezeko la asilimia 13.

#### *4.18.2 Uanzishwaji wa Kanzidata ya Wakulima*

*101. Mheshimiwa Spika*, Wizara imeanzisha Mfumo wa Usajili wa Wakulima (*Farmers Registration System-FRS*) na kutengeneza kanzidata ya wakulima ambayo itasaidia kuwatambua na kuwapatia vitambulisho, kuainisha mahitaji yao ikiwemo pembejeo za kilimo, huduma za kifedha na masoko na hatimae kuweka mipango ya kuwashudumla. Hadi Aprili, 2020 jumla ya wakulima 1,275,220 katika mazao nane makuu ya kibiaresha ambayo ni korosho, pamba, kahawa, chai, mkonge, pareto, tumbaku na sukari wamesajiliwa kuititia mfumo huo sawa na asilimia 88.1 ya wakulima wote wa mazao hayo nchini (Kiambatisho Na: 16).

#### *4.18.3 Bima ya mazao*

*102. Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa huduma za Bima ikiwemo Mamlaka ya Kudhibiti Shughuli za Bima nchini (TIRA), Shirika la Bima la Taifa (NIC), kampuni binafsi tano (5) za bima zimeanzisha Bima ya Mazao kwa lengo la kumsadia mkulima kujikinga na athari za majanga ya asili na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kupata dhamana ya mkopo. Hadi sasa, wakulima 1,279,884 wa mazao ya biashara wamesajiliwa na kutengeneza kanzidata kwa lengo la kuwatambua na kusaidia katika utoaji wa huduma za kilimo ikiwemo huduma ya bima ya mazao.

*103. Mheshimiwa Spika*, Hadi sasa jumla ya Kampuni sita (6) za Bima zinashiriki zoezi za utoaji huduma za Bima ya mazao. Kampuni hizo ni pamoja na Jubilee Insurance inayohudumia vikundi vya wakulima 55 wa zao la mahindi katika mikoa ya

Nyanda za Juu Kusini; AUP inayohudumia wakulima 44,000 wa mazao ya mahindi, maharage, mazao ya bustani na alizeti katika mikoa ya Dar es salaam, Dodoma, Morogoro, Shinyanga, Mwanza, Arusha, Zanzibar, Mbeya, na Mtware; MGEN Insurance inayohudumia wakulima 4,000 wa mpunga, mahindi na alizeti katika mikoa ya Dodoma, Singida, Njombe, Morogoro na Iringa. Kampuni nyingine ni pamoja na NIC, Reliance na Acre Africa. Hadi Desemba 2019 thamani ya kinga ya bima ya mazao yaliyoainishwa ni Shilingi 1,483,382,400.



*Waziri wa Kilimo Mhe. Japhet Hasunga (katikati) Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Anthony Mtaka (Kulia) pamoja na Mtendaji Mkuu wa Shirika la Taifa la Bima Dkt. Elirehemu Doriye wakiwa na Viongozi wengine wa Serikali na Chama cha Mapinduzi mkoa wa Simiyu tarehe 7 Agosti 2019 mara baada ya Waziri Hasunga kuzindua rasmi Bima ya Mazao kwa Wakulima wa pamba.*

#### *4.18.4 Usajili wa Wadau*

*104. Mheshimiwa Spika, pia Wizara imeendelea na juhudzi za kutambua mchango wa sekta binafsi katika Sekta ya Kilimo ambapo imekamilisha mfumo wa kuwasajili wadau wote wa sekta ya kilimo ikiwemo Sekta Binafsi (Stakeholders mapping).*

Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, jumla ya wadau wa sekta binafsi 564 wamesajiliwa ambapo Wazalishaji na wasambazaji wa pembejeo ni 198, Wazalishaji wa bidhaa za kilimo 103 na wasindikaji 363. Aidha, jumla ya miradi 105 inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo yenye thamani ya Shilingi Trilion 3.3 imesajiliwa kwenye mfumo. Mfumo huo utaiwezesha Serikali kutambua juhudhi na uwekezaji wa wadau wote na kuimarisha ushirikiano kati yao na Serikali katika kuendeleza sekta ya kilimo kuititia program ya ASDP II.

#### *4.18.5 Mfumo wa M-Kilimo*

105. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inakamilisha mfumo wa M-Kilimo ambao utasaidia kuwaelemisha wakulima kuhusu kilimo bora cha mazao na kuwaunganisha wakulima na wanunuzi wa mazao. Vilevile, mfumo huo utawawezesha wakulima na wataalam wa kilimo kuwasiliana kwa kutuma ujumbe kwa njia ya simu za viganjani. Majoribio ya mfumo huo yatafanyika katika wilaya za Bahi, Kongwa na Chamwino Mwezi Mei, 2020.

#### *4.18.6 Mfumo wa Taarifa za Kilimo (Dashboard)*

106. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inakamilisha mfumo wa taarifa za kilimo (*Dashboard*). Lengo la mfumo huo ni kuwezesha kupatikana kwa taarifa fupi zilizochambuliwa kwa njia ya kielektroniki zinazopima mafanikio ya viashiria vyya malengo mbalimbali yaliyowekwa na Wizara. Mfumo huo utaiwezesha Wizara kuchukua hatua za haraka na madhubuti kwa ajili ya kupata ufumbuzi pale inapobainika malengo yaliyotarajiwa hayajafikiwa.

### **4.19 Kutoa Huduma za Ushauri Kuhusu Utafiti, Mafunzo na Usambazaji Taarifa za Kilimo na Sayansi Shirikishi**

#### *4.19.1 Ushauri kuhusu utafiti*

107. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kuititia TARIimeendelea kutoa ushauri kuhusu matokeo ya utafiti na matumizi ya teknolojia mbalimbali za uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo.

Kupitia Siku ya Chakula Duniani, TARI ilitoa ushauri na kuwahimiza wadau wa kilimo kuhusu matumizi ya teknolojia zilizofanyiwa utafiti na zenye matokeo makubwa kama vile usindikaji na uchanganyaji wa mazao lishe ili kupata bidhaa zenye ubora wa lishe kama unga lishe.

*108. Mheshimiwa Spika*, vilevile TARI kwa kushirikiana na Baraza la Nafaka la Ukanda wa Afrika Mashariki (*Eastern Africa Grain Council* – EAGC) iliratibu maonesho ya kilimo bishara kupitia TARI llonga na Uyole ambapo jumla ya wadau 1,256 na 2,410 mtawalia walishiriki. Pia, TARI Kibaha iliadhimisha siku ya wadau wa zao la miwa kwa lengo la kuonesha teknolojia za uzalishaji na usindikaji wa bidhaa za miwa. Wadau 700 kutoka Kilombero na 250 kutoka Kibaha walishiriki maonesho hayo. Vilevile, TARI Makutupora iliadhimisha siku za wakulima tatu (3) kwa wakulima na wadau 200 katika mnyororo wa thamani wa mazao ya zabibu, ulezi, muhogo, korosho, mtama, uwele, kunde, mbaazi, alizeti, viazi vitamu na ufuta.

#### 4.19.2 Usambazaji Taarifa za Kilimo na Sayansi Shirikishi

*109. Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuweka msukumo katika kusambaza teknolojia mbalimbali kwa wakulima kupitia maonesho ya kilimo, mashamba darasa na vyombo vya habari. Katika mwaka 2019/2020, Wizara imesambaza teknolojia za kilimo kupitia maonesho ya kilimo Nanenane yaliyofanyika kitaifa mkoani Simiyu katika Uwanja wa Nyakabindi pamoja na Kanda saba (7) za maonesho.

*110. Mheshimiwa Spika*, katika maonesho hayo elimu kuhusu upatikanaji wa mtaji kwa ajili ya kuwekeza kwenye kilimo, kanuni bora za uzalishaji wa mazao, matumizi sahihi ya pembejeo, zana bora za kilimo, kuongeza thamani mazao ya kilimo na upatikanaji wa masoko ilitolewa kwa wadau wa kilimo 1,283. Washiriki wa maonesho hayo walitoka sekta ya umma, sekta binafsi, taasisi za Serikali, taasisi zisizokuwa za kiserikali, Wabia wa Maendeleo, taasisi za fedha na vikundi vya wakulima. Aidha, kupitia maonesho hayo, wakulima 1,950 walipatiwa elimu ya matumizi bora ya ardhi ikiwemo hifadhi

ya udongo na maji mashambani kupitia vipeperushi, modeli na mafunzo darasani.

*111. Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Mkoa wa Singida pamoja na FAO imeadhimisha Siku ya Chakula Duniani iliyofanyika kitaifa Mkoani Singida. Katika maadhimisho hayo teknolojia za uzalishaji wa mazao ya chakula kwenye maeneo yenye ukame na hifadhi bora ya mazao baada ya kuvuna zilioneshwa. Vilevile, jumla ya washiriki 593 (me 403 na ke 190) walifanyiwa tathmini ya hali ya lishe kwa kutumia Uwiano wa Uzito na Urefu (BMI) ambapo watu 305 (51.4%) kati yao walibainika kuwa na uzito uliopitiliza na hivyo kupatiwa ushauri wa lishe bora.

*112. Mheshimiwa Spika*, matumizi ya mazao ya vyakula vya asili yalihamasishwa ambapo milo kamili iliyotokana na vyakula vyenye asili ya makabila ya mikoa ya Singida, Mbeya na Mwanza viliandaliwa na kuonjwa. Lengo la onesho hilo ni kuhamasisha matumizi ya vyakula vya asili ili kuongeza wigo wa matumizi ya chakula na kupunguza changamoto za upungufu wa chakula katika kaya.

**4.20** Mapitio ya Sera za Sekta Ndogo ya Mazao na Sheria zake ili Kuweka Mazingira Mazuri ya Uwekezaji katika Kilimo

*113. Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kupitia Sera na Sheria mbalimbali kwa lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji katika Kilimo ambapo, katika mwaka 2019/2020, Wizara imeandaa mapendekezo ya kurekebisha na kutunga sheria mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa mifumo ya kitaasisi na Bodi za Mazao. Sheria hizo ni pamoja na marekebisho ya Sheria ya Ushirika ya Mwaka 2013 ambayo mapendekezo yake yapo katika ngazi ya kupata ridhaa ya Serikali na mapendekezo ya kutunga Sheria ya Afya ya Mimea (*The Plant Health Act, 2020*) ambayo imependekeza kuanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Mimea (*Tanzania Plant Health Authority -TAPHA*). Muswada wa Sheria ya Afya ya Mimea umesomwa kwa mara ya kwanza katika mukutano wa 18 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau inapitia Sera ya Taifa ya

Kilimo ya Mwaka 2013 na kuandaa Mkakati wake wa utekelezaji kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika sekta ya kilimo.

#### **4.21 Kuimarisha Uratibu na Ufuatiliaji na Tathmini ya Sekta ya Mazao**

114. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuimarisha mifumo ya Uratibu, upatikanaji wa Takwimu za kilimo, Ufuatiliaji na Tathmini ya Sekta ya Mazao kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Viwanda na Biashara, TAMISEMI, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Zanzibar. Wizara pia imeendelea kushiriki katika maandalizi ya Sensa ya kilimo (*National Sample Census of Agriculture – NSCA 2018/2019*) iliyotarajiwa kufanyika mwezi Aprili, 2020 chini ya usimamizi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS). Hatua ya uorodheshaji wa kaya za sekta ya kilimo imekamilika na hatua inayofuata ni kuendesha mafunzo kwa wakufunzi watakaowafundisha wakusanyaji wa takwimu kabla ya kuanza kukusanya takwimu hizo. Hata hivyo, mafunzo hayo hayakukamilika kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID 19.

115. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imekusanya takwimu za uzalishaji wa mazao ya kilimo kutoka Bodi za mazao na Halmashauri za Wilaya kwa kutumia mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za kilimo (*Agriculture Routine Data System-ARDS*). Ili kurahisisha ukusanyaji wa takwimu hizo kutoka ngazi za kijiji, Wizara imeendesha mafunzo kuhusu matumizi ya mfumo wa ARDS kwa Maafisa Kilimo, Maafisa Umwagiliaji, Maafisa Ushirika wa Wilaya (DAICOs) na wasimamizi wa mfumo wa takwimu za kilimo katika Halmashauri 185. Aidha, Wizara inakamilisha maandalizi ya kitabu cha takwimu za msingi za kilimo (*Basic Data Booklet 2018/2019 for Agriculture*).

#### **4.22 Kuimarisha Huduma za Upimaji wa Matabaka na Ubora wa Ardhi Kuendana na Mahitaji ya Mazao ya Kilimo Ki-ikolojia**

116. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha huduma za upimaji wa matabaka na ubora wa ardhi, katika mwaka 2019/2020, Wizara imeandaa rasimu ya Mpango Kabambe wa Taifa wa

Matumizi Bora ya Ardhi ya Kilimo wa miaka 15 (2020/2021 – 2035/2036) ili kusimamia matumizi bora ya ardhi ya kilimo, kupunguza mgogoro ya ardhi na kuongeza uzalishaji na tija katika mazao ya kilimo. Vilevile, Wizara imehakiki mashamba 43 ya uwekezaji yenyewe ukubwa wa hekta 124,924.13 katika Mkoa wa Tanga na kubaini kuwa hekta 27,007 hazijaendelezwa kwa ajili ya kilimo kama ilivyokusudiwa. Taratibu za kuwapata wawekezaji wengine wenyewe nia na uwezo wa kuendeleza maeneo hayo unafanyika.

117. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia TARI kwa kushirikiana na Kampuni ya Yara na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imeendelea kudhibiti tindikali kwenye udongo ulioathirika kwa kutumia teknolojia ya chokaa. Teknolojia hiyo, imetumika katika vijiji 36 vya Wilaya ya Mbozi-Songwe kwenye mashamba ya mahindi. Matumizi ya teknolojia hiyo yamepunguza kiwango cha tindikali kutoka 4.2 kufikia kiwango cha 5.4 hadi 6.4 na hivyo kuongeza tija katika zao la mahindi kutoka wastani wa magunia nane (8) hadi magunia 18 kwa ekari.

118. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia TARI na kwa kushirikiana na Kampuni ya mbolea ya OCP imepima udongo na kutoa mapendekezo ya viwango vya matumizi bora ya mbolea ili kuongeza uzalishaji wa viazi mviringo katika wilaya za Makete, Rungwe, Mbeya, Mbozi, Wanging'ombe, Halmashauri ya Mji Njombe, Halmashauri ya wilaya ya Njombe, Mufindi, Kilolo na Busokelo. Vilevile, uhakiki wa eneo la TARI Uyole lenye mgogoro na wananchi wa Sae na Ituha umefanyika na taarifa yenyewe mapendekezo ya ufumbuzi wa mgogoro huo imewasilishwa Serikalini. Wizara pia, imepima maeneo ya vituo vidogo vya Mbimba na Milundikwa na kutoa ekari 50 (Mbimba) na ekari 1,000 (Mlindukwa) kwa ajili ya kupewa wananchi kwa matumizi ya kijamii.

#### **4.23 Kuratibu utekelezaji wa Mikakati ya Maendeleo ya Mazao**

119. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuratibu na kutekeleza mkakati wa maendeleo ya mazao kwa kuimarisha

utafiti, upatikanaji na matumizi ya pembejeo, udhibiti wa visumbufu vya mazao, huduma za ugani, uongezaji wa thamani na upatikanaji wa masoko.

### Zao la Korosho

120. *Mheshimiwa Spika*, Zao la korosho ni moja ya mazao ya kimkakati yanayoliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni na kipato kwa wakulima. Aidha, maeneo ya uzalishaji korosho hapa nchini yameongezeka na hivyo kuongezeka kwa mahitaji ya mbegu bora. Wizara kupitia TARI Naliendele kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya zinazolima zao la korosho pamoja na wazalishaji binafsi imezalisha tani 111.2 na imesambaza tani 81.97 za mbegu bora za korosho. Katika mbegu zilizosambazwa tani 50 zilipelekwa nchini Zambia. Hadi Machi, 2020 mbegu hizo zimesambazwa katika mikoa 20 (Kiambatisho Na. 17). Aidha, TARI Naliendele imezalisha miche bora ya korosho 51,438 na kusambaza miche 38,338 ya kutosheleza ekari 1,420 kwa wakulima. Miche hiyo imesambazwa katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Singida, Ruvuma, Dodoma, Tanga, Morogoro na Pwani. Miche huuzwa kwa wakulima kwa wastani wa bei ya Shilingi 500 kwa mche mmoja wa kawaida na Shilingi 1,000 kwa mche mmoja uliobebeshwa.

121. *Mheshimiwa Spika*, katika msimu wa 2019/2020 mahitaji ya viuatilifu vya zao la korosho nchini yalikadiriwa kufikia tani 30,000 za salfa ya unga (Sulphur 99.5% dust) na lita 350,000 za viuatilifu vya maji (*water based pesticides*). Hadi Machi 2020, Bodi ya Korosho imesambaza tani 19,631 za Salfa ya Unga na lita 280,201 za viuatilifu vya maji kwa wakulima kupitia vituo vya mauzo vilivyopo katika Wilaya mbalimbali zinazozalisha korosho nchini kwa lengo la kudhibiti visumbufu vya zao la korosho. Vilevile, bodi imetoa elimu ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu vya zao la korosho kwa wakulima 364 na Maafisa ugani 352 kutoka mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma. Bodii pia, imetoa pikipiki 4 kwa maafisa ugani katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima wa korosho. Aidha, bodi imetoa mafunzo ya kudhibiti ubora wa korosho ghafi

kwa wataalam 62 wa udhibiti ubora katika maghala ya mnada na watendaji wa AMCOS 1,102.

122. *Mheshimiwa Spika*, uzalishaji wa korosho ghafi kwa msimu wa 2019/2020 ni tani 232,527.55 ikilinganishwa na tani 224,552 za msimu wa 2018/2019. Aidha, Bodi ya Korosho imeendelea kusajili wakulima wa korosho kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa za Wakulima (*Cashew Farmers Information System*) ambapo hadi Machi, 2020 wakulima 309,006 wamesajiliwa sawa na asilimia 97.05 ya lengo la kusajili wakulima 318,407.

#### Zao la Pareto

123. *Mheshimiwa Spika*, katika msimu wa 2019/2020, Kituo cha Utafiti wa Kilimo TARI – Uyole kimezalisha mbegu bora za pareto kilo 5,300 sawa na asilimia 85.5 ya mahitaji ya mbegu ya kilo 6,200 kwa mwaka. Katika msimu wa mwaka 2018/2019 uzalishaji wa pareto ulikuwa tani 2,014. Aidha, hadi Machi, 2020, uzalishaji wa pareto umefikia tani 1,627 sawa na asilimia 62.57 ya lengo la kuzalisha tani 2,600 na uzalishaji unaendelea. Bodi pia ilipanga kuongeza ubora wa maua hadi asilimia 1.5 ambapo hadi Machi 2020 ubora umefikia asilimia 1.3.

#### Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari

124. *Mheshimiwa Spika*, hadi Aprili, 2020 uzalishaji wa Sukari ulifikia tani 298,948.61 sawa na asilimia 86 ya lengo la kuzalisha tani 345,296 za Sukari. Hata hivyo uzalishaji wa sukari ulikumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uchakavu wa mitambo ya viwanda, kusimama kwa uzalishaji kwa mwezi mmoja katika kiwanda cha Mtibwa kutoptana na kuharibika kwa mitambo, mlipuko wa ugonjwa wa vidung’ata wa njano na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha. Ili kukabiliana na upungufu huo, tani 40,000 za sukari zimeingizwa nchini ili kufidia pengo la uzalishaji wa ndani katika msimu wa 2019/2020.

125. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na jitihada za Serikali za kuingiza sukari ya kuziba pengo, kumekuwepo na changamoto ya kupanda kwa bei ya sukari kusikokuwa kwa

kawaida. Kutokana na hali hiyo, Wizara kupitia Bodi ya Sukari baada ya kufanya uchambuzi wa kina, na kwa kutumia Sheria ya Tasnia ya Sukari Sehemu ya nne (4)(e) Kifungu cha 11A ilichukua hatua ya kutangaza bei elekezi ya jumla na rejareja ya sukari katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kwa lengo la kukabiliana na wafanyabiashara wasio waaminifu.

126. *Mheshimiwa Spika*, Bodi ya Sukari imetoa mafunzo ya kilimo bora cha miwa kwa maafisa ugani 17 kutoka Mbigiri (Mkulazi) na Dabalo (Chamwino) ambao watatumia maarifa na ujuzi waliyopata kuwafundisha wakulima wadogo katika maeneo yao. Aidha, Bodi imekubaliana na TEMDO kutengeneza “hot water treatment plant” itakayowezesha wakulima wadogo kupata mbegu bora. Pia Bodi imeendelea kusajili wakulima wa miwa ambapo hadi Machi 2020, wakulima 6,745 wamesajiliwa sawa na asilimia 92.92 ya lengo na vitambulisho 5,488 vimetolewa kwa wakulima.

127. *Mheshimiwa Spika*, Bodi ya Sukari inaendelea kuratibu uongezaji wa maeneo ya kilimo cha miwa katika maeneo ya uzalishaji wa miwa kwa ajili ya kutengeneza sukari. Maeneo hayo ni yanayomilikiwa na Bagamoyo Sugar Co. Ltd (hekta 2,280), Kagera Sugar Co. Ltd (hekta 2,300), TPC (hekta na Mkulazi II (hekta 1,500) ambapo jumla ya hekta 6,480 zitapandwa.

#### Zao la Kahawa

128. *Mheshimiwa Spika*, katika msimu wa 2019/2020, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (TaCRI) katika Vituo vya Lyamungo, Mbinga, Mwayaya, Maruku, Ugano na Tarime kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika imezalisha miche bora ya kahawa 7,059,835 na kusambazwa kwa wakulima kulingana na mahitaji (Kiambatisho Na. 18).

129. *Mheshimiwa Spika*, hadi Machi, 2020 uzalishaji wa kahawa ulifikia tani 55,979. Kati ya kiasi hicho, tani 22,320 ni kahawa aina ya Robusta, tani 32,057 ni Arabika laini na tani 1,602 ni Arabika ngumu. Pia, Bodi ya Kahawa iliratibu uuzwaji wa kahawa tani 21,929 zenye thamani ya Dola za Marekani

47,666,919 katika minada 17 ya Kanda, na tani 25,574 zenye thamani ya Dola za Marekani 39,860,860 kuititia soko la moja kwa moja.

130. *Mheshimiwa Spika*, Bodi imeendelea kuhamasisha unywaji wa kahawa ambapo umeongezeka kutoka asilimia 8.21 hadi asilimia 8.43. Aidha, Bodi imeitangaza kahawa inayozalishwa nchini kuititia maonesho ya Kimataifa ya SCAJ 2019 yaliyofanyika Tokyo Japani ambapo wanunuzi wawili (2) walijitokeza kununua kahawa ya Tanzania. Vilevile, Bodi ilivijengea uwezo wa kufanya biashara vyama vyaa ushirika 120 ambapo vyama vyaa ushirika vyaa KCU na KDCU viliuza asilimia 61 ya kahawa iliyouzwa katika soko.

131. *Mheshimiwa Spika*, ili kuongeza ubora wa kahawa, Bodi imehamasisha matumizi ya mashine za kukoboa kahawa (Central Pulpuly Units – CPU) katika kuchakata kahawa aina ya Arabika na uboreshwaji wa maabara za kahawa kwa kununua vifaa vyaa kisasa. Pia, mafunzo kwa wanafunzi 50 wa cheti cha ubora wa kahawa na biashara yametolewa katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU). Aidha, Bodi imesajili wakulima 305,260 wakiwemo wakulima wadogo 305,159 na Wakulima wakubwa 101. Usajili huo ni sawa na asilimia 67.82 kwa wakulima wadogo na asilimia 100 kwa wakubwa.



*Uzalishaji wa miche bora ya kahawa kutoka Kituo cha Utafiti wa Kahawa (TACRI) nao umeongezeka. Lengo ni kuongeza tija na uzalishaji ili kuifanya Tanzania kuwa kinara wa zao hilo katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kat*

## Zao la Mkonge

132. *Mheshimiwa Spika*, hadi Machi 2020, uzalishaji wa mkonge ulifikia tani 35,551.86 na uzalishaji wa bidhaa za mkonge ulifikia tani 5,701. Aidha, mauzo ya mkonge ndani ya nchi ni tani 12,673.96 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 37 na mauzo nje ya nchi ni tani 21,043.95 yenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 34.75. Pia, bidhaa za mkonge zilizouzwa ndani ya nchi ni tani 2,214.77 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 8.78 na bidhaa zilizouzwa nje ya nchi ni tani 3,146 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 6.56.

133. *Mheshimiwa Spika*, Bodi imeendelea kuongeza maeneo ya uzalishaji wa *mkonge* ambapo kufikia Machi 2019, hekta 5,529.50 zimepandwa mkonge mpya. Aidha, Bodi imesajili jumla ya wakulima wadogo wa mkonge 2,365 na wakulima wakubwa 22 sawa na asilimia 30.9 kwa wakulima wadogo na asilimia 100 kwa wakubwa. Vilevile, sekta ya mkonge imetoe ajira 129,022 kupitia mashamba na viwanda vyaa mkonge.



*Eneo la kilimo cha mkonge limeongezeka*

Zao la Pamba

134. *Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Bodi ya Pamba imeendelea kusimamia upatikanaji wa mbegu bora za pamba nchini.* Hadi Machi 2020, upatikanaji wa mbegu bora za pamba UKM 08 umefikia tani 35,000 kwa mbegu zenye manyoya. Aidha, katika mwaka 2019/2020, Bodi ilipanga kusambaza tani 20,000 za mbegu ya pamba kwa wakulima ambapo hadi Machi, 2020 usambazaji wa mbegu hizo umefikia tani 17,942 sawa na asilimia 90 ya lengo. Vilevile, Bodi ilisambaza viuadudu lita 6,070,000 sawa na asilimia 86.7 ya lengo la kusambaza lita 7,000,000. Pia vinyunyizi 23,000,000 vilisambazwa kwa wakulima sawa asilimia 115 ya lengo la kusambaza vinyunyizi 20,000,000.

135. *Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa pamba ulifikia tani 352,405.29 katika msimu wa 2018/2019 sawa na asilimia 78 ya lengo la kuzalisha tani 450,000.* Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba na AMCOS imeendelea kuratibu na kusimamia ununuzi wa pamba ambapo hadi Machi 2020 tani 352,405.29 zenye thamani ya Shilingi 422,900,000,000 zimekusanywa. Kati ya hizo, tani 348,726.62 zenye thamani ya Shilingi 418,700,000,000 zimenunuliwa kwa bei ya Shilingi 1,200 kwa kilo na kupelekwa viwandani. Aidha, hadi Machi 2020, Bodi imesajili wakulima 556,306 sawa na asilimia 98.81 ya lengo.



*Mhe. Hussein Bashe Naibu Waziri Kilimo alipotembelea maabara ya pamba katika majengo ya Bodi ya Pamba mkoani Shinyanga tarehe 30 Novembra, 2019. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba Bwana Marco Mtunga.*

136. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, Bodi imetoa leseni za ununuzi wa pamba kwa Kampuni 25 kwa ajili ya kununua pamba katika msimu wa mwaka 2019/2020. Katil ya kampuni zilizopewa leseni, kampuni 21 ndizo zillizonunua pamba katika maeneo mbalimbali. Kampuni hizo ni *Alliance Ginneries, Afrisian Ginning, Birchand Oil Mill Ltd, Biosustain (T) Ltd, Fresho Investment, Gaki Investment, Lugeye Investment, KCCL, Kahama Oil Mill, ICK Cotton Oil, Matongo Farming, MetL, Mwatex (2001) Ltd, NGS Investment, NIDA Textile, Nsagali Co. Ltd, Olam (T) Ltd, S&C Ginning Co. Ltd, BioRe, SM Holdings na Vitreco*. Aidha, usafi na ubora wa pamba umeimarika na daraja la Ganny ya juu imeongezeka kutoka asilimia 43 hadi asilimia 45.



*Usafi na ubora wa pamba umeimarika. Daraja la juu la Pamba kutoka asilimia 43 hadi asilimia 45.*

137. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha soko la pamba, Wizara imekipatia Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kazi ya kuandaa taarifa ya kina ya uwekezaji katika viwanda vyta pamba. Taarifa hiyo itatoa dira ya namna ya kuanzisha viwanda vikiwemo vyta kuchambua pamba na inatarajiwa kukamilika kabla ya Julai, 2020.

#### Zao la Tumbaku

138. *Mheshimiwa Spika*, hadi Machi, 2020 upatikanaji wa mbegu bora za tumbaku ulifikia kilo 400 sawa na asilimia 149.2 ya mahitaji ya kilo 268. Aidha, upatikanaji wa mbolea ulifikia tani 6,026 za mbolea aina ya NPK 10:18:24 na tani 1,326 za mbolea aina ya CAN ambazo zilisambazwa kwa wakulima kupitia Vyama vya Msingi. Vilevile, upatikanaji wa viuadudu ulifikia chupa 105,737 za Bamidas (30g) na chupa 189,849 za Bamethrine (Kiambatisho Na. 19).

139. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 tani 70,824.21 za tumbaku zenyet thamani ya Shilingi 231,694,899,410 zimezalishwa na kununuliwa. Wizara kuititia Bodi ya Tumbaku imewezesha kupatikana kwa wanunuza wapya wanenye (4) ambao ni *Grand Tobacco Ltd*, *Magefa Growers Ltd*, *Petrobena East Africa Ltd* na *Pachtech Co. Ltd*. Ili kuongeza upatikanaji wa mbegu bora Pia, aina mpya nne (4) za mbegu ya tumbaku zinafanyiwa majoribio na TORITA. Pia, maandalizi ya ujenzi wa kiwanda kipyaa cha kuchakata tumbaku yanaendelea katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo (Tabora) ambapo kitajengwa kwa ushirikiano wa wakulima na Halmashauri ya Wilaya ya Urambo. Vilevile, wakulima wa tumbaku 53,758 wamesajiliwa ambao ni sawa na asilimia 116.87 ya lengo la kusajili wakulima 46,000. Bodi pia imefanya ukaguzi na usajili wa vituo 1,578 vya kuchambua na kufungia tumbaku na vituo 632 vya kuuzia tumbaku. Aidha, ubora wa tumbaku umeongezeka kutoka asilimila 87 mwaka 2018/2019 hadi asilimia 93 mwaka 2019/2020.

140. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha kuwa mkulima wa tumbaku anapata bei nzuri, Wizara imefanya mazungumzo na wanunuza tumbaku waliopo nchini na pia kutafuta wanunuza wapya. Kutokana na jitihada hizo wanunuza tumbaku wameongezeka kutoka wanunuza wanenye (4) mwaka 2015 na kufikia wanunuza wanane (8) Machi, 2020. Makampuni hayo ni Tanzania Leaf Company Limited (TLTC), Alliance one Tobacco Tanzania Limited (AOTL), Premium Active Tanzania Limited (PATL), Japanees Tobacco International Leaf Services (JTILS), Magefa Growers Ltd, Grand Tobacco Ltd, Petrobena na Jespan.

Zao la Chai

141. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Wizara kuititia Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA) kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Njombe na Rungwe kuititia vikundi vya wakulima, wakulima binafsi na Vyama vya Ushirika imezalisha miche bora ya chai 3,998,000 na kusambaza kwa wakulima. Vilevile, miche 9,910,000 inaendelea kutunzwa katika vitalu ambapo miche 810,000

inatunzwa na Wakala katika Wilaya za Tarime na Mufindi na miche 9,100,000 inatunzwa na sekta binafsi (kampuni ya NOSC, WATCO na MOG). Miche hiyo itapandwa katika Wilaya za Mufindi, Tarime, Njombe na Rungwe.

142. *Mheshimiwa Spika*, zao la chai huvunwa kwa kipindi cha mwaka mzima ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2020 uzalishaji wa chai kavu umefikia tani 11,185 kati ya hizo, wakulima wadogo wa chai wamezalisha tani 4,811. Vilevile, uhamasishaji wa unywaji wa chai umeendelea, ambapo hadi Machi 2020, chai iliyochanganya na kufungwa kwenye vikasha ilikuwa tani 2,700 sawa na unywaji wa gramu 65 kwa mtu kwa mwaka.

143. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2019, tija ya chai kavu kwa wakulima wadogo illkuwa kilo 415 kwa hekta ikilinganishwa na kilo 428 kwa kipindi hicho cha mwaka 2018. Aidha, tija ya chai kavu kwa wakulima wakubwa imefikia kilo 522 kwa hekta katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019 ikilinganishwa na kilo 760 kwa kipindi hicho cha mwaka 2018. Upungufu huo wa tija umetokana na barafu ilioanguka katika Ukanda wa Nyanda za juu Kusini ambapo kuna uzalishaji mkubwa wa chai.

144. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Bodi ya Chai Tanzania imeendelea kuhamasisha wakulima kufufua mashamba ya chai ambapo shamba la chai la Mlangani katika Tarafa ya Lupembe lenye ukubwa wa hekta 200 limefuliwa kwa asilimia 60. Vilevile, ukarabati wa miundombinu ya mashamba ya chai yanayomilikiwa na vijiji vya Tarafa ya Lupembe-Njombe umekamilika kwa asilimia 50.

145. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuimarisha soko la majani mabichi ya chai kwa wakulima wadogo na kuongeza ajira. Katika mwaka 2019/2020, Bodi ya Chai kwa kushirikiana na PSSSF imekamilisha andiko la kufufua kiwanda cha chai cha Mponde-Tanga. Tayari kampuni itakayosimamia uendeshaji wa kiwanda hicho imeundwa.

146. *Mheshimiwa Spika*, wastani wa ubora wa majani mabichi ya chai umeongezeka kutoka asilimia 50 hadi 60. Mauzo ya chai kavu nje ya nchi katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Januari, 2020 ni tani 11,270 yenye thamani ya Dola za Marekani 15,877,037 ikilinganishwa na tani 13,312 yenye thamani ya Dola za Marekani 21,031,225 kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Januari, 2019. Mauzo hayo yameshuka kutokana na kuyumba kwa soko la chai la Dunia. Aidha, hadi Machi 2019, Bodi imesajili jumla ya wakulima 31,092 sawa na asilimia 69 ya lengo.



*Wastani wa ubora wa majani mabichi ya chai umeongezeka kutoka asilimia 50 hadi 60.*

#### Zao la Mpunga

147. *Mheshimiwa Spika*, katika msimu 2018/2019 uzalishaji wa zao la mpunga umefikia tani 3,174,766. Katika mwaka 2019/2020 upatikanaji wa mbegu bora za mpunga ulikuwa tani 614.66. Kati ya tani hizo tani 597.46 zimezalishwa nchini, tani 12.70 ni bakaa ya msimu uliopita na tani 4.50 zimeagizwa toka nje ya nchi. Wizara kuititia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekarabati kinu cha kukobia mpunga chenye uwezo wa tani 3.5 kwa saa kilichopo katika kijiji cha Madibira – Mbarali; na imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa kuendeleza zao la Mpunga Awamu ya Pili – NRDS II (2019/2020 – 2029/2030) ambaao ulizinduliwa Desemba, 2019. Mkakati huo unalenga kuongeza tija kutoka wastani wa tani 2 kwa hekta hadi tani 4 kwa hekta na kupunguza upotevu baada ya mavuno kutoka asilimia 30 hadi asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

### Zao la Mahindi

148. *Mheshimiwa Spika*, katika msimu wa 2018/2019 uzalishaji wa zao la mahindi ulifikia tani 5,652,005 sawa na asilimia 71 ya lengo la tani 8,000,000. Lengo lililowekwa halikufikiwa kutokana na upungufu wa mvua za vuli na mvua za msimu kwa baadhi ya mikoa inayopata mvua hizo. Katika hatua nyingine, Wizara imesimamia upatikanaji wa tani 32,638.51 za mbegu bora za mahindi kwa ajili ya msimu wa 2019/2020 na imetoa mafunzo kuhusu udhibiti wa viwavijeshi vamizi kwa wakulima 2,080 wa mahindi kutoka mikoa ya Singida (385), Shinyanga (425), Simiyu (495), Tabora (530) na Morogoro (245).

### Zao la Ngano

149. *Mheshimiwa Spika*, upatikanaji wa mbegu bora za ngano nchini katika msimu wa 2019/2020 umefikia tani 63.70 ambazo zimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima. Katika mwaka 2018/2019, uzalishaji wa ngano ulifikia tani 63,388 ikilinganishwa na malengo ya kuzalisha tani 76,400. Hadi Machi 2020, Wizara imehamasisha kilimo cha zao hilo katika Ukanda wa Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini na imeongeza maeneo mapya ya uzalishaji ambayo ni Mbarali na shamba la Kapunga. Aidha, wizara imehamasisha matumizi ya mbegu bora, kutoa mafunzo ya kanuni za kilimo bora, kuimarisha upatikanaji wa masoko na utafiti wa zao hilo.

### Zao la Muhogo

150. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020 Wizara imeendelea kuimarisha uzalishaji wa zao la muhogo ambapo hadi kufikia Machi 2020 uzalishaji wa mbegu za muhogo umefikia pingili 38,860,300 sawa na asilimia 97 ya lengo la kuzalisha pingili milioni 40. Mbegu hizo zimesambazwa katika Halmashauri 43 za Kanda za Kusini, Mashariki na Ziwa. Kiasi hicho cha vipando kinatosheleza kupanda hekta 3,886. Aidha, aina tisa (9) za mbegu bora za muhogo zimegunduliwa na kupendekezwa kutumika kwa wakulima katika kanda ya ziwa. Mbegu hizo zina sifa ya kuhimili ugonjwa wa michirizi kahawia na batobato, na zinatoa mavuno kati ya tani 25 hadi 30 kwa hekta.

151. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuhamasisha ununuzi wa muhogo ambapo kampuni nne za Dar Canton, Jielong Holdings, TAEPZ na EPOCH Agricultural Development Company zimenunua jumla ya tani 300 za muhogo mkavu kutoka kwa wakulima. Ili kuongeza ufanisi katika tasnia ndogo ya muhogo, Wizara imewezesha uanzishwaji wa jukwaa la umoja wa wazalishaji na wasindikaji wa muhogo tanzania (*Tanzania Cassava Producers and Processors Association – TACAPPA*).

#### Zao la Mtama na Uwele

152. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka 2019/2020, upatikanaji wa mbegu bora za mtama na uwele ulikuwa tani 85.24. Uzalishaji wa mazao hayo kwa msimu wa 2018/2019 ulikuwa tani 1,018,173, sawa na asilimia 67.8 ya lengo la kuzalisha tani 1,500,000. Kutokana na umuhimu wa zao la mtama na uwele hususan katika maeneo yanayopata mvua chini ya wastani, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafisi imeendelea kuhamasisha matumizi ya mbegu bora za mtama na uwele zenye kutoa mavuno ya wastani wa tani 2.5 kwa hekta ili kukidhi mahitaji ya chakula na malighafi za viwanda. Aidha, Wizara kupitia TARI imeendelea kushirikiana na Kampuni ya Bia Tanzania kwa kufanya tathmini ya mbegu sita (6) aina ya masia, tegemeo, sila, hakika, PAC501 na NAC01 pamoja na viwango sahihi vya mbolea ambavyo vitatoa punje za mtama zenye ubora wa kutengeneza bia.

#### Mazao ya Mafuta

153. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha upatikanaji wa mafuta ya kula nchini, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhamasisha uzalishaji na usindikaji wa mbegu za mafuta. Katika msimu wa mwaka 2018/19 uzalishaji wa mazao ya mafuta ya alizeti, karanga, ufuta, michikichi na soya uliongezeka kufikia tani 1,230,767 sawa na ongezeko la asilimia 11.0 ya uzalishaji wa tani 1,109,142 kwa msimu wa mwaka 2017/18. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mazao ya mbegu za mafuta hususan ufuta katika masoko ya nje na kusababisha kupanda

kwa bei ya ufuta na kuanza kutumika mfumo wa mauzo kupitia Soko la Bidhaa Tanzania. Uzalishaji wa mazao hayo ni kama unavyoonekana katika (Kiambatisho Na. 20).

154. *Mheshimiwa Spika*, katika msimu wa 2019/2020, Wizara imewezechesa upatikanaji wa mbegu ya alizeti tani 488.87 ambapo kati ya hizo, tani 333.87 zimezalishwa ndani ya nchi, 142.70 zimeagizwa kutoka nje ya nchi na tani 12.30 ni bakaa ya msimu wa 2018/2019. Aidha, Wizara kupitia TARI, imegundua na kupendekeza kwa wakulima aina mbili (2) za mbegu bora za alizeti zenye sifa ya kutoa mavuno mengi na kiwango kikubwa cha mafuta ikilinganishwa na mbegu zilizopo. Vilevile, kampuni binafsi zimegundua aina saba (7) za mbegu bora za alizeti. Pia, TARI imeendelea kusafisha mbegu ya alizeti aina ya RECORD ili kuirudishia ubora wake.



*Mbegu bora ya alizeti aina ya TARI – ILO2019 ambayo Wakulima wanahamasishwa kuitumia ili kuongeza tija na uzalishaji kwa kuwa inatoa mavuno mengi na ina kiwango kikubwa cha mafuta.*

155. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuhamasisha upatikanaji wa mbegu bora za chikichi ambapo katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia TARI, ASA, Jeshi la Kujenga Taifa, Magereza, Sekretarieti za Mikoa na Sekta Binafsi imezalisha mbegu bora 1,775,200. ASA imezalisha miche 9,000 ya michikichi ambayo imesambazwa kwa wakulima. Aidha, ASA imojiwekea mpango wa kukuza miche 85,000 (kutegemea na upatikanaji wa mbegu – pre-geminated

seeds) kwa mwezi ili kufikia lengo la kupata miche 1,000,000 kwa mwaka. Aidha, Wizara kupitia TARI imehamasisha kilimo cha zao la michikichi katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Mbeya na Morogoro.

#### Zao la Nazi

156. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia TARI imeendelea kufanya utafiti wa minazi ili kupata aina bora ya minazi inayostahimili magonjwa. TARI imeainisha mbegu ya asili *East African Tall kwamba* inastahimili ugonjwa wa mnyauko wa minazi ambapo hadi Machi 2020, miche 6,000 imezalishwa na kusambaza kwa wakulima katika mikoa ya Mwanza na Pwani. TARI pia, inaendelea na utafiti na uhamasishaji wa kanuni za kilimo bora cha minazi. Aidha, uzalishaji wa zao la nazi kwa mwaka 2018/19 ulifkia tani 143,728.



*Naibu Waziri wa Kilimo Mhe Omary Mgumba (Mb) akipanda mti wa mchikichi ikiwa ni ishara ya kuzindua upanuzi wa shamba la zao hilo katika Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Bulombora wilayani Uvinza, Februari 17, 2019. Wakati wa ziara ya Waziri Mkuu Mhe Kassim Majaliwa yenye lengo la kuhamasisha ufuluaji wa zao la michikichi.*

#### Zao la Zabibu

157. *Mheshimiwa Spika*, upatikanaji wa miche bora ya zabibu katika msimu wa 2019/2020 umefkia miche 1,405,477. Miche hiyo ya zabibu imezalishwa na Wizara kupitia TARI na

imesambazwa kwa wakulima. Pia, Wizara imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa zabibu ambapo katika mwaka 2018/2019 uzalishaji umefikia tani 16,138 katika eneo la hekta 2,458 linalolimwa zabibu Mkoani Dodoma ikilinganishwa na tani 15,017 mwaka 2017/2018. Aidha, kiasi cha tani 2,171 za zabibu kimesindikwa Mkoani Dodoma kupitia viwanda vikubwa viwili (2) na vidogo tisa (9).

#### **4.24 Kuimarisha Masuala Mtambuka**

158. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuzingatia masuala mtambuka katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa rasilimali watu; kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo; lishe; mazingira; jinsia na kuendeleza mapambano dhidi ya VVU na Ukimwi.

##### *Usimamizi wa Rasilimali Watu*

159. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendela kuhakikisha inakuwa na watumishi wakutosha na wenyewe weledi ambao wataweza kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake. Katika mwaka 2019/2020 Wizara imeajiri Watumishi wapya 73 na kupandisha vyeo watumishi 228. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya watumishi 23 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 90 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ikiwemo elimu kuhusu utawala bora na maadili ya Utumishi wa Umma.

##### *Jinsia*

160. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuzingatia masuala ya jinsia katika Mipango ya kilimo. Katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la UN-Women imepitilia Sera ya Kilimo 2013 ili kubaini maeneo ya kisera yenye mlengo wa jinsia yanayohitajika kurekebishwa. Aidha, Wizara imesambaza nakala 22,000 za kitabu cha vikaragosi cha watoto wa shule za msingi darasa la nne hadi la sita kinachohusu masuala ya jinsia katika kilimo ili kuhamasisha watoto kufahamu masuala ya kilimo na jinsia.

*Mazingira*

161. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imesambaza Mwongozo wa Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi na kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani, Mazingira na Mipango 223 wa Halmashauri 26 za Wilaya za Karatu, Mbulu, Longido, Simanjiro, Kiteto, Itilima, Bariadi, Meatu, Maswa, Kibaha TC, Kisarawe, Rufiji, Mkuranga, Kibiti, Butiama, Bunda, Musoma DC, Tarime, Bukoba DC, Kyerwa, Muleba, Biharamuro, Uvinza, Kasulu, Kibondo na Kakonko. Aidha, nakala 256 za mwongozo huo na Kitabu cha Mbinu na Kiongozi cha Mwalimu vimesambazwa. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia mradi wa Kilimo Himilivu kwa Kutumia Mbinu za Kiikolojia imewawezesha wakulima na wafugaji kuibua shughuli mbadala za kuongeza kipato ili kupunguza uharibifu wa mazingira kutoka katika Wilaya za Mvomero, Simanjiro, Mpwapwa na Kishapu.

*VVU na UKIMWI*

162. *Mheshimiwa Spika*, Katika kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI mahali pa kazi, Wizara imeendelea kuwahamasisha watumishi kupima afya ili kutambua hali zao. Katika mwaka 2019/2020, watumishi 16 waliojitambulisha kwa mwajiri kuwa wanaishi na VVU wameendelea kupatiwa Shilingi 100,000 kila mwezi kwa ajili ya kuwawezesha kupata lishe bora. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa vifaa kinga kwa watumishi na kuwekwa katika maeneo yanayofikiwa na watumishi wengi. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kupima ili kujuu hali za afya.

**5. KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/2021**

*Masuala Muhimu Yaliyozingatiwa*

163. *Mheshimiwa Spika*, Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/2021 ya Wizara ya Kilimo imeandaliwa kwa kuzingatia maelekezo yaliyomo kwenye Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/2021. Mpango huo umezingatia Dira

ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya (2016/2017 – 2020/2021); Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs); na Mpango wa Uwekezaji katika Kilimo na Usalama wa Chakula Tanzania (TAFSIP).

164. *Mheshimiwa Spika*, masuala mengine yaliyozingatiwa ni pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015; Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013; na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Pia, imezingatia masuala mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabianchi, UKIMWI, ajira kwa vijana na kutokomeza ajira kwa watoto katika sekta ya kilimo.

165. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara itatekeleza Maeneo 10 ya vipaumbele kuititia Fungu 43, 24 na 05 katika Idara, Vitengo, Tume na Taasisi za Wizara. Mpango wa bajeti umeweka msisitizo kwenye kilimo kitakachohakikisha usalama wa chakula ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa chakula na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda.

166. *Mheshimiwa Spika*, Maeneo ya kipaumbele ni pamoja na: Kuendelea na utekelezaji wa Progamu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II); Kuboresha mifumo ya kitaasisi, Bodi na Sheria za Kilimo kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya mazao ya kilimo; kuunganisha wakulima wadogo na mashamba makubwa ili kuendeleza kilimo cha kibiashara, kupata ujuzi na maarifa ya kilimo chenye tija, kurahisisha upatikanaji wa huduma za pembejeo na masoko; Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji, maghala, masoko na miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo; na Kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za mazao na upatikanaji wa pembejeo nyingine za kilimo na kuzisambaza kwa wakulima.

167. *Mheshimiwa Spika*, maeneo mengine yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya ushirika pamoja na kuweka mifumo

itakayoongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wanaushirika na wadau wengine wa sekta ya kilimo; kuongeza matumizi ya teknolojia bora katika uzalishaji wa mazao na tija; kuimarisha Vituo vya Utafiti, Vyuo vya Mafunzo na Vituo vya Mafunzo kwa Wakulima kwa kujenga miundombinu wezeshi na kuboresha maarifa na ujuzi kwa watafiti, wakufunzi na wazalishaji kwa lengo kukuza kilimo; kuimarisha huduma za upimaji wa matabaka na ubora wa udongo kuendana na mahitaji ya mazao ya kilimo kimaeneo; na kuimarisha masuala mtambuka katika kilimo.

### 5.1 Kuendelea na Utekelezaji wa Progamu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)

*168. Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021 Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na Wizara za Sekta ya kilimo pamoja na Sekta Binafsi kuendeleza mazao ya kipaumbele kama yalivyoainishwa kwenye ASDP II ambayo ni pamba, kahawa, miwa, korosho, chai, mahindi, mpunga, mtama, uwele, muhogo, mazao ya bustani, mazao ya mafuta, viazi na mazao ya mikunde na migomba. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti vya kilimo, udhibiti wa visumbufu vya mimea, huduma za ugani, usajili wa wakulima na bima ya mazao.

### 5.2 Kuboresha Mifumo ya Kitaasisi, Bodi na Sheria kwa Ajili ya Kuimarisha Usimamizi wa Maendeleo ya Mazao ya Kilimo

*169. Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea na mapitio ya Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013 na Mkakati wa Utekelezaji wake ili kuwa na Sera yenye kujibu changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo. Vilevile, Wizara itaendelea kutunga na kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali zilizopo katika sekta ya kilimo ambazo zitabainika kuwa na mapungufu kwa lengo la kuzifanyia maboresho ili kupunguza ama kuondoa changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo. Sheria zitakazotungwa au kufanyiwa marekebisho ni pamoja na Sheria zilizoanzisha Taasisi na Bodi zilizo chini ya Wizara, Sheria ya Kilimo, Sheria ya Afya ya mimea, Sheria ya Tasnia ya Sukari na Sheria ya Ushirika.

170. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya kilimo imekuwa na mifuko mbalimbali ya kusaidia mazao ili mkulima aweze kuongeza uzalishaji na tija. Mifuko hiyo illenga kuongeza uzalishaji, kukuza tija katika kilimo, kukuza masoko, miundombinu pamoja na kutumia zana bora za kilimo na teknolojia za kisasa. Pamoja na malengo ya mifuko hiyo, kumekuwepo na changamoto zilizosababisha mkulima kushindwa kukua kiuchumi kutokana na kushindwa kutumia michango yao kama dhamana ya kupata mikopo kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao za kilimo. Changamoto hizo zilisababisha Serikali kusitisha mifuko hiyo.

171. *Mheshimiwa Spika*, kusitishwa kwa mifuko hiyo kumesababisha kukosekana kwa mfumo madhubuti wa kumwezesha mkulima kugharamia shughuli zake katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, katika mwaka 2020/2021, Wizara itaandaa andiko la kuanzisha mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo utakaoshirikisha wabia wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi, sekta ya fedha, na wawekezaji ili kuukuza mfuko na kuwezesha miradi kwenye mnyororo ya thamani ya mazao, afya na maendeleo ya watu. Mfuko huo utakuwa unasimamiwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za fedha zinazohimiza uwazi na utunzaji wa mitaji tofauti na mifuko ya zamani ambayo ilikuwa ni vigumu kushirikisha wadau kuwekeza kwa vile haikuundwa kwa kanuni za uwekezaji.

### 5.3 Kuunganisha Wakulima Wadogo na Mashamba Makubwa ili Kuendeleza Kilimo cha Kibiashara

172. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara itahakiki mashamba 25 ya uwekezaji ya Mkulazi, Mvuha, Muhoro, Manda, Mahurunga, Mkongo, Misegese, Luiche, Kiberege, Kihansi, Kisegese, Kasulu, Kisaki, Kilosa kwa mpepo, Kumsenga, Kitengule, Bagamoyo, Tawi, Luipa, Ngalimila, Lukulilo, Rufiji delta, Ngohelanga, Pangani na Itete na kuandaa mpango kina wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo.

173. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itawezesha kupatikana kwa Hati za Haki Miliki za Kimila kwa wakulima 400 wanaozunguka

mashamba sita (6) kati ya 25 yatakayokuwa yamehakikiwa ili kuwezesha wakulima wadogo kuwa na uhakika wa umiliki wa mashamba yao na kutumia kama dhamana kwa ajili ya kupata mikopo kwenye taasisi za fedha. Aidha, Wizara itatoa elimu ya kuzuia mmomonyoko wa udongo katika maeneo ya kilimo yaliyoathirika katika lindimaji (*catchment area*) nne (4) za Ruaha, Kilombero, Ruvu na Pangani ili ardhi ya wakulima wa maeneo hayo iwe endelevu na kuwa na tija katika uzalishaji.

5.4 Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji, Maghala, Masoko na Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya Kilimo

*Uendelezaji wa Miundombinu ya umwagiliaji*

174. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara imepanga kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kuimarisha vyama vya umwagiliaji maji. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na: - kukamilisha ujenzi na ukarabati wa skimu 17 za umwagiliaji zenye ukubwa wa hekta 8,536 kuitia ASDP II. Skimu hizo ni Kirya – Mwanga (hekta 800), Igende – Misungwi (hekta 150), Endagaw – Hanang (hekta 276), Kibwaya – Morogoro DC (hekta 200), Ikweha – Mufindi DC (hekta 560), Isenyela – Mbarali (hekta 1000), Lwanyo – Mbarali (hekta 630), Msia – Mbozi (hekta 100), Karema – Tanganyika DC (hekta 2000), Idudumo-Nzega DC (hekta 200), Eyasi Mang’ola – Karatu (hekta 750), Kitere – Mtwaro DC (hekta 450), Mabunga – Kyela DC (hekta 250), Makangaga – Kilwa (hekta 250), Narunyu – Lindi (hekta 720), Katunguru – Sengerema (hekta 200) na Euga – Ulanga (hekta 440).

175. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itakamilisha ujenzi na ukarabati wa skimu tano (5) ambazo ni; Kigugu – Mvomero (hekta 195), Msolwa Ujamaa (hekta 40), Njage (hekta 75) – Kilombero, Mvumi (hekta 249) na Kilangali Seed farm (hekta 400) – Kilosa kuitia mradi wa ERPP; itatoa mafunzo kwa wakulima na wakulima viongozi 1,000 katika uandaaji wa mipango ya matunzo na uendeshaji wa skimu pamoja na usimamizi wa rasilimali maji katika skimu 50. Aidha, Wizara

itakamilisha upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa nyaraka za zabuni katika skimu ya Mkombozi (Iringa vijiji-hekta 10,000) pamoja na upembuzi yakinifu na Usanifu wa mabwawa na skimu za Luiche (Ujiji, Kigoma – hekta 3,000) na Ibanda (Sengerema/Geita – hekta 1,200). Vilevile, Wizara itafanya upembuzi yakinifu na usanifu na kuandaa nyaraka za zabuni katika skimu za Illemba (Sumbawanga – hekta 800) na Makwale (Kyela – hekta 3,500) pamoja na mabwawa ya Nyisanzi (Chato – hekta 260), Kisese (Kondoaa-hekta 2,000), Msia (Mbozi – hekta 100), Idudumo (Nzega-hekta 200) na Masasi (Chato – hekta 530).

176. *Mheshimiwa Spika*, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuanzisha mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji. Mfuko huo unaanzishwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 4 ya Mwaka 2013 kifungu cha 52 (1) kinachoelekeza kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji ili kuwa na uhakika wa Maendeleo endelevu ya Sekta ya Umwagiliaji na Kifungu cha 52 (2) kinachoainisha vyanzo vyta mapato vya mfuko ambavyo haviingiliani na vyanzo vyta kodi au tozo zilizopo katika sheria nyingine za ukusanyaji wa mapato. Aidha, matumizi ya fedha za Mfuko huu yatazingatia matakwa ya kifungu cha 53 cha Sheria ya Umwagiliaji.

#### *Uendelezaji wa Miundombinu ya Maghala na Masoko*

177. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara imepanga kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi wa NFRA kwa kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa ghala sita (6) na vihenge nane (8) vya kisasa vyenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 250,000. Ujenzi wa ghala utaendelea kufanyika katika kanda za Dodoma, Songea, Makambako, Mbozi, Sumbawanga, Mpanda, Babati na Shinyanga. Vilevile, Wakala utakarabati ghala tano (5) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 37,500 za nafaka katika kanda zake. Aidha, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko itajenga vihenge tisa (9) vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 94,000 za nafaka na ghala mbili (2) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 za nafaka jijini Mwanza na Dodoma.

178. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kuititia Mradi wa TANIPAC itaimarisha Kituo cha Taifa cha Udhibiti wa Magonjwa ya Kibailojoja wilayani Kibaha kwa kujenga karantini na maabara ya uchunguzi ili kudhibiti magonjwa na uchafuzi wa mazao unaosababishwa na sumukuvu; itajenga Maabara Kuu ya Kilimo Jijini Dodoma itakayosaidia kuimarisha udhibiti wa ubora na usalama wa mazao ya kilimo hususan mazao ya chakula; itajenga Kituo Mahiri cha Usimamizi wa Mazao ya Nafaka baada ya kuvuna katika eneo la Mтанана - Kibaigwa; itajenga ghala 12 zenyewe uwezo wa kuhifadhi tani 2,000 kila moja katika wilaya za Kasulu, Kibondo, Itilima, Nzega, Bukombe, Chemba, Babati, Gairo, Kiteto, Nanyumbu, Buchosa na Namtumbo kwa lengo la kudhibiti sumukuvu; na kufundisha vijana 400 teknolojia ya kutengeneza Vihenge vya Kisasa (Metal Silos).

#### *Masoko ya Mazao*

179. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara itaendelea kufuatilia upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na taasisi nyingine ikiwemo TMX na TANTRADE; itaimarisha matumizi ya mifumo ya masoko ikiwa ni pamoja na soko la bidhaa, Stakabadhi za Ghala, minada kuititia vyama vya ushirika na kilimo cha mkataba; kuititia NFRA itaimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao kwa kununua tani 300,000 za nafaka zikiwemo tani 277,000 za mahindi, tani 16,000 za mpunga na tani 7,000 za mtama pamoja na kuhudumia mahitaji ya dharura ya chakula na kukabiliana na mfumuko wa bei. Aidha, Wizara kuititia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) itanunua na kuuza tani 500,000 za nafaka na tani 1,200,000 za muhogo mkavu.

180. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendesha kampeni ya kitaifa ya utoaji elimu ya Udhibiti wa Sumukuvu kwa wadau wakiwemo wakulima na watunga sera kwa kushirikiana na TBS, VETA na SIDO; na kuititia SAGCOT na wabia wake, itawaunganisha wakulima 12,500 katika mifumo ya kompyuta ikiwemo Ubia-Soko ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za masoko na pembejeo, na kuboresha uratibu wa maboresho

ya sera kwa mazao ya Mbogamboga na Matunda, Mpunga, Alizeti, Miwa, Chai, na Ufugaji wa Kuku na Samaki.

*181. Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara itaaniszisha kituo kimoja cha huduma (one stop centre) kitakachoshughulikia usindikaji na usafirishaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi kupitia bandari ya Dar Es Salaam eneo la kurasini linalomilikiwa na Mamlaka ya EPZA.

5.5 Kuimarisha Uzalishaji wa Mbegu Bora za Mazao na Upatikanaji wa Pembejeo Nyingine za Kilimo na Kuzisambaza kwa Wakulima

*182. Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia taasisi za ASA, TOSCI, TARI, TPRI, TFRA na sekta binafsi itaimarisha upatikanaji, utumiaji na udhibiti wa pembejeo ili kuongeza tija, kipato na usalama wa chakula na lishe kwa kutekeleza yafuatayo: -

*Kufanya utafiti wa kilimo na kuzalisha teknolojia kwa mazao ya kimkakati*

*183. Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia TARI itafanya utafiti ili kugundua mbegu bora 15 za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde, mazao ya mizizi na mbegu za mafuta; itaendelea kutunza aina 520 za mbegu za asili za mpunga katika kituo cha utafiti cha TARI Ifakara; itafanya utafiti wa kusafisha mbegu aina ya Super Magugu katika Wilaya ya Babati; kupitia TaCRI itaendelea kufanya utafiti wa kahawa aina fupi ya Arabika chotara na Robusta; itazalisha na kusambaza miche bora ya kahawa 15,042,975; itatoa mafunzo kuhusu kanuni bora za utunzaji wa kahawa kwa wakulima 2,581, wakulima wahamasishaji 69, vikundi vyya wakulima wa kahawa 57 na maafisa ugani 288. Pia, itaongeza eneo la bustani ya kuzalisha miche ya kahawa katika kanda sita; na kuendeleza utafiti wa matumizi ya chokaa (*application of lime*) katika kurekebisha rutuba ya udongo.

*184. Mheshimiwa Spika*, Wizara, kupitia TORITA itakamilisha taratibu za kusajili *mbegu* mpya za tumbaku zitakazopendekezwa na wakulima; itatathmini mbegu aina

ya KRK26R isiyoshambuliwa na kirusi cha tumbaku (*Tobacco Mosaic Virus-TMV*); itaendelea kushirikiana na Taasisi ya Utafititi wa Tumbaku Zimbabwe (TRB Kutsaga Zimbabwe) ili kutathmini mbegu mpya za KRK75 na T68. Vilevile, itashirikiana na Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela (NM-AIST) kuendelea kutafiti teknolojia mbadala ya kukausha tumbaku ikiwemo nishati ya juu na vitofali vilivytengenezwa kwa kutumia masalia ya kioqaniki.

## *Uzalishaji wa mbegu*

185. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kuititia ASA itaongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 1,436 hadi tani 5,000 kwa kupanua eneo la uzalishaji kutoka hekta 1,017 hadi hekta 2,800; itazalisha miche ya michikichi 1,000,000, miche ya matunda 560,000 na pingili za muhogo 1,800,000; itaongeza upatikanaji wa mbegu za ufuta na alizeti kufikia tani 1,325; itajenga na kuboresha miundombinu ya uzalishaji wa mbegu ikiwa ni pamoja na kujenga miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza eneo la kuzalisha mbegu linalomwagiliwa kutoka hekta 600 hadi hekta 850 kwenye maeneo yanayomilikiwa na ASA.

186. *Mheshimiwa Spika*, ASA pia itakarabati na kujenga ofisi na ghala za kuhifadhi mbegu, kununua matrektu na zana za kilimo, magari ya kufanya kazi mashambani na usambazaji wa mbegu; itazalisha mbegu na kusambaza kwa wakulima na makampuni binafsi ya mbegu kiasi cha tani 3,627. Kati ya hizo tani 301.88 ni mazao ya nafaka, tani 326.48 mazao jamii ya mikunde na tani 290.204 ni mazao ya mafuta. Aidha, TARI itazalisha miche, pingili na vikonyo 21,000,000 kwa mazao ya korosho (miche 629,629) muhogo (pingili 7,682,674), katani (miche 440,548), viazi vitamu (vikonyo 723,664), viazi mviringo (vikonyo 1,000,000) miwa (miche 393,698), migomba (miche 2,936,984), nazi (miche 587,396.87), zabibu (miche 1,405,477) na michikichi (miche 5,000,000).

## *Udhibiti Ubora wa Mbegu*

187. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021 Wizara kuititia TOSCI itaimarisha uthibiti na udhibiti wa ubora wa

mbegu kwa kufundisha wagunduzi 25 wa mbegu za mazao; itaandaa miongozo ya kufanya majaribio ya Uhalisia na Umahiri wa aina mpya za mbegu za mazao mawili (2) ya miti; itafanya kaguzi katika Wilaya zote Tanzania Bara kutambua mbegu ambazo muda wake umeisha katika maghala na maduka na kuchukua hatua za kisheria; itafuatilia na kuchukua hatua za kisheria kwa matukio ya mbegu bandia; itasajili wafanyabiashara 300 wa mbegu na wakulima wadogo 400 wa mbegu za QDS; na itatoa mafunzo kwa wakaguzi wa mbegu wa Wilaya 25 na wakaguzi 25 wa afya ya mimea PHS waliopo mipakani. *Udhhibit wa Ubora wa Mbolea*

188. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka 2020/2021, Wizara kuititia TFRA itawezesha na kusimamia uzalishaji wa mbolea tani 30,000 nchini, uingizwaji wa mbolea tani 580,000 na usafirishaji wa tani 150,000 za mbolea nje ya nchi. Pia itaendelea kudhibiti ubora wa mbolea nchini, kusimamia utoshelevu, upatikanaji, usambazaji na unafuu wa bei za mbolea kwa wakulima; itatoa mafunzo ya ukaguzi wa mbolea kwa maafisa kilimo 30 na kuwajengea uwezo wakaguzi wa mbolea 70 wa Halmashauri za Wilaya. Vilevile, itakagua makampuni 13 yanayozalisha mbolea na kukagua wafanyabiashara wa mbolea 1,050 kwenye mikoa yote; itajenga na kununua vifaa vyta maabara vyta kupima ubora wa mbolea kwa kushirikiana na TBS, SUA, TPRI na GCLA ili kudhibiti uingizaji wa mbolea bandia na zisizosajiliwa.

189. *Mheshimiwa Spika*, TFRA pia itaimarisha mfumo wa kukusanya takwimu kwa kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa Halmashauri 169 na kuwapatia mafunzo wafanyabiashara wa mbolea 1,500 na vyama vyta ushirika 30 kuhusu ubora, uhifadhi, biashara na matumizi ya mbolea. Vilevile, itachapisha nakala mbili (2) zinazoonesha matokeo ya matumizi sahihi ya mbolea; itahamasisha ujenzi wa viwanda vyta uchanganyaji wa mbolea (*Blending Plants*) pamoja na viwanda vitatu (3) vyta kuzalisha mbolea kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini; itaimarisha mfumo wa ununuzi wa pamoja na usambazaji wa mbolea kwa kutumia vyama vyta ushirika; na itasajili wafanyabiashara 1,200, kutoa

leseni 2,700 za biashara na vibali 500 vya uingizaji mbolea nchini.

*Udhhibitit wa Ubora wa Viuatilifu*

190. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia TPRI itafungua vituo vinne (4) vya ukaguzi wa viuatilifu na mimea katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Dodoma na Kigoma. Vilevile, itaimarisha mifumo ya kanzidata na ATMIS kwa wafanyabiashara wa viuatilifu na waingizao mimea na itaboresha miundombinu ya maabara mbili (2) kwa ajili ya kupata Ithibati; itabuni teknolojia rahisi za uhifadhi wa mazao kwa kutumia mbinu husishi (IPM); na itatathmini na kusajili viuatilifu vinavyohitajika na tasnia tofauti na kuhimiza matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa kutoa mafunzo katika kanda saba (7) za kilimo.

*Udhhibitit wa Visumbufu vya Mimea na Mazao*

191. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021 Wizara itanunua lita 270,300 na kilo 5,000 za viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao; itafanya savei za kutathimini uwepo wa kweleakwelea, Panya na Nzige wekundu katika mikoa ya Mbeya, Mara, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Simiyu, Geita, Songwe, Ruvuma, Tanga, Pwani, Rukwa, Kigoma, Katavi, Lindi na Iringa; itaimarisha kituo cha kudhibiti visumbufu kwa njia ya Anga (KILIMO ANGA) kwa kukipatia vitendea kazi ikiwemo mafuta ya ndege ili kukabiliana na milipuko ya visumbufu; na itakarabati vituo 10 vya mipakani na kuvizezesha kununua vifaa vya ukaguzi ili kuongeza ufanisi.

5.6 Kuimarisha Usimamizi wa Maendeleo ya Ushirika kwa Kuweka Mifumo Itakayoongeza Ufanisi

192. *Mheshimiwa Spika*, kwa muda mrefu ushirika umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa viongozi wa ushirika wenye uwezo wa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa majukumu ya vyama kwa ufanisi. Hali hiyo imesababisha kukithiri kwa vitendo vya ubadhirifu wa

fedha na mali za wanaushirika na hivyo kuwakatisha tamaa wakulima kuijunga kwenye vyama hivyo.

193. *Mheshimiwa Spika*, katika kuangalia namna bora ya kuongeza ufanisi katika usimamizi na udhibiti wa uendeshaji wa vyama vya ushirika vya mazao ya kilimo na masoko nchini, katika mwaka 2020/2021, Wizara itafanya marekebisho ya Sheria ya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 ili kurekebisha mapungufu yaliyokuwepo kwenye sheria iliyopo na kuimarisha eneo la usimamizi wa vyama vya ushirika nchini.

194. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kuititia Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaendelea kuimarisha usimamizi kwenye vyama vya ushirika kwa kukagua hesabu za vyama 7,615 vya ushirika na kufuta vyama vilivyoshindwa kutimiza majukumu kwa mujibu wa masharti ya kuandikishwa. Aidha, Tume itafuatilia mali za vyama vya ushirika zillzochukuliwa kinyume na taratibu na kuhakikisha zinarudishwa na kusimamiwa kikamilifu. Katika kuongeza kasi ya udhibiti na ukaguzi wa vyama, Tume itatoa mafunzo kwa viongozi, watendaji na wanachama, kuhusu haki na wajibu wao pamoja na elimu ya ujasiriamali.

195. *Mheshimiwa Spika*, mambo mengine yatakayotekelezwa na Tume ni pamoja na kuanzisha na kusajili SACCOS 1,500 kwenye maeneo yenye AMCOS; kusajili vyama 1,000 vya ushirika kutoka sekta nyingine; kuwaunganisha wakulima na benki ili kurahisisha malipo yao; kuzindua mifumo miwili ya kusimamia shughuli za vyama vya Ushirika; na kuhuisha Daftari la Vyama vya Ushirika kielektroniki.

## 5.7 Kuongeza Matumizi ya Teknolojia Bora katika Uzalishaji wa Mazao ili Kuongeza Uzalishaji na Tija

### *Zana za Kilimo*

196. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za matumizi ya zana bora za kilimo kwa wakulima kwa gharama nafuu. Katika mwaka 2020/2021, Wizara itaviwezesha vituo vitatu (3) vya kutoa huduma za zana za kilimo (*Agri-mechanization hub*) katika mikoa ya

Mwanza, Morogoro na Njombe kwa kuvipatia zana za kilimo ikiwemo matrepta, mashine za kupandia, kunyunyizia na kuvunia mazao. Hatua hii itasogezza huduma za zana za kilimo kwa wakulima ambao hawana uwezo wa kununua zana za hizo pamoja huduma nyingine za kilimo ikiwemo pembejeo. Vilevile, kupitia vituo hivyo wakulima na maafisa ugani watapatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia mpya ya zana za kilimo.

197. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kushirikiana na sekte binafsi katika kuongeza upatikanaji na matumizi ya zana za kilimo ili kupunguza matumizi ya jembe la mkono na kuongeza uzalishaji. Aidha, itafanya mapitio ya Mkakati wa Matumizi Bora ya Zana za Kilimo (*Tanzania Agricultural Mechanization Strategy – TAMS*) wa mwaka 2006 ili uendane na mahitaji ya sasa ya sayansi na teknolojia.

198. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) itatoa mikopo 300 yenye thamani ya Shilingi 4,598,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa mitambo ya mashambani; pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi; matrepta ya mikono; ukarabati wa zana za kilimo, miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi; uendeshajji wa shughuli za shamba; ununuzi wa ardhii kwa ajili ya kilimo, mifugo na ufugaji wa samaki; zana unganishi; zana za kusindika mazao; na kutoa mikopo kwa vikundi vya umwagiliaji (Kiambatisho Na. 21). Vilevile, itakusanya asilimia 90 ya marejesho ya mikopo itakayokuwa imeiva ambayo ni kiasi cha Shilingi 5,508,291,668; na itaweka *mfumowa* TEHAMA ili kuboresha usimamizi wa mikopo.

#### *Huduma za Ugani*

199. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara itavipatia vitendea kazi (Vifaa vya TEHAMA na pikipiki) Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (WARCs) 24 vilivyopo katika mikoa 10 ya Geita, Morogoro, Simiyu, Dodoma, Songwe, Lindi, Tabora, Mwanza, Kigoma na Mtwara; Itajenga vitalu nyumba 10 katika WARC<sub>s</sub> 10 za mikoa ya Geita, Morogoro, Simiyu, Dodoma, Songwe, Lindi, Tabora, Mwanza, Kigoma na Mtwara

kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kilimo kwa vijana; itashirikiana na wadau wa kilimo kuhuisha na kuisambaza Miongozo sita (6) ya kuendesha na kusimamia huduma za ugani ili iendane na mahitaji ya sasa; itaendelea kutumia mifumo ya kielektronia katika kupeleka elimu ya kilimo kwa wakulima wapatao 1,275,217.

200. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itasajili watoa huduma za ugani 520 kwa njia ya mtandao; itaendelea kuratibu Maonesho ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) yatakayofanyika Kitaifa katika kanda ya ziwa mashariki Mkoani Simiyu katika uwanja wa Nyakabindi na katika kanda nyingine saba (7) ambazo ni Nzuguni – Dodoma kanda ya kati, Mwalimu J.K. Nyerere – Morogoro kanda ya mashariki, Ngongo – Lindi kanda ya kusini, John Mwakangale – Mbeya kanda ya nyanda za juu kusini, Thembi – Arusha kanda ya Kaskazini, Fatuma Mwasa – Tabora kanda ya magharibi na Nyamhongolo – Mwanza kanda Ziwa Magharibi.

201. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) kutoa mafunzo kwa wakulima viongozi 370, Maafisa Ugani 185, sekta binafsi 185 kutoka Halmashauri za Wilaya 185 na kuimarisha matumizi ya TEHAMA (M-Kilimo) ili kuwafikishia taarifa mbalimbali za kilimo na masoko. Pia, Wizara itashirikiana na SAGCOT na Wabia wake kutoa mafunzo ya matumizi ya Chokaa-Kilimo kwa wakulima 150 na Maafisa Ugani 500 kutoka mikoa ya Iringa, Njombe, Songwe na Mbeya; ili kudhibiti tindikali (soil acidity) katika udongo. Hii itaenda sambamba na upimaji udongo kwa mashamba ya wakulima hao.

#### *Uzalishaji wa Mazao ya Asili ya Biashara Zao la Kahawa*

202. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kuitia Bodi ya Kahawa itaongeza uzalishaji wa kahawa kutoka tani 55,979 mwaka 2019/2020 hadi tani 90,000 mwaka 2020/2021. Lengo hilo litafikiwa kwa kuongeza upatikanaji wa miche bora ya kahawa kutoka miche 7,059,835 mwaka 2019/2020 hadi miche 20,000,000 mwaka 2020/2021. Aidha, bodi

itahamasisha matumizi ya mbolea kwa wakulima ikiwemo kuongeza upatikanaji wa mikopo ya mbolea kwa kushirikiana na wadau, itaaniszha mashamba darasa 80 na kusambaza nakala 5,743 za vipeperushi vya kanuni za kilimo bora cha kahawa katika Halmashauri 69. Vilevile, Bodi itaendelea kusajili na kutoa vitambulisho kwa wakulima wa kahawa ili kurahisisha utoaji wa huduma.

203. *Mheshimiwa Spika*, Mambo mengine yatakayotekelezwa ni pamoja na kuimarishe vyama vya ushirika 400 kwa kutoa elimu ya masoko, kutangaza kahawa ya Tanzania katika masoko ya kimataifa, kuongeza soko la ndani kwa kuhamasisha unywaji wa kahawa ya ndani na kuandaa mikakati ya kutegeneza chapa ya bidhaa bora ya kahawa na kutangaza kahawa ya Tanzania katika masoko ya kimataifa ili kuongeza soko. Aidha, itahamasisha matumizi sahihi ya *Central Pulpuly Unit – CPU* ili kuongeza ubora wa kahawa, kuongeza thamani ya kahawa kwa asilimia 16, na kununua vifungashio bora vya kahawa.

#### Zao la Mkonge

204. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Bodi ya Mkonge imelenga kuongeza uzalishaji wa mkonge kutoka tani 35,551 mwaka 2019/2020 hadi kufikia tani 125,428 mwaka 2020/2021 na tija kutoka tani 1.1 hadi tani 2.5 kwa hekta. Aidha, itaaniszha vitalu vya mkonge katika Wilaya 5 za Kishapu, Bariadi, Meatu, Serengeti na Same ili kuongeza upatikanaji wa mbegu na kuongeza idadi ya wakulima wadogo wa mkonge kutoka 6,885 hadi kufikia 11,664.

205. *Mheshimiwa Spika*, katika jitihada za kuimarishe soko la mkonge, Bodi itaongeza wigo wa masoko mapya Afrika na Mashariki ya Kati ikiwa ni pamoja na kuongeza bidhaa za mkonge kutoka tani 5,701 hadi kufikia tani 11,500. Vilevile, itahamasisha matumizi ya bidhaa za mkonge ndani ya nchi vikiwemo vifungashio vitokanavyo na zao hilo kama vile magunia kwa ajili ya ufungashaji wa mazao ya kahawa, korosho, tumbaku, pamba na nafaka. Aidha, Bodi itahamasisha ujenzi wa viwanda 2 vya kutengeneza bidhaa

mpya za mkunge katika Wilaya za Korogwe na Handeni ili kumhahakishia mkulima kuwa na uhakika wa soko.

#### Zao la Pamba

*206. Mheshimiwa Spika*, Wizara ina mkakati wa miaka mitano unaolenga kuongeza uzalishaji wa pamba kutoka tani 348,775 mwaka 2019/2020 hadi tani 1,000,000 mwaka 2024/2025. Ili kufikia lengo hilo, Wizara kwa kushirikiana na TADB imeandaa mpango wa kufufua vinu saba (7) vya kuchambulia pamba (Ginneries) ili kuhakikisha pamba yote inayolimwa nchini inaongezwa thamani kabla ya kuuzwa nje ya nchi. Vinu hivyo ni pamoja na *Chato Cooperative Union* (Geita), *Kahama Cooperative Union* (Shinyanga), *Nyanza Cooperative Union* (Mwanza), *Mara Cooperative Union* (Mara), *Shinyanga regional Cooprative Union* (Sola – Shinyanga, Luguru – Simiyu na Masumbwe – Geita). Ufufuaji wa vinu hivyo utagharimu takribani Shilingi bilioni 19.9 na mtaji wa kuviedesha unakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 80. Aidha, Wizara itakamilisha taratibu za kisheria za kubadili umiliki wa vinu hivyo na kuunda upya mfumo wa uendeshaji wake.

*207. Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia bodi itatekeleza mkakati huo kwa kuongeza uzalishaji kutoka tani 348,882 mwaka 2019/2020 hadi tani 400,000 mwaka 2020/2021 ambapo itasambaza chupa 8,000,000 za viuadudu na vinyunyizi 20,000,000 moja kwa moja kwa wakulima kupitia AMCOS; kusambaza mbegu bora tani 18,318 aina ya UKM 08; kuhamasisha kanuni za kilimo bora; kutumia mfumo wa ununuzi wa pamoja wa viuadudu ili kuongeza upatikanaji na kupunguza bei.

#### Zao la Tumbaku

*208. Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku imepanga kuongeza uzalishaji kutoka tani 63,000 mwaka 2019/2020 hadi kufikia tani 65,000, tija kutoka tani 1.4 kwa hekta hadi kufikia tani 1.5 kwa hekta na ubora wa tumbaku kutoka asilimia 93 hadi asilimia 94. Aidha, mwongozo wa upandaji miti na kuchimba visima

utaandaliwa ili kutoa elimu ya kupanda na kutunza miti, kuhifadhi mazingira pamoja na kupata maji ya kumwagilia hususan wakati wa kiangazi. Vilevile, Wizara itaendelea kusajili wakulima wa tumbaku na kutoa vitambulisho. Katika kuimarisha soko la tumbaku, Wizara kwa kushirikiana na Bodi itaanlisha makampuni madogomadogo ya ndani kwa ajili ya kununua tumbaku ili kupunguza utegemezi wa makampuni makubwa.

#### Zao la Korosho

209. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Bodi ya Korosho itaongeza uzalishaji kutoka tani 232,000 mwaka 2019/2020 hadi tani 300,000 mwaka 2020/2021 na tija kutoka wastani wa kilo 10 za korosho ghafi kwa mti kwa mwaka hadi kufikia kilo 15 za korosho ghafi kwa mti kwa mwaka. Ili kufikia lengo hilo Bodi itaratibu na kusimamia usambazaji wa mbegu na miche bora ya mikorosho 15,000,000. Aidha, Bodi itanunua viuatilifu kwa mfumo wa pamoja na kusimamia usambazaji wa tani 30,000 za salfa na lita 350,000 za viuatilifu na kutoa mafunzo ya kilimo bora cha korosho pamoja na matumizi sahihi ya viuatilifu vya zao la korosho kwa wakulima na maafisa ugani.

210. *Mheshimiwa Spika*, Bodi pia itahamasisha kilimo cha mashamba makubwa ya pamoja (*block farming*) katika maeneo mapya yanayolima korosho ikiwa ni pamoja na Itigi, Ikungi, Nguruka, Kibondo, Ushetu, Mlele, Mpanda Vijijini, Mpwapwa na Kongwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji. Bodi pia itaendelea kusajili wakulima wa korosho na kutoa vitambulisho. Vilevile, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango itakamilisha uhakiki na malipo ya awamu ya pili kwa wazalishaji wa miche ya korosho kwa mikoa ya Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Songwe, Iringa na Njombe.

211. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Bodi inaendelea kutekeleza Mkakati ambao moja ya malengo ni kuongeza ubanguaji wa korosho kutoka asilimia 20 na kufikia asilimia 60 ya uzalishaji ifikapo 2023/2024. Katika mwaka 2020/2021, Bodi itahamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogovidogo kutoka viwanda 230 hadi 250 kupitia vikundi vya ubanguaji wa

korosho; viwanda vya kati vitano (5) vyenye uwezo wa kubangua tani 1,000 hadi 5,000 kwa mwaka; na kuanzisha viwanda vipyta viwili (2) vyenye uwezo wa kubangua korosho ghafi tani 5,000 kwa mwaka.

212. *Mheshimiwa Spika*, Bodi itaendelea kuimarisha masoko ya korosho kupitia majukwaa mbalimbali na kusimamia mfumo wa mauzo ya korosho kwa njia ya mtandao. Aidha, itaongeza wigo wa masoko mapya ya Korosho katika nchi za Marekani, Ulaya, China, UAE na nyingine Barani Afrika. Vilevile, Bodi itahamasisha matumizi ya korosho iliyobanguliwa katika masoko ya ndani.

#### Zao la Chai

213. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Bodi ya Chai imelenga kuongeza uzalishaji wa chai kavu kutoka tani 38,000 mwaka 2019/2020 hadi tani 40,000 mwaka 2020/2021 na kusimamia uongezwaji wa ubora wa majani mabichi ya chai kutoka asilimia 60 mwaka 2019/2020 hadi asilimia 70 mwaka 2020/2021. Katika kuongeza uzalishaji, Bodi itahamasisha ufufuaji wa mashamba makubwa ya chai yaliyotelekezwa katika Wilaya za Njombe, Lushoto, Bukoba, Muleba na Kilolo. Aidha, miche 1,000,000 ya chai kwa ajili ya wakulima wadogo itazalishwa sambamba na kuimarisha huduma za ugani kwa wakulima wadogo wa chai kwa kuongeza maafisa ugani wa TSHTDA kutoka 17 hadi 37.

214. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha soko la zao la chai, Wizara kupitia Bodi itaaniszha mnada wa chai (DSM) utakaoendeshwa kwa mfumo wa soko la bidhaa na kutambulika kimataifa. Uanzishwaji wa mnada huo utaitambulisha chai inayozalishwa nchini kwa mataifa ya nje, utaongeza bei ya chai kwa wakulima na kulongeza taifa mapato. Pia, Bodi itahuisha kanzidata ya wakulima wa chai ili kufahamu wadau wanaoingia katika kilimo cha chai kwa lengo la kuweka mipango endelevu.

#### Zao la Miwa

215. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Bodi ya Sukari imepanga kuongeza uzalishaji wa sukari

katika viwanda vilivyopo kutoka tani 298,948.61 mwaka 2019/2020 hadi tani 424,663 na hivyo kupunguza uingizwaji wa sukari nchini kutoka tani 207,439 mwaka 2019/2020 hadi tani 162,102. Aidha, tija kwa wakulima wadogo itaongezeka kutoka tani 50 kwa hekta mwaka 2019/2020 hadi tani 60 kwa hekta mwaka 2020/2021. Ongezeko hilo litatokana na uhamasishaji wa matumizi ya teknolojia za kilimo bora na uanzishwaji wa viwanda vikubwa, vyakati na vidogo. Aidha, viwanda vyana ndani vitahamasishwa ili vianze kuzalisha sukari ya viwandani takriban tani 50,000.

### Zao la Pareto

216. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kuititia Bodi ya Pareto imepanga kuongeza uzalishaji wa pareto kutoka tani 2,600 mwaka 2019/2020 hadi tani 2,800 mwaka 2020/2021 kwa kuhamasisha kanuni za kilimo bora. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na TARI-Uyole itaendelea kufanya utafiti wa aina 10 za mbegu bora ili kupata aina bora za pareto zitakazotoa kiwango kikubwa cha mavuno ya katika ya kilo 800-1500 na ubora (*Pyrethrin content*) kuanzia asilimia 1.7 hadi 2.1. Ili kuondoa udanganyifu katika ubora na kumlinda mkulima, Bodi itaweka mtaalam wa maabara katika kiwanda cha pareto Mufindi ili kuthibitisha kiwango cha sumu kutoka kwenye maua ya pareto.

### Mazao ya Chakula

217. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula yakiwemo mahindi, mpunga, mtama, uwele, muhogo, viazi, ngano, mikunde, migomba na mazao ya bustani. Katika mwaka 2020/2021 Wizara itasimamia upatikanaji wa pembejeo na matumizi ya kanuni za kilimo bora. Aidha, katika kujihakikishia usalama wa chakula, lishe na kuongeza wigo wa soko na ajira kwa watanzania, Wizara itatoa elimu kuhusu matumizi ya teknolojia za kupunguza upotewe na kuongeza thamani ya mazao kwa wadau katika mnyororo wa thamani wa mazao ya chakula katika Halmashauri 32 za Kanda za Ziwa, Kati na Kaskazini.

218. *Mheshimiwa Spika*, Wizara pia, itasambaza nakala 3,000 za Mkakati wa Kitaifa wa Kupunguza Upotevu wa Mazao Baada ya Kuvuna na nakala 320 za Mpango wa Utekelezaji katika Kanda za Ziwa, Kati na Kaskazini na kuendelea kufanya tathmini ya uzalishaji na upatikanaji wa chakula na kutoa taarifa ya hali ya chakula nchini. Maeneo mengine ni pamoa na utekelezaji Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Zao la Mpunga Awamu ya Pili – NRDS II (2019/2020 – 2029/2030).

219. *Mheshimiwa Spika*, Mahitaji ya ngano nchini kwa mwaka ni tani 1,000,000 na uzalishaji wa ngano kwa mwaka ni tani 60,000. Hali hii inapelekea kutegemea uagizaji wa ngano kutoka nje na hivyo kupoteza fedha nyngi za kigeni. Katika kukabiliana na hali hiyo, Wizara itaendelea kuhamasisha kilimo cha ngano nchini kwa kuwa tafiti zinaonesha kwamba mashamba ya mpunga baada ya kuvunwa yanaweza kulimwa ngano na kuvuna ndani ya kipindi cha miezi mitatu.

220. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha zao la shayiri nchini, Wizara itawasilisha mapendekezo kwa Wizara ya Fedha na Mipango ya kupunguza kodi kwa kimea kinachozalishwa na kusindikwa nchini ili kuongeza uzalishaji wa shayiri na viwanda vinavyosindika shayiri hapa nchini. Vilevile, Wizara itahakikisha kuwa mwekezaji anayemiliki kinu cha kusindika kimea kilichopo Kilimanjaro anakifufua au anapewa mwekezaji mwininge ili kiweze kusindika kimea kinachozalishwa nchini na hivyo kuwanufaisha wakulima na kupunguza uagizaji wa shayiri kutoka nje.

#### *Mazao ya Bustani*

221. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na TAHA itaendelea kuhamasisha kilimo cha mazao ya bustani, kutathmini na kuainisha maabara zitakazofanyiwa maboresho ili ziweze kupima ubora wa mazao ya bustani kwa kukidhi viwango vya kimataifa (*International Accreditation*). Hatua hii itawezesha mazao ya bustani kushindana katika masoko ya kimataifa, kumnufaisha mkulima na kuongeza mapato yatokanayo na mauzo nje ya nchi.

222. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itasimika miundombinu ya kuhifadhi bidhaa za mazao ya bustani katika kiwanja cha ndege cha Songwe ili kurahisisha usafirishaji wa mazao hayo katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi kutangaza mazao ya bustani ikiwa ni pamoja na maonesho ya kimataifa na kampeni maalum za kutangaza bidhaa za Tanzania. Vilevile, Wizara itahamasisha uanzishwaji wa ushirika katika mazao ya bustani ili kurahisisha utoaji wa huduma ikiwemo ugani, pembejeo, mitaji, teknolojia bora za kupunguza upotevu baada ya kuvuna na kuwaunganisha wakulima na masoko.

#### 5.8 Kuimarisha Vituo vya Utafiti, Vyuo vya Mafunzo na Vituo vya Wakulima

##### *Kuimarisha Vituo vya Utafiti*

223. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara itakarabati ofisi na kuvipatia vifaa muhimu vituo vitano (5) vya utafiti vya Ukiriguru, Ilionga, Kihinga, Selian na Tumbi; itaboresha miundombinu ya mashamba ya uzalishaji wa mbegu kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora kwa Vituo vya Ilionga, Uyole, Ukiriguru, Selian na Kihinga; itaboresha miundombinu ya umwagiliaji ya Vituo vya Utafiti vya Ilionga, Naliendele, Ukiriguru na miundombinu ya uhifadhi wa mbegu katika Vituo vya Uyole, Ilionga na Seliani; itajenga kituo cha TARI Kihinga Kigoma kwa ajili ya utafiti na kuendeleza zao la michikichi ikiwa ni pamoja na kujenga miundombinu ya utafiti na uzalishaji wa miche na vitendea kazi kwa kununua matreka saba na zana zake; itajenga Makao Makuu ya TARI katika kiwanja chake cha Chamwino Dodoma; itawajengea uwezo watafiti kwa kuwapa mafunzo ya muda mrefu ambapo watafiti watano (5) wataanza masomo katika Shahada ya Kwanza, 10 Shahada ya Uzamili, na watano (5) Shahada ya Uzamivu.

224. *Mheshimiwa Spika* TARI itafanya utafiti na kugundua teknolojia tano (5) za usindikaji wa mazao ya korosho, muhogo, viazi vitamu na zabibu; itanunua na kusimika mashine ya kufanya utafiti wa usindikaji wa korosho yenye

uwezo wa kusindika tani za korosho 1,800 kwa mwaka katika kituo cha TARI Naliendele; na itaandaa mizania ya mazao ya mpunga, mahindi na alizeti ili kutoa mapendekezo kwa wakulima juu ya gharama na faida inayopatikana katika kutumia teknolojia ukilinganisha na kilimo cha mazoea.

#### *Vyuo na Vituo vya Mafunzo kwa Wakulima*

225. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara itadahili wanafunzi 2,600 ngazi ya Astashahada na Stashahada katika vyuo 14 vya mafunzo ya kilimo; itaendelea na ukarabati wa miundombinu chakavu ya vyuo vya MATI Ukitriguru, Ilionga, Mlingano, Maruku, Tumbi, Igurusu, Mtwaru, HORTI Tengeru na KATC; itanunua vifaa vya umwagiliaji (*irrigation pump, electrical/solar panel and main delivery line*) na kuweka mifumo ya teknolojia hizo kwa ajili ya shamba la mafunzo ya teknolojia za umwagiliaji MATI Igurusu; itawezesha mafunzo kwa watumishi 11 ngazi ya shahada ya uzamili na watumishi saba (7) ngazi ya shahada ya kwanza katika Vyuo vikuu vya hapa nchini.

226. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itawezesha mafunzo ya muda mfupi kwa wakufunzi 50 kuhusu mbinu za kufundishia ili kuwajengea wakufunzi umahiri wa kufundisha kwa ufanisi zaidi; itahuisha mitaala miwili (2) iliyopitwa na wakati ili iweze kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia; na itawezesha upimaji wa ardhi ya vyuo vya mafunzo ya kilimo viwili (2) na kuvipatia Hatimiliki. Wizara kwa kushirikiana na SAGCOT na wabia wa zao la viazi mviringo, itazalisha tani 1,090 za mbegu bora za viazi mviringo na kutoa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji wa zao hilo kwa wakulima 2,500. Aidha, aina mpya zipatazo 10 za mbegu bora zitathibitishwa.

#### 5.9 Kuimarisha Huduma za Upimaji wa Matabaka na Ubora wa Udongo

227. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara itahakiki na kuandaa ramani za udongo za kiikolojia katika mashamba ya uwekezaji na wakulima wadogo katika mikoa nane (8) ya Morogoro, Singida, Katavi, Kigoma, Lindi, Rukwa,

Tabora na Mtwara na kuimarisha kanzidata ya ardhi ya kilimo; itafanya utafiti ili kugundua teknolojia tano (5) za rutuba ya udongo na hifadhi ya ardhi na kuzisambaza kwa wakulima ikiwa ni pamoa na kutoa mapendekezo ya matumizi ya aina mbili za mbolea (OCP Fertilizer), hifadhi ya udongo na maji na teknolojia tatu (3) za viwango vya matumizi ya mbolea; itapima sampuli 4,000 za udongo kutoka katika maeneo mbalimbali ili kubaini na kupendekeza viwango vya matumizi ya mbolea katika maeneo husika; na itaboresha ramani za udongo zilizopo zinazoonesha virutubishi vya *Carbon* na *PH* kwa lengo la kuongeza taarifa za virutubisho vingine na kusambaza katika Wilaya zote za Tanzania. Ramani hizo zitasaidia kutoa mapendekezo ya matumizi ya aina na viwango vya mbolea.

### 5.10 Kuimarisha Masuala Mtambuka katika Kilimo

#### *Usimamizi wa Rasilimali Watu*

228. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka 2020/2021 Wizara imepanga kuajiri watumishi wapya 245, kupandisha vyeo watumishi 351 na kutoa mafunzo kwa watumishi 120.

#### *Ushiriki Wa Vijana Katika Kilimo*

229. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na Wadau itafuatilia utekelezaji wa maazimio ya makongamano saba (7) ya vijana yaliyofanyika mwaka 2019/2020; itaanza mapitio ya Mkakati wa Vijana kushiriki katika kilimo kwa kuzingatia masuala yaliyoibuliwa katika makongamano; na itashirikiana na SUGECO kutafuta wafadhili watakaowezesha kuwapeleka vijana 150 nchini Marekani na 100 Israel kwa ajili ya kuongeza ujuzi zaidi. Aidha, vijana 400 watapata mafunzo ya kilimo biashara na ujasiliamali katika kituo cha Mkongo Wilayani Rufiji.

#### *Lishe*

230. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara itashirikiana na wadau kuendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Lishe na kukamilisha Mkakati wa Kutekeleza Lishe

Katika Sekta ya Kilimo. Mkakati huu utawezesha sekta kupunguza tatizo la utapiamlo na kuchangia katika kufikia malengo ya lishe nchini, kikanda na kimataifa ambayo ni pamoja na udumavu kutoka asilimia 32 mwaka 2018 hadi asilimia 25 mwaka 2021; na itaendelea kuhamasisha uzalishaji na kuhimiza matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubisho yakiwemo maharage lishe, mahindi lishe na viazi lishe ili kuimarisha hali ya lishe katika mikoa ya Ruvuma, Kagera, Mbeya, Songwe, Njombe, Dodoma, Morogoro, Mtwara, Rukwa na Tanga ambayo imebainika kuwa na changamoto ya lishe.

*Jinsia*

231. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa jinsia itaendelea kuhusisha masuala ya jinsia katika shughuli za kilimo ambapo jitihada zitawekwa zaidi katika kuhakikisha bajeti, mipango, mikakati na miradi ya kuendeleza kilimo inazingatia na kuakisi usawa wa kijinsia.

*Mazingira*

232. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kupunguza athari za mazingira zinazotokana na shughuli za kilimo. Katika mwaka 2020/2021, Wizara itahimiza matumizi ya zana za kilimo hifadhi kwa kuhamasisha wasambazaji na wabunifu wa teknolojia hizo kubuni, kutengeneza na kusambaza kwa wakulima ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Wizara itaendelea kusambaza Mwongozo wa Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa wataalamu kwa ngazi ya Wilaya katika Halmashauri za Wilaya 90. Vilevile, itawajengea uwezo wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo kinachohifadhi mazingira na kuwasaidia kuandaa mipango ya usimamizi wa mazingira na jamii katika vijiji 21 vinavyozunguka Ziwa Manyara.

*VVU na UKIMWI*

233. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa afya itaendelea kutoa elimu

kuhusu VVU na UKIMWI kwa wafanyakazi wa Wizara ili kupunguza na kuzuia maambukizi mapya kwa watumishi wa Wizara. Vilevile, Wizara itaendelea kuwahudumia watumishi walioathirika na kuhamasisha watumishi kupima afya zao ili kujua hali zao. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa Watumishi kuhusu ugonjwa wa COVID-19 na namna bora ya kujikinga na ugonjwa huo.

## **6. SHUKRANI**

234. *Mheshimiwa Spika*, kabla sijamaliza hotuba yangu naomba nitoe shukrani za dhati kwa taasisi, makundi, na wadau mbalimbali tunaoshirikiana katika kuendeleza kilimo cha Tanzania. Kwanza, ninawashukuru kwa dhati Wakurugenzi wa Idara na Wakuu wa Vitengo; Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; watumishi wote wa Wizara; na wadau wa Sekta ya Kilimo kwa juhudhi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2019/2020 pamoja na kuandaa Hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba, nitaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2020/2021.

235. *Mheshimiwa Spika*, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia Wizara katika juhudhi za kuendeleza kilimo. Nachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Japan, Marekani, Uingereza, Ireland, Malaysia, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Misri, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uhlanzi, Vietnam, Canada na Poland. Ninayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, ENABEL, GIZ, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, ILRI na CABI. Nyingine ni EAC, SADC, AVRDC, AGRA, KILIMO TRUST, CIP, CIAT/PABRA, UNEP, WARDA, Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani (DLCO-EA) na HELVETAS. Wadau wengine ni Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu (IRLCO-CSA), Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust, Rockefeller Foundation, Clinton Foundation, Aga Khan Foundation, Unilever, Kampuni za TAHA fresh Limited, Africado

*na Rugwe Avocado Company na Asasi zisizo za kiserikali nyingi ambazo hatuwezi kuzitaja zote hapa.*

236. *Mheshimiwa Spika*, natoa shukrani za wakulima wote nchi nzima kwa kazi kubwa wanazofanya kuendeleza kilimo nchini. Ni wazi kuwa mafanikio haya makubwa ya kilimo yanatokana na jududi na ushirikiano mkubwa na serikali. Kipeke nirudie kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Vwawa kwa namna wanavyoniunga mkono na kunipa ushirikiano. Aidha, napenda kuwahimiza kufanya kazi kwa bidii ili kupata mafanikio katika maisha yao. Naomba wote watumbue kuwa kilimo ni maisha, uchumi, biashara, viwanda na ajira.

## **7. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021**

### **7.1 Makusanyo ya Maduhuli**

237. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi 5,793,400,000 kutokana na ada za ukaguzi wa mazao yanayouzwa nje ya nchi au kuingizwa nchini, uuzaaji wa nyaraka za zabuni, ukodishaji wa mitambo ya Tume ya Umwagiliaji. Kati ya fedha hizo, Shilingi 3,480,000,000 zitakusanywa katika Fungu 43 na Shilingi 2,313,400,000 zitakusanywa kwenye Fungu Na.5.

### **7.2 Fedha kwa Mafungu yote (43,24 na 05)**

238. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufuliidhinishe jumla ya Shilingi 229,839,808,000 kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 kama ifuatavyo;

#### **7.2.1 Fedha kwa Fungu 43**

239. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 202,504,117,000 kupitia Fungu 43 kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 137,273,144,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi 82,180,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 55,093,144,000 ni

fedha za nje. Aidha, Shilingi 65,230,973,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Shilingi 43,599,187,000 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 21,631,786,450 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

#### 7.2.2 Fedha kwa Fungu 05

240. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya Shilingi 17,726,845,000 zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi 12,801,180,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi 3,000,000,000 ni fedha za Ndani na Shilingi 9,801,180,000 ni fedha za Nje. Aidha, kati ya fedha zinazoombwwa, Shilingi 4,925,665,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi 4,040,481,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Tume na Shilingi 885,184,000 ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo.

#### 7.2.3 Fedha kwa Fungu 24

241. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya Shilingi 9,608,846,000 zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi 7,059,837,000 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 2,549,009,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

242. *Mheshimiwa Spika*, hotuba hii pia inapatikana katikatovutiyawizara: [www.kilimo.go.tz](http://www.kilimo.go.tz)

### 8. HITIMISHO

243. *Mheshimiwa Spika*, NAOMBA KUTOA HOJA.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana kwa hotuba hii nzuri, nzito iliyosheheni mambo mengi sana. Waheshimiwa Wabunge itabidi muipitie kwa umakini sana na bahati nzuri mnazo nakala zake kwenye tablets zenu itawasaidia sana katika kuchangia hoja hii ambayo Mheshimwa waziri ameiweka mezani. (*Makofii*)

Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati. Kabla Mwenyekiti wa Kamati hajaanza niwakaribishe Waheshimiwa Naibu Mawaziri kama wapo kule Msekwa na kadhalika wanaoweza baadhi yao wakajongea hapa kuongezaongeza kidogo. Karibu sana Mwenyekiti.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya ya kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. Nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa ya kuwasilisha ripoti inayohusu taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa kazi nzuri unayoifanya hapa Bungeni kwa kuliongoza Bunge lako hili tukufu kwa weledi mkubwa na hatua unazozichukua za kupambana na janga kubwa la *Corona*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ya kizalendo anayoifanya katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kutoa pole kwa kifo cha ndugu yetu Mheshimiwa Balozi Augustine Mahige aliyetangulia mbele ya haki. Bwana ametoa na Bwana ametwaa jina la Bwana lihimidiwe.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu katika jimbo la Mufindi Kaskazini kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwataki kila kheri Waislam popote duniani katika mfungo wa mwenzi wa Ramadhani. Ramadhani Kareem.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yetu hii ya Kamati iingie kama ilivyo kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inafafanua mambo matano yafuatayo: -

(i) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020;

(ii) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020;

(iii) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020;

(iv) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021; na

Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021;

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipochambua maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo takribani tisa. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Kamati imeridhishwa kwa namna Serikali ilivyozingatia na kutekeleza ushauri wa Kamati. Aidha, yapo masuala kadhaa yaliyotolewa ushauri lakini hadi Kamati inaandaa taarifa hii bado utekelezaji wake umekuwa siyo wa kuridhisha. Baadhi ya hoja za Kamati ambazo hazijanyiwa kazi ni kama zilivyoainishwa katika kipengele namba moja mpaka nne.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Kilimo - Fungu 43, liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 208.044 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 64.467 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 143.577 ni Fedha za Maendeleo, ambapo shilingi bilioni 82 zilikuwa ni fedha za ndani na bilioni 64.577 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kufikia Februari, 2020 Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotolewa ni shilingi bilioni 35.583 ambazo ni sawa na asilimilia 55 ya kiasi kilichoidhinishwa. Kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa zilikuwa ni shilingi bilioni 21.414 sawa na asilimia 19.92 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa na kutumika ni shilingi bilioni 5.60 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 15.454 ni fedha za nje. Aidha, fedha za ndani za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa ni asilimia 49 ya fedha zillyoidhinishwa na fedha za nje zilizotolewa ni asilimia 9 ya bajeti iliyyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kutoa asilimia 99 ya fedha za ndani kwenye Miradi ya Maendeleo ikilinganishwa na asilimia 9 zilizotolewa kutoka vyanzo vya nje. Mwenendo huu unaonyesha utayari wa Serikali kujitegemea katika kupeleka maendeleo kwa wananchi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya maduhuli. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Kilimo, Fungu 43 ilikadiriwa kukusanya mapato ya shilingi bilioni 3.472. Hadi kufikia Februari, 2020 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 2.376 ambayo ni sawa na asilimia 68.44 ya malengo ya ukusanyaji. Kwa mwaka wa fedha uliomalizika ukusanyaji wa maduhuli umeshuka kwa takribani asilimia 4. Kamati imesikitishwa kwa kushuka kwa makusanyo ya maduhuli yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Fungu 24. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Fungu 24, liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 8.327 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha

hizo shilingi bilioni 4.578 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Tume na Ushirika na shilingi bilioni 1.548 ni mishahara ya watumishi *COWASCO*. Aidha, bajeti kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Tume ya Ushirika ni shilingi bilioni 1.548 na shilingi milioni 650 ni kwa ajili ya *COWASCO*.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Tume ya Umwagiliaji, Fungu 5 iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 37.485 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.983 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 32.501 ni fedha za maendeleo ambapo shilingi bilioni 3 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 29.50 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2020, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi bilioni 3.671 fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 14.6 na hakuna fedha yoyote ya ndani iliyotolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kamati iliamini kwamba kilimo cha umwagiliaji kingesaidia kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa malighafi za viwanda pamoja na kuongzeza fedha za kigeni ambazo zingetokana na mauzo ya bidhaa za kilimo kuuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya maduhuli. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Fungu 5 ilikadiria kukusanya shilingi milioni 15 kutoka kwenye vyanzo vya ndani. Hadi kufikia Februari 2020, Tume ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi milioni 129 ambayo ni sawa na asilimia 860.59 ya malengo ya ukusanyaji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha za ndani. Ili kutekeleza ipasavyo matakwa ya Kanuni ya 99, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Mwanza na Kagera. Katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea taasisi za sekta binafsi zinazojishughulisha na kilimo kwa ajili ya kutathmini utekelezaji wa Sera ya Ushirikisho wa Sekta Binafsi (*Public Private Partnership*) katika kukuza uchumi kuititia kilimo. Katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea na

kukagua uwekezaji katika maeneo kadhaa kama yalivyoainishwa katika taarifa ya Kamati. Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini mafanikio na changamoto mbalimbali kama yalivyoainishwa katika taarifa ya Kamati mliyopewa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa bajeti na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati iipokea na kuchambua mpango wa bajeti wa Wizara ya Kilimo na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2020/2021 tarehe 25 mpaka 26 Machi, 2020. Mpango ambao umeandaliwa kwa kuzingatia matakwa na miongozo kama ilivyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa mafungu yote ya Wizara ni kama yalivyoainishwa katika taarifa mliyopewa.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Uchambuzi wa bajeti wa Wizara ya Kilimo unajumuisha mafungu matatu ambayo ni Fungu 43 - Wizara ya Kilimo; Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Fungu 5 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo kupitia Fungu 43 inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.202,504,117,000; Fungu 24 linaomba kuidhinishiwa Sh.9,608,846,000; na Fungu 5 linaomba kuidhinishiwa Sh.17,726,800,045. Kwa ujumla, Wizara ya Kilimo kupitia mafungu yote matatu inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.229,339,800,008. Aidha, Wizara kwa kupitia Fungu 43 na Fungu 5 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 inatarajia kukusanya jumla ya maduhuli kiasi cha Sh.16,281,800,080.

Mheshimiwa Spika, tathimini ya malengo kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, mpango wa bajeti wa Wizara ulijielekeza kwenye kilimo kitakachohakikisha usalama wa chakula ili kukabiliana na tatizo la njaa na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda. Kamati katika tathmini yake imebaini changamoto mbalimbali zinazoweza kukwamisha utekelezaji wa malengo

ya Wizara. Mathalani athari ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu unaosababishwa na *virus* vya Corona, *Covid- 19* kwenye sekta ya kilimo; kuchelewa kutolewa kwa dhamana ya Serikali kwenye miradi mikuba ya uwekezaji kwa makampuni ya sekta ya binafsi; na ukosefu wa umeme wa uhakika na athari zake katika uchumi wa viwanda na kilimo.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati. Ili kuweka kumbukumbu rasmi, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa kipindi cha uhai wa Bunge la Kumi na Moja, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji imeshatoa ushauri mbalimbali utakaosaidia kuinua sekta ya kilimo nchini. Ukrejea Taarifa Rasmi za Bunge utakuta maeneo ambayo yamewahi kutolewa ushauri yamo na yanaainishwa katika taarifa kipengele (a) mpaka (o).

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niwasilishe maoni na ushauri wa Kamati yaliyotokana na Kamati kufanya uchambuzi kwenye maombi ya fedha kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021, kama ifuatavyo:-

(1) Ili kutekeleza kwa vitendo sera ya ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza uchumi pamoa na azma ya Serikali ya uchumi wa viwanda, Kamati inaishauri Serikali kutumia wataalam wake kuharakisha maamuzi ya kutoa dhamana kwa ajili ya viwanda viliviyokidhi matakwa ya Sheria ya *Government Loans, Gurantees, Grants Act, 1974 (Amendment) Act, 2003* ili kuwezesha viwanda ambavyo vimekidhi matakwa ya kisheria kupata mikopo kwa wakati. Hatua hizi madhubuti zitasaidia kuwezesha viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji.

(2) Katika kukabiliana na athari ya janga la ugonjwa wa Homa ya Mapafu unaosababishwa na *virus* vya Corona, *Covid- 19* na kupelekea shughuli za kilimo kuathirika kwa kiasi kikubwa Serikali inapaswa kusaidia kwa kutoa ruzuku kwa wakulima, kuangalia uwezekano wa kupunguza na kuondoa riba za mikopo kuititia taasisi za fedha au kuongeza muda wa kulipa mikopo iliyokwishatolewa ili kuwezesha wakulima wa kilimo kuendelea kuzalisha. Aidha, ni vyema Serikali

ikachukua taha dhari kwa kuweka akiba ya chakula kwa kuwa upo uwezekano wa nchi nyngi duniani kukabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula.

(3) Ili kukabiliana na changamoto za muda mrefu za uhaba wa sukari nchini, ni vyema Serikali kufanya mapitio ya Sheria ya Tasnia ya Sukari ya 2001 (*Sugar Industry Act 2001*) ili kubaini pamoja na mambo mengine mapungufu ya sheria yanayokwamisha benki za ndani na za nje kushindwa kutoa mikopo kwa viwanda vya sukari kwa kuhofia Serikali kuendelea kutoa vibali kwa wafanyabiashara kuagiza sukari nje ya nchi ambayo huuzwa kwa bei nafuu kuliko sukari zinazozalishwa hapa nchini.

(4) Ili kukabiliana na changamoto ya muda mrefu ya uhaba wa mbolea nchini na kwa madhumuni ya utekelezaji wa sera ya uchumi wa viwanda, Kamati Inashauri ili kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha mbolea Serikali itekeleze yafuatayo:-

(i) Serikali ianzishe mkakati wa makusudi kwa kupitia Maafisa Ugani kuhamasisha wakulima kutumia mbolea zilizotengenezwa nchini zenyne mchanganyiko wa virutubisho vinavyohitajika katika udongo na mimea kwa madhumuni ya kusaidia wakulima katika kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo.

(ii) Kabla ya kutoa vibali vya kuagiza mbolea nje ya nchi, ni vyema tathmini ikafanyika ili kufahamu mbolea inayozalishwa nchini na pungufu ndiyo iagizwe. Utaratibu unaopendekezwa kutumika hapa ni kama ule uliopo kwenye sekta ndogo ya sukari ambapo sukari inayozalishwa nchini hutumika kwanza kabla ya kuagiza sukari iliyopungua.

(iii) Kanuni za Mfumo wa Uagizaji wa Mbolea ya *Bulk Procurement* zifanyiwe marekebisho ili zitoe kipaumbele na kumlinda mzalishaji wa mbolea wa ndani tofauti na ilivyo sasa ambayo muagizaji anapewa upendeleo.

(iv) Baadhi ya kodi na tozo zinazolipwa na watengenezaji wa mbolea hapa nchini hazilipwi na waagizaji wa mbolea. Suala hili linasababisha ongezeko la gharama ya uzalishaji na kuleta ushindani usio sawa kwenye sekta na kumuumiza mkulima. Kwa mfano, VAT inatozwa kwa mtengenezaji wa mbolea wa ndani wakati muagizaji wa mbolea hatozwi kodi yoyote. Hivyo, Kamati inashauri Serikali itathmini kodi hii na kumuondolea mzalishaji na kuwa VAT zero rate.

(v) Ili kukabiliana na changamoto inayolalamikiwa na Wizara mbalimbali kuhusu ucheleweshaji wa maamuzi ya msingi ya kitaifa yanayotegemewa kufanywa Wizara ya Fedha na Mipango, Kamati inashauri Serikali kutafakari kwa kina suala hili. Kwa mfano Benki ya Maendeleo ya Kilimo inatoa mikopo kwa wakulima ilhali Waziri mwenye dhamana ya Kilimo hana mamlaka juu ya benki hii. Vilevile soko la bidhaa Tanzania ambalo linahusika moja kwa moja na mauzo ya bidhaa za nafaka kwa njia ya kielektroniki liko chini ya Wizara ya Fedha na Waziri mwenye dhamana na kilimo hana mamlaka juu yake.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyevitii wa Bunge kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkituongoza kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge letu la Kumi na Moja na kuliwezesha Bunge letu kutimiza wajibu wake wa kuisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi kwa mujibu wa Katiba.

Aidha, nawashukuru kwa dhati wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa katika kipindi chote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake. Kwa ajili ya kumbukumbu ya Bunge lako la Kumi na Moja, naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa za Bunge (*Hansard*) kama yalivyoorodheshwa kwenye taarifa ya Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hiki ni kipindi cha mwisho katika Bunge hili la Kumi na Moja, napenda kutumia fursa hii kuwatachia wajumbe wa Kamati, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kila la kheri katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2020. Panapo majaliwa ya Mwenyezi Mungu aturejesha sote kama tulivyo katika Bunge la Kumi na Mbili ili kuendelea kuendesha gurudumu la ujenzi wa Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba; Katibu Mkuu, Ndugu Gerald Musabila Kusaya; Naibu Katibu Mkuu Profesa Siza Donald Tumbo pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano walioipatia Kamati yangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai; Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati, ndugu yangu Michael Chikokoto; Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati, Ndugu Gerald Magili, kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kwa namna ya kipekee nashukuru Sekretarieti ya Kamati yangu ambayo ni Ndugu Vigili Mtui, Ndugu Rachel Nyega na Ndugu Jane Ndulesi kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa katika hoja ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makof*)

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA  
MAJI TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI  
YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020  
PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA  
WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

---

### 1.0 MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

#### 1.1. Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Kilimo ambayo ina mafungu matatu ambayo ni Fungu 43 (Wizara ya Kilimo), Fungu 24 (Tume ya Maendeleo ya Ushirika) na Fungu 05 (Tume ya Taifa ya Umwagiliaji).

#### 1.2. Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia maelezo hayo ya utangulizi, Taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yafuatayo: -

- a) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;
- b) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

- c) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.
- d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na
- e) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

## **SEHEMU YA PILI**

---

### **2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipochambua maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo takribani tisa (9). Aidha, Kamati ilipokuwa inatekeleza majukumu yake ilitoa maoni mengine licha ya hayo yaliyotolewa wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, Kamati imeridhishwa kwa namna Serikali ilivyozingatia na kutekeleza ushauri wa Kamati. Aidha, yapo maswala kadhaa yaliyotolewa ushauri lakini hadi Kamati inaandaa Taarifa hii bado utekelezaji wake umekuwa sio wa kuridhisha. Sehemu hii itabainisha baadhi ya hoja za Kamati ambazo hazikufanyiwa kazi. Kamati ilishauri: -

- i) Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu na za kisheria wahuksika waliobainika kuingiza nchini pembejeo zisizo na ubora na kupelekea madhara kwenye uzalishaji wa korosho katika msimu wa mwaka 2018/2019.
- ii) Serikali kuwa na Mipango ya muda mrefu na muda mfupi wa kujenga maghala ya kuhifadhia korosho;
- iii) Serikali ikamilishe malipo yaliyosalia kwa wakulima wa korosho ambao bado hawajalipwa; na

iv) Kupitia Sera ya Kilimo ya Mwaka 2013 pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Kilimo.

## **2.1 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 5 ulijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika na eneo la ukusanywaji maduhuli kwa kulinganisha na makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanya hadi mwezi Februari, 2020.

### **2.1.1 WIZARA YA KILIMO - FUNGU 43**

#### **a) Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Kilimo - **Fungu 43**, liliidhinishiwa jumla ya shilingi **208,044,783,140:00** kati ya fedha hizo shilingi **64,467,747,000.00** ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi **143,577,036,140:00** ni Fedha za Maendeleo, ambapo shilingi **82,000,000,000:00** zilikuwa ni Fedha za Ndani na **61,577,036,140:00** ni Fedha za Nje.

#### **b) Mwenendo wa utoaji Fedha zilizoidhinishwa**

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2020 fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotolewa ni shilingi **35,583,620,455.00** ambazo ni sawa na **asilimilia 55 %** ya kiasi kilichoidhinishwa. Kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa zilikuwa shilingi **21,414,787,233.00** sawa na **asilimia 14.92%** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa na kutumika ni shilingi **5,960,000,000:00** ni Fedha za Ndani na shilingi **15,454,787,233:00** ni Fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika**, japokuwa Fedha za Miradi ya Maendeleo za Ndani zilizotolewa ni chini ya **asilimia 50** hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kutoa **asilimia 49** ya Fedha za Ndani kwenye Miradi ya Maendeleo ikilinganishwa na

**asilimia 9** zilizotolewa kutoka vyanzo nya nje. Mwenendo huu unaonyesha utayari wa Serikali kujitegemea katika kupeleka maendeleo kwa wananchi wake. Aidha, Kamati inasisisitiza umuhimu wa fedha zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge kutolewa kama zilivyoidhinishwa na kwa wakati.

### c) Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Kilimo Fungu 43 ilikadiria kukusanya Mapato ya shilingi **3,472,515,000:00**. Hadi kufikia Februari 2020, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **2,376,509,461:00** ambayo ni sawa na **asilimia 68.44** ya malengo ya ukusanyaji. Kwa Mwaka wa Fedha unaomalizika ukusanyaji wa maduhuli umeshuka kwa takribani **asilimia 4**, Kamati imesikitishwa na kushuka kwa makusanyo ya maduhuli yaliyokusudiwa.

#### 2.1.2 TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA - FUNGU 24

##### a) Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa na kutolewa

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Tume ya Maendeleo ya Ushirika - **Fungu 24** liliidhinishwa jumla ya shilingi **8,327,070,000:00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kati ya fedha hizo, shilingi **4,578,420,000:00** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Tume na shilingi **1,548,950,000:00** ni mishahara ya Watumishi wa COASCO. Aidha, bajeti kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Tume ya Ushirika ni shilingi **1,549,009,000:00** na shilingi **650,691,000:00** zitatumwiwa na COASCO.

#### 2.1.3 TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI - FUNGU 05

##### a) Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa na kutolewa

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - **Fungu 05**, liliidhinishwa jumla ya shilingi **37,485,090,830.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi **4,983,628,217:00** ni Fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi

**32,501,462,613:00** ni Fedha za Maendeleo, ambapo shilingi **3,000,000,000.00** ni Fedha za Ndani na **29,501,462,613:00** ni Fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Februali 2020, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **3,671,040,022.25:00** Fedha za Nje kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambayo ni sawa na **asilimia 14.6** na hakuna fedha yoyote ya ndani iliyotolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejiliza kwa nini kila mara inaishauri Serikali kupeleka fedha za ndani kwenye Tume ya Umwagiliaji kwa ajili ya kuhakikisha Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji unatekelezwa lakini hakuna utekelezaji wa jambo hili?

**Mheshimiwa Spika**, tathimini ya Kamati imebaini kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo hakuna fedha za ndani za miradi ya maendeleo zinazotolewa kutokana na sababu mbalimbali zifuatazo: -

- (i) Kwa sasa nchi ina utoshelevu wa chakula kwa zaidi ya **asilimia 119**.
- (ii) Kwa muda mrefu kama nchi tumekuwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa masoko ya uhakika ya bidhaa za kilimo nje ya nchi.
- (iii) Kukosekana kwa viwanda vya kutosha kwa ajili ya kuchakata mazao ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kwamba hali hii imepekelea Serikali kutoona haja ya kutoa fedha za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwani lengo la kilimo cha umwagiliaji ni kuhakikisha usalama wa chakula pamoja na kuongeza uzalishaji wakati uzalishaji uliopo haujatumika ipasavyo. Aidha, hapo awali Kamati ili amini kwamba kilimo cha umwagiliaji kingesaidia kuhakikisha upatikanaji wa

uhakika wa malighafi za viwanda pamoja na kuongeza fedha za kigeni ambazo zingetokana na mauzo ya bidhaa za kilimo kuuzwa nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia tahimini hii Kamati inaishauri Serikali kuwa ili kutekeleza kwa vitendo kilimo cha umwagiliaji ni lazima kuwepo kwa vichochoeo vya msingi vya kuongeza uzalishaji ambavyo ni kuanzisha na kuendeleza viwanda kwa ajili ya kuchakata mazao ya kilimo pamoja na kupata masoko ya uhakika ili bidhaa za kilimo ziweze kuuzwa nje ya nchi.

### **b) Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - **Fungu 05** ilikadiria kukusanya Mapato ya shilingi **15,000,000.00** kutoka kwenye vyanzo vya ndani. Hadi kufikia Februari, 2020 Tume illikuwa imekusanya jumla ya shilingi **129,087,868:50** ambayo ni sawa na **asilimia 860.59 %** ya malengo ya ukusanyaji. Ongezeko hili limetokana na mapato yaliyotokana na chanzo kipycha ukodishaji wa mitambo iliyonunuliwa katika Mwaka wa fedha 2018/2019 na 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza ongezeko kubwa la ukusanyaji wa madhuli, hatua hii inadhihirisha kuwa endapo Serikali itawekeza vya kutosha katika sekta mbalimbali hakuna shaka kwamba tija nayo itaongezeka.

## **2.2 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGWEWA FEDHA KWA MWAKA 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 98(1) inaitaka Kamati kufanya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. Msingi wa Kamati kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha ni kufanya ukaguzi wa tathimini halisi ya fedha iliyotumika (*Value for Money*) na namna miradi iliyotekelawa inavyonufaisha wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza ipasavyo matakwa ya Kanuni hiyo, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Mwanza

na Kagera. Katika ziara hizo, Kamati ilitembelea Taasisi za sekta binafsi zinazojishughulisha na Kilimo kwa ajili ya kutathimini utekelezaji wa Sera ya Ushiriki wa Sekta Binafsi (Public, Private Partnership) katika kukuza uchumi kupitia kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hiyo Kamati ilitembelea: -

Mashamba ya miwa na Kiwanda cha Sukari Kagera;

Mashamba ya kahawa yanayomilikiwa na Kiwanda cha Kahawa cha Amir Hamza (T) Ltd.

Kiwanda cha kuzalisha Kawaha cha Tanganyika *Instant Coffee kinachomilikiwa* vyama vyaa ushirika wa KCUNA KDCU pamoja na Serikali.

Shamba la mahindi linalomilikiwa na Kampuni ya *Global Agency Limited*; na

Chama Kikuu cha Ushirika wa Kahawa cha Wilaya za Karagwe na Kerwa (KDCU)

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hiyo Kamati ilibaini changamoto mbalimbali zifuatazo:-

1) **Kampuni ya Global Agency Limited**

**Mheshimiwa Spika**, kampuni ya *Global Agency Limited* ni kampuni ya kitanzania ambayo inamiliki shamba lenye ukubwa wa **ekari 7,000** lilitoko mkoani Kagera. Mwaka 2018 kampuni hii ilipata mkopo wa **shilingi bilioni 12.174** kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za kuendeleza shamba hilo la mahindi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipofanya ziara katika shamba hilo ilikuta vifaa vyaa kilimo vyaa kisasa vilivyonunuliwa kupitia mkopo huo havifanyi kazi kwa sababu kampuni hiyo hajjaweza kukamilishiwa bakaa ya **shilingi bilioni 2.587** kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili awamu ya pili ya matumizi

ya vifaa hivyo iweze kuanza kazi na kukamilisha kazi zilizokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kuchelewa kutolewa kwa kiasi cha fedha za mkopo zilizosalia kumepelekea mradi kushindwa kutekelezwa kwa wakati na hivyo kutofikia malengo na kucheleweshwa kwa matarajio yaliyokusudiwa. Matarajio ya mradi huu yalikuwa kuongeza ajira kwa vijana, kuwesesa wakulima wa nje (*outgrowers*) kuwa na soko la uhakika la mahindi katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati ili kupata fedha za kigeni.

## 2) Kiwanda cha Sukari cha Kagera

**Mheshimiwa Spika**, kiwanda cha Sukari cha Kagera kilianzishwa na kumilikiwa na Serikali mwaka 1982 baada ya kiwanda cha awali kuharibiwa wakati wa vita ya Kagera. Mwaka 2001 baada ya Sera ya Ubinafsishwaji, viwanda vyote vilivyokuwa havifanyi vizuri kutokana na ukosefu wa mitaji na uongozi mbovu kikiwepo kiwanda cha sukari Kagera kilibinafishwa na kukabidiwa Kampuni ya ***Super Group*** ambayo inamilikiwa na watanzania ambapo kilibadilishwa jina na kuitwa Kagera *Sugar Limited*.

**Mheshimiwa Spika**, tangu kubinafsishwa kwa kiwanda hiki muwekezaji ameweza kufanya upanuzi wa kiwanda ili kuongeza uzalishaji wa kiwanda kwa lengo la kupunguza na kuondokana na changamoto ya uhaba wa sukari nchini ambayo imekuwa ikiligharimu Taifa fedha nydingi za kigeni kuagiza sukari nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipofanya ziara katika Kiwanda cha Sukari Kagera ilibaini uwekezaji mkubwa umefanyika na ambao umegawanyika kwa awamu mbili; awamu ya kwanza imehusisha upanuzi kwenye maeneo yafuatayo: -

- a) Kufanya upanuzi wa shamba la miwa kwa ajili ya malighafi ya kiwanda na kufikia hekta 14,000.
- b) Kukarabati kiwanda kwa kununua mashine bora za kisasa za kilimo na za kuendeshea mitambo ya kiwanda ili kuongeza

uzalishaji kutoka tani 95 za sasa na kufikia tani 170 mwaka 2021/2022 kwa lengo la kupunguza tatizo la upungufu wa sukari nchini;

c) Kwa kushirikiana na Serikali kuboresha miundombinu ya barabara kwa ajili ya kutoa malighafi za kiwanda mashambani pamoja na kurahisisha usafirishaji wa sukari kutoka kiwandani kupeleka sokoni;

d) Kujenga miundombinu ya umwagiliaji pamoja na kujenga kituo cha kuzalisha umeme (*sub station*) ili kuwa na uhakika wa maji kwa ajili ya kumwagilia mashamba ya miwa pamoja na kuhakikisha kiwanda kinakuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika kwa wakati wote.

**Mhesimiwa Spika**, uwekezaji huo mkubwa uliofanyika umeleta manufaa mbalimbali kama vile:-

Kiwanda kimeweza kuajili wafanyakazi wa kudumu katika kada mbalimbali takribani elfu sita (6,000) ambao hulipa kodi ya Serikali kuititia mishahara yao;

Kuanzisha programu mbalimbali za kuwafundisha wakulima wadogo wanaozunguka eneo la kiwanda kwa kuwafundisha njia bora za kilimo cha miwa, kuwapa pembejeo na zana bora za kilimo pamoja na kuwa na uhakika wa soko la mazao ya miwa na hilyo kupunguza umaskini katika eneo la kiwanda na sehemu za jirani; na

Kuongeza pato la mkoa wa Kagera kwa kulipa ushuru mbalimbali wa Serikali na Halimashauri pamoja na kushirikiana na Serikali ya Mkoa, Halimashauri na vijiji katika kuchangia uboreshaji wa huduma za kijamii kama vile elimu na afya.

**Mhesimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa matarajio ya kiwanda cha sukari Kagera ni kuongeza uzalishaji ili pamoja na sukari inayozalishwa na viwanda vya Kilombero *Sugar*, Mtibwa *Sugar* na TPC ni kumaliza tatizo la sukari nchini ifikapo Mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika**, malengo ya kiwanda cha sukari cha Kagera yatafikiwa tu endapo kiwanda hiki kitaweza kuwa na mtaji wa kutekeleza malengo hayo yaliyobainishwa. Kwa sasa Kiwanda kinakabiliwa na changamoto ya kupata dhamana ya Serikali ili benki za kimataifa ziweze kukikopesha kiwanda hiki kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 78** ambazo upatikanaje wake kupitia benki za ndani ya nchi ni mgumu kwa kuwa kiasi hiki ni kikubwa kuliko uwezo wa benki nyngi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina amini kupatikana kwa dhamana ya Serikali kutawezesha kupata mikopo kutoka benki zilizoko nje ya nchi na kukamilisha kazi ya utanuzi wa kiwanda kwa awamu ya pili.

### 3) Kiwanda cha Kahawa cha Amir Hamza (T) Ltd

**Mheshimiwa Spika**, kiwanda cha kahawa cha Amir Hamza (T)Ltd ni kiwanda kinachomilikiwa na Mtanzania na kilianza kazi mwaka 1994 mkoani Kagera. Kiwanda kinafanya kazi ya kuongeza thamani ya zao la kahawa kwa kutekeleza kwa vitendo adhima ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kukuza uchumi wa viwanda pamoja na kuboresha maisha ya wakulima.

**Mheshimiwa Spika**, tangu kuanzishwa kwa kiwanda hiki, kumekuwa na mafanikio mbalimbali, yafuatayo ni baadhi ya mafanikio yaliyofikiwa: -

(i) Ni kiwanda kikubwa Afrika Mashariki na Kati kinachosindika kahawa mumunyifu (*Instant Coffee*) na hivyo kuwezesha kuitangaza Kahawa ya Tanzania ndani na nje ya nchi na hivyo Kuongeza Pato la Taifa kwa kuingiza fedha za kigeni kutokana na mauzo ya kahawa mumunyifu nje ya nchi.

(ii) Kulipa kodi na michango mbalimbali ya Serikali na Jamii na kusaidia kuongeza ajira na kuinua uchumi wa mkoa wa Kagera. Hadi sasa kiwanda kimetoa ajira kwa watu sabini (70), na matarajio ya kiwanda kitakapokamiliika kitakuwa na wafanyakazi wa kudumu 200 na 600 wa muda;

(iii) Kuboresha hali ya maisha ya wakulima wa kahawa kutokana na kununua kahawa moja kwa moja kutoka vyama vyaa ushirika na hivyo kusaidia pia kuimarka kwa vyama vyaa ushirika nya kahawa mkoani Kagera; na

(iv) Kuongezeka kwa uzalishaji wa zao la kahawa kwa kutoa miche bora ya kahawa kwa wakulima, huduma za ugani na pembejeo kwa wakulima.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuanzishwa kwa mkataba wa *African Continental Free Trade Area* (AfCFTA) kumepelekea kuanzia Julai 2020 kuwa na eneo la soko huru la Bara la Afrika ambalo litatoa fursa kubwa ya kibiashara ambapo kwa upande wa kahawa inatarajiwa Afrika kuwa soko kuu jipya na kuzidi masoko ya Ulaya Mashariki katika matumizi ya kahawa kutokana na idadi kubwa ya watu walioko ndani ya bara hili.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na fursa hiyo kiwanda cha kuzalisha kahawa cha Amir Hamza (T) Ltd kimejipanga kuchangamkia fursa hiyo kwa utanuzi wa kiwanda kwa kuongeza mitambo ya kisasa na shughuli za uzalishaji ili kuhudumia soko kubwa lilioko barani Afrika na Ulaya kwa ujumla kwa: -

(a) Kufungua maduka ya kahawa (*Coffee Shops*) katika miji mikubwa hapa nchini na nchi jirani;

(b) Kutekeleza mradi wa kilimo cha kahawa katika shamba la ekari 1,000;

(c) Kuanzisha na Kujenga kituo cha kufundishia wakulima (*Community Farmers Training Centre*);

(d) Kuanzisha kituo cha taaluma ya kahawa (*Coffee Academy*); na

(e) Kuanzisha kituo cha ufundu kwa vijana (*Vocational Training Centre*).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ukweli kwamba nchi yetu ina uwezo wa kuzalisha kahawa nyngi kutokana na ukubwa wa ardhi, nguvu kazi na hali ya hewa nzuri iliyopo kwenye maeneo yanayolima kahawa nchini, aidha, kahawa yetu ni miongoni mwa kahawa zinazoongoza kwa kuwa na radha bora kabisa duniani, hata hivyo bado hatujaweza kutumia vizuri fursa ya soko la kahawa liliopo Afrika na Ulaya Mashariki kutokana na changamoto zinazovikabili viwanda vyta kuzalisha na kusindika kahawa kikiwemo kiwanda cha Amir Hamza (T)Ltd.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipotembelea kiwanda hiki ilibaini changamoto zinazokwamisha uzalishaji wa kiwanda ni nyngi, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na ucheleweshaji na ukosefu wa fedha za kumalizia kiwanda (*CAPEX*) pamoja na fedha za uendeshaji (*Working Capital*).

**Mheshimiwa Spika**, kiwanda hiki kiliomba mkopo kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) tangu mwaka 2015 na kukubaliwa na kupewa *offer letter* na kisha kupewa mkopo wa **USD 9,265,000:00** ambazo hazijatolewa hadi leo badala yake deni limeongezeka kutokana na riba na adhabu kitaalam inajulikana kama *Interest with Capitalization of Interest and Penalties* na kufikia **USD 27 milioni**.

**Mheshimiwa Spika**, uongozi wa kiwanda ulifanya jitihada kwa benki zingine, ambapo benki ya NMB *Bank Limited* ilikubali kukipatia kiwanda mkopo kwa ajili ya *Working Capital* ya **USD milioni 8** na Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) wakaahaidi kutoa CAPEX baadae walishindwa kutekeleza ahadi yao, ndipo NMB *Bank Limited* walikubali kuwapatia CAPEX na *Working Capital*.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na sababu za mabadiliko ya kiungozi ndani ya benki, pesa za CAPEX kutoka NMB *Bank Limited* zilichelewa hadi Machi, 2020 ndio zilipatikana kwa bahati mbaya wakati zinatoka janga la **COVID 19** lilikuwa limeshaingia ulimwenguni na wanunizi wakubwa wa Kahawa ya kiwanda hiki ni nchi za Ulaya Mashariki ambako maduka ya vioski vyta kunywa kahawa (*Coffee Shops*) yalikuwa

yamefungwa kutokana na *Lockdown* iliyotangazwa katika nchi nyingi za Ulaya.

**Mheshimiwa Spika**, Working Capital ya NMB benki imetumika japokuwa kiwanda hakijakamilika kikamilifu lakini pia hakuna mauzo ya kahawa yaliyofanyika kutokana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na kirusi cha Corona.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia hali hiyo, Kamati ilipokea ombi la kiwanda kwa kuitaka Serikali kuingilia na kusaidia baada ya juhudhi binafsi za kiwanda kushindikana Kupunguzwa kwa deni la Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) pamoja na riba ya kutoka **asilimia 11** hadi **asilimia 5** ili kusaidia kukijengea uwezo kiwanda kuendelea kuzalisha pamoja na kukinusuru kiwanda kafilisika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipofanya ziara katika Mkoa wa Kagera ilibaini kuwa Mkoa wa Kagera una jumla ya viwanda vya kukoboa kahawa vipatavyo 14 hata hivyo viwanda hivi vinakabiliwa na changamoto ya umeme kwani mkoa wote kwa muda mrefu sasa unategemea kupata umeme kutoka nchi ya Uganda.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilielezwa kuwa hapo awali umeme wa Uganda ulikuwa wa uhakika kuliko unaotoka kwenye gridi ya Taifa. Hivi sasa umeme wa kutoka Uganda umekuwa usio na uhakika kwa kuwa unakatika mara kwa mara bila kujua utarudi baada ya muda gani na hivyo kuathiri uzalishaji viwandani.

**4) Chama cha Ushirika Wilaya ya Karagwe na Kyerwa - Karagwe District Cooperative Union Ltd (KDCU)**

**Mheshimiwa Spika**, Chama cha Ushirika Wilaya ya Karagwe na Kyerwa - KDCU kinahudumia Wilaya mbili ambazo ni Wilaya ya Karagwe na Kyerwa zenyé jumla ya wanachama 64,300 katika vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) 117 (Wilaya ya Karagwe AMCOS 43 na Kyerwa - AMCOS 74).

**Mheshimiwa Spika**, Wilaya hizi mbili kwa pamoja huzalisha kahawa aina ya robusta zaidi ya **asilimia 70** ya kahawa yote inayozalishwa Mkoa wa Kagera na zaidi ya **asilimia 40** ya kahawa yote Nchi nzima. Nia na Madhumuni ya *KDCU Ltd* kama Chama Kikuu cha Ushirika ni kuinua, kustawisha na kuboresha hali ya wanachama wake katika mahitaji mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na kimazingira kwa kufuata taratibu za uendeshaji za kidemokrasia, Misingi, Sheria ya Vyama vyta Ushirika na Kanuni zake.

**Mheshimiwa Spika**, Chama cha Ushirika KDCU kilianzishwa ili kukabiliana na mfumo wa ununuzi holela wa kahawa uliojulikana kwa jina la Butura ambapo walangazi walitumia shida za wakulima maskini kununua kahawa yao ikiwa bado changa kwa bei wanayopanga wao na hivyo kufanya mkulima kukosa maamuzi yoyote juu ya kahawa yake.

**Mheshimiwa Spika**, Mfumo huu pia ulipelekea vijana wengi ambaeo ndio nguvu kazi kujikita katika shughuli za udalali wa kahawa na biashara ya magendo na kuacha kabisa kulima kahawa na kusababisha uzalishaji wa zao la kahawa kudhoofika.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile mfumo wa kununua kahawa ya wakulima kwa njia ya magendo ulipelekea kukosekana kwa takwimu sahihi za uzalishaji wa zao la kahawa kutokana na tabia ya walangazi kuficha takwimu sahihi ili kukwepa kulipa kodi za Serikali na Manispaa.

**Mheshimiwa Spika**, mfumo wa huu pia ulisababisha kuongezeka kwa biashara ya magendo ya kahawa kwenda nchi jirani kushamiri kutokana na kila mlanguzi kufanya anavyotaka bila kufuata utaratibu na kunufaisha nchi jirani kunufaika zaidi kwani zilliweza kutengeneza ajira pamoja na kunufaika na mapato mengine yaliyotokana na mnyororo wa thamani wa zao la kahawa na huku wakulima wetu wakibaki kwenye umaskini uliokithiri.

**Mheshimiwa Spika**, mfumo wa ununuzi wa kahawa nje ya ushirika ulimnufaisha Mlangazi/dalali wa kahawa ya mkulima

badala ya mkulima mwenyewe. Mkulima alirubuniwa kwa kupewa bei ndogo sana wakati kahawa yake ikiwa changa('Butura') au maua. Vilevile mfumo wa 'Butura' na magendo ulidhoofisha vyama vyaya ushirika vyaya msingi/chama Kikuu na kuvisababishia kuingia katika madeni makubwa ambayo yaliharibu ustawi wa wakulima.

**Mheshimiwa Spika**, mali za ushirika ziliwekwa rehani kwa sababu ya madeni yaliyotokana na vyama hivyo kuendeshwa kwa hasara. Aidha, Katika mfumo wa ununuzi holela, kahawa ilivunwa na kuanikwa pasipo utaratibu wowote na kupelekea kahawa yetu kukosa ubora na hivyo kukosa ushindani katika soko la kimataifa hali hii ilipelekea kuharibu taswira na heshima ya nchi yetu katika tasnia ya kahawa.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia changamoto hizo, Serikali iliagiza kahawa yote ya wakulima kununuliwa kupitia mfumo rasmi wa ushirika ambapo mfumo huu umesaidia kuwakomboa wakulima wanyonge katika mikono na minyororo ya walangazi wa kahawa kwa njia ya "BUTURA".

**Mheshimiwa Spika**, hivi sasa Wakulima huuza kahawa yao kupitia AMCOS na Chama Kikuu cha Ushirika kwa bei halisi ya soko. Mfumo wa ushirika umesaidia pia kupatikana kwa takwimu sahihi kuhusu wakulima wa kahawa pamoja na takwimu za uzalishaji. Upatikanaji wa takwimu hizi unasaldia sana utengenezaji, usimamizi na uboreshaji wa zao la kahawa, sambamba na kuiwezesha Serikali kupata mapato stahiki yatokanayo na zao la kahawa.

##### **5) Kiwanda cha Kusindika Kahawa cha Tanganyika Instant Coffee (TANICA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kiwanda cha Kusindika Kahawa cha Tanganyika *Instant Coffee* (TANICA) kinalimikiwa na Vyama viwili vyaya Ushirika vyaya KCU na KDCU pamoja na Serikali. Kamati ilipofanya ziara katika kiwanda hiki ilibaini kuwa kwa muda mrefu uongozi wa kiwanda hiki ultumia vibaya madaraka yake na kupelekea kiwanda kuijendesha kwa hasara na kukabiliwa na madeni.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hiyo, Kamati ilipokea taarifa ya madeni ya kiwanda ambayo ilionyesha kiwanda kinakabiliwa na deni kubwa linalotokana na mkopo kutoka benki ya **CRDB** ambao riba yake ni **asilimia 18** ikilinganishwa na riba inayotolewa na benki ya Maendeleo ya kilimo (**TADB**) ambayo riba yake ni **asilimia 10** tu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kutaka uafunuzi kutoka kwa Serikali kwanini kiwanda kinachomilikiwa na Serikali na Wanaushirika kisipate mkopo wenyewe riba nafuu kutoka Serikalini, Serikali iliagiza Benki ya Maendeleo ya Kilimo kuchukua deni lote la TANICA kutoka CRDB ili kiwanda kianze kulipa riba ya asilimia 10 badla ya riba ya asilimia 18. Kamati inapongeza hatua hii kwani itasaidia kiwanda hiki kuendelea kuzalisha kwa faida. Aidha, Kamati iliagiza hatua za kisheria na kinidhamu zichukuliwe dhidi ya waliokuwa viongozi wa TANICA kwa ubadhirifu wa mali ya umma.

**6) Kiwanda cha mbolea cha Minjingu (*Minjingu Mines & Fertiliser Limited - MMFL*)**

**Mheshimiwa Spika**, kiwanda cha mbolea cha Minjingu awali kipoanza uzalishaji kilianza kwa kutengeneza mbolea yenye kirutubisho kimoja cha Phosphate. Katika miaka ya hivi karibuni, kiwanda kimeweza kuboresha uzalishaji wa mbolea ya Minjingu, hivi sasa kiwanda kinatengeneza mbolea mchanganyiko zenye virutubisho vingi na viwango tofauti vya ubora na kupelekea kiwanda hiki kuwa kiwanda pekee katika Ukanda wa Afrika Mashariki kinachotengeneza mbolea zenye viwango tofauti vya virutubisho vinavyokidhi mahitaji ya mimea na afya ya udongo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa sasa kiwanda kinatengeneza aina tofauti za mbolea zilizopendekezwa na watafiti wa mbolea nchini kwa kuongeza virutubisho kama *Nitrogen*, *Potassium*, *Sulphur*, *Boron* ambazo huagizwa kutoka nje ya nchi hivyo kuufanya mbolea inayozalishwa na kiwanda kuwa na ubora unaofaa kwa ardhi na mazingira ya nchi yetu kwani mbolea inayozalishwa kiwandani hapo imethibitishwa na, Taasisi ya Vituo vya Utafiti wa Kilimo (*Tanzania Agricultural Research*

*Institute – TARI )* kuwa inafaa kwa mazao aina ya Mahindi, Mpanga, Chai, Tumbaku, Pamba na Kahawa.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile, ubora wa mbolea ya minjingu umethibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (*Tanzania Bureau of Standards-TBS*) na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (*Tanzania Fertilizer Regulatory Authority - TFRA*) Hivyo, Kamati inaona hakuna sababu ya kuwa na wasiwasi kuhusu ubora wa mbolea inayozalishwa na kiwanda hiki.

**Mheshimiwa Spika**, uwezo wa kiwanda kuzalisha mbolea kwa mwaka ni tani **100,000** za mbolea za aina mbalimbali, aidha kiwanda kina mpango wa kupanua wigo wa uzalishaji wa mbolea na kufikia **tani 500,000** ifikapo mwaka **2025/ 2026**, hata hivyo ongezeko hili la uzalishaji wa mbolea nchini litawekezana tu endapo Serikali itafanya juhudzi za makusudi kwa kuweka mazingira wezeshi kwa viwanda vya ndani kuzalisha mbolea kwa wingi na sio kama hali ilivyo sasa ambapo upungufu wa mbolea hufidiwa kwa Selikali kutoa vibali kwa wasambazaji wakubwa wa mbolea kuagiza mbolea nje ya nchi .

**Mheshimiwa Spika**, uagizaji wa mbolea nje ya nchiunakwamisha juhudzi za viwanda vya ndani kuendelea, unakosesha ajira kwa vijana lakini pia unainyima Serikali mapato yatokanayo na kodi mbalimbali wakati huo huo unavisaidia viwanda vya nje kuendelea kuimarika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini ili kulinda viwanda vya ndani vya kutengeneza mbolea na kufikia adhma ya Serikali kufikia uchumi wa kati kupitia viwanda ifikapo 2025, ni vyema Serikali ikazingatia na kutekeleza maswala yafuatayo ambayo yamekuwa vikwazo kwa Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu na wazalisahji wengine wa mbolea hapa nchini.

a) Kuanza kutumika kwa utaratibu wa makumbaliano ya Utatu (Tripartite Agreements) ili Bodi za Mazao/ Ushirika/ Wasindikaji / Mabenki kuhakisha wanawolu mbolea zinazotengenezwa nchini kwa ajili ya kutumiwa na wakulima kulingana na mahitaji halisi; na

b) Ni muhimu kwa miradi ya Serikali kutekelezwa kwa kuhakikisha inatumia mbolea zinazotengenezwa nchini.

#### **7) Utekelezaji wa Progamu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili**

**Mheshimiwa Spika**, Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili inaelezea pamoja na mambo mengine umuhimu wa kilimo biashara kupitia soko la mtandao. Aidha, Sheria ya Mazao inaeleza kuwa soko la mtandao linasaidia kutangaza mazao na bei dunia nzima kutokana na ukweli kwamba dunia nzima inaona mnada unavyofanyika.

**Mheshimiwa Spika**, faida zingine za soko la mazao mtandaoni ni pamoja na mkulima kunufaika na soko la mazao yake na hilyo kuongezeka kwa pato la mkulima na pato Taifa kutokana na mazao ya wakulimwa kuuzwa kwa bei halisi ya dunia, kwa mfano; **bei ya kilo moja ya korosho kwenye soko la mtandao kwa sasa ni takribani shilingi 80,000 wakati bei ya kilo moja ya korosho kupitia vyama vya msingi ni kati ya shilingi 3,000 – 3,500.**

**Mheshimiwa Spika**, faida nyingine ya soko la mazao mtandaoni ni kwa mkulima kuhifadhiwa vizuri mazao yake bila kuharibika kwa kuliwa na wadudu na pia mkulima kuwa na uhakika wa bei ya mazao sokoni.

**Mheshimiwa Spika**, uzoefu wa nchi nyingine zinazofanya biashara ya mazao kupitia siko la mtandao zimeonyesha mafanikio makubwa ya kuchumi, kwa mfano nchi ya India kwa sasa uchumi wake kwa kiasi kikubwa unategemea biashara ya mazao kupitia mtandaoni kwenye soko la dunia.

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu haiwezi kuingia kwenye soko la mazao mtandaoni bila kuwa na vihenge na maghala ya kisasa kwa ajili ya kuhifadhi mazao lakini pia kupitia vihenge na maghala ya kisasa ndipo dunia inaweza kuona hali halisi ya mazao yanayouzwa yakiwa ghalani. Aidha, nchini Tanzania hupotevu wa mazao kabla ya kufika sokoni

unakadiliwa kuwa **asilimia 50** na hivyo kuisababishia nchi hasara ya **USD 938 milioni** kwa mwaka **2018/2019** pekee.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hasara hii, nchi yetu tangu **mwaka 2014** haijaweza kukopa kutoka Shirika la Fedha Duniani kwa kuwa kiwango cha Tanzania kukopa ni **USD 900 milioni**. Ili Shirika la Fedha la Dunia liweze kuipatia nchi yetu mkopo, pamoja na masharti mengine, sharti moja wapo ni kutakiwa kujenga vihenge na maghala ya kisasa ili kupunguza kiwango kikubwa cha upotevu wa mazao kabla ya kufika sokoni. Kwa kuzingatia sharti hili, Serikali kuititia Wakala wa Taifa Hifadhi ya Chakula inajenga **vihenge 36** kwa ajili ya kuhifadhi chakula.

**Mheshimiwa Spika**, vihenge vinavyojengwa na Wakala wa Taifa Hifadhi ya Chakula vitatumika kuhifadhia chakula hata hivyo vihenge vinavyojengwa na Wakala wa Taifa Hifadhi ya Chakula haviwezi kutumika kwenye soko la mauzo ya bidhaa mtandaoni kwa sababu bidhaa zinazohifadhiwa kwenye vihenge hivi havina teknolojia ya mtandao wa kuwezesha bidhaa iliyoko ghalani kuonekana kwenye soko la mazao mtandaoni.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia chanagmoto hizo, Shirika lisilo la kiserikali la *Advanced African Solution LLC* (ADAS) lenye makao makuu yake nchini Marekani linalenga kuwawezesha wakulima wadogo kwa kuhakikisha nchi za Afrika zinajitosheleza kwa chakuala. Kwa vile Tanzania utoshelevu wa chakula ni zaidi ya **asilimia 100**, Shirika hili liko tayari kuipatia nchi yetu mkopo usio na riba na utakorudishwa baada ya miaka 30 kwa utaratibu wa *revolving fund* ili kujenga vihenge na maghala ya kisasa kwa ajili ya kuhifadhi mazao lakini pia kusaidia nchi yetu kushiriki kikamilifu kuititia soko la mazao mtandaoni.

**Mheshimiwa Spika**, nchi za Afrika ambazo zimeshanufaika na mkopo wa aina hii ni pamoja na Ethiopia, Zambaia na Kenya. Kwa upande wa Tanzania japo utekelezaji wa mradi huu umechukua muda mrefu kwa lengo la kujiridhisha, kwa sasa mradi huu unafahamika na kukubaliwa na Mheshimiwa Rais

na Wizara ya kilimo imeshatoa kibali kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, changamoto iko kwa Wizara ya Fedha na Mipango ambapo wao wanafanya mazungumzo ili kujiridhisha kama kweli huu ni mkopo usio na riba.

**Mheshimiwa Spika**, ni kweli kabisa hilo ni jukumu la Wizara ya Fedha na Mipango kwa niaba ya Serikali, kinachohitajika kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ni *Letter of Intent* baada ya kujiridhisha, hata hivyo barua hiyo hadi sasa hajatoka, Kamati inamaoni kuwa mazungumzo hayo yamechukua muda mrefu na hivyo kuathiri maslahi mapana yaliyolengwa katika utekelezaji wa mradi huu.

### **2.3 MPANGO WA BAJETI NA UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 tarehe 25 - 26 Machi, 2020. Mpango ambao umeandaliwa kwa kuzingatia: -

- a) Maelekezo yaliyoko kwenye Mwongozo wa Mpango wa Bajeti ya Serikali wa Mwaka 2020/2021.
- b) Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025) Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (*Five Year Development Plan Phase II – FYDP II*);
- c) Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals – SDGs*);
- d) Mpango wa Uwekezaji katika Kilimo na Usalama wa Chakula Tanzania (*Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan – TAFSIP*);
- e) Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013.
- f) Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili na;

g) Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2015-2020.

### **2.3.1 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Waziri aliileza Kamati kuwa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kwa Fungu 43 umejielekeza kuimarisha ushirikiano na Wizara za Sekta Binafsi ili kuendeleza mazao ya kipaumbele yaliyoainishwa kwenye programu ya kuendeleza Kilimo Awamu ya Pili (ASDP 11) ambayo ni pamoja na pamba, kahawa, miwa, korosho, chai, mahindi, mpunga, mtama, uwele, muhogo, mazao ya bustani, mazao ya mafuta, viazi na mazao ya mikunde na migomba. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti vya kilimo, udhibiti wa visumbufu vya mimea, huduma za ugani, usajili wa wakulima na bima ya mazao.

### **2.4 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo, unajumuisha Mafungu Matatu ambayo ni: -

(a) Fungu 43 – Wizara ya Kilimo;

(b) Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika; na

(c) Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mafungu yote Matatu Wizara imepanga kutekeleza Malengo yenyе Mikakati nane (8) ambapo kipaumbele kimewekwa katika: -

(i) Kuunganisha Wakulima Wadogo na Mashamba Makubwa ili kuendeleza kilimo biashara;

(ii) Ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji, Maghala, Masoko na Miundombinu ya kuhifadhia mazao ya Kilimo;

- (iii) Kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za mazao na upatikanaji wa pembejeo nyingine za kilimo na kuzisambaza kwa wakulima;
- (iv) Kuongeza matumizi ya Teknolojia Bora katika uzalishaji wa mazao ili kuongeza uzalishaji na Tija;
- (v) Kuimarisha Vituo vya Utafiti, Vyuo vya Mafunzo na Vituo vya wakulima;
- (vi) Kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya Ushirika kwa kuweka mifumo itakayoongeza ufanisi; na
- (vii) Kuimarisha huduma za upimaji wa matabaka na ubora wa udongo;

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza maeneo hayo ya vipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Kilimo, kupitia **Fungu 43** inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **202,504,117,000:00**, **Fungu 24** linaomba kuidhinishiwa shilingi **9,608,846,000:00** na **Fungu 05** linaomba kuidhinishiwa shilingi **17,726,845,000:00** Kwa ujumla Wizara ya Kilimo, kupitia Mafungu yote Matatu inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **229,839,808,000:00**. Aidha, Wizara kupitia Fungu 43 na Fungu 05 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 inatarajia kukusanya jumla ya maduhuli kiasi cha shilingi **16,281,180,000:00**.

#### **2.4.1. Wizara ya Kilimo- Fungu 43**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 **Fungu 43** inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **202,504,117,000:00** Kati ya Fedha hizo, shilingi **65,230,973,000:00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **137,273,144,000:00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, shilingi **82,000,000,000:00** ni Fedha za Ndani na shilingi **61,577,036,140:00** ni Fedha za Nje.

#### **2.4.2. Tume ya Maendeleo ya Ushirika- Fungu 24**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara kupitia **Fungu 24** inaomba kuidhinishiwa jumla ya

shilingi **9,608,846,000:00**. Kiasi kinachoombwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Fungu 24 zinakasimiwa kupitia Fungu 43 ambalo linahusu Wizara ya Kilimo.

#### **2.4.3. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji- Fungu 05**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara kupitia Tume ya Umwagiliaji - **Fungu 05** inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **17,726,845,000:00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi **4,925,665,000:00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kwa upande wa kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara imetengewa shilingi **12,801,180,000:00**, kati ya fedha hizo shilingi **3,000,000,000:00** sawa na **asilimia 23.4** ni Fedha za Ndani na shilingi **9,801,180,000:00** sawa na **asilimia 76.6** ni Fedha za Nje.

### **2.5. TATHIMINI YA MALENGO KWA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini Malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2020/2021 na kubaini kuwa malengo mengi yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti wa Mwaka huu yamejirudia kutoka malengo yaliyoainishwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kamati inaamini kujirudia kwa malengo yaliyoainishwa ni muendelezo wenyewe lengo la kuhakikisha kilimo kinachangia kutoa malighafi za viwanda ili kuifikiwa Tanzania kwenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

#### **2.5.1. Tathimini ya Jumla ya Malengo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Mpango wa Bajeti ya Wizara utajielekeza kwenye kilimo kitakachohakikisha usalama wa chakula ili kukabiliana na tatizo la njaa na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya

viwanda. Kamati katika tathimini yake imebaini changamoto mbalimbali zinazoweza kukwamisha utekelezaji wa malengo ya Wizara. Changamoto hizo ni pamoja na: -

**1. Athari zitokanazo na madhara ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu unaosababishwa na Virusi vya Corona (COVID -19) kwenye Sekta ya Kilimo.**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni mionganoni mwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na Bara la Afrika ambazo uchumi wake kwa kiasi kikubwa unatokana na shughuli za kilimo kwa kuza mazao yake nje ya nchi. Kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona umeathiri uchumi wa nchi nyingi duniani, ambapo nchi nyingi zilizoathirika kiuchumi ni wateja wakubwa wa mazao ya blashara yanayozalishwa nchini kama pamba, korosho, na kahawa.

**Mheshimiwa Spika**, ripoti ya Benki ya Dunia inaonesha uchumi wa dunia na hususani uchumi wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa takribani miaka 25 iliyopita haijapata mtikisiko wa uchumi mkubwa kiasi hiki kama mtikisiko huu uliosababishwa na Homa ya Mapafu ambapo takwimu zinaonesha uchumi wa nchi hizi utashuka kutoka **asilimia 2.1** mpaka **5.1** mwaka huu kutoka **asilimia 2.4** mwaka jana.

**Mheshimiwa Spika**, tafsiri yake hii ni kuwa shughuli za kilimo na mapato yatokanayo na mazao ya kilimo yatashuka kutokana na ukweli kwamba mazao yetu ya kibashara kama Pamba, Korosho, Kahawa, Tumbaku ambayo kwa kiasi kikubwa huuzwa nje ya nchi na kuiletea nchi fedha za kigeni upo uwezekano mkubwa wa masoko ya mazao hayo kuathirika kutokana na mtikisiko wa uchumi wa dunia.

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa bajeti inayowasilishwa ni lazima ionyeshe mkakati wa makusudi wa kuinusuru sekta ya kilimo kwa kuhakikisha upatikanaji wa soko la uhakika wa

mazao ya biashara na kimkakati na kuepusha kudorola kwa sekta na kuathiri pato la wakulima na Taifa kwa ujumla.

**2. Fursa kwa mazao ya kilimo zinazoweza kupatikana kutokana na Ugonjwa wa Homa ya Mapafu unaosababishwa na Virusi vya Corona**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwepo viashiria vya mdororo wa sekta mbalimbali ikiwepo sekta ya kilimo, Kamati inaamini kwamba changamoto hiyo ni fursa kwa nchi yetu kutokana na kuwa na uwezo wa kuzalisha chakula cha ziada na hata kuweza kuza nje ya nchi hususan kipindi hiki cha janga la **COVID - 19**. Kamati inaamini kwamba endapo tutajipanga vizuri kuititia Kilimo cha Umwagiliaji, ardhi kubwa na yenyе rutuba, nguvu kazi iliyopo nchini upo uwezekano wa nchi yetu kufaidika kuititia kilimo hasa katika eneo la Ukanda huu.

**3. Kuchelewa kutolewa kwa Dhamana za Serikali kwenye Miradi mikubwa ya Uwekezaji kwa Kampuni za Watu Binafsi**

**Mheshimiwa Spika**, wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake imebaini kuwa upo ukiritimba mkubwa unaofanywa na Serikali ili kuwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kuongeza pato la Serikali, kuongeza ajira, kuinua uchumi wa wakulima, na kushiriki kikamilifu katika kuisaidia Serikali kutekeleza adhima ya uchumi wa viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo haya yamethibitisha na Kamati ilipofanya ziara katika Kiwanda cha kuzalisha sukari cha Kagera, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa licha ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na uongozi wa kiwanda katika kuongeza uzalishaji na kupunguza tatizo la muda mrefu la uhaba wa sukari nchini, bado Serikali kuititia Wizara ya Fedha na Mipango inachukua muda mrefu kutoa dhamana kwa kiwanda hiki ili kiwanda kiweze kupata mikopo kutoka benki mbalimbali nje ya nchi ambazo zimejiridhisha kuwa Kiwanda cha Sukari Kagera kinao uwezo wa kurudisha mikopo hiyo kwa wakati, kinachotakiwa tu ni dhamana ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba Sheria ya *The Government Loans, Guarantees, Grants Act, 1974* ikisomwa

pamoja na *The Government Loans, Guaranteees, Grants (Amendment) Act, 2003* imefafanua vizuri katika sehemu ya Nne, Kifungu cha 13 – “*Where on the advice by the National Committee, the Minister is satisfied that it is in the public interest that the guarantee repayment of any principal money and the payment of the interest and other charges on any loan raised either within or outside Tanzania by a local government authority or parastatal body requires a government guaranteee, the Minister, shall proceed to issue such a guarantee for and on behalf of the Government*” i na 13 A - (C) “*the parastatal organization or body corporate for whose benefit such a guarantee is given, demonstrates to the satisfaction of the Minister, that it has provided adequate securities to cover the loan in the event of default by such parastatal organization or body corporate*”.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na sheria nzuri zilizotungwa na Bunge lako Tukufu zinafafanua utaratibu wa kufuata ili kampuni iweze kupata dhamana ya Serikali ikiwa ni pamoja na kujiridhisha kama dhamana itakayotolewa ina: -

a) **Maslahi kwa Taifa;** kwa tathimini ya Kamati maslahi kwa taifa yatatokana na kupanua wigo wa kodi ya Serikali, kutengeneza ajira, kukuza uchumi wa viwanda na kuondoa tatizo la muda mrefu la upungufu wa sukari nchini na kuuza sukari nyingine nje ya nchi na hivyo kuliingizia taifa fedha za kigeni.

b) **Tija ya utekelezaji wa mradi (Viability of the project);** Kamati imekagua upanuzi wa Kiwanda cha sukari Kagera na kuridhika kuwa mradi huu ukipewa dhamana kwa ajili ya kiwanda kupata mkopo ili kuongeza mtaji na kukiwa na usimamizi madhubuti kutoka Serikalini na kwenye uongozi wa kiwanda, mkopo utakaotolewa utalipika.

#### 4. **Ukosefu wa Umeme wa Uhakika na athari zake katika Uchumi wa Viwanda na Sekta ya Kilimo**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake ilibaini kuwa wakulima wa mazao mbalimbali wameitikia

wito wa Serikali wa kuzalisha mazao ambayo ni malighafi ya viwanda vilipo nchini. Hata hivyo changamoto kubwa inayovikabili viwanda vya ndani ni kukosekana kwa umeme wa uhakika na hivyo viwanda kushindwa kuzalisha kulingana na makusudio ya kiwanda. Hali hii imepelekea wenye viwanda pia kununua mazao kidogo kulingana na uwezo wa viwanda kuzalisha.

**Mheshimiwa Spika**, hali hii imejiridhisha kwenye kiwanda cha kusindika kahawa cha Amir Hamza (T) Ltd ambako Kamati ilielezwa Mkoa wa Kagera unategemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa umeme kutoka Uganda. Ili kusaidia kuepukana na tatizo hili Kamati imefuatilia jitihada zinazofanywa na Serikali ili kusaidia mkoa wa Kagera kupata umeme wa uhakika kutoka gridi ya Taifa kuititia **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji ya Rusumo – MW 80**.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahu unahu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 80** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera na unahuisha nchi tatu (3) za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo sawa kwa kila nchi. Mradi unaghanimu **Dola za Marekani milioni 113** sawa na takriban **Shilingi bilioni 261.75** kwa ufadhilli wa Benki ya Dunia kwa upande wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza uwekezaji huu unaofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, hata hivyo Kamati inaanini mpango huu ni wa muda mrefu na kwamba upo uwezekano wa kutekeleza mipango ya muda mfupi ili kusaidia viwanda vyetu viweze kufanya kazi kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia hali hiyo, Kamati inapendekeza Serikali kuititia Wizara ya Nishati kupeleka umeme kwa kutumia genereta za ziada zilizokuwa zikitumiwa na mkoaa ambayo imeingizwa kwenye gridi ya Taifa kwani kwa sasa genereta hizo hazitumiki hivyo zinaweza kupelekwa mkoani

Kagera ili zikae *standby* kwa ajili ya kutumika kipindi umeme wa Uganda unapokuwa si wa uhakika.

## **SEHEMU YA TATU**

---

### **3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuweka kumbukumbu rasmi, napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa tangu kwa kipindi cha uhai wa Bunge la Kumi na Moja, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji imeshatoa ushauri mbalimbali na Bunge kuazimia Serikali ikatekeleza mapendekezo ya Kamati kwa lengo la kuinua Sekta ya Kilimo nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Wabunge wakirejea Taarifa Rasmi za Bunge watakuta maeneo ambayo yamewahi kutolewa ushauri ni pamoja na: -

- (a) Umuhimu wa kutekeleza Azimio la Abuja na badea Malabo kwa kutenga asilimia 10 ya Pato la Taifa kwa ajili ya kuendeleza sekta ya Kilimo;
- (b) Umuhimu wa kuiwezesha kifedha vituo vya utafiti ili wataalamu wa utafiti waweze kufanya tafiti zenyne manufaa kwa nchi yetu badala ya kutegemea fedha za utafiti kutoka kwa wadau wa maendeleo ambapo fedha hizo huambatana na masharti ya tafiti wanazotaka;
- (c) Umuhimu wa kuiwezesha kifedha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili kuweza kutekeleza miradi ya kimkati itakayosaidia kuwa na uhakika wa kilimo katika msimu wa mwaka mzima bila kutegemea kilimo cha mvua ambacho sio cha uhakika kwa sasa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa;
- (d) Umuhimu wa kuiwezesha kifedha Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARULA) ili pamoja na mambo mengine, iboreshe mtandao wa barabara za vijijini kwa lengo la kuwezesha mazao ya wakulima kufika sokoni kwa wakati;

- (e) Umuhimu wa kuiwezesha kifedha Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na uendelezaji wa mbegu za kilimo (ASA) ili kuhakikisha nchi inakuwa na usalama wa chakula unaotokana na matumizi sahihi ya mbegu bora ambazo zitapatikana kwa urahisi na kuwafikia wakulima kwa wakati na kwa gharama nafuu;
- (f) Umuhimu wa matumizi sahihi ya viuatirifu, mbolea, pembejeo, na dhana bora za kilimo katika kufikia uchumi wa viwanda;
- (g) Uhaba wa maafisa ugani na madhara yake katika kuongeza tija kwenye kilimo kwa ajili ya kuchangia malighafi za viwanda kwa bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo pamoja na chagamoto ya maafisa ugani kuwajibika Ofisi ya Rais – TAMISEMI badala ya kuwajibika moja kwa moja kwenye Wizara yenye dhamana na kilimo;
- (h) Umuhimu wa kufanya sensa ya mazao na sense ya wakulima kwa ajili ya kuwatambua, kuwashudumia kwa urahisi na kuwa na takwimu sahihi za mazao yanyodhalishwa nchini pamoja na kuwa na takwimu sahihi za mchango wa sekta ya kilimo kwenye pato la Taifa;
- (i) Umuhimu wa kukamilisha mapema maboresho ya Sera ya Kilimo na kuanzishwa kwa Sheria ya Kilimo ambayo itashughulikia changamoto zote zinazohusu sekta ya kilimo nchini ikiwa ni pamoja na kukifanya kilimo cha Tanzania kuwa Kilimo biashara badala ya kilimo cha chakula na kujikimu;
- (j) Umuhimu wa kuwa na viwanja vya ndege vya kimkakati pamoja na ndege za mizigo kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa mazao aina ya mboga mboga, matunda na viungo ambayo ni rahisi kuharibika lakini pia mazao haya yana soko kubwa kwenye Jumuiya za Kimataifa;
- (k) Umuhimu na uwezekano wa Serikali kuongezea mtaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo, ili benki hii iweze kuwakifika wakulima wengi zaidi na kuwapa mikopo yenye riba nafuu;

- (l) Serikali kuona umuhimu wa kuondoa kodi na tozo nyingi kuititia tozo na kodi kandamizi kama zilivyoanishwa kwenye *Blue Print* ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikikwamisha ukuaji wa sekta ya kilimo;
- (m) Umuhimu wa kuharakisha ujenzi wa viwanda vya mbolea nchini ili kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mbolea nje ya nchi ambayo mara nyingi haipatikani kwa wakati; hata ikipatikana inauzwa kwa gharama kubwa ambazo wakulima wengi hawamudu;
- (n) Umuhimu wa kuihimiza kilimo mseto na kilimo hifadhi ili kupunguza matumizi ya kemikali katika mazao ya kilimo, matumizi ya kemikali kwenye kilimo yanapelekea athari kwa afya za binadamu na mimea; na
- (o) Umuhimu wa Vyama Vikuu vya Msingi vya Ushirika kununua mazao kutoka kwa wakulima kwa bei nzuri hatua ambayo itasaidiwa kuwajengea wakulima uwezo wa kimapato na hivyo kukosekana mwanya wa walanguzi kuwarubuni wakulima.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya ushauri huu umetekelewa, baadhi utekelezaji wake unaendelea kwa awamu, na baadhi haujafanyiwa kazi. Kamati inahisih Serikali kufanya kazi maeneo yote ambayo bado utekelezaji wake unasuasua.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba sasa niwasilishe maoni na ushauri wa Kamati uliotokana na Kamati kufanya uchambuzi kwenye maombi ya Fedha kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama ifuatavyo: -

1. Ili kutekeleza kwa vitendo Sera ya ushiriki wa Sekta Binafsi katika kukuza uchumi pamoja na adhima ya Serikali ya Uchumi wa Viwanda, Kamati inaishauri Serikali kutumia wataalamu wake kuharakisha maamuzi ya kutoa dhamana kwa viwanda vilivyokidhi matakwa ya Sheria ya *The Government Loans, Gurantees and Grants (Ammendment)*,

Act 2003 ili kuwezesha viwanda ambavyo vimekidhi matakwa ya sheria hii kupata mikopo hiyo kwa wakati. Hatua hizi madhubuti zitasaidia kuwezesha viwanda nya ndani kuongeza uzalishaji.

2. Ili kukabiliana na janga la Ugonjwa wa Homa ya Mapafu unaosababishwa na virusi nya corona (COVID-19) na kupelekea shughuli za kilimo kuathirika kwa kiasi kikubwa zinapaswa kusaidiwa kwa Serikali kutoa ruzuku kwa wakulima, kuangalia uwezekano wa kupunguza au kuondoa riba za mikopo kuititia taasisi za fedha na au kuongeza muda wa kulipa mikopo iliyokwisha tolewa ili kuwezesha wakulima na kilimo kuendelea kuzalisha. Aidha, ni vyema Serikali ikachukua tahadhali kwa kuweka akiba ya chakula kwa kuwa upo uwezekano wa nchi nyngi duniani kukabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula.

3. Ili kukabiliana na changamoto ya muda mrefu ya uhaba wa sukari nchini, ni vyema Serikali kufanya mapitio ya Sheria ya Tasnia ya Sukari ya Mwaka 2001(*Sugar Industry Act, 2001*) ili kubaini pamoja na mambo mengine mapungufu ya kisheria yanayokwamisha benki za ndani na za nje kushindwa kutoa mikopo kwa viwanda nya sukari kwa kuhofia Serikali kuendelea kutoa vibali kwa wafanyakishara kuagiza sukari nje ya nchi ambayo huuzwa kwa bei nafuu kuliko sukari inayozalishwa hapa nchini.

4. Ili kukabiliana na changamoto ya muda mrefu ya uhaba wa mbolea nchini na kwa madhumini ya utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Viwanda. Kamati inashauri ili kulinda viwanda nya ndani vinavyozalisha mbolea Serikali itekeleze yafuatayo:-

(a) Serikali ianzishe mkakati wa makusudi kuititia maafisa ugani kuhamamisha wakulima kutumia mbolea zinazotengenezwa nchini zenyet mchanganyiko wa virutubisho vinavyohitajika katika udongo na mimea kwa madhumuni ya kuwasaidia wakulima katika kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo.

(ii) Kabla ya kutoa vibali ya kuagiza mbole nje ya nchi, ni vyema tathimini ikafanyika ili kufahamu mbolea inayozalishwa nchini na pungufu ndio iagizwe. Utaratibu unaopendekezwa kutumika hapa ni kama ule uliko kwenye sekta ndogo ya sukari ambapo sukari iliyozalishwa nchini hutumika kwanza kabla ya kuagiza sukari iliyopungua.

(iii) Kanuni ya Mfumo wa Uagizaji wa Mbolea (BPS - 2017) zifanyiwe marekebisho ili zitoe kipaumbele na kumlinda mzalishaji wa mbolea wa ndani tofauti na ilivyo sasa ambapo mwagizaji anapewa upendeleo; na

(iv) Baadhi ya kodi na tozo zinazolipwa na watengenezaji wa mbolea hapa nchini hazilipwi na waagizaji wa mbolea. Suala hili linasababisha ongezeko la gharama ya uzalishaji na kuleta ushindani usio sawa kwenye Sekta na kumuumiza mkulima. Kwa mfano; VAT inatozwa kwa mtengenezaji wa mbolea wa ndani, wakati mwagizaji wa mbolea hatozwi kodi hizo. Kamati inashauri Serikali itathimini kodi hii na kumuobolea mzalishaji na kuwa VAT **Zero Rated**.

5. Ili kukabiliana na changamoto inayolalamikiwa na Wizara mbalimbali kuhusu ucheleweshaji wa maamuzi ya msingi ya kitaifa yanayotegemea kufanywa na Wizara ya Fedha na Mipango, Kamati inashauri Serikali kutafakari kwa kina suala hili kwa mfano; Benki ya Maendeleo ya Kilimo inatoa mikopo kwa wakulima, ili hali Waziri mwenye dhamana na kilimo hana mamlaka juu ya benki hii. Vilevile Soko la Bidhaa Tanzania ambalo linahusika moja kwa moja na mauzo ya bidhaa za nafaka kwa njia ya kieletroniki liko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ambapo Waziri mwenye dhamana na kilimo hana mamlaka juu ya hili.

## **SEHEMU YA NNE**

---

### **4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti

wa Bunge, kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkituongoza kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge la Kumi na Moja na kuliwezesha Bunge letu kutimiza wajibu wake wa kuisimamia Serikali kwa niaba ya Wananchi kwa mujibu wa Katiba. Aidha, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa katika kipindi chote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyooitaoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

- |  |              |
|--|--------------|
| 1. Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa Mb             | Mwenyekiti   |
| 2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb      | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb           | Mjumbe       |
| 4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb | "            |
| 5. Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani, Mb           | "            |
| 6. Mhe. Kangi Alphaxad Lugola, Mb            | "            |
| 7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb             | "            |
| 8. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb          | "            |
| 9. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb            | "            |
| 10. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb                | "            |
| 11. Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb             | "            |
| 12. Mhe. Justine Joseph Monko                | "            |
| 13. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb            | "            |
| 14. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb            | "            |
| 15. Mhe. Pascal Yohana Haonga                | "            |
| 16. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb            | "            |
| 17. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb            | "            |
| 18. Mhe. Devotha Methew Minja, Mb            | "            |
| 19. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb                 | "            |
| 20. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb                 | "            |
| 21. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb       | "            |
| 22. Mhe. Juma Ali Juma, Mb                   | "            |
| 23. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb            | "            |
| 24. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb             | "            |
| 25. Mhe. Anthony Calist Komu, Mb             | "            |

26. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb

"

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa hiki ni kikao cha mwisho katika Bunge hili la Kumi na Moja, napenda kutumia fursa hii kuwatakia Wajumbe wa Kamati na Wabunge wenzangu wote kila la kheri katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2020 na panapo majaliwa ya Mwenyezi Mungu, turejee sote kama tulivyo katika Bunge la Kumi na Mbili ili kuendeleza gurudumu la ujenzi wa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga, (Mb) na Manaibu Waziri Mhe. Hussein Mohamed Bashe (Mb) na Mhe. Omary Tebweta Mgumba (Mb), Katibu Mkuu Ndg. Gerald Musabila Kusaya na Naibu Katibu Mkuu Prof. Siza Donald Tumbo pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge Ndg. Gerald Magili, kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kwa namna ya kipekee naishukuru Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Virgil Mtui na Ndg. Rachel Nyega na Ndg. Jane Ndulesi kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa katika hoja ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb)

**MWENYEKITI,  
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,  
MIFUGO NA MAJI**

12 Mei, 2020

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa. Tunakushukuru sana wewe pamoja na wajumbe wote wa Kamati hii ya Kilimo na Maji kwa kazi nzuri sana ambayo mmekuwa mkiifanya pamoja na Wizara ya Kilimo. (*Makofii*)

Sasa Waheshimiwa kama mnavyojua Wizara hii ina wadau wengi, kwa hiyo, nina maombi mengi sana hapa. Sasa ili kuwatendea haki Wabunge mliong wengi hebu nijaribu kwa dakika saba saba, kadri tunavyoendelea nikiona bado majina ni mengi basi tutapungua kuja kwenye dakika tano tano. Tuanze na dakika saba na tukubaliane kwamba itapigwa kengele moja tu, ikishapigwa hiyo moja basi dakika zako zimekwisha. Basi tuanze na Mheshimiwa Nape Nnauye na atafuatiwa na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliofanya kuhakikisha mambo yanakwenda sawasawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, moja ya tatizo kubwa sana kwenye sekta ya kilimo ilikuwa ni mrundikano wa tozo nydingi sana. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali ya Awamu ya Tano kwa uamuzi wa kizalendo sana wa kuondoa tozo. Nimeona hapa mmeondoa tozo zaidi ya 105, nadhani huu ulikuwa ni uamuzi mkubwa sana. Kwa sababu nina hakika uamuzi huu utakuwa umeleta *gap* kwenye mapato ya Serikali lakini mnajua namna mnavyofidia ila mmemsaidia mkulima wa Tanzania kwa kumuondolea mzigo mkubwa wa tozo zaidi ya 105. Huu ni uamuzi mzuri na

umetokana na maelekezo ya llani ya Uchaguzi, kwa hiyo, naipongeza Serikali Awamu ya Tano wa uamuzi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niipongeze pia Serikali msimu uliopita wa zao la korosho umekwenda vizuri sana ukilinganisha na msimu ule mwингine ambao tulikuwa na mivutano ya hapa na pale. Umeenda vizuri kwa sababu ya uamuzi wa Serikali wa kuachia Vyama vya Ushirika visimamie jambo hili na wao kama Serikali wakavisimamia, nadhani hii ndio imetuletea utulivu huu. Ni matumaini kwamba Serikali wataendelea na utaratibu ambao kwa kweli ni maelekezo ya llani ya Uchaguzi kuuimarisha ushirika katika nchi yetu kwa kuwapa majukumu haya wakayafanya wenyewe. Namna bora ya kuimarisha ushirika ni kuwaruhusu wafanye majukumu haya wenyewe na tumeona kwenye zao la korosho msimu huu mambo yamekwenda vizuri sana. Nachukua nafasi hii kwa niaba ya wakulima wa korosho kuishukuru Serikali kwa uamuzi wa kusimamia, yale ambayo yalipungua nina hakika kwamba tutarekebisha ili mambo yaende vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika hili niwaombe wenzangu wa Serikali, nimeona mmewapa jukumu la kununua pembejeo Vyama vyenyere vya Ushirika. Hili jambo ni zuri sana kwa sababu ndiyo eneo lao, wao wanajua mahitaji, wakulima ni kwao, uchungu ni wa kwao, ninyi simamieni tu mambo yaende sawa lakini wafanye wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa namshauri Mheshimiwa Waziri na kwenye magunia wafanye hivyo hivyo, waachieni wanunue wenyewe, jiondoeni kwenye maneno ambayo hayana msingi. Msimu uliopita moja ya eneo ambalo lilipata tabu kidogo ni suala la ununuzi wa magunia. Nimeanza kusikia maneno tena kama vile mnataka Bodi ya Mazao Mchanganyiko ndiyo wafanye, sijui kina nani wafanye, kwa nini tunaweka watu katikati? Waachieni Vyama vya Ushirika wenyewe wafanye. Kwanza wakulima ni wa kwao, wao ndiyo wana uwezo wa kuingia mikataba na mabenki, kwa hiyo tutapunguza hata gharama za magunia yenyewe, ondoeni watu wa katikati. Kama ambavyo mmeanza vizuri kwa kuwaachia majukumu wanajiiimarisha vizuri endeleeni hivyo

hivyo na kwenye masuala ya magunia hebu jiondoeni waachieni wenyewe wafanye. Wanajua mahitaji yao, wanajua wakulima wao, ninyi wasaidieni kuwaunganisha na kule ambako magunia yanapatikana. Mtakuwa mmefanya jambo kubwa, jambo zuri na kwa sababu ni mwaka wa uchaguzi hebu tusiingize mikono yetu huko, tuendelee kusimamia kama mlivyosimamia mwanzo na mimi nina hakika zao hili litakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwenye llani ya Uchaguzi tulizungumza haja ya kuanzisha na kusimamia mashamba darasa kwenye ngazi ya kata. Sasa kwa miaka zaidi ya 40 tumekuwa na Sherehe za Wakulima, mwanzoni zilikuwa zinaitwa Sabasaba sasa zinaitwa Nanenane lakini ukiangalia tuna Kanda nadhani tisa, kwa hali ya kawaida hizi Sherehe za Nanenane zimebaki kuwa za wakubwa fulani na kwa kweli ni wao ndiyo wanakutana kila mwaka, kama sherehe fulani hivi. Kimsingi lengo ilikuwa tuimarishe kule kwenye kata ili tu-*transfer teknolojia*. Kwa sababu leo katika Kanda, kwa mfano, Dodoma kuwaleta wakulima kuja hapa ni uongo watakuja wale tu ambao wana uwezo na wengi wao ni viongozi lakini mkulima wa kweli lazima tummfuate kwenye kata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu, pamoja na kazi nzuri iliyofanyika, sasa hebu twendeni, llani inasema tuanzishe mashamba darasa kwenye kata, hii Nanenane ingekuwa inafanyika kwenye kata, zile gharama za kuwaleta watu hapa zisingekuwa za msingi. Kwa hiyo, nashauri tupeleke sherehe hizi huko na tuzisimamie na mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naipongeza Serikali, nawashukuru kwa kazi nzuri mnayofanya na nawatakia kile la kheri. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nape Nnauye.

Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Selasini atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, nadhani yuko kule Msekwa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati kwa kutuletea hotuba ambayo tunaijadili jioni hii ya leo na nawapongeza kwa hotuba walizozitoa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, niwashukuru Watanzania wote waliotupa pole kutokana na msiba wa kaka yangu Dkt. Masumbuko Lamwai ambaye tulifanya mazishi yake siku ya Ijumaa. Kipekee nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wewe Mheshimiwa Spika, Mawaziri, Wabunge wenzangu, Majali pamoja na Mahakimu, Mawakili pamoja na Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi ambacho Dkt. Lamwai alikuwa Mwanasheria kwa kutupigia simu na kutupa pole. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, leo tuko hapa huko mtaani kuna maneno maneno hivi kwamba kuna baadhi yetu tumeondolewa kwenye chama na wengine kujielea. Sasa vyombo vyahabari vimeniuliza sana sitaki kuongelea jambo hili lakini kila nikitafakari nakumbuka Mkutano wa Katiba hasara kubwa tuliyopata.

Mheshimiwa Spika, kwenye Katiba Pendekewa utakumbuka kulikuwa na pendekizo la Tume Huru ya Uchaguzi na kulikuwa pia na pendekizo la muda maalum wa Wabunge. Sasa hivi kuna kilio cha Katiba Mpya sasa kila nikiona haya yanayotokea hapa yakukataakata mambo, nakumbuka tulivyokataa lile Bunge la Katiba na matokeo yake tukapata hasara hii kubwa ya Tume Huru ya Uchaguzi. Kumbe sisi tunaohusika na jambo hilo pengine tungelizwa tungeweza kusaidia ili tusiingie kwenye hasara kubwa zaidi. Kwa hiyo, hili nafikiri tutaliacha, nitaongea huko na Waandishi wanaoniuliza lakini nipo na ninaendelea kuwahudumia watu wangu.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza sana katika Bunge hili kuhusu zao la kahawa. Bahati nzuri sana Mheshimiwa Waziri kule kwake Mbozi Kahawa inalimwa. Naendelea kuiomba Serikali na kuikumbusha wakulima wa kahawa wanatumia gharama kubwa sana katika kupata kilo ya kahawa lakini mauzo ya kahawa yako chini sana jambo ambalo linawafanya wakulima kukata tama. Matokeo yake kama kule kwetu Rombo wanabadilisha lile zao na ndizi ambazo hazina faida yoyote kubwa kwao ni kwa sababu wanapata fedha za mara moja basi wanakuwa na hamu ya kuendelea kulima zao la ndizi. Tunaiomba Serikali iangalie namna ya kupunguza gharama za uzalishaji kwenye zao la kahawa na vilevile kusimamia soko ili wakulima waweze kupata kipato cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni zao lilielowekwa upande wa matunda la parachichi. Zao la parachichi limekua na muamko na msukumo mkubwa sana lakini soko lake pia nalo lina mashaka. Kule kwetu Rombo wenzetu kutoka Kenya wanakuja kununua maparachichi wanayasafirisha katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, katika hili nakumbusha Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye Mei Mosi pale Moshi aliongea na wadau na wakamuomba ile *half mile* kule Rombo itolewe kwa wananchi ili waweze kulima parachichi. Naomba sana kama Wizara italichukua hilo ili iweze kujadiliana na Wizara ya Maliasili eneo lile liweze kutolewa kwa wananchi kwa ajili ya kulima zao la parachichi ambalo kule linastawi vizuri sana na kulitafutia soko ili wananchi waweze kupata kipato cha kutosha na Serikali iweze kupata mapato kutokana na zao hili.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo napenda kulizungumza jioni ya leo ni kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Mwaka huu mvua zimenyesha nyingi sana na mito ya misimu mingi sana katika Wilaya ya Rombo kwa mfano Mto Marwe,

Mto Ungwasi na mingine imejaa maji na maji yote yamekimbilia Kenya.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka nilishawahi kutoa pendekezo hapa kwamba makorongo ya mito hii ambayo ni ya msimu yangeweza yakinatengenezwa, yakapatikana mabwawa halafu baadaye tukaweza kutumia maji yale kwa ajili ya kilimo hata na mifugo kwa sababu yale maji yanapotea tu. Siyo Rombo peke yake hata hapa kwako Kongwa, Kibaigwa maji mengi yanatoka Kiteto sana sana yanaharibu tu barabara pale na mazao ya wakulima lakini ungefanyika utafiti wa kuweza kujenga mabwawa makubwa . Siera Leone waliweza, sasa hivi kuna *manmade lakes* kubwa sana ambazo zinatokana na maji haya ya mvua. Kama tungefanya hivyo nchi hii tungeweza tukapata *source* kubwa sana ya maji kwa ajili ya umwagiliaji, mifugo yetu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nafikiri hayo yanatosha na nazidi kuunga mkono misimamo ambayo inachukuliwa ili Wabunge tuweze kufanya kazi kwa sababu katika utaratibu wa Mabunge yote duniani walio wachache wanasilizwa, walio wengi wanaamua. Haiwezekani hata siku moja walio wachache kila mara wakafikiria kwamba hoja zao zitapita, sijui ni Bunge gani katika dunia hii hilo linawezekana. (*Makof*)

Kwa hiyo, mimi nafikiri ni wakati muafaka sisi tulio wachache tulete hoja zetu, tuzijenge kwa nguvu zetu zote, tuzifanyie utafiti kwa nguvu zetu zote ziingie katika mfumo ili tuweze kuwaambia Watanzania kwamba ile ni kazi yetu badala ya kukaa pbeni. Kwa mfano, hii hoja ya kilimo tuna hasara kubwa kwa sababu hakuna mawazo mbadala, hakuna maoni lakini maoni yapo tena inawezekana ni mazuri sana lakini kwa sababu nafikiri za kisiasa au kwa sabbau za kibinafsi tunajikuta hatuna maoni hayo. Tuna fikra ya *political mileage*, hii ni hasara kwa Bunge nah ii ni hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nakushukuru kwa nafasi. (*Makof*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Joseph Selasini kwa mchango wako na kweli sehemu ya tatizo letu mojawapo kubwa ni hilo, wachache wanataka kuamua, wengi wawe wanasakiiza, demokrasia ya namna hiyo haiko popote pale, wengi wataamua, ndiyo demokrasia na wachache watasikilizwa.

Mheshimiwa Sakaya kama unanisikia kule Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pudensiana Kikwembe.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Kilimo ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushauri wetu kila mwaka kwenye Wizara hii ya Kilimo lakini bado lile Agizo la Makubaliano ya SADC ya kupanga 10% ya bajeti ya nchi zetu iende kwenye kilimo bado hatujaweza kuifikia. Ukiangalia fedha inayotengwa kwenye bajeti hii ya Wizara ya Kilimo kwenye nchi yetu ya Tanzania na umuhimu wa Wizara yenye sekta ambayo inaa jiri *almost* watu zaidi ya asilimia 75 ya Taifa hili haiendani na umuhimu na *sensitivity* ya Wizara hii ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba niseme kwamba zao la tumbaku limeleta mchango mkubwa sana kwenye uchumi wa Taifa hili lakini miaka yote limeendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali ambazo kiukweli nyingine ziko ndani ya Serikali wanashindwa kuzitatua. Changamoto mojawapo ambayo tunaililia kila siku ni suala la masoko. Mwaka jana Kampuni zilikuwa tatu tu; *GTI, Alliance One, TLTC*; mwaka jana TLTC kutokana na ushuru mkubwa na tozo mbalimbali ikashindwa kustahamili ikasema inaondoka. Tulivyoihoji Serikali wakasema wameongea nao, wame-reconcile kampuni iendelee leo kwa bahati mbaya sana wamefunga viwanda vyao viwili Mkoa wa Morogoro, wameondoka kwenye soko hawapo tena. Hili ni pigo kubwa sana kwa wakulima wa tumbaku kwa sababu wanalima masoko hakuna, wanabakiwa na makisio makubwa na

tumbaku inaharibika au kununuliwa kwa bei ya makinikia hii ni hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka jana huo huo Bodi ya Tumbaku ikaleta makampuni mengine mawili ambayo ni Magefa pamoja na Grand kwamba watakuja kununua zao la tumbaku na wakasema kwamba wanaanza kununua makisio yaliyokuwa yamebaki kwa maana ya ziada iliyo kuwa imebaki mwaka jana. Magefa wakanunua tumbaku tangu tarehe 02/12/2019 ya kiasi cha USD 600,000. Mpaka leo napoongea hawajalipa hata shilingi moja kwa wakulima. Haya ni maumivu mengine, kampuni imeletwa na Bodi ya Tumbaku haina uwezo leo ni miezi sita mkulima analia hajalipwa hata shilingi moja.

Mheshimiwa Spika, leo Kampuni hizo hizo mbili; Grand pamoja na Magefa wameingia mkataba na wakulima kulla tumbaku zilizopo mashambani sasa hivi leo tunaona ni maumivu mengine ikiwa hawajaweza kulipa makinikia tangu mwaka jana uwezo wa kununua tumbaku mpya mashambani wanaipata wapi? Kwa hiyo, kuna hatari kubwa mwaka huu tumbaku nydingi ya wakulima ikabaki tena kwenye maghala haina wanunu zi.

Mheshimiwa Spika, pia tangu mwaka juzi kuna kampuni nydingine ambayo inataka sana kununua tumbaku katika Mkoa wa Tabora na maeneo mengine inaitwa BAT lakini imezungushwa kweli kweli. Hii kampuni ili wahi kununua tambaku mwanzoni baadaye ikaenda Kenya, nadhani ilipata misukosuko na urasimu wakaenda Kenya kununua tumbaku. Sasa hivi wame-settle kule Kenya wana viwanda vyao kule wamekuja mwaka jana wanataka waanze kununua tumbaku hapa Tanzania leo ni mwaka wa pili wanazungushwa hawajapewa vibali waanze kununua tumbaku.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali watuambie ni kwa nini BAT mpaka leo hawapewi kibali waanze kununua tumbaku. Pia Serikali ituambie nini mkakati wake kuhakikisha kwamba tumbaku ilionunuliwa na Magefa ya zaidi ya Dola

600,000 inalipwa kwa wakulima. Vilevile watuambie zile tumbaku ambazo ziko mashambani ambapo Magefa na Grand ndiyo wanunuzi na ambao wameonyesha uwezo mdogo sana wa kununua tumbaku zitanunuliwa kwa namna gani? Kwa hiyo, ni lazima tupate majibu leo.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la ajabu, tumbaku inayolimwa kwa shida kubwa sana, pembejeo mfuko mmoja ni Sh.100,000 mpaka Sh.120,000, anaweka dawa mwenyewe shambani, hakuna zao lenye mateso kama tumbaku lakini leo tumbaku inanunuliwa kwa Dola 0.55, ni mateso na ni maumivu. Ndiyo maana mkulima wa tumbaku habadiliki.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali wakati wa *kuwind up* Mheshimiwa Waziri atuambie namna gani tumbaku ya Tabora itanunuliwa na asilimia 60 ya tumbaku yote Mkoa wa Tobora inalimwa Kaliua. Kwa hiyo, wakulima wa Kaliua ndiyo watakaoathirika zaidi na mateso haya ambayo kwa kiasi kikubwa ni kwamba Serikali imeshindwa kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona zao la tumbaku lina matatizo kutokana na kwamba hatuna viwanda, tulikubaliana na Serikali na ikaahidi kujenga kiwanda Mkoa wa Tabora kwa ajili ya kupunguza usumbufu wa kupeleka tumbaku mbali na kuleta ajira kwa vijana wa Mkoa wa Tabora. Leo ni mwaka wa nne, kwa nini kiwanda pale Urambo hakijengwi ambapo tayari kuna eneo limetengwa na makubaliano yameingiwa. Naomba kujua kwa nini Serikali haijengi kiwanda katika Mkoa wa Tabora?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, hii Kampuni ya *BAT* ilikuwa na uwezo wa kutumia kiwanda chochote hapa nchini lakini hamna viwanda, *TLTC* ameshafunga viwanda. Naomba sana suala la tumbaku inayoingiza kipato kikubwa liangaliwe kwa maslahi ya Wanakaliua na Taifa. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Sakaya, Kamishina.

Sasa Waheshimiwa kwa kweli orodha yangu ni ndefu, ili niwatendeeni haki turudi kwenye dakika tano tano sasa ili angalau mfikie mahali fulani. Tuanze na Mheshimiwa Dkt. Pudensiana Kikwembe atafuatiwa na Mheshimiwa Destery Boniventura Kiswaga kule Msekwa.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwani bado ananipigania. Pili, napenda kuwapongeza Mawaziri wote wa sekta zote na Manaibu Waziri chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa uongozi mahiri ambao uko chini ya Jemedari wetu, Rais wetu mpandwa Dkt. John Pombe Magufuli ambaye ni Simba wa Yuda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru wewe mwenyewe kwa uongozi wako wa Bunge pamoja na Naibu Spika, Dkt. Tulia na Wenyeviti wote wa Bunge pamoja na watumishi wote wa Bunge na Wabunge wote kwa ujumla kwa namna ambavyo tumekuwa tukishirikiana nao namna ya kuwasilisha hoja zetu. Wewe umekuwa ni kiongozi ambaye umekuwa ukizisukuma hoja hizi kwa Serikali na zimeweza kufanyiwa kazi. Kwa kweli, nawshukuruni sana Mawaziri wote chini ya Serikali hii.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja katika suala zima la stakabadhi ghalani. Suala hili limekuwa na kizaazaas hasa ukizingatia kumekuwa na mtafaruku. Najua nia ya Serikali ni njema katika kutaka kukusanya kodi na kukuza wigo wa kupata mapato lakini niiombe Serikali kuitia hili suala la stakabadhi ghalani kumekuwa na matamshi ambayo Mheshimiwa Rais alikwishayaelekeza namna gani wakulima wasibughudhiwe namna ya kupanga mazao yao yauzwe wapi na yanunuliwe wapi.

Mheshimiwa Spika, naliongelea hili kwa sababu ni juzi tu wiki iliyopita Ijumaa ndiyo limetoka kusuluhihwa ndani ya Jimbo langu la Kavuu katika Kata ya IKuba. Kwanza kabisa,

napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ameweza kutoa ushirikiano wa karibu kabisa pamoja na Serikali Mkoa wa Katavi. Kwa namna ya pekee kikishukuru Chama cha Mapinduzi katika Mkoa wa Katavi kinachoongozwa na Ndugu yangu Mzee Beda Katani, Katibu wake dada yangu Lucy Boniface pamoja na M-NEC wetu Mheshimiwa Gilbert Kinyonto lakinia pia pamoja na mlezi wetu wa Mkoa, Mheshimiwa Pereira wakiongozwa na Dkt. Bashiru, Katibu Mkuu wetu wa Chama cha Mapinduzi kwa namna ambavyo wameweza kutoa ushirikiano na kuweza kulitatau tatizo hili katika Jimbo langu la Kavuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumuomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na suluhisho lote lililokwishatokea katika Jimbo letu la Kavuu, wananchi wa Kavuu tunakuomba asilimia 90 ni wakulima, kuwe na aina mbili za masoko basi; la kwanza ambalo litamruhusu mkulima kuuza mazao yake kwa bei aliyopenda ili mwenyewe achague bei atakayouza.

Mheshimiwa Spika, hilo suala la stakabadhi ghalani basi liweze kufanyiwa utaratibu upya na likaelimishwe kwa wananchi ili lisiveze kuleta mtafaruku na Serikali kwa sababu mkulima yule kalima mwenyewe, kanunua mbegu mwenyewe, kaweka mbolea mwenyewe lakini inapofika kwenye mazao yake tunaanza kumpangia bei jambo ambalo linaleta mtafaruku mkubwa kwa wananchi hasa ukizingatia sasa hivi familia nyingi zimerudi nyumbani, watoto wamerudi nyumbani, mkulima anataka auze mazao yake ili aweze kulisha familia nyumbani kutokana na janga hili la *Corona*. Kwa hiyo, niwaombe sana Serikali twende nalo kwa utaratibu.

Mheshimiwa Spika, narudi kushukuru uongozi wangu wa Chama, Mkoa wa Katavi ukiongozwa na Mzee Beda Katani, kwa kweli wameweza kulishughulikia jambo hili kwa burasa na limeweza kwenda vizuri. Kwa hiyo, tuwe na masoko ambapo la kwanza linamhusu mkulima moja kwa moja ambapo atauza bidhaa zake mwenyewe na lingine hilo ambalo labda kama kuna wanununzi wengine nje ya Mkoa, tunajua lengo ni zuri la kutaka kukusanya kodi na kutunisha

mfuko wa mkulima lakini pia tu-*handle* hilo jambo kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine napenda kuongelea suala la miradi yangu miwili ya maji; ya Umwagilianji Mwamapuli pamoja na Kirida. Naomba miradi hii iingizwe kwenye mpango.

**SPIKA:** Bahati mbaya muda hauko upande wako.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nawatachia kila la kheri Wabunge wote na Waheshimiwa Mawaziri kwa namna ambavyo tutaendelea huko mbele na nina hakika kwa kudra ya Mwenyezi Mungu wote tutarudi katika mjengo huu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Kiswaga kule Msekwa atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Salma Kikwete ajiandae.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza naomba niipongeze Serikali kwa kazi kubwa inayoendelea kufanya; Wizara ya Kilimo yenye, Waziri, Manaibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na Wasaidizi wake. Kazi kubwa ambapo mmeanza kuboresha kilimo Watanzania tunaiona. Yako mambo madogo ambayo tunaweza kuyashauri ambayo kimsingi Wizara wakati mwingine inaweza kuwa inatoa miongozo ambayo haijaifanyia utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, mfano, Wizara imetoa mwongozo wa namna mazao ya mikunde yatakavyonunuliwa kwenye Ushirika. Wanasema kwamba mwananchi wa kawaida apeleke kwenye Ushirika akauze halafu baadaye Ushirika upeleke kwenye mnada.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, *nature* ya mazao haya ya kwetu, mfano, Magu, wakulima wanakuwa na kilo 20, 30 akizidi sana kilo 40. Anapokwenda kuuza ni ana shida labda

akasage, akanunue dawa na matumizi madogo madogo. Sasa unapomuelekeza kwenda kuuza kwenye Ushirika halafu akopwe, asubiri siku zaidi ya kumi ndiyo zipelekwe kwenye mnada bila bei elekezi, tunamrudisha mkulima huyu kwenye ubwanyenye ambao tumeshatoka huko.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alisema kwamba hatutaingilia mazao ya wakulima ina maana sasa ninyi Wizara mmeanza kukiuka agizo la Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mliwahi kutamka kwamba hamtaingilia mazao ya wakulima lakini mnatengeneza mfumo wa *TMX* kupeleka kwenye mnada bila bei elekezi. Ushauri wangu ni kwamba kama tunaanzisha suala hili tuwezeshe Ushirika uwe na fedha ili mkulima anapopeleka mazao yake moja kwa moja aweze kulipwa na hawa watu wa Ushirika wao wapeleke sasa kwenye soko ili waweze kuuza kwenye mnada, tutakuwa tumemsaldia mwananchi. Leo huko Magu kuna hali mbaya sana, wakulima wameshindwa kuuza choroko zao na wameshindwa wapeleke wapi, wameweka tu ndani, hebu pia tuone namna ya kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wakati Mheshimiwa Waziri anatoa mwongozo huu kuna wafanyabiashara waliokuwa wamenunua choroko ambao wana shehena zaidi ya tani 400 ziko ndani hazijauzwa. Wamepeleka kwenye mnada soko likashuka, soko la kwanza Sh.1,200, soko la tatu ikafika Sh.980. Kwa hiyo, wafanyabiashara hawa wameingia hasara, je, Serikali tutafidia hizi hasara zinazotokana na miongozo ambayo haina tija?

Mheshimiwa Spika, hebu tujigeuze tujiulize, je, hizo shehena zingekuwa za Mheshimiwa Waziri ingekuwaje au tunapoandaa mwongozo huu na shangazi na bibi wapo unamwandalia mwongozo wa kwenda kukopwa ni sasasawa? Naomba tutafakari hili na tubadilishe mwelekeo hasa Magu. Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ikiwezekana twendeni Magu tukazungumze na hawa wafanyabiashara pamoja na wakulima ili tuone namna

ya kuweza kuwasaidia ili wafurahie Serikali yao ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa sana na hapa mimi natoa ushauri. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa hakuna sababu ya mwaka huu Mheshimiwa Rais kufanya kampeni kwenye majimbo yetu, tuko sisi ambao tunaweza kufanya kampeni huko yeye akaye tu na waandishi wa habari aseme Watanzania nipeni kura ili tuweze kupunguza gharama ambazo Mheshimiwa Rais anaweza kuzitumia ziende kwenye mradi mingine.

Mheshimiwa Spika, wewe nawe umetikiswa sana lakini pamoja na kutikiswa umesimama imara na siyo muyumbifu, tunakupongeza sana. Huwezi kuwa jemedari bila kupigana vita, umepigana vita, Mheshimiwa Rais amepigana vita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo yamefanywa na Serikali hii ni makubwa. Mheshimiwa Rais amenunua ndege, amejenga reli ya *Standard Gauge*, haya yote ni mambo yalikuwa yameshindikana na huyu tunamuita ni Rais wa mambo yaliyokuwa yameshindikana. Haya mambo hayajawahi kufanya dunia hata kuamua tu kwamba hatuwezi kukaa ndani kwa sababu ya *Corona* hili ni jambo la kianaume, lazima Mheshimiwa Rais apongezwe.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana mheshimiwa Destery Boniventura Kiswaga.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, naleta ombi kwako kama inawewekana tulete mapendelekezo ya kumpa...

**SPIKA:** Nakushukuru sana.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, huyu ni baba wa pili wa Taifa la Tanzania kwa mambo makubwa aliyoafanya kwa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Magu, Destery Boniventura Kiswaga. Hiyo maana yake sasa shughuli inakuja kuanzia Julai, Agosti, Septemba, moto utawaka kila mahali unaweza ukaona hiyo ni *just introduction to the camp*.

Tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Vrajjal Soni na Mheshimiwa Salma Kikwete ajiandae. Mheshimiwa Jitu Soni Msekwa, dakika tano.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia siku ya leo. Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri na timu nzima ya Wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya na pia kwa kupokea maoni mbalimbali ya Kamati na kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo machache ambayo napenda nishauri Serikali iweze kuyafanyia kazi ili kuboresha sekta hii ya kilimo. Eneo la kwanza naomba Serikali iangalie namna ya kuendelea kuboresha na kuweka bajeti ya kutosha kwenye utafiti ili vituo vyetu vya utafiti viweze kufanya kazi vizuri zaidi na waweze kutoa huduma kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, pili ni Benki yetu ya Kilimo. Serikali ingeongeza mtaji katika Benki ya TADB. Pia Benki ya Kilimo 20% ya fedha hizo zingetengwa kwa ajili ya umwangiliaji ili sekta ya umwagiliaji pia iweze kupata fedha kwa kuititia sekta binafsi badala ya kutegemea Serikali kujenga miundombinu yote ya umwangiliaji.

Mheshimiwa Spika, mbali na hayo, kulikuwa na mapendekezo ya Kamati pia kuwa sekta ya mbogamboga na matunda yaani *horticulture* imeshika kasi na ndiyo *quick win* inaweza kuleta mafanikio makubwa hasa kwa wakulima kwa kupata fedha nyingi na faida kubwa. Serikali ingeangalia namna ya kuunda Wakala wa *horticulture*, badala ya kuwa kitengo kidogo ndani ya Wizara ingekuwa na Wakala wa kudumu wa *horticulture* ili ifanye kazi vizuri zaidi. Leo ukiangalia mazao yale ya asili tayari *horticulture* yameshayapita kwa mbali hayo mazao ambayo yana bodi zake.

Mheshimiwa Spika, mbali na hiyo pia napenda Serikali iendelee kuangalia namna ya kulinda viwanda vyta ndani, viwanda vyote ambavyo vinasindika mazao mbalimbali ya kilimo lakini pia kiwanda cha mbolea ambapo tunaweza kuzalisha mbolea yenye viwango na tayari *TBS* pamoja na TARI wamethibitisha viwango hivyo ni vizuri. Badala ya kuangiza kutoka nje vile ambavyo tunaweza kuzalisha ndani ya nchi basi tuweze kutumia bidhaa ya Kitanzania ambapo fedha zote zitaendelea kubaki humu na kuzunguka katika uchumi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tuna maeneo mbalimbali ambapo tunaangiza mbogamboga na matunda kutoka nje ni vizuri tukawekeza ili bidhaa hizo ziweze kuzalishwa hapa nchini. Niipongeze Wizara kwa kufikiria na tayari mchakato umeanza wa kupitia upya na kuja na sera na sheria ya kilimo ambapo patakuwa na mageuzi makubwa. Muhimu katika hilo pia Serikali iangalie namna ya kulinda ardhi za kilimo. Sasa hivi ardhi yetu yenye rutuba kubwa inachukuliwa kwa ajili ya makazi na kujenga viwanda yaani inabadilishiwa matumizi baadaye ardhi ya kilimo yenye rutuba itatoweza na tutakuwa na kazi ngumu kuwekeza katika maeneo mengine. Ni vizuri hata katika mji kwa mfano wa Dodoma zabibu itatoweza tusipokuwa waangalifu. Ni vizuri mashamba ambayo yapo ndani ya miji yalindwe kabisa kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini mbali na hiyo Serikali iendelee kutimiza ile azma ya kuhakikisha kwamba ile *blueprint* inafanyiwa kazi ili viwanda vyote vyta ndani viweze

kushindana na vya nje. Tunaipongeza Serikali tayari imechukuwa hatua kubwa lakini sasa itekeleze yote kwa mpigo ili tuwe na mabadiliko makubwa kwa haraka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Wizara, uongozi huu sasa umeleta mabadiliko makubwa hasa katika sekta ya ushirika. Muhimu kuliko yote lazima tujue lazima ushirika uwe wa hiari siyo ushirika wa kulizamisha. Ni vizuri jambo hilo likaeleweka, ushirika ushindane na sekta binafsi kama ilivyo katika maeneo mbalimbali duniani ili mkulima asiingiliwe katika mazao yake hasa kuhusiana na bei, Serikali ibaki kudhibiti na kurekebisha mahali ambapo hapajakaa vizuri. Mambo haya yakifanyiwa kazi nina uhakika sekta ya kilimo itakua.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la bajeti. Kama tulivyokubaliana kwenye *Malabo Declaration* pamoja na Maputo kwamba asilimia 10 ya bajeti lende kwenye kilimo. Ukiangalia afya leo hii Serikali imejitahidi sana hata tukijumlisha yale mengine wanayosema kwamba yanaenda kwenye sekta ya kilimo kwa mfano barabara, nishati, miundombinu, tunaipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa na nzuri inayofanya lakini bado bajeti ya maendeleo ambayo inaenda vijiji ambapo kuna kilimo haijafikia ile 10%. Boresheni kila kitu lakini bajeti iwe 10%, ikifika hapo mtaona mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Spika, kilimo kikiweza kufanya vizuri na mwananchi mmoja mmoja akiwa na uchumi mzuri basi na Serikali itapata kodi na mapato moja kwa moja kutoka kwenye nguvu ambayo wananchi watatumia (*consuming power*). Kwa hiyo, tunaomba Serikali iendelee kuboresha sekta ya kilimo ili na yenye we iweze kupata mapato ya kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, tumependekeza kwa miaka minne sasa Serikali iondoe kodi kwenye mitambo ya kuchimba maji na mitambo ya kutengeneza mabwawa na malambo. Kama wengi walivyosema tukifanya hivyo tutaweza kujenga wenye we badala ya kutegemea Serikali kutujengea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni. Tunaendelea na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Hatimaye nimshukuru Rais wangu mpPENDWA Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kunitfea na kuwa mionganini mwa wale wateule wake 10 kuingia kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya katika kipindi chake cha miaka mitano. Mambo aliyoafanya ni makubwa sana na yanaonekana, mwenye macho haambiwi tazama, anayaona kila kona ya nchi yetu ya Tanzania. Hongera sana Mheshimiwa Rais wetu, tuko nyuma yako na tunakuunga mkono. Kutokana na kazi hizi nzuri na kubwa ulizozifanya hakuna mashaka hata kidogo mwaka 2020 utapita kwa kura nydingi na za kishindo ambazo hazijawahi kutokea. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nikupongeze na wewe kwa kazi kubwa na nzuri ya kulismamia Bunge hili ambalo ni Bunge lenye mabadiliko makubwa mionganini mwao wakiwa vijana ni wengi, wenye miamko mikubwa lakini umeweza kuifanya kazi yako kwa vizuri na kwa umakini mkubwa. Hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa kazi kubwa na nzuri na uwasilishaji wake mzuri ambao ameweza kuuonyesha pamoja na Manaibu Mawaziri wote pamoja na wataalam wenu mmefanya kazi

kubwa na nzuri, hongereni sana tena sana. Nawapongeza na Mawaziri wote kwa kazi kubwa mlionifanya bila kumsahau Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu ambaye ndiye anasimamia Serikali hii hapa Bunge. Hongera sana kwa kazi hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka niwapongeze kwa mafanikio makubwa ambayo mmeyapata kwenye Wizara ya Kilimo. Tunaamini na tunajua kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu. Chakula ndiyo mhimili, ndiyo uhai wa mwanadamu na ndiyo kila kitu. Bila chakula kwa kweli mwanadamu hana mafanikio na anakuwa katika unyonge. Mmeongeza tani milioni 2.7 za ziada, ina maana kwamba hapo tatizo la chakula hakuna.

Mheshimiwa Spika, sasa nachotaka kusema ni nini? Nachotaka kusema ni kwamba, kwa kuwa tumeongeza hizi tani millioni 2.7 kama tukijikita kwenye kilimo cha umwagiliaji ina maana hizi tani zinaweza kuongezeka zaidi ya mara tatu au zaidi. Kupanga ni kuchagua, tunajua na tunaamini kwamba katika nchi zetu hizi za Afrika Mashariki wengi wanategemea chakula kutoka kwetu wakati wanapopata matatizo.

Sasa sisi tukijikita huku ina maana kwamba tutakuwa na chakula cha ndani, tutakuwa na chakula cha kuuza nje ya mipaka yetu ndani ya Afrika Mashariki lakini vilevile tutakuwa na chakula cha kuuza maeneo mengi ndani ya Bara letu ukizingatia kwamba sisi tuna miundombinu mizuri. Sisi tuna mito, maziwa na mabonde mazuri, tukiamua kuzalisha huko kwa kweli tunaweza tukazalisha na tukaona maajabu makubwa ndani ya taifa letu. Ushauri wangu tuongeze tija kwenye kilimo cha umwagiliaji kitatusaidia sana. Hilo la kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili, tunapofanya kilimo cha umwagiliaji lazima tutengeneze mazingira ya kuwa na Maafisa Ugani wa kutosha. Hongereni sana kwa kuongeza Maafisa Ugani wengi ambaao wanaweza wakaenea maeneo mbalimbali. Hata hivyo, tufanye jambo moja, tuwasaidie vitendea kazi kwani hawana. Sasa utasimamiae kazi wakati

kitendea kazi hakuna. Kwa hiyo, hili ni lazima tuangalie kwa mapana yake ili tuweze kuwarahisishia kazi zao ambazo wanazifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie, tumeambiwa katika hotuba asilimia 93 ya mbegu zinazalishwa hapa nchini lakini kuna tatizo tulipata mafuriko makubwa katika kona zote za nchi yetu. Wananchi walitakiwa waendelee na maisha yao baada ya mafuriko yale lakini tulipokuwa tunahitaji mbegu kidogo hapa kulikuwa na upungufu. Ushauri wangu ni lazima tufanye juhudhi ya kuwa na mbegu nydingi sisi wenyewe pindi itakapotokea dharura ili ziweze kuwasaidia wananchi kuendelea na maisha yao. Hii itasaidia sana tena sana, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, sikutaka niseme mengi, hayo yanatosha na muda wangu umenitupa mkono lakini nimpongeze sana na niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano mkubwa mlionipatia nikiwa hapa Bungeni. Nawatakia kila la kheri na mafanikio, mtakaporudi wawachague kwa kura nydingi hatimaye mrudi tena Bungeni ili tuendelee kuchapa kazi hasa Mheshimiwa Spika tunakutakia kila la kheri. Wananchi kule waone kwamba hakuna mwingine zaidi ya Spika wewe Mheshimiwa Job Ndugai. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniskiliza. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana mama yetu Mheshimiwa Salma Kikwete. Tunakushukuru sana na sisi tumefarijika sana kuwa nawe, umetutia moyo, umekuwa nasi hasa kwenye michezo. Hatukutarajia wala hatukutegemea lakini umechanganyika nasi na kwa kweli hatuwezi uwepo wako katika Bunge hili la Kumi na Moja, ahsante sana. (*Makof*)

Tunaendelea na Mheshimiwa David Silinde atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava kule Msekwa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipatia fursa hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijakwenda kwenye hoja kama mbili tatu za Jimbo langu, jambo la kwanza niwashukuru sana wananchi wa Mombasa ambao wamenipa ushirikiano mkubwa kwa kipindi cha miaka mitano.

Vilevile niishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Ninayasema haya kwa sababu wananchi wa Mombasa wamenituma niyaseme haya na wanasema kitu kimoja ambacho niliambiwa kule Mombasa, ukienda Bungeni fanya siasa zinazovuka mipaka, hicho ndicho walichoniambia.

Mimi kama mwana diplomasia ninayetarajia kuwa mwana diplomasia mkubwa siku za mbele lazima nifanyes hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kikubwa vilevile nikushukuru na wewe kwa ushirikiano wako na utendaji wako mkubwa ambao umeuonyesha kwetu katika kipindi chote cha miaka mitano. Wananchi wa Mombasa walitamani kweli wasikie ninawajibu lakini niwaambie tu kwa kifupi, tumesikia kwenye vyombo vyaya habari Mbunge wao amefukuzwa kwa kutimiza wajibu wake wa kibunge, jukumu ambalo wao ndiyo walinituma kuja kulifanya katika Bunge lako. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi natambua nina wajibu kwa taifa langu, nina wajibu kwa wananchi kwa maana ya Jimbo langu, nina wajibu vilevile kwa chama changu lakini nina wajibu kwa dhamira yangu pia. Kwa hiyo, haya yote nimekuwa nikiyatekeleza kwa kipindi chote na nitaendelea kufanya na naamini *Inshallah* Mwenyezi Mungu akitujalia Oktoba tutorudi tena na tutaifanya hii kazi ya wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mombasa wanashukuru sana kwa Mradi wa Maji wa Naming'ong'o ulioko Makao Makuu ya Chitete. Mradi ule umeleta matokeo makubwa sana, leo ardhi imepanda thamani, tunazalisha

muda wote, hatuna tatizo kama ambayo yalikuwepo awali. Mradi huu tuliuomba miaka mingi na katika kipindi changu umeweza kutekelezeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini tuna maombi mapya, tunataka kwenye Bonde la Kamsamba kule Serikali iweze kuangalia kule kupeleka mradi wa umwagiliaji kwa sababu tuna idadi kubwa ya watu kule karibu na Ziwa Rukwa. Mlileta mradi naamini tutapata faida kubwa kama ambavyo wamepata wananchi wa eneo la Chitete, Kata ya Chitete, Tarafa ya Msangano.

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Mheshimiwa Waziri akizungumzia athari ya Covid-19 katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya kilimo. Nikiri wazi kwamba Covid-19 kwa maana ya *Corona Virus* ni janga la dunia nzima siyo janga la Tanzania peke yake wala siyo janga la Chama cha Mapinduzi au la CHADEMA, hili ni janga letu sote na tunapaswa tupambanie hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilizungumza hapa siku tatu zilizopita, duniani kote vyama vyote vya siasa kwenye kila nchi vinaungana kwenye matatizo ya pamoja. Vyama huwa havishindani kwenye matatizo ambayo yanaweza kupelekea vifo vya wananchi wake. Kwa hiyo, nimeona tutumie fursa hii kuwaambia Watanzania kuna matatizo lazima muungane, mnaweza mkatofautiana kwenye mitizamo lakini yanapofika majanga makubwa kama haya, unaweza kuona pale *President Trump* na Nancy Pelosi ambaye ni Spika wamekuwa na tofauti zao lakini kwenye janga la *Corona* unaona wote wanazungumza lugha moja ili kusaidia taifa lao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, majanga kama haya yanapotokea tungependa Bodi ya *NRFA* pamoja na Bodi ya Mazao Mchanganyiko katika kipindi cha sasa ianze kununua mazao yale wakati huo huo waweze kutoa fursa kwa wananchi kuuza yale mazao yao nje ili waweze kupata faida zaidi. Kwa sababu hakuna tatizo linalokuja bila faida, kuna upande kunakuwa ni tatizo lakini na sisi lazima tufikiri kichumi,

ufikiri namna gani tunaweza kutumia nafasi hii ili kuwasaidia wananchi wetu waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, Halmashauri ya Momba moja ya zao la biashara tunalolima ni ufuta. Sasa umeletwa mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye Tarafa Kamsamba kwa maana ya Kata ya Kamsamba, Mpapa, Ivuna na Mkomba. Sasa hivi kuna shida kidogo kwani kumekuwa na mgogoro na wananchi wamebaki na ufuta wao nyumbani hawapeleki sehemu zilizopangwa. Tatizo hapa lilitotokea ni kwamba wananchi wameletewa elimu ya stakabadhi ghalani wakati wa mavuno badala ya kuambiwa kabla ya mavuno, hiyo ni changamoto na mpaka sasa hivi hawajui faida yake.

Mheshimiwa Spika, leo wanaambiwa peleka mazao yako ghalani halafu baada ya siku 4 au 5 ndiyo bei itapatikana. Sasa katika hali ya kawaida wananchi wana-*prefer more cash recently*yaani wale wachuuzi wanapokuja kule kwa wanakijiji wanunuua kwa wakati huo huo na kutoa hela pale pale. Leo mwananchi unamwambia peleka mazao yako ghalani halafu utapata hela yako baada ya siku nne hakuna mwananchi anayeweza kuelewa. Kwa hiyo, jambo langu ambalo naliomba Serikali cha kwanza iende ikatoe elimu kwa wananchi na kuonyesha faida kubwa zitakazopatikana kwa kutumia mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba sekta ya kilimo mchango wake umekuwa mkubwa sana kwenye pato ghafi la taifa. Sisi wote ni mashahidi, zaidi ya asilimia 28 kila mwaka lakini uwekezaji wake uko chini. Utaangalia hapa uwekezaji kwa mfano mapato ya ndani yamepelekwa asilimia 49 lakini kwenye mchango (*contribution*) yake kwenye GDP ni kubwa sana. Kwa hiyo, kwa sababu ni sekta inayoajiri watu wengi ni muhimu sasa Serikali ikaongeza kiwango kikubwa cha pesa kuhakikisha kwamba sekta hii inakuwa na manufaa na tija kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba kuwasilisha, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa David Silinde kwa mchango wako mzuri.

Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava nilishakutaja na atafuatiwa na Mheshimiwa Engineer Edwin Amandus Ngonyani ambao wote wako Msekwa.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema anayetupa uzima. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na kwa kazi kubwa anayofanya na niwapongeze pia wasaidizi wake wote kwenye Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda niende haraka haraka kwenye mchango wangu. Killimo cha umwagiliaji kinaongeza eneo la kulima, tija na kinatusaidia kuongeza vipindi vyta kuendesha kilimo. Niipongeze Serikali kuanzia 2015 mpaka sasa tumeweza kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 460,000 mpaka 690,000 sawa na asilimia 33. Hii ni hatua kubwa na nzuri, nipongeze Serikali kwa hatua hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunalo eneo kubwa sana kwa ajili ya kulima na tunayo maji mengi sana tusipokuwa na uwezo wa kutunza na kuhifadhi maji haya kwa ajili ya kutumia kwa kilimo hatuwezi kufanya vizuri zaidi kwenye kilimo. Niombe Wizara ijitahidi kuangalia namna ya kuendelea kuwekeza kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, tulifanya ziara na Mheshimiwa Mkuu na Naibu Waziri wa Kilimo alikuwepo kule Mombo, tunayo skimu ina hekta 220 lakini wakulima wanaweza kulima hekta 100 kwa mzunguko au hekta 120 kwa sababu hakuna uwezo wa kuhifadhi maji. Walipewa ahadi ya kujengewa bwawa kwa ajili ya kuhifadhi maji kwa ajili ya skimu ya Momba na skimu ya Kwamkumbo yenye hekta 1,300 lakini bado halijajengwa. Najua Mheshimiwa Naibu Waziri atakapokuja

kwenye majumuisho atawaambia wananchi wa Momba na Korogwe nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, pia tuombe kwa dharura ukarabati wa baadhi ya maeneo ikiwemo skimu ya Makangara na skimu ya Songea. Tulipoteza hekta karibu 800 za mpunga kwa sababu ya mvua nyingi za mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni zao la chai. Bado hatujafanya vizuri kama nchi kwenye uzalishaji wa zao la chai na kwenye bei ya chai. Mwaka 2018/2019 tumezalisha kilo milioni 37 ukilinganisha na majirani zetu Kenya kwa mwaka huo huo walizalisha kilo milioni 490. Ukichunguza ni kwa nini utagundua wenzetu wanawekeza haswa kwenye kuangalia miche bora na mbegu za kisasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukienda Kenya kwenye zao la chai asilimia 80 ya chai waliyokuwa nayo Kenya sasa hivi ni miche ya kisasa na bora. Sisi Tanzania asilimia 67 tuna miche ya zamani yenye zaidi ya miaka hata 50. Niombi sana Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai tuwekeze kwenye kuwatafutia wananchi na wakulima wetu mbegu bora ili wawewe kulima kilimo kizuri na cha kisasa. Pia watusaidie kwenye upande wa bei maana ni ndogo sana, wananchi wanaolima chai maeneo ya Bungu na maeneo mengine wanapata tabu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia nikumbushe Wizara tumesubiri kwa muda mrefu kufunguliwa Kiwanda cha Mponde kinawasaidiwa watu wa Lushoto na Korogwe. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie tumefikia wapi kwenye kufungua na kurudisha kile kiwanda cha Mponde. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia taarifa zilizopo Bodi ya Chai na Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai yako maeneo ambayo yakipata viwanda vipyta yatatusaidia kuongeza tija na thamani ya chai yetu ikiwemo maeneo ya Mufindi na Sakare kule Korogwe. Tunahitaji Wakala wa Wakulima Wadogo watuwekee mpango wa namna gani ya kupata

viwanda vipya tuweze kuwasaidia wananchi wetu waweze kuchakata chai vizuri na waweze kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa upande wa zao la mkonge. Nimpongeze Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Kilimo, amefanya kazi nzuri sana alipokuwa kwenye ile timu maalum ya kurudisha mali na zao la mkonge kwenye Mkoa wa Tanga. Niwaombe tu Wizara ya Kilimo wakutane na watu wa Wizara ya Ardhi na TAMISEMI mtusaidie kwani mashamba makubwa ya Bodi ya Mkonge wanayopewa wakulima wapewe hati angalau ziweze kuwasaidia kupata mikopo kwenye vyombo vya fedha waweze kufanya kilimo kizuri tofauti na wanavyofanya sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia bado tuna changamoto ya mbegu bora kwenye zao la mkonge. Tunapanda mbegu za kuokota kutoka kwenye maotoe ya mkonge. Niombe sana Wizara na taasisi zinazohusika mtusaidie kupata mbegu bora ya mkonge kwa wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inawezekana tukawa na changamoto ya fedha kwa ajili ya kupata hizi mbegu bora lakini sisi Mkoa wa Tanga tunashauri tuwe na sehemu kwa ajili ya kupata mbegu bora za wakulima wetu ili wakulima waweze kufanya kilimo kizuri kiwe na tija na tuweze kupata bei nzuri.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Timotheo.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia 100. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Timotheo Mnzava. Nategemea Mheshimiwa Waziri amekusikia kuhusu msisitizo wa mbegu bora.

Mheshimiwa Engineer Edwin Amandus Ngonyani atafuatiwa na Mwenyekiti wa LAAC, Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa pumzi na kupata fursa ya kuchangia leo.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia na maadam muda ni mfupi nikuombe sana, sijui kuna namna gani lakini wenzangu wengine wamesema kama nitapata fursa nitakuja Kongwa kuhakikisha kwamba unarudi na unaendelea kulongoza Bunge hili. Nasema hivyo kwa sababu unaakisi kabisa madhumuni na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano. Tunakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuishukuru na kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na katika sekta hii ya kilimo, Mheshimiwa Hasunga na Manaibu wake ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Bashe niwashukuru sana. Kuna mambo mmeyafanya yametugusa Wanantomtumbo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba kusema yale ambayo wananchi wa Namtumbo wanapenda uyasikie. Moja, wananchi wa Namtumbo wana uwezo wa kuilisha Tanzania kwa chakula wanachohitaji ni mbolea, viuatillifu, mbegu, masoko pamoja na skimu zao za umwagiliaji. Nikianzia na skimu za umwagiliaji wanazo skimu zina miaka zaidi ya miaka 15 hazifanyi kazi kinachohitajika ni hela ndogo sana. Halmashauri imejaribu kuweka bajeti lakini miaka yote kiwango cha fedha kinachoenda ni kidogo. Hii miradi ilikuwa ni ya Serikali Kuu hebu pelekeni fedha mkakamilishe skimu hizo ziweze kuanza kufanya kazi na wananchi wa Namtumbo tuilishe Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pili ni suala la mbegu, sisi tunaendelea kutumia mbegu zetu za asili, kila siku humu Bungeni nasikia kuna mbegu mbalimbali zimefanyiwa utafiti na taasisi zetu za utafiti zilizo chini ya TARI lakini kule kwetu

hatuzioni. Naomba sana mtafute njia ya kuzalisha zaidi kile ambacho kinafanyiwa utafiti na tafiti zetu. Njia pekee ya kufanya hivyo kwanza ni kuhakikisha TARI na taasisi zake zote zilizo chini yake zinapewa fedha inazoomba ili waweze kusambaza mbegu, viuatilifu na mbolea. Upande wa mbolea wananchi wa Namtumbo wanasesma bei ya sukari ikishuka kidogo Watanzania tunalamika sana lakini bei ya mbolea imepanda mara kumi hakuna anayeisemea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sisi tulizoea kununua mbolea kwa Sh.7,000 mfuko wa kilo 50 sasa hivi tunalazimika kununua kwa zaidi ya Sh.60,000 na wakulima wale bei ya mazao wanayopata ni ndogo, kile wanachozalisha hakiwawezeshi wao kununua mbolea. Nikuombe na najua una uwezo huo ukitoa mawazo hayo katika Serikali ya Awamu ya Tano, nina uhakika itakubalika wekeni ruzuku ya kutosha katika mbolea, viuatilifu na mbegu. Mkitufanyia hayo sisi tuna uwezo wa kulisha Tanzania nzima. Wapo wengine walioniambia kwamba hata walau wangeweka mfuko mmoja Sh.10,000 au Sh.20,000 lakini 60,000 uwezo wa kununua na hasa muda wenyewe ni kipindi cha masika watu hawana fedha inakuwa ngumu sana. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri hebu liangalie suala hili la mbolea.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele imelia.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Japo muda hautoshi lakini Mheshimiwa *Engineer Ngonyani* amesitisiza umuhimu wa mbegu bora, skimu za umwagiliaji, pembejeo kwa wakati, madawa kwa maana ya viuatilifu lakini masoko.

Nlikutaja Mheshimiwa Mwenyekiti wa *LAAC*, ndiyo unayefuata na baada ya hapo Mheshimiwa Dkt. Balozi Diodorus Kamala kule Msekwa ajiandae.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kusema chochote katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameshughulikia suala la Corona. Kwa kweli linahitaji maamuzi magumu na nimpongeze sana kwa maamuzi haya. Kutokana na maamuzi yake ndio imefanya mpaka sasa tupo katika hali hii. Mimi binafsi nampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la korosho na hasa zile za msimu 2018/2019 ambazo malipo yake yalichelewa. Niipongeze Serikali kwa kuanza kufanya malipo ya msimu ule wa 2018/2019, ni jambo jema. Nipongeze hata kwa maamuzi ya kuhamisha sasa kituo kile cha malipo kutoka Mtwara kuja Dodoma kwa sababu hapa ndipo kwenye Wabunge, sasa tunaweza kufuatilia malipo ya wakulima. Kama kuna mkulima yejote ambaye bado hajalipwa basi awasiliane na sisi Waheshimiwa Wabunge tutafuatilia malipo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ni muhimu pia kasi ikaongezeka kwa sababu wapo ambao bado hawajalipwa. Pia Wizara ijiandae vyema na maandalizi ya pembejeo pamoja na magunia kwa sababu msimu sasa unakaribia. Pia tuwakumbuke wadau wengine wakubwa ambao hawajalipwa, wale wasafirishaji maana zao la korosho kuna *issue* ya usafirishaji, hili ni kundi kubwa ambalo nalo bado halijalipwa. Serikali iliangalie kundi hili kwa sababu walishawishiwa na Serikali na wengine walikwenda hata benki kukopa bado hawajalipwa. Naomba kundi hili nalo liangaliwe ni muhimu likalipwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la kilimo cha ufuta. Sisi watu wa Mkoa wa Lindi na Mikoa ya Kusini ni wazalishaji wazuri wa ufuta na tumepata tija kubwa katika zao la ufuta kwa sababu ya mfumo wa stakabadhi ghalani. Kwa kweli mfumo wa stakabadhi ghalani mwanzoni tulikuwa

na mashaka na tukaona kwamba hatuwezi kufanikiwa lakini sasa hivi sidhani kama yupo mkulima wa Lindi au Mtwara utamwambia kwamba mfumo wa stakabadhi ghalani haufai akakuelewa. Niwaombe wale wa mikoa mingine ambao bado hawajaanza waanze kwani ni mfumo ambao una tija kubwa kwa wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakulima wa Kilwa wamenituma wakisitiza kwamba wao wanahitaji mfumo wa stakabadhi ghalani kama ulivyofanyika katika msimu uliopita na siyo vinginevyo. Yapo maelekezo ambayo kidogo wakulima yanawapa mashaka kwamba mfumo wa stakabadhi ghalani kwa mwaka huu minada itafanyika wakulima watapeleka mazao kwenye Chama cha Msingi lakini baadaye mazao yale yatasafirishwa kwenda kwenye ghala kuu, kwa mfano kule kwangu yatachukuliwa Njinjo, Kipatimu na sehemu nyingine yatapelekwa katika ghala kuu la Ngarukuru ndipo mnada ufanyike. Jambo hili limewatia mashaka sana wakulima na wana wasiwasi juu ya usalama wa mazao yao na wasiwasi mkubwa ni ucheleweshaji wa malipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naendelea kusisitiza kwamba kwa sababu ya hali hiyo, tuendelee na mfumo ule ule. Mwaka huu kutokana na hali ya hewa miundombinu ya barabara imeharibika kabisa, kwa hiyo, tukisema tusafirishe mazao ya wakulima kutoka katika Chama cha Msingi kupeleka kwenye ghala kuu ndipo mnada ufanyike malipo kwa wakulima yatachelewa na hivyo kufanya wakulima kutokuwa hali nzuri. Naomba Serikali na viongozi walizingatie hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine nizungumzie utekelezaji wa shughuli nyingine za Serikali zilizofanyika katika kipindi ambacho watu wengi wapo kwenye kilimo. Kuna suala la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpigakura limefanyika kwa Mkoa wa Lindi kuanzia tarehe 1 mpaka tarehe 4. Zoezi hili halikufanyika kwa mafanikio kwa sababu kwanza taarifa yenye we ilikuwa haikutosha lakini la pili watu wengi sasa wapo kwenye kilimo na kituo cha uboreshaji kinakuwa kimoja tu katika makao makuu ya kata. Kwa hiyo, wapigakura

wanalazimika wasafiri kwa umbali wa zaidi ya kilometra 10, 20 au 30 kwenda kufanya marekebisho ya taarifa zao, suala hilo limekuwa gumu sana kwa wapiga kura wengi.

Mheshimiwa Spika, Tume sijui kuna shida gani, inaonyesha kwamba watu wengi waliojiandikisha 2015 taarifa zao ndiyo zina matatizo. Naomba hili Tume mliangalie lile zoezi halikufanikiwa, tafuteni wasaa mwingine zoezi lirudiwe kwa sababu wapiga kura wengi hawajarekebisha hizo taarifa zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine nizungumzie suala la kilimo cha miwa katika Bonge la Mto Rufiji. Tuna tatizo la sukari lakini hili tatizo tuone kama ni fursa. Tuna maeneo ambayo bado hatujayashughulikia kwa shughuli za kilimo. Niishauri Serikali iwashawishi wawekezaji waje kuwekeza kilimo cha miwa katika Bonde la Mto Rufiji. Nafikiri itatusaidia kutengeneza ajira lakini itatusaidia kupunguza tatizo hili la upungufu wa sukari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale kwa mchango wako. Pamoja na mengine umeongelea stakabadhi ghalani; ni kweli Mheshimiwa Waziri sijui kama muda utapatikana au Naibu Mawaziri, kuzungumzia kidogo hili jambo la stakabadhi ghalani maana yake limeleta *confusion* kubwa sana kwa wananchi. Hata Mkoa wa Dodoma hapa nao ndiyo wanataka kuanza kwa mara ya kwanza lakini wamechanganyikiwa hawajui washike lipi baada ya matangazo ya hivi karibuni ya Wizara ya Kilimo.

Tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia. Jambo la kwanza nikushukuru sana, nilikuomba ruhusa nifuatane na Kamati ya Kilimo walipokwenda Jimboni kwangu kutembelea

shughuli mbalimbali. Kwa hiyo, nakushukuru kwa ruhusa uliyonipa.

Mheshimiwa Spika, katika ziara ile ya Kamati ya Kilimo, Kamati pamoja na mimi tulibaini kwamba Kiwanda cha *Kagera Sugar* kina mpango mkubwa kinaoutekeleza wa kulima hekta 14,000 za miwa. Walitueleza kwamba wakilima hizo hekta hizo wataweza kuongeza tani za uzalishaji wa sukari kutoka tani 95,000 wanazozalisha sasa hadi tani 170,000. Wakifanya hivyo, Kamati yako ilielezwa kwa kweli suala la upungufu wa sukari na baadhi kuwa wanalazimika kupewa ruhusa ya kuagiza sukari nje litakuwa limefikia mwisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo walitueleza ni kwamba pale watazalisha umeme wenye uwezo wa megawati 20. Pia watafanya na mambo mengine makubwa, wataongeza ajira kutoka watu 6,000 waliopo sasa hadi watu 11,000. Jambo hilo ni kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, changamoto waliyotueleza, mimi nillisikia nikiwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba wanalazimika kukopa kwenye mabenki ya biashara hapa nchini ambayo yanatoza riba kubwa na kuna mabenki mengi sana ya kimataifa yanependa yawakopeshe kwa gharama ndogo lakini wanachohitaji Serikali itoe neno kwamba wakopesheni hao, kazi wanayoifanya ni muhimu na sukari Tanzania tunaihitaji na ajira wanazotengeneza wanazihitaji. Sasa nikubaliane na ushauri wa Kamati iliyoutoa kwenye taarifa yao kwamba Serikali iangalie jinsi ya kusaidia kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo napenda kulichangia kwa haraka; katika ziara ile tulibaini kuna tatizo moja la mabenki kuwa na ukiritimba wa kutoa fedha kwa baadhi ya taasisi ambazo wanakubali kufanya nazo biashara. Nitatumia mifano miwili tu ambayo pia iko ndani ya taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mfano wa kwanza, kuna Kampuni inaitwa *Global Agency*, wao hawa wanalima mahindi. Tayari wana soko Uganda, Rwanda na Burundi na Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilikubali kuwapa mkopo wa bilioni 12, ikatoa bilioni 10 lakini bilioni 2.1 inakataa kuitoa. Kwa kweli walipotoa bilioni 10, hao Benki ya Maendeleo ya Kilimo walilipa moja kwa moja kwa *supplier* aliyetoe mitambo na mitambo hiyo tuliona sisi na Wajumbe wa Kamati iko pale shambani lakini haitumiki kwa sababu hawajapewa fedha za kufanya vitu vingine vidogovidogo vya kufanya ile mitambo iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nikueleze hiyo benki kuna wakati fulani ilizungumza na waliotoa ile mitambo ili waifungie mitambo ile isifanye kazi kwa sababu ambazo hazikuwa za kweli, lakini baadaye benki ikagundua ilikuwa imekosea ikafunguliwa. Yule *Global Agency* alikuwa tayari kupeleka hiyo benki kwenye mahakama ili alipwe fidia lakini mimi kama Mbunge nikashauri kwamba hebu waache kwanza hawa, hizi ni benki tunazilea, ni beki zetu. Ukiwapeleka hao mahakamani utakuwa umenipeleka mimi kama Mbunge wako, hebu waache kwanza tuone, labda watakuwa na akili huko mbele ya safari wataweza kumalizia hela hiyo lakini mpaka sasa hawajaachia fedha hizo. Kamati imeshauri kwamba ni vizuri fedha hiyo iachiwe na mimi kama Mbunge siku zijazo ntafanya uamuzi wa kutoa ushauri mwingine kama benki hiyo itaendelea kufanya hivyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, taasisi nyngine inaitwa Amiri Hamza, hawa wana changamoto kama waliyopata *Global Agency*. Wao walipata mkopo wa dola milioni 9 kutoka *TIB* wakaahidiwa kwamba watapewa hela nyngine lakini zikacheleweshwa. Matokeo yake ule mkopo umeongezeka kutoka bilioni tisa mpaka dola milioni 27. Sasa hizi tabia za mabenki zinakubali au hazikubali halafu zinachelewesha, nadhani akili hii wanayoitumia siyo nzuri na haitatusaidia kujenga Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichangie kwa ufupi kwamba hivi karibuni tutazindua kiwanda kidogo lakini

muhimu sana cha alizeti, katika Kata ya Kitobo. Kiwanda hicho tumekijenga kwa kutumia fedha ya Mfuko wa Jimbo na kwa kweli ni kati ya mambo niliyowaomba wapiga kura kwamba mkinipa Ubunge sitatumia fedha za Mfuko wa Jimbo kununua mipira au sukari au kufanya sherehe, nitatumia fedha hizo kwa shughuli za maendeleo na nimefanya hivyo na tutaendelea kufaya hivyo tukipata fursa nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kwa kumalizia, nitoe shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Watanzania kwa kutoa shilingi bilioni 40 za kujenga mradi mkubwa wa maji wa Kyaka Bunazi. Kwa kweli Mheshimiwa Rais ameingia katika historia ya kuleta mradi mkubwa wa maji katika Jimbo la Nkenge na amefanya hivyo Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala akiwa Mbunge na haijawahi kutokea. Naunganana na Wabunge wenzangu kumpongeza kwa kazi nzuri aliyofanya, namuombea asisite kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze pia na wewe kwa jinsi ambavyo umelifanya Bunge kuwa Bunge Mtandao. Niseme hata wale Wagiriki waliotupa mimi na wewe jina wakatuita Mr. More Water, tulikunyuwa maji mengi lakini yalitusaidia tukaishi na leo hii umeweza kuleta Bunge mtandao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala, umenikumbusha mbali. Tulipokuwa Wabunge vijana kabisa tumeingia kwenye Bunge hili mwaka 2000, tulipata bahati ya kwenda Ugiriki kwenye safari ambayo haikuwa ya Kibunge, ilikuwa ya Umoja wa Mataifa hivi lakini ina dola mia tu kwa wiki nzima tuliyotakiwa kukaa huko. Sasa ile jioni tumefika tukagundua kwamba m Kutano hauanzi siku ile, unaanza kesho yake asubuhi, kwa hiyo, hakuna kilichokuwa kimelipwa kwa siku ile. Kwa hiyo, tulipoingia kwenye eneo la chakula cha jioni pale hapakuwa na chochote chetu sisi na mimi na

Mheshimiwa Dkt. Kamala hatukuwa hata na shilingi mfukoni, Wabunge vijana, yule mhudumu kulikuwa na mikate pale mezani akija anasema ehee, tunamwambia *more water*, akirudi tena tunamwambia *more bread*, tulishambulia ile mikate tukaweza kuishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Goodluck Mlinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Niendelee kukupongeza kwa kulisimamia Bunge letu vizuri.

Mheshimiwa Spika, nina hoja zangu mbili. Hoja ya kwanza, katika Jimbo langu la Ulanga, bahati nzuri na wewe uliishi maeneo ya Mbunga karibia na Selous, wanalima sana ufuta katika Kata za Mwaya, Mbuga, Ilionga, Ruaha, Chilombola na Yuga. Kwa hiyo, katika kata 21 kata 7 ni wakulima wakubwa wa ufuta. Wakulima wamezoea wanalima ufuta wao wanakwenda wanauza.

Mheshimiwa Spika, sasa kilichotokea hivi karibuni baada ya kuvuna ufuta, Serikali ikatoa maelekezo kuwa hawaruhusiwi kuuza tena ufuta ule mpaka kwa mtindo wa stakabadhi ghalani na vyama vya ushirika ambayo mwanzo havikuwahi kuwepo. Sasa hali hiyo imeleta taharuki sana mpaka najiuliza Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo ana agenda na Jimbo langu la Ulanga? Kwa nini alete agenda hii ambayo haikuwepo katika kipindi hiki ambacho kinakaribia na uchaguzi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi binafsi sasa hivi siwezi kufika. Naibu Waziri Bashe ni shuhuda, Naibu Waziri Mgumba ni shuhuda; nimekuwa nikipata usumbufu mkubwa mpaka nimetoa namba zao za simu na mpaka sasa hivi hakuna kinacholeweka. Japokuwa kuna Janga la *Corona* natarajia kuwaleta wananchi wangu wa Ulanga katika Mji huu wa Dodoma ikiwemo na ofisi yako ili tupate ufumbuzi wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, kilimo kinatoa ajira nyingi sana kwa Tanzania, kinaajiri takribani asilimia 80 ya Watanzania lakini hakina tija. Nimefanya uchunguzi ili kilimo hiki kiwe na tija inatakiwa kuwe na mitaji, je, inapatikanaje? Katika Bunge lijalo nafikiria kuleta Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Ajira ili watumishi wawe wanastaifu kuanzia miaka 45 hadi 50 ili watoke waende wakalime sasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kitendo hicho kwanza hawa watastaifu wakiwa na umri wa miaka 45 mpaka 50 watakuwa na mitaji. Pili, kitendo hicho kitaleta kilimo chenye tija kwa sababu watakolima watakuwa na mitaji. Tatu, kitatoa chakula kingi kwa sababu watakolima watakuwa wanalima kilimo chenye tija na kwa sababu wana mitaji watazalisha chakula kingi na cha kutosha. Nne, tutapata fedha za kigeni, nimefanya uchunguzi Nchi za Kenya, Sudani Kusini, Kongo, wote wanategemea chakula kutoka kwetu, kwa hiyo, tutapata fedha nyingi za kigeni. Mwisho kitatoa ajira nyingi kwa vijana, kwa sababu leo hii tumeshuhudia vijana wengi wamemaliza vyuo wakiwa wanazagaa mitaani na hawana mtaji. Kwa hiyo, hii ajira ambayo itaachwa na hawa watu watastaifu wakiwa na umri wa miaka 45 mpaka 50, vijana wataingia na Serikali yetu itachangamka kwa sababu ya damu changa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja lakini nataka majibu ya maswali yangu kuhusiana na zao la ufuta. Ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Goodluck Mlinga kwa hoja yako ya watumishi kustaifu katika miaka 45 na 50, kwa kweli ni hoja muhimu. Mtu mwagine akiisikiliza hivi anaweza akaona kama sijui vipi, lakini zipo nchi kadhaa, nimewahi kuzungumzia siku za nyuma Ireland walikuwa na *policy* hii, natumaini bado wanayo labda, ukipewa nafasi yoyote ya Mkuu wa Idara au Mkurugenzi *maximum* ni miaka kumi baada ya hapo lazima uende mtaani ukatekeleze zile sera ulizokuwa unazipanga ukiwa Serikalini. Hii itasaidia sana kuwa na sera ambazo zinatekelezeka.

Sasa hivi kuna kundi la watu ambaao wanatengenezea watu sera, wao ni *permanent and pensionable*, wanadhani hawana mpango wa kuja kujunga upande wa pili. Kwa hiyo, watu wakijua hilo, mimi naamini Mheshimiwa Mlinga uko sahihi kabisa. Hata mimi natamani sana hili lije lifike siku moja, wawe wanakwenda upande wa pili, wakiwa wanakwenda upande wa pili utaona sera zinabadi lika sana. Kwa sababu baada ya muda huyuhuyu Mkurugenzi wa Kilimo lazima aende akalime, hawez tena kuweka mambo ya hovyo ya viuatilifu *fake*, haiwezekani, lazima watatengeneza vitu ambavyo kesho na keshokutwa na wao wakienda *ku-practise* vitawenza kutekelezeka.

Tunaendelea na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage endapo upo kule Msekwa. Ahsante, Mheshimiwa Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuungana na wenzangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze sana kwa kumpongeza Waziri wa Kilimo pamoja na wasaidizi wake; Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu pamoja na Wizara kwa ujumla na Mwenyekiti wetu wa Kamati kwa kazi nzuri ambayo iko mbele yetu chini ya jemedari wetu Dkt. Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi kule Njombe tunalima sana mazao ya biashara, viazi mviringo, mahindi na zao kubwa ambalo limepamba moto sasa la parachichi. Napenda kuishauri Serikali, Maafisa Ugani wako chini ya Wizara ya TAMISEMI, nadhani ili shughuli hii iende vizuri, ni vizuri hawa sasa wawe chini ya Wizara ya Kilimo ili wanapotoa maelekezo kwa Maafisa Ugani kwa sabbau ndiyo wanaosimamia kule shughuli hii itakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile upande wa mbembejeo hasa mbolea. Njombe kule sisi tunaitumia sana Urea na DAP kwa mazao haya niliyoyataja. Tunaishukuru sana Serikali kwa bei elekezi ambayo imekuwa ikitoa na watu wetu

wanaweza kununua. Tatizo kubwa lililopo na niombe Serikali iendelee kusimamia, wapo watu wakati wa kuuza mbolea hizi wanauzu bei ya ghali, wakiulizwa wanasema hii siyo ya bei elekezi. Sasa hili limekuwa ni changamoto kwetu sisi kule Njombe.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali isimamie suala ambalo kipindi fulani mwaka jana, mwaka juzi kwenye Kamati yetu tulielezwa kwamba kuna mwekezaji anataka kujenga kiwanda cha mbolea, hasa hii ya *DAP* na Urea, itatusaidia sana.

Naiomba Serikali isimamie bei itapungua itaendana na mazao ambayo tunalima, maana bei ya mbolea iko juu na mazao tunayouza hayaendani nayo. Pia Serikali kuititia Wizara ya Kilimo mtusaidie kutafuta masoko ili wakulima wetu wasipate shida.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa niende kwa changamoto ya nchi ambapo imekumbwa na majanga makubwa mawili. Moja, mvua imenyesha sana katika nchi yetu na imeharibu miundombinu. Serikali sasa inajipanga kuomba inarekebisha miundombinu ambayo ilikuwa imeshajenga na imeharibika.

Mheshimiwa Spika, la pili ni tatizo kubwa hili la Corona. Wewe umefanya kazi kubwa ya kuiunga mkono Serikali kwa namna ambavyo Rais wetu, Waziri wa Afya-Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na Naibu wake kwa kazi hii kubwa ambayo wanaifanya. Kwa kweli ni lazima tuwapongeze sana kwa niaba ya Watanzania. Ombi langu kama itakupendezza; nadhani sasa kwa kuunga mkono jitihada za Serikali chini ya Rais wetu na sisi Wabunge, Bunge lako tuchangie *perdiem* mbili au *sitting* mbili, tukatwe ili tuunge mkono kwenye mfuko huu wa ugonjwa wa Corona.

Mheshimiwa Spika, wako watu hapa wakati wanachangia walizungumzia juu ya watumishi mbalimbali nchini kwamba Serikali ione umuhimu wa kuwaongeza mishahara. Mimi nakubaliana lakini tumekumbwa na majanga haya mawili; tumuache Rais wetu ainue uchumi

kwanza haya yatafuata baadaye. Sasa hivi katika mchango huu ambao nausema ni vizuri watumishi wote nao washiriki kuchangia, wakikatwa hata shilingi elfu kumi kila mmoja zitaongeza mfuko.

Vilevile na makampuni mbalimbali nayo yachangie, hata kampuni yangu mimi niko tayari na wafanyakazi zaidi ya 150 niwakate Sh.10,000 kila mmoja zikachangie kwenye mfuko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo niishukuru sana Wizara ya Ardhi. Kule kwangu Makambako, Magongo watu ilikuwa wahame. Naishukuru Wizara ya Ardhi kupitia Waziri na Naibu wake hawakuweza kuhama.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Rais wetu kwa kazi alizofanya, kwenye Jimbo langu ni nyingi na nchi nzima, siwezi kuzitaja hapa muda umeisha, vyama vyote nya upinzani vimuache apite bila kupingwa. Tubaki sisi Wabunge na Madiwani tukapambane huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilisema nilipochangia katika Wizara ya TAMISEMI, hukuwepo siku ile, wewe umekuwa ukifanya kazi kubwa ya Watanzania, siyo wa Jimbo lako, Watanzania. Sasa kutohana na hili unalofanya la Watanzania tunakuombea wewe Spika watu wa Kongwa wakupitishe bila kupingwa, kazi ni kubwa. Pia Mheshimiwa Tulia kule Mbeya apite bila kupingwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Lukuvi ndugu yangu kwa kazi uliyowafanya Wanamakambako tunakuombea upite bila kupingwa. Mheshimiwa Jenista nilisema siku ile nilipokuwa kwenye Wizara ya TAMISEMI na Mawaziri wote tunawapongeza kwa kazi nzuri, Mungu awabariki. Mheshimiwa Majaliwa tulimuombea kule asiwepo mpinzani kwa kazi nzuri anayoifanya Waziri Mkuu. Pia Mheshimiwa Mabula, Naibu Waziri wa Ardhi, apite bila kupingwa. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sanga. Mzee mzima huyo, basi na watu wote mseme Amina. (*Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Amina.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Charles Mwijage, upo Msekwa?

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nipo.

**SPIKA:** Ahsante, endelea kuchangia Mheshimiwa, atafuata Mheshimiwa Daniel Nsazugwanko.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchagia sekta hii muhimu ya kilimo. Napoanza nataka nitoe pongezi kwa wakulima. Leo katika kukamilisha mwaka wa tano taifa hili halijawahi kulala njaa. Tumeweza kupata chakula kwa sababu wakulima walifanya kazi chini ya maelezo ya kitaalam ya Wizara husika lakini chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ndiyo inabeba sekta nyingine. Wako watu wa sekta za usafirishaji wanafanya kazi hizo kwa sababu kilimo kipo. Iko sekta ya viwanda, viwanda vinabebwa na kilimo. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuwapongeza wakulima wote wa Tanzania kwa namna walivyoibeba nchi hii kwa miaka mitano na kuweza kutupatia chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kwenye Mpango wa III wa Miaka Mitano ambao unalenga kuweka ushindani ili kuzalisha mazao au bidhaa kwa gharama nzuri na kuuza nchi za nje. Napendekeza kwa Serikali yangu kwamba tunapopanga Mpango wa Miaka Mitano ule wa III basi tuhakikishe tunawekeza katika kuweka miradi ya kimkakati ya kuzalisha chakula kingi, hasa mazao ya nafaka lakini mazao tutakayozalisha tuwe na vihenge vikubwa ili tujenge uwezo wa kuhifadhi nafaka nyingi ambazo zitaiwezesha nchi

hii kuwa na chakula cha kutosha kwa miaka mitatu mpaka miaka minne. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hizo nchi mnazozisikia zina kiburi cha *lockdown* ni kwa sababu zina kiburi cha chakula. Huwezi kufanya *lockdown* kama huna chakula. Watu wa Thailand na China hawana shida wana chakula. Sasa majanga huwa hayaagi, kama *Corona* ambavyo haikutuaga basi tufanye utaratibu wa kuwa na chakula kingi lakini zaidi ya hapo tuwe na kiburi cha kuwauzia jirani zetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano tumeshuhudia mtikisiko wa mazao na ugomvi. Niishauri Serikali na Wizara ya Kilimo kuwekeza katika tija, *the productivity*. Nchi nyine hawaangalii bei wanaangalia tija. Kwa mfano, kahawa, Vietnam anaweza kuzalisha tani 13 katika eneo lilelile ambalo Tanzania tunazalisha tani tatu za kahawa. Upande wa korosho, *Ivory Coast* wanafanya vizuri *per acre* kuliko tunavyofanya Tanzania. Bahati nzuri Manyoni wameanza vizuri, mti mmoja Manyoni unazalisha kilo 100 wakati mti huohuo kwa Tanzania sehemu nyine unazalisha kilo 30. Tunapaswa twende kwa mtindo wa Manyoni, *the productivity*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili kuondoa mambo ya kuangalia bei tuangalie tija. Watu wa Afrika Magharibi kuna nchi wanazalisha pamba kilo 1,200 wakati katika eneo la Usukumanî eneo lilelile linazalisha kilo 300. Kwa hiyo, tutoke kwenye bei twende kwenye tija.

Mheshimiwa Spika, niwaeleze watu wa TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, hizi mvua zilizokuja tuzione ni fursa. Kuna maji mengi yamekusanyika hata maeneo kame kama Dodoma. Sasa yale madimbwi ya maji muyatumie kuweza kulima mazao ya harakaharaka. Kile chakula mtakachozalisha cha muda mfupi na muda wa kati kiweze kutusaidia kuwa na chakula cha kutosha. Siyo siri dunia hii itakumbwa na tatizo la chakula.

Mheshimiwa Spika, nitofautiane na Wizara ya Kilimo, nawaomba chondechonde msiwe na haraka ya kuuza chakula nchi za nje, mtakwenda kuhemea nje mtakuta chakula kipo. Sukari iwape mfano, tumekwenda kununua sukari imechelewa kuja kwa sababu mfumo wa usafirishaji duniani ume-*collapse*, lakini utakwenda kununua chakula Argentina utakileta saa ngapi? Kwa hiyo, tujenge uwezo wa kuwasaidia wakulima ili chakula tulichonacho tuweze kukihifadhi ili janga la *Corona* liweze kuisha. Niombe TAMISEMI waambie Wakurugenzi wapige la mgambo watu walime. Maji yapo watu walime. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho nataka kushauri, kuna matrekta pale *NDC*, chukueni matrekta yale tulishakopa tutalipa. Chukua matrekta mugawe kwenye Halmashauri zinazoweza kulima. Wape matrekta bure walime, Wakurugenzi wale wana *degree*, watendaji wana *degree*, wayasimamie tulime kwa wingi tuzalishe chakula ili tuendelee kuwa na shibe daima na milele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la hali ya hewa, watu wa hali ya hewa watusaidie. Leo hii tunapopata mvua nyingi wawe kwenye nafasi ya kutuambia kiangazi kitakuwa na hali gani. Watutabirie ili tusifanye kazi za kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles John Mwijage.

Nimekwishakutaja Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko na Mheshimiwa Abdallah Chikota kule Msekwa ajiandae.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nakushukuru kwa yote.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na kuwapa hongera sana wenzetu wa Wizara ya Kilimo, Waziri Hasunga na timu yake ya Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wenzenu wote mnaofanya kazi hii. Mmefanya kazi nzuri na kwa takwimu zinazoneshwa kwenye hotuba ni kwamba nchi hii

ina usalama wa chakula kwa zaidi ya 100%. Hilo ni jambo jema sana, hongereni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nina mawili ya harakaharaka, nianze na zao la kahawa. Zao la kahawa linakufa, bei iko chini sana. Nashukuru Waziri Bashe tumelizingumza jambo hili na amefanya vizuri kutupatia wanunuzi ambao watakuja kununua kahawa ya Mkoa wa Kigoma. Nimekushukuru sana kwa jambo hili, lakini kwa ujumla wake zao la kahawa linazidi kufa, uzalishaji uko chini sana kwa sababu bei yake iko chini sana na wakulima wengi maeneo mengi Bukoba, Kilimanjaro, Mbozi, Kigoma, wanafikiria kuacha kulima kahawa. Nafikiri lazima wenzetu wa Wizara ya Kilimo pengine na watu wa Wizara ya Biashara mkae chini mje na mkakati wa namna ya kulifufua zao hili la kahawa vinginevyo baada ya muda si mrefu zao hili linaweza likafa au tukazalisha kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu umekuwa *champion* wa zao za michikichi, hongera sana. Umekuja kwetu Kigoma zaidi ya mara tatu ukizungumza habari ya michikichi. Jitihada zako na Serikali mpaka sasa kule Kigoma tuna Miche zaidi ya milioni moja na laki nane. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niombe tu kupitia kwako na watu wa Wizara ya Kilimo, wenzetu wa *TARI* sasa waongeze ule mnyororo wa maarifa ya kuzalisha miche ya michikichi wajikite kwenye vikundi vya wakulima, ili hatimaye zao hili liweze kutamalaki na miaka mitatu, minne ijayo tuweze kujitosheleza kwa mafuta ya kula. Serikali inatumia pesa nyngi sana kuagiza mafuta ya kula. Katika mazingira haya tuliyonayo ya *Corona* tegemeo pekee itakuwa sasa ni kilimo cha michikichi katika Mkoa wa Kigoma ambapo tutazalisha mafuta mengi sana na hatimaye tutajitosheleza kwa chakula. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niombe wenzetu wa *TARI* kupitia Wizara ya Kilimo muwaongezee fedha na uwezo ili waendelee kufanya kazi na wajitanue zaidi. Nakumbuka

mahitaji ya miche katika Mkoa wa Kigoma peke yake ni takribani milioni nne, tuko kama nusu hivi. Kwa hiyo, tunahitaji juhudii kubwa zaidi miche iweze kuongezeka na hatimaye tujitosheleze kwa mafuta ya kula.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo limenitia faraja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia juu kile Kitengo cha Masoko katika Wizara ya Kilimo ambacho kazi yake itakuwa ni kutafuta masoko, kufanya utafiti na ulinganisho wa bei. Kile ni kitengo muhimu sana kwani mazao mengi ya wakulima bei zake ziko chini sana. Kwa mfano zao la muhogo, tunalima muhogo mwingi sana lakini bei ni ndogo sana. Bei ambayo makampuni ya Kichina yanatoa sasa hivi kwa kilo moja ya muhogo mkavu ni Sh.300 tu lakini nina hakika kama ungefanyika utafiti pengine bei ya muhogo ingekuwa iko juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia kwa muda mchache uliobaki Mheshimiwa Waziri ni Chuo cha Kilimo cha Mbondo. Chuo hiki kilianzishwa na *World Bank* miaka mingi sana, kina zaidi ya ekari 1,860 lakini kinatumika kidogo sana, kinapokea wanafunzi wachache sana.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana niliomba kupitia Wizara yako Mheshimiwa kwamba kwa sababu Mkoa wa Kigoma sisi hatuna maabara ya udongo; ili udongo upimwe lazima udongo upelekwe Maruku ya Bukoba au Tumbi ya Tabora. Sasa nilikuwa naomba ombi langu la mwaka jana kwamba angalia uwezekano wa chuo hiki cha Mbondo kule Kasulu, Kigoma kiwe ni *branch* ya Mlingano tuweze kuwa na maabara ya udongo ili udongo uweze kupimwa paleple Kigoma na hatimaye hata matumizi ya mbolea yatakuwa na maana zaidi kujua ni mbolea ipi inahitajika kuliko kuleta mbolea wakati mwingine inakuwa haihitajiki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo napenda kulisema ni kukupa wewe mwenyewe hongera na pole kidogo kwa jinsi unavyohangaika na wimbi hili la wapinzani wetu. Mimi haya mambo nimeyafundisha kidogo

kwenye *Bunge Foundation*, wewe unajua. Unachokifanya unatukumbusha utamaduni wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola wala hakuna kingine kwamba, wapinzani hawa hawana uhuru wa peke yao, haiwezekani, wala hawawezi kufanya wanavyotaka.

Mheshimiwa Spika, inanikumbusha kwamba kuna haja sasa Bunge ijalo, maadamu tuna matarajio ya wengi kurejea humu, tufundishane vizuri ili tuelewane vizuri. Huwezi kuwa mpinzani halafu ukawa unapinga kila kitu na unafanya unavyotaka, ameleeza vizuri Mheshimiwa Selasini juu ya jambo hili. Wapinzani wetu wana miiko yake kama ambavyo sisi chama tawala tuna miiko yetu. Walio wengi katika Bunge ndiyo wanatunga sera zao na wale wachache kazi yao ni kutoa mawazo yao mbadala kama yapo na ni juu ya walio wengi kuyachukua au kuyakataa.

Mheshimiwa Spika, sasa naona unahangaika sana na hawa, tukupe pole lakini ukihangaishwa wewe tunahangaishwa sisi wote. Pole sana lakini unafanya kazi nzuri sana na *inshallah* mambo yatakwenda vizuri na tutamaliza Bunge salama na nina hakika wananchi wako wa Jimbo lako hapo watakurejesha tu katika kazi yako hii.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja kwa 100% na Waziri Mkuu kwa michikichi hiyo tunasema tena hongera sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwa hakika Mheshimiwa Waziri Mkuu amejitahidi sana katika kufufua zao la mchikichi. Sasa Kigoma msipotumia fursa hii ya Waziri Mkuu huyu mkafufua michikichi kwa kweli hamna wa kumlaumu maana amewapa kila aina ya *support*, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Abdallah Chikota kule Msekwa, utafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili kuchangia sekta hii ya kilimo ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyotoa miongozo yake kuhusu sekta hii na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyosimamia yale mazao sita ya kimkakati. Wote ni mashahidi tumemuona Waziri Mkuu akitoa maelekezo kuhusu tumbaku, korosho, kahawa na mazao mengine. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kipekee niwapongeze viongozi wa Wizara hii, Mheshimiwa Waziri Hasunga na Naibu wake wawili, Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Omary. Mawaziri hawa mara kwa mara wamekuwa wakishughulika kutatua kero mbalimbali kwenye sekta ya kilimo na kipekee niwapongeze walivyosimamia msimu huu kwa zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu kama walivyosema wenzangu changamoto kwenye zao la korosho zimepungua, kama sio kwisha kabisa kwa sababu tumeona kwanza mnada ulikuwa wa wazi, ule mtindo wa ku-*bid*siku mbili kabla ununuzi wa korosho ulifutwa na wafanyabiashara walikuwa wanabid korosho palepale wazi wakati wakulima wanashuhudia, hongereni sana. Vilevile malipo kwa wakulima, iliweka *time limit* ya siku nne. Tumeshuhudia sasa wakulima wakilipwa kwa wakati na hivyo kupunguza manung'uniko katika msimu huu.

Mheshimiwa Spika, nina mambo mawili ya kuishauri Serikali yangu irekebishe. Suala la kwanza kama walivyosema Wabunge wenzangu waliopita ni suala la vifungashio, magunia. Naiomba Wizara isimamie ipasavyo ili kuhakikisha kwamba magunia yanapatikana kwa wakati. Magunia yasipopatikana kwa wakati ubora wa korosho unaathirika.

Mheshimiwa Spika, vilevile suala la upatikanaji wa vifungashio kwa wakati lisiachiwe tu Bodi ya Korosho. Tumeona maelekezo hapa yametolewa kwamba msimu wa mwaka huu itakuwa Bodi ya Korosho na Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Naomba hata vyama vyaa ushirika wapewe kazi hii ili kupunguza kabisa upungufu wa magunia katika msimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la lingine ni kuhusu pembejeo. Naomba sana pembejeo ya *sulphur* ipatikane kwa wakati na iwe na ubora unaotakiwa ili isiathiri zao letu la korosho. Kuna dalili zote ambazo zinaonekana sasa hivi kwamba viuatilifu na pembejeo zinazoingia sokoni hazina ubora na hivyo kuporomosha uzalishaji wa korosho yetu. Naomba sana, Wizara mmeanza vizuri, Waziri na Naibu wako mnahangaika sana, hebu simamieni upatikanaji wa viuatilifu na pembejeo bora ili uzalishaji wa korosho yetu uweze kuongezeka. Tunaweza kabisa kuongeza uzalishaji wa korosho na tukawa wazalishaji wa kwanza Afrika, hilo linawezekana kabisa kwa sababu msimu wa 2018/2019 tulishafikia tani 215,000. Kwa hiyo, tukiongeza usimamizi kwenye korosho tunaweza tukaongoza Afrika kwa uzalishaji wa zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu ushirika. Ushirika ilitegemewa iwe kimbilio la wakulima lakini ushirika wetu una changamoto nyingi sana. Mimi najiuliza changamoto ni nini, ni Sheria yetu Namba 6 ya mwaka 2013, ni Mrajisi hana meno, tatizo ni Tume ya Maendeleo ya Ushirika haina ubavu au kuna changamoto katika Shirika letu la Ulaguzi (*COWASCO*) kwa sababu ushirika sasa hivi siyo kimbilio la wakulima. Kwa sababu Wizara ya Kilimo ina wataalam wengi na Mheshimiwa Hasunga unaweza, hebu unda timu ndogo ya wataalam kutoka kwenye sekta mbalimbali wauchunguze ushirika ili waje na mapendekezo ambayo Serikali itafanya maamuzi ili kama tatizo ni sheria basi iletwe Bungeni tuirekebishe, kama ni Mrajisi basi apewe meno ili tujenge ushirika wenye watumishi waadilifu, ushirika ambaa unajibu kero za wakulima, ushirika ambaa utakuwa unakopesheka, ukienda kwenye mabenki

utapata fedha za kununua mazao badala ya sasa hivi kukopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota. Nilikwishakutaja Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu na Mheshimiwa Latifah Hassan Chande Kigwalilo kule Msekwa atafuatia. Mheshimiwa Balozi.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kazi ambayo wanafanya Mheshimiwa Waziri ndugu yangu Hasunga na Naibu Mawaziri Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Omari ni kubwa sana na wanastahili pongezi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakwenda moja kwa moja kwenye mambo ambayo nataka kuyazungumzia, la kwanza ni zao la mkonge. Kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ziara yake Mkoa wa Tanga hivi karibuni naamini kabisa italeta mafanikio makubwa sana kwenye zao la mkonge.

Mheshimiwa Spika, zao la mkonge ni zao ambalo sisi wana Tanga tulikuwa tunalitegemea sana kiuchumi na hata nchi illitegemea sana kiuchumi. Zao la mkonge bei ambayo ipo kwenye soko la dunia ni kubwa sana. Sasa ufufuaji wa zao hili au ujio wa Waziri Mkuu kwa kweli huenda zao hili likaanza kufufuka tena kwa sababu pamoja na kamati ambayo ameiunda Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda kwenye Kitivo chetu cha Mlingano ambacho kinapanda mbegu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi pale Muheza tuna mashamba ambayo Mheshimiwa Rais alifuta hati, karibu mashamba sita ambayo yalikuwa yanalimwa mkonge. Mashamba yale Mheshimiwa Rais aliamuru tuwape

wakulima, wana Muheza ambao wako pale. Zoezi la kuwagawia linakaribia kumalizika lakini tunaomba kwamba Waziri aweze kuamuru Kituo cha Mlingano ambacho kinazalisha mbegu na Waziri Mkuu alikwenda pale na akaambiwa mbegu za kisasa za mkonge zimeanza kuzalishwa basi zizalishwe kwa wingi na tuwape bure wakulima wetu ambao tumewagawia mashamba yale. Nafikiri ombi hili likiweza kukubalika kwa njia moja au nyingine tunaweza kusaidia sana ufufuaji wa zao la mkonge.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo nataka kuongelea ni zao la chai. Sisi kule Muheza tunalima chai kwa kiwango kikubwa sana kwenye Milima ya Amani. Kama nilivyozungumza kwenye bajeti iliyopita suala la mnada ambapo hawa wakulima wa chai, Kampuni ya *UTCO* inatoa chai Muheza inapeleka Mombasa, sasa suala hili kwa kweli ni kero kubwa. Nakumbuka kabisa Naibu Waziri Bashe tulifanya kikao na ukaamuru kwamba tutaanza kuweka mnada wa chai hapahapa badala ya kupeleka Mombasa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia takwimu hapa inaonekana kwamba Kenya wanalima chai nyingi kuliko sisi. Sasa ile chai ambayo ndiyo tunaipeleka Kenya kwenye mnada si ajabu ndiyo ambayo imejumlishwa na inaonekana kwamba zao la chai Kenya ni kubwa kuliko kwetu. Kwa hiyo, suala la kuwekwa mnada hapa nchini ni muhimu sana na naomba Waziri uliangalie.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ninalotaka kuongelea ni viungo. Sisi tunalima viungo mbalimbali, hiliki, mdalasini, karafuu, pilipili manga kwa wingi sana. Hivi karibuni tumepata bahati ya kufunguliwa kiwanda pale na kimeanza kufanya kazi na tunategemea Waziri Mkuu aje kumalizia ziara yake kwa kukifungua. Kiwanda kile kimeanza kusafirisha baadhi ya viungo kama hiliki na karafuu kwenda nje. Ombi ambalo tunaliomba ni tuletewe wataalam ili waweze kuangalia wakulima wa viungo watalimaje kwa kilimo cha kisasa ili tuweze kuzalisha kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Adadi Rajab. Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande Kigwalilo akiwa kule Msekwa na atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchangia juu ya ucheleweshwaji wa malipo ya korosho kwa ajili ya wakulima wa korosho katika Mikoa ya Kusini. Kwanza itambulike kwamba mimi natokea Liwale katika Mkoa wa Lindi ambapo zao la korosho ndiyo zao kuu linalotegemewa katika uchumi. Kwa hivyo, nina maslahi ya moja kwa moja katika zao hili la korosho.

Mheshimiwa Spika, malipo ya korosho kwa wakulima yameendelea kuchelewa na kuwayumbisha wakulima hawa kiuchumi. Baadhi ya wakulima hawa wanategemea malipo hayo ili waweze kuwekeza katika zao la ufuta ambapo misimu inafuatana. Kwa kucheleweshwa huku wanashindwa kuijendeleza katika zao la ufuta na hata wananyimwa mikopo katika Benki ya Kilimo kutokana na kwamba Benki ya Kilimo tayari kuna madeni wanayowadai wakulima wengine ambao walikopa na wakashindwa kulipa kwa sababu tu ya kucheleweshewa malipo hayo. Baada ya kusema hayo, naishauri Serikali iweke mfumo madhubuti wa kuhakikisha kwamba wakulima wanalipwa madeni hayo ili wasiyumbishwe kiuchumi na waweze pia kuwekeza katika kilimo cha ufuta na vilimo vingine na kujendeleza wenyewe kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwenye Bodi ya Korosho mpaka sasa hivi Bodi hii inaendeshwa na Mkurugenzi huku ikiwa haina wajumbe wa Bodi. Naishauri Serikali iweze kufanya uteuzi wa wajumbe wa Bodi ya Korosho haraka iwezekanavyo ili kuhakikisha inatekeleza kazi zake kwa ufanisi na inaweza kusimamia Bodi hii kwa ufanisi katika kuendeleza tasnia hii ya kilimo cha korosho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, napenda kuongea sasa juu ya upungufu wa upatikanaji wa mbegu bora hapa nchini. Imebainika kwamba kumekuwa na uhitaji mkubwa wa mbegu bora hapa nchini na Taasisi ya Ukaguzi wa Mbegu (*TOSC*) imeshindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi. Jambo hili limethibitishwa na ripoti ya *CAG* ya mwaka 2019 Machi, iliyoonesha kwamba wakulima kutoka Morogoro, Manyara, Moshi, Arusha hususan Wilaya za Hai na Meru wamelalamika juu ya mbegu kutokuwa na ubora kusababisha mazao kuwa hafifu. Mbegu hizo zilizoainishwa zilithibitishwa na *TOSC* lakini Taarifa ya *CAG* imeonesha kwamba taasisi hii haikuweka rekodi kwa uhalisia ulioko. Hivyo tunaishauri Serikali ihakikishe kwamba hii taasisi inafanya kazi yake kwa umakini zaidi ili kuhakikisha kwamba kilimo hakifeli na wakulima hawafelishwi na ukosaji huu wa mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, mbali na hili suala la kuwa na mbegu *fake* katika masoko hapa nchini lakini pia kitu cha kusikitisha zaidi ni kwamba Wizara ya Kilimo pamoja na Taasisi zake zimeshindwa kubaini mahitaji ya kiwango cha mbegu zinazohitajika hapa nchini. Hili limethibitishwa na Taarifa ya *CAG* na hata maafisa wa Wizara ya Kilimo walikiri hili mbele ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kuangalia kwenye vitabu vyatupu *Volume IV* ambavyo vimeonesha bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo ni shilingi bilioni 137.27 lakini hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya sekta hii ndogo ya mbegu. Naishauri Serikali iweze kutenga fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya sekta hii ndogo ya mbegu na kwa ajili ya kufanya utafiti wa mahitaji ya mbegu nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile naishauri Serikali au naweza kumuomba hapa Waziri wa Wizara ya Kilimo aje atueleze ni kwa jinsi gani ataweza kufanya mageuzi ya kilimo kama hakutakuwa na uwekezaji katika sekta ya mbegu.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lathifah. Tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri na wa kweli. Sekta ya mbegu Mheshimiwa Waziri ni utata mkubwa na huwezi kuwa na kilimo bila mbegu. Mbegu za mazao ya nafaka, mafuta ni tatizo kubwa mno. Unakuta juhudini kubwa ya kilimo imefanyika lakini unaona aina ya mbegu zilizopandwa si mbegu bora hata kidogo na wananchi wanapoteza nguvu kubwa sana. Kwa hiyo, hoja hii ya mbegu ni muhimu sana tuifuatilie.

Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq nilikutaja na Mheshimiwa Makamu wa Mwenyekiti Dkt. Christine Gabriel Ishengoma atafuata.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia. Sambamba na hilo, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya njema kuweza kuchangia hoja hii katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niungane na Wabunge wenzangu wote kuendelea kukuombea Mungu ili akijaalia basi katika uchaguzi ujao tutakapokuwa na uhai sisi wanawake wa Mkoa wa Dodoma tunakuhakikishia kwamba tutakupigia kura zote, tutahakikisha kwamba tunapambana. Sisi wanawake wa Dodoma ambao tunajivunia wewe kuwa Spika wetu hakika tunakuhakikishia hilo tutalifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya hotuba yake ya makadirio ya mapato na matumizi na fedha ya Wizara ya Kilimo mwaka 2020/2021. Niwapongeze Naibu Mawaziri na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii, Waziri wetu amezungumzia kuhusu kukua kwa kilimo kwa asilimia 5.2 na kuendelea kukua katika upatikanaji wa mazao kwa asilimia

5.8. Naipongeza sana Wizara kwa kufanya kazi hii. Sambamba na hilo, naomba niipongeze tena Serikali kwa kutenga kiasi cha pesa shilingi billioni 37.5 kwa ajili ya Fungu 5 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Pamoja na pongezi hizo, nina ushauri kidogo ambao nataka kuutoa kwa ajili ya hii Tume ya Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji ambapo bado kuna mambo kadhaa ambayo inahitajika yafanyike ili kusudi iweze kuwa na tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri kwamba katika Tume hii ya Umwagiliaji inaonekana mpaka sasa hivi bado Waziri hajamteua mtendaji Mkuu ambaye atasimamia Tume hii. Kwa hiyo, naomba Waziri aliharakishe jambo hili ili ikiwezekana apatikane Mtendaji Mkuu ili kusudi kazi ziweze kufanyika kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo bado ya Idara ya Mipango, Idara ya Ununuzi na Ugavi, Mkaguzi wa Ndani kuna watu ambao wanakaimu. Kwa hiyo, naomba Waziri ahakikishe kwamba hawa Wakuu wa Idara hizi ambao wana taaluma hizo waweze kupatikana ili kusudi kuweze kufanyika utendaji wenye tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe ushauri kwamba wawepo wataalam wabobezi wa kutosha wenye uzoefu katika kusanifu miundombinu ya umwagiliaji ili kuleta tija na ufanisi zaidi. Sasa hivi imeonekana kwamba bado watendaji ni wachache, kwa hiyo, hebu Wizara ione hili jambo inalifanyiaje kazi.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na miradi ya umwagiliaji ambayo ni gharama kubwa sana lakini haikidhi mahitaji kwa wananchi pamoja na wanufaika. Nikichukulia kwa mfano, sisi katika Wilaya ya Chamwino tuna miradi ambayo ilikuwa inafadhiliwa na *WFP*katika Vijiji vya Suli, Fufu na Kipoli lakini miradi hii imejengwa chini ya kiwango. Kwa hiyo, naomba Wizara ione umuhimu wa kulifuatilia jambo hili kwa sababu katika ile miradi bado kunahitajika kujengwe visima vya ziada walau vitatu, vitatu katika haya maeneo ya umwagiliaji ili kusudi kuwe na uwezekano wa kuyajaza maji

yale matenki na hatimaye wananchi waweze kufanya kilimo cha umwagiliaji kuepukana na njaa na kuwa na usalama wa chakula katika Mkoa mzima wa Dodoma na hasa Wilaya ya Chamwino.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri mwingine kwamba kama ikiwezekana basi hebu Wizara au Waziri aone umuhimu wa kutengeneza safu ya wataalam wabobezi wenyewe uwezo na weledi wa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi ili kusudi hili suala zima la umwagiliaji liweze kupata tija. Pia ile miradi ambayo ina changamoto iundwe timu maalum ili kusudi wataalam waweze kupitia upya na kuona kuna tatizo gani ili kusudi miradi hii iweze kusanifiwa vizuri na kuleta tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 37 wa hotuba hii Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu suala la ugunduzi wa mbegu. Naipongeza sana Serikali wa hilo lakini nilitamani na sisi Dodoma mbegu ya zabibu iweze kufanyiwa utafiti zaidi ili kusudi tuweze kupata mbegu za kutosha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante kwa kunipa nafasi. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fatma Toufiq. Nilishaahidi kwamba Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ndiye anayefuata.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu, pia nakushukuru wewe mwenyewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Kilimo. Pili nakubaliana na yote yaliyoongelewa na Kamati yetu ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji wote hasa kwa vipaumbele vya mwaka 2020/2021. Vipaumbele walivyoviweka vinajitosheleza na vizuri sana. Ushauri ninaoutoa, waweze

kuvisimamia na kuvifuatilia kusudi viweze kutekelezeka kama walivyoviweka. Ikiwa hivyo, tutaweza kukuza uchumi wa nchi yetu ya Tanzania na pato la wananchi.

Mheshimiwa Spika, nikija kwa vipaumbele, kwa Mkoa wangu wa Morogoro kwenye vipaumbele hasa kwenye mazao ya mkakati naomba waweze kuangalia kwa kilimo cha mpunga ambapo Morogoro ni ghala la chakula, kilimo cha mahindi, alizeti, ufuta pamoja na mazao ya bustani ikiwemo nyanya na vitunguu. Morogoro tunajitosheleza na tunaweza kulisha Taifa kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, huwezi kufanya kilimo kilicho sawasawa bila ya utafiti. Kwa hiyo, naomba na nashauri taasisi za utafiti waweze kupewa fedha za kutosha na zile tutakazozipitisha humu Bungeni waweze kuzipata kwa wakati kusudi utafiti uweze kufanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Kwa miradi ya maendeleo tumeona sisi wenyewe kuwa hawatengewi fedha na hasa kwa mfululizo wa miaka mitatu. Sisi tunaamini kuwa kilimo cha umwagiliaji ndicho kitakachowenza kusaidia Taifa letu kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, naomba fedha zote za Tume zilizotengwa ziweze kupelekwa kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mazao ya bustani ni muhimu sana kwa sababu yanachukua muda mfupi kustawishwa na yanaleta pato kwa ujumla kwa mwananchi. Tatizo au changamoto iliyopo ni mbegu. Mara kwa mara tumechunguza tumeona kuwa mbegu nyingi za mazao ya bustani zinatoka nje lakini siku za nyuma zilikuwa zinazalishwa hapa nchini huko Tengeru na Cholima Morogoro lakini sasa hivi hazizalishwi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna ASA ambayo ni Taasisi ya Uzalishaji wa Mbegu. Tunaomba waweze kupewa fedha za kutosha ili waweze kuzalisha hizi mbegu za bustani na mbegu zingine ambazo zina ubora wake.

Mheshimiwa Spika, masoko na yenyewe naomba yaangaliwe. Nashukuru kuwa kinaanzishwa Kitengo cha Masoko ambacho siku za nyuma kilikuwepo. Kitengo hiki kilikuwepo Wizara ya Kilimo kikatolewa kikapelekwa kwingine lakini sasa hivi kinarudi nashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, viwanda vya mbolea vya ndani ikiwemo na Minjingu na viwanda vingine, naomba vipewe kipaumbele kusudi tuweze kutumia pesa za ndani kwa kutumia mbolea yetu ya ndani ambayo ni mbolea nzuri sasa hivi imeboreshwa haina tatizo. Pia tunaweza kufanya shamba darasa kusudi wakulima waweze kuona ni kitu gani tunaongelea.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa udongo ni jambo muhimu sana. Unakuta wakulima wengi wanalima lakini hawana utaalam wa uchunguzi wa udongo. Kwa hiyo, naishauri Serikali iweze kufanya uchunguzi wa udongo nchi nzima. Kazi hii ilishafanyika kwenye Chuo cha Mlingano ambapo walifanya uchunguzi wa udongo nchi nzima. Kwa hiyo, hapa nawakumbusha wafuatilie kuona uchunguzi wa udongo uliofanyika kwenye mikoa yote na kama kuna maboreshwu iweze kufanyika tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kidogo kuhusu Afisa Ugani. Afisa Ugani wapo na ambao hawaajaajiriwa waweze kuajiriwa. Afisa Ugani wanatoa elimu ya kilimo, huwezi kufanya kilimo bila ya Afisa Ugani. Afisa Ugani watoe elimu ya kilimo kwenye mashamba darasa, matumizi ya mbolea na pembejeo na viuatilifu ambavyo vinasumbua sana wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Serikali kwa kuendelea kuimarishe hali ya lishe. Nchi yetu ilikuwa na udumavu mkali lakini sasa hivi naona kuwa inaimarisha lishe. Kwa hiyo, naipongeza Serikali inafanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya uhaba wa sukari naomba changamoto za Kiwanda cha Kagera Sugar ziweze kutatuliwa. Pia Kiwanda hiki kikiungana na viwanda vya

Kilombero, Morogoro; Mtibwa, Morogoro; TPC, Kilimanjaro pamoja na Mkulazi I na Mkulazi II, Morogoro, naamini changamoto ya sukari itaisha. Kwa hiyo, naomba tuviangalie na kutatua changamoto zinazovikabili viwanda hivi.

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya mazao. Mazao mpaka yafike sokoni yanapotea kwa asilimia 50. Kwa hiyo, ujenzi wa maghala pamoja na vihenge ni muhimu sana kwenye nchi yetu ili kupunguza upotevu wa mazao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na Mwenyezi Mungu akubariki na awabariki wanawake wa Morogoro ambaao walinipa kura. Naomba wanipe kura tena niendelee kuwatetea. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma kwa mchango wako. Ningeshauri basi Mheshimiwa Dkt. Ishengoma awe ndio mchangiaji wetu wa mwisho kwa maana hiyo ili tuwape nafasi Waheshimiwa Naibu Mawaziri na Mheshimiwa Waziri waweze kuititia hoja zetu. Kama mlivyoona hoja za kilimo ni nyingi sana, natambua muda hautoshi kwa upande wao lakini basi wajaribu kuititia kwa huu muda tutakaokuwa nao.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombé Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Kilimo, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenyewe ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge hasa katika kipindi hiki tunapopambana na janga la Covid-19.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, imetekeleza kwa ufanisi mkubwa miradi mingi ya kilimo na pia kuboresha mfumo wa taasisi zilizo chini ya Wizara hii ikiwemo vyama vya ushirika. Pia kuwepo mkakati mahsusni wa kuboresha kilimo cha umwagiliaji na uende sambamba na ujenzi wa mabwawa yanayotokana na uvunaji wa maji ya mvua. Serikali iendelee kuimarisha vyama vya ushirika kwa vile hii ni nguzo kubwa ya maendeleo katika sekta ya kilimo na masoko ya mazao ya kilimo. Uboreshaji wa ushirika uende sambamba na kuimarisha mfumo wa stakabadhi ghalani ambayo ni msingi pia wa kuanzishwa na kuendeleza Soko la Bidhaa (TMX).

Mheshimiwa Spika, katika hiki kipindi cha changamoto za Covid-19 tunachopitia kuna athari kubwa za kiuchumi, lakini wakati huo huo zinaweza funguka fursa za mahitaji makubwa ya mazao yetu ya chakula na hata mazao mengine ya biashara. Napendekeza Serikali kuendelea kutoa msukumo kwenye kilimo cha tija ili tuongeze tija kwenye uzalishaji wa chakula ili kuwepo na ziada kubwa kwa soko la nje. Kutokana na uwekezaji kwenye kilimo, mkulima kwenye ekari moja anaweza kuzalisha zaidi ya tani nne za nafaka kutoka nusu tani ya sasa. Hata kwenye mazao ya biashara kama kahawa kuna fursa ya kuongeza uzalishaji kwa asilimia zaidi ya 300. Serikali iboreshe mfumo wa uagizaji wa mbolea na pia usambazaji kwa wakulima utoe unafuu wa bei kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya zao la pareto ni makubwa zaidi ukilinganisha na uzalishaji ambao ni asilimia kumi tu. Tanzania inaongoza kwa uzalishaji wa pareto Afrika na ya pili duniani, lakini kuna changamoto kubwa ya soko kwa wakulima wa Tanzania kupelekea ununuvi usiokuwa wa upinzani. Kutokana na kutokuwa na ununuvi wa ushindani, wakulima wanaambulia asilimia kumi tu ya bei ya soko la nje.

Nashauri Serikali itoe kipaumbele cha kilimo cha pareto na kusimamia soko ikiwa ni pamoja na kuongeza

thamani ya pareto hapa nchini. Pia Serikali iandae mkakati wa soko la kahawa ili kuboresha bei ya kahawa ya Tanzania angalau ilingane na bei za nchi zingine za Afrika Mashariki kama Kenya na Ethiopia kwa kahawa ya Arabica.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, naanza kuwa kuunga mkono hoja. Aidha, naipongeza sana Wizara pamoja na timu yao yote katika utekelezaji wa majukumu yao katika kiwango kinachordhisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio katika Wizara ya Kilimo, bado wakulima wa zao la mpunga wanakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na soko la uhakika hivyo husababisha kudumaza uchumi kwa wale wanaojihushisha na kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha bajeti zilizopita Wizara ilipanga katika kuimarisha soko la mpunga kuliingiza zao hilo katika Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula badala ya kununua zao la mahindi peke yake. Lakini katika utekelezaji halisi wa mkakati huu wa Serikali kuimarisha soko la zao la mpunga umekuwa hafifu sana. Bado zao hili la mpunga halijapewa kipaumbele kuwa kununuliwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula. Kupitia bajeti hii ninaiomba Serikali sasa ianze kutekeleza mkakati huu wa Wakala kununua mpunga ili kuimarisha soko.

Mheshimiwa Spika, migogoro katika Wilaya ya Malinyi; Serikali imejenga skimu moja ya kilimo cha umwagiliaji kwa gharama kubwa sana zaidi ya bilioni 6, lakini mradi huo umekamilika na kukabidhiwa ukiwa uko chini ya kiwango watarajiwa katika kutekeleza matumizi yake. Mfano skimu haikujengwa barabara za kwenda mashambani, mifereji midogo (*secondary canals*) hazikusakafiwa hivyo kutokana na mvua za masika mifereji yote imefunikwa na sana haifanyi kazi. Kwa changamoto hizo skimu hii hatumii katika kipindi cha kiangazi.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikitoa taarifa hii kuwa Serikali mara kadhaa kuitia maswali Bungeni, michango yangu katika bajeti za Wizara lakini hakuna hatua zilizochukuliwa na Wizara kwa ujumla. Ninaiomba sasa kwa mara nyingine tena kushughulikia mapungufu haya ili skimu hii ya Itete, Malinyi ifanye kazi kwa kikamilifu kama ilivyokusudiwa mwanzo wakati ilipojengwa.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nawapongeza kwa jinsi wanavyoendelea kuyaendeleza mazao ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, wakazi wa Mkoa wa Kagera, wengi wao ni wakulima wa zao kuu la biashara ni kahawa. Naipongeza Serikali kwa juhudzi zake za kukomesha magendo ya kahawa. Kitendo hiki kinawanufaisha wakulima wanapata bei nzuri zaidi. Pamoja na hayo bei ya kahawa Mkoani Kagera bado iko chini sana kati ya shilingi 1,000 na shilingi 1,100 kwa kilo. Napendekeza Serikali iendelee kuwawezesha vyama vyaya msingi kuongeza thamani badala ya kuuza kahawa ghafi.

Pili wafanyabiashara wa kahawa wahakikishe kahawa inauzwa nje ikiwa tayari kutumika badala ya kuuza *semi processed*. Nawapongeza kwa mkakati wenu wa kuhamasisha unywaji wa kahawa nchini. Nashauri uwepo siku ya unywaji wa kahawa, kila migahawa wawe na *coffee shop* na wananchi wahimizwe kunywa kahawa ili badala ya kutegemea soko la nje tu, tukuze solo la ndani pia.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera kuendelea kutegemea zao kuu moja ni mbaya kwani bei ya dunia ikaanguka wakulima wanapata hasara. Kama nilivyokwisha shauri, napendekeza nchi iwe na mfuko wa kumfidia mkulima endapo bei ya kahawa duniani itaanguka.

Mheshimiwa Spika, sababu ya ugonjwa wa Corona vyama vyaya ushirika wa akiba na mikopo vimeathirika. Wateja/

wanachama waliokopa hawarejeshi vizuri sababu mzunguko wa fedha kwenye jamii imepungua. Baadhi ya vyama hivi nimekosa kutoka benki. Kwa kutambua kuwa ushirika ndilo kimbilio la mkulima na mwananchi wa kawaida, je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia *SACCOS* zisianguke katika kipindi hiki cha Corona?

Pia Mkoani Kagera kuna mazao ambayo yana bei nzuri, mfano zao la vanilla. Kilo moja inauzwa zaidi ya shilingi 100,000. Napendekeza Serikali itoe fedha za kuendeleza zao la vanilla Mkoani Kagera ili mkulima apate bei nzuri ya zao hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja mkono na kuchangia hoja kama ifuatavyo; nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa kazi nzuri ambayo wanaofanya.

Mheshimiwa Spika, napongeza hatua za hivi karibuni za kuanza kufufua zao la mkonge ambalo uzalishaji wake sio mzuri ukilinganisha na hapo nyuma. Mkonge ulikuwa unakuza uchumi wa Mkoa wa Tanga na nchi kwa ujumla. Kitendo cha Mheshimiwa Waziri Mkuu kuunda Kamati na kuja ye ye mwenyewe mkoani Tanga na kutembelea Kituo cha Mlingano ni jambo la kupongeza sana. Sisi Muheza tunayo mashamba ambayo Mheshimiwa Rais amefuta hati za mashamba sita na kuamuru mashamba hayo tuwagawie wananchi wa Muheza. Zoezi hilo la ugawaji linakaribia kumalizika hivi karibuni. Hoja ambayo naomba iangaliwe ni kuamuru Kituo cha Mlingano kizalishe mbegu nyingi za mkonge wa kisasa na zigawiwe kwa wananchi hawa tuliowagawia mashamba bure, kitendo hicho kinaweza kuamsha ari ya Wana-Muheza na Tanga kwa ujumla na kuongeza ongezeko la mkonge kwa ujumla ukitilia maanani kwamba mashamba hayo hayo ndio yaliyokuwa yanalimwa mkonge. Ni muhimu suala hili likafikiriwa kwa umakini wake.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri Mheshimiwa Omari Mgumba ulikuwepo kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nafikiri umenielewa ninachokizungumza.

Mheshimiwa Spika, sisi Muheza tunalima chai maeneo ya Milima ya Amani na kuna makampuni karibu matatu, hoja ambayo naileta hapa ni suala la mnada ambapo bado baadhi yake wanapeleka chai hiyo Mombasa kwenye mnada. Suala hili Wizara mlikwisha sema kwamba mtaanzisha mnada hapa nchini, sijui suala hili mmefikia wapi kwani tunapoteza mapato mengi bila sababu za msingi. Aidha, nashukuru Wizara kwa kuruhusu kampuni ya *EUTCO* kuanza kuchakata na ku-*brand* chai yao na kuanza kuuza hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Muheza tunalima viungo mbalimbali kama pilipilli manga, karafuu, mdalasini, illiki na kadhalika, sasa hivi tumepata bahati na kuna kiwanda kimeanzishwa ambacho nimeanza kupokea malighafi hizi na kuzichakata na kusafirisha nje ya nchi viungo hivi. Tunachokiomba ni Wizara kutuletea Mabwana Shamba ambao watatoa mafundisho maalum kwa wakulima wa viungo ili tuweze kuzalisha kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo nawashukuru sana na kuwapongeza kwa kazi nzuri.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kukushukru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii. Aidha, napenda kukupongeza wewe kwa namna unavyoliendesha Bunge letu tukufu kwa uadilifu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Wizara hii, Naibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwakilisha kwa umakini mkubwa hotuba ya Wizara yao. Wameonesha mshikamano mzuri na mkubwa kwenye utendaji wa Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo na nianze na pembejeo za kilimo. Kama inavyojulikana kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi katika nchi yetu, naipongeza Serikali yetu kwa namna inazochukua juhudzi za kuendeleza kilimo katika nchi yetu. Juhudi zake zinaonekana na kila mwananchi mwema wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudzi zote hizo bado upatikanaji wa pembejeo za kilimo bado haujaridhisha. Baadhi ya wakulima bado hawana uhakika wa upatikanaji wa pembejeo. Kuna sehemu wakulima wanachelewa kupata pembejeo kulingana na msimu, hii inapelekeea kupata mazao hafifu au kukosa kabisa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali kuweka msimamo madhubuti katika kusimamia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ughali wa vitendea kazi vya kulimia; vitendea kazi ni jambo muhimu sana katika kila sekta. Lazima wakulima wawe na urahisi wa kupata vifaa hivi. Kwa mfano, bei ya trekta moja hapa nchini ni kubwa sana kiasi ambacho kwa wakulima wetu wadogo hawawezi kumudu kununua, hii inapelekeea wakulima wetu kutopata malengo yao.

Ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kutengeneza mazingira mazuri kwa wakulima ili kupata vifaa vya kulimia kama matrekta kwa bei nafuu ambayo wataweza kumudu kununua.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Spika, wakulima nchini wanakabiliwa na upatikanaji wa mbegu bora za kilimo.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa nchi hii wanakabiliwa na upungufu mkubwa wa mbegu bora na

baadhi ya maeneo nchini wakulima walilalamikia ubora wa mbegu kuwa hauna uzalishaji wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa ufanisi wa upatakanaji wa pembejeo za kilimo ulichapishwa *CAG* mwezi Machi, 2019 umeonesha kuwa katika mikoa ya Manyara, Morogoro, Kilimanjaro, Arusha, hususan maeneo ya Wilaya za Hai, Meru na Moshi wakulima walitoa malalamiko yao kwa *TOSC*/kuwa mbegu za mahindi aina za *Pioneer 2859, DKC 90-89, SC 627* na *SC 403* zilikuwa zina uzalishaji hafifu na *TOSC*/walithibitisha.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ule ulionesha kuwa taasisi inayopaswa kufanya kazi ya kudhibiti ubora wa mbegu (*TOSC*) imerekodi taarifa chache za mbegu *fake* wakati katika uhalisia wakulima wengi walilalamikia ubora wa mbegu hizo.

Mheshimiwa Spika, mbali na uwepo wa mbegu *fake* katika masoko ya mbegu baadhi ya mikoa jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa Wizara ya Kilimo na taasisi zake hazina uwezo wa kubaini kiwango cha mahitaji ya mbegu hapa nchini na *CAG* amethibitisha katika ripoti yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara na taasisi zake, *TOSC*/na ASA zimeshindwa kuwa na mifumo ya kubaini mahitaji ya mbegu.

Mheshimiwa Spika, Maafisa wa Wizara ya Kilimo, walikiri mbele ya *CAG* kuwa nchi nzima makadirio ya kiasi cha mbegu kinachohitajika hayakuwahi kufanywa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mwaka mpya wa fedha 2020/2021 nimeangalia kitabu cha bajeti *volume iv*, Wizara imetenga shilingi bilioni 137.27 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Wizara haijatenga fedha kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya sekta ndogo ya mbegu,

ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa mahitaji halisi ya mbegu nchini.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itenye fedha kwenye eneo la uzalishaji bora wa mbegu, hali kadhalika Waziri wa Kilimo anapokuja hapa kuhitimisha hoja yake, atueleze ni namna gani tunaweza kufanya mageuzi ya kilimo endapo hatuwezi kufanya uwekezaji kwenye eneo la uzalishaji wa mbegu bora?

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mahitaji ya mbegu yalionekana kuwa yale yale kwa miaka minne mfululizo tangu mwaka wa fedha 2014/2015 mpaka 2017/2018. Katika kipindi hicho mahitaji ya mbegu yanaonekana kuwa *metric tonne* 120,000 lakini mbegu zilizozalishwa zilikuwa *metric tonne* 11,000 tu ambayo ni sawa na asilimia 27 tu ya mahitaji yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuweka mfumo wa kidijitali utakaohusisha teknolojia ya habari katika kufanya makadirio ya mbegu kila mwaka wa fedha, ukadiriaji ufanywe kutokea kwa wakulima ili kuepuka Wizara na taasisi zake kufanya makadirio yasiyozingatia uhalisia wa hali ilivyo kwa wakulima wetu nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, taasisi inayotakiwa kuzalisha mbegu nchini ASA (*Agricultural Seed Agency*) ina uwezo mdogo sana wa kuzalisha mbegu hapa nchini, ASA uwezo wake ni kuzalisha asilimia 1.7 tu ya malengo yake ya uzalishaji wa mbegu nchini. Tangu mwaka wa fedha 2015/2016 mpaka 2017/2018 ASA ilipanga kuzalisha *metric tonne* 36,000 lakini haikuweza kuzalisha zaidi ya *metric tonne* 800 kila mwaka katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, mbegu zinazozalishwa nchini hazijitoshelezi na wala zile zinazoagizwa kutoka nje ya nchi hazitoshelezi. Hatuwezi kama nchi kuendelea kuisubiria ASA ishindwe kuzalisha mbegu bora halafu kilimo kiendelee kufeli na Wizara ipo, Waziri yupo, Katibu Mkuu yupo. Lazima tufanye maamuzi ya kuishirikisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali, hususani Wizara ya Kilimo, kuamua kufanya ushirikishwaji mpana wa sekta binafsi katika uzalishaji mbegu na kurekebisha kanuni zake za uzalishaji na usambazaji wa mbegu, kuimarisha ukaguzi wa mbegu bora na kuifanya sekta binafsi nchini ifanye biashara ya uzalishaji wa mbegu chini ya mwongozo wa ASA na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, mimi ninatokea Liwale na Mkoa wa Lindi amba moja ya shughuli kuu ya kiuchumi ni kilimo cha zao la korosho; hivyo nina maslahi ya moja kwa moja na zao hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya wakulima wa korosho, Bodi ya Korosho imebainika kuwa na uwezo dhaifu wa kulipa madeni ya muda mfupi ya ndani ya miezi 12.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa hesabu za Bodi ya Korosho Tanzania wa mwaka wa fedha 2018/2019 ulionesha kuwa Bodi ya Korosho ina kiasi kidogo cha maliza muda mfupi kuliko kiasi cha madeni ya muda mfupi. Mpaka CAG anafunga hesabu zake, mali za Bodi ya Korosho zilikuwa ni shilingi bilioni 15.70 wakati madeni ya Bodi ya Korosho yalikuwa ni shilingi bilioni 20.50.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Bodi ya Korosho bado inaendeshwa na Mkurugenzi huku bodi ikiwa haina Wajumbe, hivyo suala la usimamizi wa ufanisi wa bodi hiyo kuwa mashakani.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ifanye uteuzi wa wajumbe wa bodi hii waendelee kusimamia uendeshwaji wa mafanikio wa zao la korosho.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi kwa kazi kubwa inayofanywa na Wizara, naomba nichangie kwenye maeneo yafuatayo; kwanza kilimo cha umwagiliaji kitiliwe mkazo kwa kufanya uwekezeji mkubwa na kufufua miradi iliyoanzishwa vipindi vyaa nyuma.

Mheshimiwa Spika, mfano, kwenye Wilaya ya Ukerewe kuna mradi wa umwagiliaji wa Miyogwezi na Bugorola. Miradi hii ingweza kuzalisha chakula cha kutosha Wilaya nzima na hata nje ya Wilaya, lakini miradi hii imetelekezwa na pesa zilizowekezwa pale zaidi ya shilingi milioni 700 zimepotea bure.

Mheshimiwa Spika, nishauri miradi hii ifufuliwe ili tija na thamani ya pesa iweze kuonekana.

Pia watumishi wanaotoa elimu ya kilimo bora kwa wakulima wetu hiki vijijini waajiriwe ili kusaidia kuondoa kilimo cha mazoea na wataalam hawa wapewe vitendea kazi ili wananchi wetu wafanye kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa aina ya udongo uliopo Wilayani Ukerewe ufanyike ili ushauri utolewe kujua ni mbolea aina gani itumike na mazao aina gani yalimwe kwenye archi hiyo.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, napenda nikupongeze kwa kazi kubwa unayoifanya pamoja na Naibu wako katika kuliongoza vizuri Bunge lako tukufu. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kufanya maamuzi na mageuzi makubwa katika delta ya kilimo kwa kufuta uitirii wa kodi na tozo zilizokuwa kero kwa wakulima. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri na ya uhakika tangu walipoteuliwa kuongoza Wizara hii. Hongereni na chapeni kazi tuko nyuma yenu.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali kwa mambo machache yafuatayo; jambo la kwanza ni kuhusu upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za viuatilifu kwa wakulima wa pamba vijijini. Pamoja na juhudhi za Serikali katika jambo hilo bado kuna wakulima wengi kutopata viuatilifu kwa wakati na kwa kiwango wanachohitaji.

Niishauri Serikali kuwapata mawakala wenye uwezo na wenye tija ambao watasimamiwa na kikosi maalum toka

Bodi ya Pamba na takwimu za usambazaji ziwe zinaratibiwa na Maafisa Kilimo wa Vijiji, Kata na Taarifa kupelekwa Wizarani *on daily basis*.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili niishauri Serikali kuwaacha wenyewe wajipangie bei ya pamba yao badala ya kupangiwa na Serikali kwa kuanza na bei elekezi. Niishauri Serikali ibaki kusimamia na kutoa miongozo itakayodhibiti makampuni kutotengeza *alliance* ya kuendelea kuwanyonya wakulima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kushauri hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga hoja hii mkono. Nimpongeze Waziri na wenzake kuwa kazi nzuri katika kuongeza Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, vitu muhimu katika kuboresha kilimo ni moja, ardhi bora; pili, mbegu bora na aina ya zao; tatu, zana za kilimo; nne, maji au mvua; tano, huduma ya ugavi; sita, mbolea na viatilifu na saba, soko la mazao.

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo yakipewa umuhimu na kusimamiwa vizuri kilimo chetu kitasonga mbele na kuibua pato la Taifa kwa kupata mchango mkubwa toka kilimo.

Mheshimiwa Spika, ule utaratibu wa Serikali kuchagua mazao ya kimkakati uendelee badala ya kila Mkoa kutaka kupanda kila zao, kufanya hivyo kuna athari ya usimamizi wa ubora wa mazao na pia usimamizi wa soko.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri pia katika ujenzi wa viwanda na hasa vile vinavyopitia EPZA tuweke mkazo kwa viwanda vitakavyoongeza thamani ya mazao ili wakulima wetu wapate bei nzuri.

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja iliyoko mezani ya bajeti ya Wizara

ya Kilimo na Umwagiliaji kwa kuanza kwa kuwapongeza Waziri na Naibu Mawaziri wake pamoja na watendaji wote kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya katika Wizara hii.

Baada ya pongezi hizi, naomba kuchangia mambo machache kama ifuatavyo; na kwanza kwa kuwa Wilaya ya Longido ni moja ya Wilaya kame nchini na isiyo na mito ya kudumu, naomba Serikali iwekeze katika miradi ya kuchimba mabwawa ya umwagiliaji katika baadhi ya maeneo yanayofaa kwa kilimo hasusan katika Tarafa ya Enduimet maeneo ya Vijiji vya Tingatinga na Ngereyani.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Tingatinga na Ngareyani hufikiwa na maji mengi majira ya mvua yanayotiririka kutokea Nyanda za Juu za Mlima Kilimanjaro (Mto Ngarenairobi) na Mlima Meru (Mto Ngarenanyuki). Maji haya yangetekwa na kuhifadhiwa kwenye mabwawa makubwa, wananchi wa eneo hili wangenufaika kwa kilimo chenye tija cha uoteshaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara yanayostawi huko ambayo ni pamoja na nyanya, viazi, maharage na mahindi.

Mheshimiwa Spika, vijiji hivi viliahidiwa mabwawa na Serikali kwa muda mrefu kabla mimi hata sijawa Mbunge wa Longido na hivyo sasa naomba Serikali watekeleze ahadi hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mabwawa ya umwagiliaji, naiomba pia Serikali iwekeze katika kusanifu mfumo wa umwagiliaji kutoka Mto Ngarenanyuki ulioko Wilaya ya jirani ya Meru ili maji hayo yaweze pia kufika katika Vijiji vya Tingatinga na Ngereyani kwa ajili ya kilimo cha nyanya, zao ambalo linastawi sana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niongelee suala la dawa za kunyunyiza mazao kwa wakulima wetu wachache wa Wilaya ya Longido maana kwa sasa kuna mdudu anayepekecha mazao hasa mahindi na hata maharage hata yakiwa shambani; kwa hiyo Serikali ichangie dawa kwani tuna wakulima maskini ambao hawana uwezo wa kujinunulia dawa.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa Tarafa ya Enduimet wanategemea zao la nyanya za msimu wa mvua kama zao lao kuu la biashara; kwa hiyo naomba Serikali iwajengnee soko la nyanya.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni taarifa kuhusu adha ambayo wakulima wa vijiji viwili vyta mpakani na Kenya - Kijiji cha Irkaswaa na Kamwanga wanapata tokea Corona izuke, wiki hii Kenya imeweka maaskari wake wa Jeshi mpakani kuwadhibiti Watanzania wasivuke mpakani wakati wengi wamekodisha mashamba maeneo ya mipakani upande wa Kenya na sasa wananchi hawa wasiporohusiwa kwenda kupalilia na kuvunwa itakuwaje? Naiomba Serikali itoe msaada wa kidiplomasia kuwasaidia wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kunipa afya njema na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali fedha zinazoidhishwa na Bunge kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi hiyo.

Naishauri Serikali ijenge mabwawa katika maeneo mbalimbali ili wakati wa mvua kuweza kuvuna maji na kuyatumia kwenye umwagiliaji wa mazao kipindi cha kiangazi.

Naishauri Serikali iboreshe miundombinu kutoka mashambani hadi mijini hususan barabara ili ziweze kuitika katika majira yote ya mwaka. Pia naishauri Serikali iwatafutie wakulima soka la ndani na nje ya nchi ili waweze kuuza mazao yao.

Mwisho, naishauri Serikali ifungamanishe sekta ya kilimo na sekta ya viwanda, hii itasaidia kujua aina ya mazao ambayo yatahitajika kwa ajili ya malighafi katika viwanda.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, tuendelee kumshukuru sana Mungu kwa majaliwa ya ustawi wa Taifa letu nyakati zote katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidiplomasia nyakati zote.

Mheshimiwa Spika, tuendelee kumuomba sana Mungu atuondoshee janga hili la Corona katika nchi yetu na dunia nzima. Aidha, ninaipogezza sana Serikali kwa hatua mbalimbali kupambana na janga hili la Corona hivyo basi tuungane kwa pamoja kupambana na janga hili linalotikisa dunia.

Mheshimiwa Spika, tunawapa pole nyingi ndugu zetu Watanzania wote waliofiwa na wapendwa wao kwa namna mbalimbali. Mwenyezi Mungu awapokee katika ufalme wake usio na mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya awamu ya tano kwa jinsi ilivyotekeleza llani ya CCM ya mwaka 2015 - 2020. Hakika Serikali ya Awamu ya Tano imeg'ara sana mbele ya Watanzania na mafanikio yanaonekana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu wa kuishauri Serikali; kwanza Serikali itazame upya mfumo wa mazao ghalani kwa kuwa lengo la mpango huu ni benki ya mazao katika maeneo ya vijijini ili kuweka utaratibu wa kuhamasisha, kutafsiri, kuelimisha na kuzuia mianya yote ya udanganyifu, ubabaishaji, urasimu ambao mwisho wa siku utawakatisha tamaa wakulima.

Pili, kwa kuwa mafanikio ya kilimo yanahitaji sana rasilimali wataalam, vitendea kazi na mazingira rafiki, Serikali iajiri Maafisa Ugani walau kwa ngazi za Kata ili kusimamia kanuni za kilimo bora kwa kuanzisha mashamba darasa katika kila Kitongoji kote nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa pembejeo za kilimo nchini zimekuwa na gharama kubwa sana nchini hususan mbegu na mbolea Serikali iwekeze katika kilimo cha mashamba ya mbegu kupitia magereza na JKT na taasisi za kilimo kote nchini ili kukuza kipato cha Taifa na kuwezesha urahisi wa upatikanaji nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie na kutathimini mpango wa mnyororo wa thamani ulioanzishwa na Serikali ya Awamu ya Nne ili kufanya maboresho kwa lengo la kuleta tija zaidi na kukamilisha miradi iliyoanzisha na kupata matokeo chanya.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie uwezekano wa Maadhimisho ya Nanenane kwa ngazi ya Wilaya kwa kuwa wananchi wengi wanashindwa kushiriki mashindano ya kikanda ili kuleta hamasa, fursa, ushuhuda na kuonesha mafanikio chanya.

Pia Serikali iweke usimamizi mzuri wa ununuzi wa mazao ya wananchi kwa kutumia mizani ili kumnufaisha mkulima badala ya mfumo wa kukisia ambayo siyo kipimo sahihi. Aidha, Serikali itazame utaratibu wa kugawa nchi yetu kikanda katika kilimo cha mazao ya biashara ili kuleta uwiano wa Tanzania ya Viwanda kwa kuwa maeneo mengi nchini kwa sasa hayana uwezekano wa kuanzishwa kwa viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vyama vya ushirika nchini vimeduwa na migogoro, Serikali iangalie mfumo mzuri wa kukagua na kufunga hesabu za mwaka ili kulinda amana/mali za wanachama na kuleta ustawi mzuri wa ushirika nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho nawatakia kila la heri wewe Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wote mafanikio mema kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba tupate kuchaguliwa tena.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100% na naomba kuwasilisha.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Naibu Mawaziri wawili kwa kazi nzuri mnayofanya kwenye Wizara hii. Lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuismamia vizuri sekta hii ya kilimo ambapo imebeba wanyonge wengi wa nchi hii. Tumemuona Rais akiingilia kati wakati bei za mazao mbalimbali zinapokuwa chini kiasi cha kutaka kuwanyonya wakulima. Tumeona kwenye pamba, korosho, na kadhalika, Rais alilingilia kati na wakulima wakapata bei nzuri. Nizungumzie jambo moja tu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, tumekuwa na mgogoro wa malipo kwa wakulima wetu wanapouza mazao yao. Tatizo hili tulilliona kwenye zao la korosho mwaka 2018/2019, lakini pia tatizo hili lipo kwa wakulima wa pamba mwaka 2019/2020. Mpaka sasa tunapozungumza hapa, wakulima wa pamba hawajalipwa pesa zao karibu kiasi cha shilingi bilioni moja Mkoa wa Simiyu pekee. Tatizo hili linasababishwa na nchi yetu kutokuwa na mfumo bora wa bei na malipo kwa wakulima wetu. Hakuna mfumo rasmi ambao unaweza kuwahakikishia wakulima bei nzuri na malipo kwa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, nimesoma taarifa ya Mheshimiwa Waziri, lakini sijaona mahali pametajwa kushughulikia tatizo hili. Kuna wakati Naibu Waziri Mheshimiwa Bashe alisema Wizara itaanza mara moja utaratibu wa kuanzisha *Price Stabilization Fund*. Jambo hili limefikia wapi? Ni vyema sasa Serikali iwe na mkakati wa namna ya kutatua tatizo hili ili wananchi wakulima waweze kupata bei nzuri na malipo kwa wakulima yasiwe ya shida tena.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Kama mlivyojipanga, Waheshimiwa Naibu Mawaziri niwape dakika kumi kumi, sijui nani ataanza.

Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Mgumba halafu Mheshimiwa Waziri dakika kumi kumi halafu tutaendelea.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):**

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na kutufikisha siku ya leo kuweza kutimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nitumie nafasi hii kwa dhati kabisa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Nzega kwa imani walijonipa ya kuwaongoza katika kipindi hiki. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba sehemu kubwa ya yale tuliyowaahidi katika uchaguzi wa mwaka 2015 tumeyatekeleza. Kwa niaba yao, niwashukuru kwa dhati kabisa Waziri wa Nishati na Waziri wa Maji kwa mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria. Naishukuru Serikali kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nzega katika utekelezaji wa llani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nitumie nafasi hii kukupongeza wewe kwa dhati kabisa kwa uongozi ambao umetupa katika kipindi hiki ndani ya Bunge letu Tukufu. Umekuwa kiongozi wa Bunge lakini vilevile umekuwa kaka na rafiki. Nimshukuru sana Naibu Spika kwa ushirikiano ambao amekuwa akinipa mimi binafsi kama ndugu yake wa karibu na ushauri ambao amekuwa akinishauri kwa kipindi cha miaka hii mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niseme jambo moja tu. Nataka nitumie nafasi hii kumpa moyo wa dhati kabisa Mheshimiwa Rais. Historia yoyote ile katika dunia yetu imeonesha kwamba viongozi wengi wanaokumbana na changamoto nyingi ndiyo ambao huwacha alama. Mheshimiwa Rais amekumbana na *reforms* kubwa ambazo ameweza kuzifanya katika nchi yetu na *reform* hizi zimeweza kuleta maumivu ya muda mfupi lakini naamini kwamba miradi na mipango ambayo Serikali imekuwa nayo katika kipindi cha miaka kumi ya uongozi wake, akimaliza mwaka 2025 ataacha alama ambayo itaendelea kukumbukwa katika historia ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nimalizie kumshukuru kwa dhati kabisa Waziri wangu. Mheshimiwa Hasunga amekuwa kiongozi kaka na kwangu. Namshukuru pacha wangu Mheshimiwa Mgumba amekuwa kiongozi kwangu na kunishauri. Nawashukuru viongozi wote wa Wizarani kwa msaada walionipa katika kipindi kifupi hiki ambacho nimetumikia nafasi ya Unaibu Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo wamezi-*rais*endani ya Bunge hili. Kwanza, hoja nyngi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni za msingi ambazo sisi kama Wizara tunazipokea na tutaendelea kuzifanyia kazi kuboresha sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja imetolewa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya inayohusu sekta ya tumbaku. Ni kweli kwamba sekta ya tumbaku imekumbwa na changamoto na ni kweli kwamba tulipoingia katika msimu uliopita kulikuwa na zaidi ya tani milioni 12 za wakulima ambazo hazina soko. Ni wafanyabiashara wadogowadogo wa Kitanzania ambao Wizara ya Kilimo iliwapa kibali ndiyo walioweza *ku-pull out* mazao yote yaliyokuwa hayajanunuliwa na makampuni matatu ambayo kwa muda mrefu ndiyo yalikuwa yameshikilia sekta ya tumbaku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, makampuni haya ni Magefa, Grand Tobacco na kampuni zingine. Kwa nini tumefungulia sekta ya tumbaku kuruhusu wafanyabiashara wadogo wa Kitanzania? Ni hatari sana sekta nzima kushikiliwa na *foreign companies*. Ni vizuri tuanze *ku-groom* wafanyabiashara wa ndani. Sisi kama Wizara hatua ya kwanza tuliyochukua wafanyabiashara hawa walienda kutafuta masoko nje, sisi tulichokifanya kama Wizara ni kuwaunganisha wao na *financial institution*; wamechukua zaidi ya kilo milioni 11 ambazo zilikuwa hazina soko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, moja ya zao ambalo bado na mimi

naomba kwa Mwenyezi Mungu huko mbele moja ya sheria ambayo tunatakiwa kuibadilisha ni Sheria ya *Tobacco*. Haiwezekani zao lina *grade 67* na bado kuna *grade inaitwa reject* ambayo mkulima anatakiwa akatupe. Kwa mara ya kwanza mwaka huu tumeuza tumbaku inayoitwa *reject* kwa shilingi 500 ambayo miaka yote ilikuwa inatupwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwamba wafanyabiashara wa Kampuni ya Magefa kufika siku ya tarehe 24 watakuwa wamemalizia tumbaku zilizokuwa zimebaki ambazo ni tani 1,020 za mwaka jana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara ili wanunuzi wasitengeneze *cartel* tuliamua kwamba tumbaku ile yote baada ya wao kusaini *commitment* tukaihamishia Tabora ili itakapofika wakati wa kununua wanunuzi wasiseme tumbaku ya mwaka huu imechanganywa na ya mwaka jana.

Kwa hiyo, tumeamua kuiweka Tabora na tumewaunganisha na *CRDB Bank* na *NMB* na sasa hivi wapo kwenye hatua za mwisho za maongezi dola laki 6 hizo zitalipwa siku ya tarehe 24 na wakulima hawa watakuwa wamepata soko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakulima wa Wilaya ya Serengeti kwa miaka miwili wamehanganya na zao la tumbaku la Wilaya ile lakini walioenda kulinunua zao hili ni hawa wafanyabiashara wa Kitanzania, tuwatie moyo. Jukumu letu kama Serikali ni kuwasaidia kuwaunganisha na taasisi za fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja imesemwa na Waheshimiwa Wabunge ya stakabadhi ghalani. Kwanza ni vizuri sisi ndani ya Serikali na wenzetu waliopo katika *Local Government* wakaelewa mfumo wa stakabadhi ghalani siyo wa kukusanya ushuru bali msingi wake ni *price discovery*. Mfumo huu ulivyofanya vizuri Kanda ya Kusini tumeupeleka katika baadhi ya maeneo mengine. Leo wakulima wa choroko katika Wilaya ya Igunga wameuza choroko yao 1,370 kijijini *without anymakato* kwa sababu tumetengeneza *transparency* na watu wameshindana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo na sisi katika Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Waziri ameshatoa maelekezo tutakuwa na kikao kesho na wenzetu wa Mkoa wa Dodoma kulimaliza tatizo liliopo katika Mkoa wa Dodoma kuhusu stakabadhi ghalani. Hatuwezi kutekeleza stakabadhi ghalani maeneo ambayo hayana miundombinu stahiki. Tumesema wazi, hivi ni vitu vya *understanding*, tumeandika barua na tumetoa uelewa. Hii *TMX* sheria imepitishwa na Bunge letu la *commodity market exchange* ni *climax* ya mfumo wa stakabadhi ghalani, mkulima ana *aggregate* katika *primary level*. Mimi nimekuja humu ndani na karatasi ambazo tutazisambaza katika Wilaya na Mikoa watu waelewe nini maana ya stakabadhi ghalani, kuna *primary market* na *secondary market*, nia yetu mkulima asiteseke katika jambo hili. Kwa hiyo, nilitaka niseme jambo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mkulima wa nchi yetu na sisi Serikalini na wenzetu haya ndiyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba asiteswe na zao lake. Sisi tunachokifanya ni kujenga mazingira, mtu wa kwanza anayesimamia usalama wa nchi yetu ni mkulima kwa sababu anatuhakikishia *100% food security*. Sisi tulifungua mipaka makusudi ili *value for money* na *value* ya *time* ya mkulima aliyowekeza aweze kupata. Hatutoingilia bei lakini hatutoruhusu mkulima akanyonywa, hili jambo halitotokea. (*Makof/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kumejengwa hoja ushirika, tunakiri ushirika una changamoto na changamoto iliyopo ni suala la tabia tu, hakuna sheria inaweza kumbadilisha mwizi. Mnada umefanyika, fedha imelipwa, mtu anapotea na fedha. Hili ni suala la tabia tu na hulka na sisi tutawafunga, tunawakamata kila siku na tutaendelea kufanya namna hii. Hatuwezi kumfanya mkulima wa nchi hii akawa *punching box* na hili jambo halitoruhusiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto ya *Covid*, ni kweli ipo lakini kwetu sisi ni fursa. Kwenye hotuba imesemwa vizuri na Mheshimiwa Waziri kwamba mazao yetu ya chakula pamoja na kujipanga sisi kuhakikisha kwamba tunanunua zaidi ya tani ya 300,000 kwa ajili ya hifadhi zetu lakini bado

tutaruhusu *trading* ili wakulima wetu waweze kupata soko.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi *CPB, NFRA* na taasisi zetu zimeanza kununua mahindi, wataenda kushindana. Mimi nitamshangaa mkulima wa Tanzania atakayeza mahindi yake chini ya Sh.500, nitamshangaa sana. Wacha tukashindane, sisi Serikali ni jukumu letu kuhifadhi, tunafanya jukumu letu la kuhifadhi lakini hatutomzuia mkulima kuuza lakini wakati huo tutalinda maslahi na usalama wa nchi.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingi zimezungumzwa kuhusu bajeti. Ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wakafahamu, fedha zinazoenda kwenye sekta ya kilimo ambazo ni *off budget* kwa maana ya zillizopo nje ya bajeti kwa kipindi cha miaka minne ni zaidi shilingi trilioni 3 lakini fedha hizi zinaenda wapi? Ndiyo nataka niwaambieni ni lazima tukubali kwamba kuna upungufu wa fedha za kibajeti lakini zipo fedha nyingi zinazoenda katika sekta ya kilimo. Kama Wizara tumeamua kufanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza tuna *streamline* hizi fedha zote ziende kutoa matokeo kwenye sekta ya kilimo. Mbili, tumeamua sasa ndani ya Wizara kuanza kutengeneza *framework/shopping list, development partner* yeoyote anayekuja kuwekeza katika sekta ya kilimo lazima iwe *demand driven* siyo mambo ya kukaa na kusema kwamba tunafanya semina elekezi. Toka tunapata uhuru fedha za semina elekezi kwenye sekta ya kilimo zimekuwepo *now is enough*, tunataka fedha za kilimo ziende moja kwa moja kumgusa mkulima na kuleta matokeo. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, tunao mpango wa *SADP II*, huu ndiyo *guiding document* na tumeelekeza *development partner* na wawekezaji wote waje. Sisi kama Wizara tunatengeneza maelekezo ni wapi fedha ziende kuwekezwa. Hatutaruhusu fedha kwenda tena kwenye masuala ya semina na mafunzo, tumeshafundishwa vyatutu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo hoja ambayo ndani ya Wizara sasa hivi tunaanza kuandaa maandiko. Nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba wataalam wetu ndani ya Wizara tumeanza kufanya kazi kubwa tatu. Moja, tunashauriana na wenzetu Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha namna ya kuja na mfumo wa kikodi utakaoongoza sekta ya kilimo. Haiwezekani kila mwaka wa fedha tunakimbizana na Mheshimiwa Dkt. Mpango punguza hapa VAT halafu tukirudi hatuoni matokeo. Tunatengeneza *roadmap* ya Wizara na hii ni *study* tunayoifanya ndani ya Wizara ya Kilimo kuja na *tax structure* kwa ajili ya *agricultural sector* ambayo itatu-*guide* kwa kipindi cha miaka mitano mpaka miaka kumi ili tuweze kuona mwelekeo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tunalifanya kazi ni *financing* ya *agricultural sector*. Mfikirie mkulima aliyepo kule Njombe anayellima zao la parachichi. Waziri wa Fedha yupo mkulima mmoja wa zabibu amekosa mkopo. Leo mkulima anaenda kukopa benki na ili parachichi iweze kuvunwa ni ndani ya miaka mitatu, benki inataka ianze kulipwa *interest* ndani ya miezi sita au mwaka mmoja aanze *repayment*, haiwezekani. Tunakuja na *study* ya *how to finance agricultural sector* katika nchi yetu, hii itatusaidia kuondoka kwenye matatizo. (*Makof/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, tunayo matatizo ya mbegu. Katika bajeti yetu ASA na TAR/tumetenga jumla ya shilingi bilioni 11 lakini zipo fedha kwenye *pipeline*, tunao mradi wa BMGF ambapo tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha kwa ajili ya kupeleka dola milioni 5 za mbegu lakini tunavutana na hawa wenzetu juu ya *administrative funds*, asilimia 33 ya hii fedha inaenda kwenye utawala. Huu ndiyo mjadala unaendelea, tunaamini siyo muda mrefu haya mambo tutayatatua. Ni dhamira ya Wizara yetu na haya ndiyo maelekezo ambayo Waziri wetu ametupa kuhakikisha tunajitegemea katika suala la mbegu. (*Makof/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ambalo nataka kusema, maelekezo ya llani ya Chama cha Mapinduzi ni kujenga ushirika, hatuwezi kujenga ushirika wa kinyonyaji.

Tutajenga ushirika utakaomsaidia mkulima na utakaompatia thamani ya jasho lake na haya ndiyo maelekezo ya chama chetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jana tumekuwa na watu wa kahawa, msimu uliopita wametoa bei ya 1,130 kule Kagera kwa ajili ya kahawa ya maganda lakini ukitazama fedha ambazo zinakwenda kwenye Chama cha Ushirika ambapo ni makato kutoka kwa mkulima kuanzia *AMCOS* mpaka chama kikuu ni bilioni 11. Tumekaa nao jana, tumewataka *TADB* wapunguze *interest* kutoka asilimia 12 mpaka asilimia 9, hizi asilimia 3 zirudi kwenye bei ya mkulima na vilevile kuwapunguzia hawa *KBCU* na *KCU* bilioni 11 ambayo ni mapato wanayobaki nayo viongozi wa ushirika. Hizi fedha zote zitarudi kwa wakulima na tunaamini mkulimwa wa Kagera mwaka kesho kahawa bei yake itakuwa siyo chini ya 2,500 mpaka 2,700 ambayo itatokana na fedha zinazotokana na jasho lao. Tunapunguza *interest rate* kutoka *TADB* ili fedha hiyo ionekane kwa wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme kitu kimoja, dhamira yetu kama Wizara ya Kilimo ni *commercialize* sekta ya kilimo. Kilimo ni biashara na wakulima lazima wapate *value* yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bashe, Naibu Waziri. Ahsante sana kwa kutupatia *vision* hiyo ya Wizara ya Kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Omari Mgumba karibu tafadhali, baada ya hapo Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Muda ni mchache lakini kwanza nikupongeze kama walivyokupongeza wenzangu lakini nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya na uzima. Nimshukuru

Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu kuendelea kunivumilia kubaki katika nafasi hii ya kumsaidia Waziri pamoja na yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwanza kumalizia pale alipoishia Mheshimiwa Bashe kwenye suala la kahawa. Katika suala hilo la kahawa kama alivyosema tumedhamiria kumkomboa mkulima hasa kule Kagera wanafahamu vyema. Vitendo wanavyofanyiwa wakulima ukiangalia ni aibu. *KDCU* na *KCU* walikwenda kununua deni chechefu zaidi ya bilioni 7 *CRDB* na *NMB*, deni hilo lote wamewabebesha wakulima walipe ndiyo maana wakulima wanalipwa bei ndogo. Ndiyo maana tumedhamiria wale wote waliosababisha deni hilo lazima tuwatafute walipe. Hatuwezi hata siku moja wakulima wakatumika kama ni daraja la kuwanufaisha watu binafsi kwa maslahi ya binafsi. Lazima tutasimamia mkulima apate kulingana na jasho lake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyngi hapa ambazo zimezungumzwa kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Kwanza niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tunayapokea mawazo yenu yote mazuri kwa sababu muda ni mchache hatuwezi kujibu kila kitu hapa lakini yote tutaenda kuyafanya kazi na mtapata majibu yenu kwa njia ya maandishi. Kwa hiyo, tutajibu tu kwa ufupi sana kutockana na kwamba sekta hii ya umwagiliaji ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali cha kwanza tulichokiona miradi ya umwagiliaji inahitaji fedha nyngi sana. Natoa mfano wa mradi mmoja tu wa pale Dakawa, tumewekeza zaidi ya bilioni 21 na umekwisha mwaka jana, tunasubiri kwenda kuzindua na miradi mingine 56. Pamoja na kuwekeza bilioni 21 kwenye mradi huo na miradi mingine mingi ya umwagiliaji wakulima wanalima baada ya kulima hata ikiharibika pampu wanapiga simu Wizara ya Kilimo au Wizara ya Fedha tupeleke pale kitu ambacho ni tofauti na miradi ile ya afya. Hata miradi ya afya tunawekeza vituo vya afya milioni 400 lakini ukienda kutibiwa pale unalipa hata hela ya kumuona daktari shilingi 6,000 au unalipia bima ya afya ili upate matibabu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa ili miradi hii iwe endelevu na tuweze kupanua kilimo cha umwagiliaji, tunafanya maboresho na mtuunge mkono Waheshimiwa Wabunge, kilimo cha umwagiliaji lazima kiwe kilimo cha biashara. Kwanza, sheria inaturuhusu lazima tuanzishe Mfuko wa Umwagiliaji wa Taifa kwa ajili ya kukusafanya fedha kutoka kwenye miradi yote ya umma ambayo tunaruhusiwa kwa mujibu wa sheria ili kuchangia mfuko huu tuweze kupanua kilimo cha umwagiliaji. Kwa huu utaratibu tunaoenda nao hatuwezi kupanua kilimo cha umwagiliaji ambapo tutahitaji miaka mingine 58 kufikisha hizo hekta milioni 2 ambazo zina uwezekano mkubwa wa kumwagilia hapa nchini. Mpaka sasa tumeendeleza tu hekta 475,000 katil ya hekta milioni 29 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaleta maboresho hayo ili miradi hii yote ya umwagiliaji tuiendeshe kwa kilimo cha biashara. Tutawekeza lakini wale watakaoitumia miradi hiyo lazima walipe pango au tozo ya uwekezaji ili Serikali ipate mapato kuendelea kupanua kilimo hiki. Hilo ndiyo litakuwa suluhisho la kupanua kilimo cha umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kwa mujibu wa sheria na kanuni, tunatakiwa tukusanye angalau asilimia tano kwenye miradi hiyo ya umwagiliaji kutoka kwenye kipato cha wakulima wa umwagiliaji lakini mpaka leo hii hizo hela hazikusanywi. Tumedhamiria kuanzia mwaka huu tunakwenda kukusanya kwa mujibu wa sheria ili pesa hizo zitumike kwa ajili ya uendelezaji, usimamizi na utunzaji wa miradi hiyo pia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza ni suala la magunia. Namshukuru sana Mheshimiwa Nape, mchango wako tumeuchukua na tutaufanya kazi. Kulikuwa na changamoto kubwa ya magunia mwaka jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niwaeleze Waheshimiwa Wabunge magunia haya ilikuwa ni jukumu la Mifuko ya Kuendeleza Mazao kuagiza miaka yote kwamba

ilikuwa ni jukumu la Serikali. Mwaka 2017 kutokana na changamoto ya Mfuko ule kuvunjwa majukumu yale yalihamishiwa Bodi ya Korosho lakini kwa miaka miwili majukumu yale yalipelekwa kwenye vyama vyetu vikuu vya ushirika waagize wenyewe. Kama ushauri wako ulivyosema kwamba tusiweke mtu wa katikati, hata siku moja vyama vya ushirika hawajawahi kuagiza wenyewe magunia kutoka kwa wazalishaji. Vyama hivi vilikuwa wanunu kutoka kwa mtu wa katikati hapo ambaye ni mfanyabiashara ambapo mwaka huu tumesema hapana. Lazima magunia aidha tuagize wenyewe Serikali au wakulima wenyewe waagize badala kumuweka mtu wa katikati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja hapa hai na tujue kwamba wizi gani ulikuwa unafanyika kwa wakulima wa korosho kule Mtwara. Ni unyama ulikuwa unafanyika Serikali hii ya Awamu ya Tano hatuwezi kukubali. Kuagiza gunia moja *CF price* mpaka likifika pale Dar es Salaam ni dola 1,000. Dola 1,000 ukikokotoa zile, ninazo hapa, natoa mfano tu ukiweka kwenye bei ya 2,320 inakuwa dola 1,000 ni sawasawa 2,320; *import duty* ni dola 580, VAT ni 520; *CNF cost* 140; *transportation cost* kwenda kule Mtwara shilingi 53; *storage* shilingi 50; jumla ni 3,615. Benki *interest* 163; jumla 3,718 lakini wakulima walikuwa wanachajiwa shilingi 4,200 kwa gunia moja.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hapo, kwa mujibu wa sheria kama gunia lile tunatumia kwa ajili ya *ku-export* tunapata *exemption TRA*, wanapata miaka yote hii 500 haipo, hela zote zilikuwa zinakwenda kwenye matumbo ya watu tumesema haiwezekani kwenda kumnyonya mkulima kiasi hicho. Ndiyo maana tukasema kama kuna umuhimu wataagiza taasisi ya Serikali, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ni taasisi tulioianzisha kwa ajili ya kufanya biashara kwa ushirikiano na wakulima wenyewe ili kama kuna punguzo lolote la tozo la ushuru iende kwa wakulima ili wakulima wafaidike. Tunafanya haya kwa nia nzuri baada ya kuona mnavyoibwa wakulima wa korosho na wajanja wachache, tukasema haiwezekani lazima iende kule kwa wakulima. Ndiyo maana tunasema tunachukua ushauri wako

lakini nia ya Serikali ni nzuri sana ili tuwaondoe pembedi hawa waliokuwa katikati ambao wanashirikiana na vikundi vichache kuwaibia wakulima wetu wa korosho Mtwara. (*Makof/ Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu kuyumba kwa bei ya kahawa. Ni kweli bei ya kahawa inayumba na inashuka sana lakini changamoto kubwa ni kutokana na uzalishaji mkubwa ulioko katika soko la dunia. Mzalishaji mkubwa Brazil kwa mfano mwaka jana ameingiza zaidi ya magunia milioni 9 ya ziada katika soko la dunia kitu ambacho kilisababisha bei kushuka na wanywaji pia wamebaki wale wale wazalishaji tumeendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja; wazalishaji wa kahawa tunauza kahawa kwa dola billioni 20 lakini mzunguko wa biashara ya kahawa ni zaidi ya dola bilioni 200, kwa hiyo, unaona mara 10 inakwenda kwenye *import country* sisi tunao-*export* tunachukua *only* 20%. Nini maana yake? Sisi wenyewe Waafrika tunazalisha lakini hatunywi kahawa matokeo yake tuna *import* kahawa sawasawa na kiwango tunacho *export* lakini tunauza kwa bei ndogo *in raw form* tunanunua kahawa kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali cha kwanza tumeweza kuhamasisha na kufanya maonyesho mbalimbali ya unywaji wa kahawa hapa nchini lakini pia kuingia katika masoko mapya soko la China, Afrika Kusini na Uarabuni kwa ajili ya unywaji wa kahawa. Kama mnavyofahamu China ni wanywaji wakubwa wa chai, sasa hivi ndiyo tumepeleka kahawa yetu kwa kushirikiana na Balozi wetu wa China, ametupa ushirikiano mzuri sana, wanaanza kunywa kahawa yetu, hivi karibuni tutafanya mazungumzo mazuri tupanue soko letu la kahawa ili kuongeza mahitaji ya kahawa duniani lakini soko letu liweze kupata bei nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tumefanya maonyesho hapa Zanzibar kama miezi minne iliyopita mwanzoni mwa Januari ili kuwaalika makampuni makubwa haya kutoka nchi

hizo za wanywaji wapya na wale wa masoko yetu ya asili ili kuja kuona muonjo wa kahawa yetu kwa sababu wakati mwingine tunapouza kule kahawa yetu inapoteza uasilia. Wameipenda na ni imani yetu kwamba tutaendelea kuongeza masoko na tukiongeza masoko mahitaji yataongezeka matokeo yake na bei pia itaongezeka. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo tukafanya maboresho minada kuweka kwenye kanda zetu zote za wazalishaji wa kahawa. Leo hii tuna mnada wa kahawa Kanda ya Ziwa kule Kagera; Ruvuma; Songwe na Kilimanjaro. Yote hii ni kuwapeleka wanunuzi karibu na wakulima ili kuweza kutoa bei nzuri zaidi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, la mwisho katika kuboresha zao la kahawa, mwaka huu tumetoa mwongozo lazima tuboreshe mfumo wa masoko yetu haya ya minada. Kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Kikwembe lazima tuweke *level mbili* za masoko. Tuweke *level/ya kwanza* minada ya masoko ya ndani na pili tunakuwa na mnada kwa ajili ya *ku-export* nje. Bila kufanya hivyo maana yake sisi tutakuwa ni wazalishaji wa mazao ya kilimo na kuuza *raw material* kwa viwanda vya Ulaya. Tumeua viwanda vya korosho, viwanda vya kahawa vina miaka miwili, mitano havipati *raw material*/kwa sababu tunawashindanisha wawekezaji wa ndani na wa nje kununua *raw material* katika soko moja. Tukasema hapana, lazima tuwe na soko la awali (*primary market*) kwa ajili ya *local trading* na *domestic processors* ili wapate *raw material* kwa ajili ya viwanda vyetu vya ndani na kuzalisha ajira na uchumi baadaye sasa tunakwenda kwenye mnada wa pili (*secondary market*) kwa ajili ya *export*, pale wataruhusiwa *only for export* wakati huo tuna uhakika viwanda vyetu vya ndani vina *raw material*/na tumetengeneza ajira. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba mtuunge mkono, nia ni nzuri lakini pia kujenga biashara na uchumi. Wale wa Mtwara mtakubaliana na mimi miaka ile ya Mtwara tulipokuwa na biashara ambayo ina masoko ya awali uchumi kule ulikuwa ni mkubwa sana. *Guest* na hotel zinajaa, shughuli

za uchumi zinafanyika, bodaboda zinafanya kazi lakini leo hakuna shughuli zote hizo, ukienda Mtwara wala hupigi simu chumba unakikuta, unaambiwa uchague vingapi. Lazima turudishe hali ile, tuweke masoko ya awali kwa ajili ya kuchangamsha uchumi ndani ya nchi halafu tuwe na soko la upili kwa *export* kwa ajili ya watu wa duniani washindane. Lengo tunataka tuimarishe uchumi wetu ndani ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu sukari, naomba univumilie kidogo kwa sababu sukari ni changamoto hapa nchini ili Waheshimiwa Wabunge wajue mipango ya Serikali tuliyokuwa nayo kwa ajili ya kuboresha zao hili la sukari. Mheshimiwa Waziri ameshasema vya kutosha na atakuja kufunga hoja wakati anapofanya majumuisho lakini tuna mipango ya muda mfupi na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya upungufu wa sukari moja ni mabadiliko ya hali ya hewa, mvua hizi zimekuwa ni nydingi mno na siku zote viwanda vyetu tunavifunga mwezi Machi kwa ajili ya kupisha matengenezo lakini kutokana na mvua nydingi mwaka huu viwanda hivi vimefungwa mapema tangu mwezi Januari kwa sababu mashamba yamejaa maji lakini pia barabara za kwenda mashambani kuvuna miwa vimeharibika lakini tatu kiwango cha sukari kwenye miwa kimepungua sana. Kwa hiyo, lazima vilikuwa vifungwe mapema lakini Serikali tuliona hilo tukawapa vibali vya kuagiza zaidi ya tani 40,000 na sukari sasa ikaanza kuingia. Kwa bahati mbaya sana wakati inaanza kuingia ndiyo tukakumbana na hii *Corona* matokeo yake zile nchi ambazo tulialgiza wakawa na *lockdown* zile meli zilifanya *cancellation* ndiyo maana inakuja kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hivyo sababu ya tatu ni wafanyabiashara ambao siyo waadilifu wameficha sukari kwa lengo wanadolijua wao la kujitajirisha wao wenyewe. Nikuhakikishie tumeshaanza kuchukua hatua na wengine tushawakamata na tushawafikisha kwenye vyombo vya sheria. Wasije kupotosha kwamba Serikali tumeingilia bei, hapana, hatutoingilia biashara lakini tutamlinda mlaji na

mkulima kwa sababu sukari inayozalishwa hapa nchini ina gharama kubwa zaidi kuliko inayozalishwa nje ya nchi kutokana na teknolojia zao kuwa kubwa. Kama sukari tuliyozalisha nchini tumeweza kuuza bei ya Sh.2,200 mpaka Sh.2,600 kwa nini sukari ya kutoka nje ambayo imezalishwa kwa gharama nafuu iuzwe kwa Sh.4,000? Tulikaa nao tumeweka zile bei zote hatukuzitoa kichwani na bei ilikuwa inatakiwa iuzwe *maximum* Sh.3,000 lakini tukaenda mpaka Sh.3,200. Huu uhuni unaofanyika hatuvezi kukubaliana nao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa wananchi wa Tanzania mtupe ushirikiano yeote anayekuuzia sukari kwa Sh.4,000 au Sh.5000 dai risiti kama hajakupa risiti toa taarifa kwa viongozi wa Kamati za Ulinzi na Usalama kwenye ngazi yako. Tunaye Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kata, Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wote hao tuko kazini kwa ajili ya kuwafichua hawa wafanyabiashara mafisadi wanaotaka kumuumiza mlaji.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (Makofi/Vigelegele)

**SPIKA:** Nashukuru sanasana. Hakika Waheshimiwa Wabunge tutakubaliana kwamba Naibu Mawaziri hawa wawili wa Wizara ya Kilimo kwa kweli wanachapa kazi na wanaelewa *subject matter* iliyo mbele yao, wanajua jinsi gani ambavyo Wizara hii ni nzito na ina changamoto nyingi sana. (Makofi)

Sasa Mheshimiwa Waziri jitahidi katika dakika 20 zilizobakia baada ya Naibu Mawaziri kukupunguzia kidogo basi na wewe jazia jazia pale unapoona inafaa. Karibu sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo siku ya leo hii na kushiriki katika mjadala huu mzito ambao umebeba wananchi walio wengi ambao wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, naomba nichukue nafasi hii kwanza kuwaomba wana Kongwa kama inawezekana wakupitishe bila kupingwa. Haiwezekani kazi kubwa unayoifanya kama Spika halafu tena uende kushindana na watu wengine huko. Watanzania wanaoona hakuna sababu. Mimi naamini wana Kongwa wana busara watatumia busara watapitisha jina lako utarudi hapa na sisi tunataka uendelee kuwa Spika, hilo naamini litawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Yeye ndiye amekuwa mhimili mkubwa katika kuendeleza kilimo cha Watanzania. Bunge hili mnakumbuka alipotoa hotuba yake alisema sitaki kusikia mkoa wowote wala wilaya yoyote ina upungufu wa chakula na hilli limewezekana katika kipindi cha miaka mitano. Kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waziri Mkuu kama kuna kazi ambazo amefanya kwa wingi naamini kabisa asilimia zaidi ya 70 ameshughulikia masuala yanayohusiana na kilimo, amefanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu amezunguka nchi nzima kila kona amezungumzia kilimo, ameunda tume nyingi zimefanya kazi ya kilimo. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi hiyo uliyoifanya kama wana Ruangwa wana busara hakuna sababu ya kumuweka mtu mwingine kugombana na wewe. Kwa kazi kubwa uliyoifanya kama Waziri Mkuu wewe usubiri kura za maoni zimeshapita, uchaguzi umeshapita urudi hapa Bungeni tuendelee kuchapa kazi. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee niwashukuru Waheshimiwa Naibu Mawaziri wameshanirahisishia kazi yote. Wamefanya kazi vizuri, wamejibu hoja mbalimbali za Wabunge, kwa kweli wamefanya kazi vizuri sana na wanansaidia sana katika kutekeleza majukumu yangu. Kwa

kweli nawapongeza sana Waheshimiwa Naibu Mawaziri. Nina imani na ninyi huko kwenu mtakakokwenda basi mtapita bila kupingwa. Wakati huko wanawapitisha bila kupingwa nina imani hata wananchi wangu wa Vwawa huko watasema na mimi Hasunga napita bila kupingwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wamechangia vizuri sana, muda haukutosha lakini hoja walizozibua ni nyingi na wamesema kwa undani na kwa umahiri mkubwa. Tumepata Wabunge ambaao wamechangia kwa kuzungumza 21 bahati mbaya hatujapata namba kamili ya Wabunge ambaao wamechangia kwa maandishi lakini kwa muda mfupi wameibua hoja nyingi sana. Ni wazi kabisa katika kipindi hiki cha dakika 20 hatutaweza kumaliza kujibu hoja zote lakini hoja nyingi tutakuja kuwajibu kwa maandishi, tutafafanua kwa undani sana namna ambavyo tumejipanga katika kuhakikisha tunasimamia kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee nipongeze sana Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji. Wamefanya kazi nzuri sana na wameibua hoja za msingi nzuri sana. Hoja nyingi wamezisema na nyingine kwa kweli hatutaweza kuzijibu lakini nitaomba niahidi tu kwamba hoja nyingi hizi tutazijibu kwa maandishi, tutatoa ufanuzi wa kutosha namna ambavyo tumejipanga katika kuchukua hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini moja ya hoja ya Kamati ni kuchukua hatua za kinidhamu na kisheria kwa wahusika waliobainika kuingiza pembejeo feki. Ni wazi kabisa na Wabunge wengi wamechangia ili kilimo kiweze kuendelea na kufanya vizuri lazima tuanzie kwenye upande wa pembejeo. Kabla ya pembejeo sisi tunasema lazima tuanze kwenye utafiti. Tukiimarisha utafiti utatupatia mbegu zilizo bora ambapo tutazipeleka kwa wakulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa wakulima wa nchi hii na kwa ardhi ya nchi hii ambayo tumebarikiwa, tuna ardhi inayofaa kwenye kilimo zaidi ya hekta milioni 44.2, ni hekta nyingi sana. Kati ya hizo milioni 29.4 zinatafaa kwenye kilimo cha umwagiliaji

Iakini angalia eneo tunalomwagilia sasa hivi ndiyo tunasema tumefika hekta 690,000 bado tuko chini.

Mheshimiwa Spika, sasa basi kama tutaweza kufanya vizuri kwenye utafiti tukapata mbegu zilizo nzuri, tukawekeza kwenye hizi hekta zinazofaa kwenye kilimo, wananchi wote tukawahamasisha kwenda kulima kilimo cha kisasa, wakatumia teknolojia ya kisasa, wakatumia mbegu nzuri na mbolea nina uhakikia nchi hii tunaweza tukawa na chakula cha kutosha, tunaweza tukapata mazao ya kutosha ya biashara na tunaweza tukajenga uchumi imara ambao unatokana na kilimo. Kwa hiyo, lazima tuanzie hapo kwenye utafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaposema pembejeo tuna mambo matatu makubwa. La kwanza ni mbegu bora Iakini la pili ni mbolea. Mimi nimesikiliza hoja za Wabunge wengi mmechangia kuhusiana na mbolea na mimi nasema katika mwaka ambao matumizi ya mbolea yamekuwa ni makubwa ni mwaka huu. Mwanzoni tulikadiria tulikuwa tunahitaji mbolea tani 586,500 Iakini hadi leo hii hatujafunga kilimo tumetumia tani 633,000 zaidi ya kile tulichotarajia na mbolea zote hizi zimekuja. Tatizo lilloluwepo siku nyingi lile la kwamba mbolea sasa zinachelewa, hazipatikani, haziji kwa wakati, zinakuja kwa bei kubwa, zinakuja hazifai, kwa timu hii ya viongozi wangu wote Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Katibu na Wakurugenzi tumelisimamia mwaka huu tumefanya vizuri hatujapata mbolea feki. Tumejitahidi sana na mbolea zote zimekuja kwa wakati na zimefika karibu kila eneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna kipindi tulitaka kupata hitilafu kwenye mbolea za urea ambao tunazinunua kwa Mfumo wa Pamoja Iakini tulichukua hatua na mbolea zimepatikana. Kwa sasa hivi hatuna tatizo, tunachokisema sisi kila Mtanzania mwenye uwezo wa kulima ni wakati muafaka sasa wa kwenda kulima. Kazi ya Serikali ni kuhakikisha pembejeo zinakuja kwa wakati, mbegu na viuatilifu vitakuja kwa wakati Watanzania wakalime. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wapo vijana wengi wanatafuta kazi mitaani na kila mahali lakini hazipatikani mimi nataka niwaambie kazi zipo kwenye kilimo. Zipo changamoto chache ambazo lazima tuziweke vizuri namna kupata mitaji, namna ya kwenda kuwekeza, teknolojia za kisasa tunazipataje, haya yote tunayafanyia kazi, tutayarekebisha, yatakaa vizuri kabisa ili Watanzania hawa, vijana na akina mama hawa waende wakawekeze kwenye kilimo na nchi yetu tupate chakula cha kutosha lakini tupate mazao mengi ya biashara yaweze kuleta fedha nyngi za kigeni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumeona nchi nyngi za jirani hazitakuwa na chakula cha kutosha lakini Tanzania mwaka huu tunacho chakula cha kutosha. Wenzetu bahati mbaya nzige walipita, maeneo mengine kuna ukame na mafuriko na sisi Tanzania kuna maeneo tuna mfuriko lakini bado uwezo wa kupata chakula cha kutosha ni mkubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nachowaomba Watanzania katika hiki chakula watakachokuwa nacho wasikimbilie kuuza nje wakinunza. Nina imani kabisa pale wanapoona kuna haja ya kuuza basi wauze na sisi kama Serikali tutahakikisha wanapata bei nzuri ambayo itakidhi mahitaji yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nimeona kuna wananchi wameanza kuuza debe la mahindi shilingi 5,000, kuna baadhi ya maeneo nimeona, nataka niwaambie mwaka huu debe la mahindi halitakiwi kupungua shilingi 10,000. Akiuza gunia moja ana mfuko wa mbolea na chenji inabaki anaenda kununua mafuta anafanya na vitu vingine. Mpunga tumepata mwingu jambo Morogoro na maeneo mengine kama Simiyu tumepata mafuriko makubwa hawatapa sana, lakini maeneo mengine pia yameibuka yamelima vizuri, nina uhakika tutapata mavuno mazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nachotaka kusema kwenye hili suala la biashara ya mazao sisi tunatamani watu wafanye biashara lakini hawa watu kutoka nje kwenda moja kwa moja

kwa mkulima mmoja mmoja kule chini ndiyo changamoto kwani usalama wa nchi utakuwa siyo mzuri.

Sisi tunachosema Halmashauri ziweke maeneo mahsus ambapo watu kutoka nje watakwenda kununua mazao mbalimbali. Kila Halmashauri waweke vituo mtu wa nje anakwenda pale anajisajili anapata kibali ananunua mazao pale anaondoka. Kwa namna hiyo itatusaidia kuwa na takwimu sahihi za kiasi gani cha mazoa kimeenda nje ya nchi. Bila kufanya hivyo tutakuwa hatuna uwezo wa kufanya vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kazi ya Wizara ya Kilimo ni kusimamia sera, miongozo, kuwasimamia Maafisa Ugani na kadhalika. Maafisa Ugani wapo TAMISEMI lakini tunashirikiana na TAMISEMI na sasa hivi tunazungumza namna ya kuwasimamia. Nchi kama Uganda wamefanya vizuri sana katika kuwasimamia Maafisa Ugani, wana miongozo mizuri sana na sisi Bunge lako tukufu mwaka 2006 lilipitisha Marekebisho ya Sheria ambapo lilitoa madaraka kwa sekta zinazohusika kusimamiwa wale wataalam wa TAMISEMI. Wapo TAMISEMI lakini sekta zinahusika zinatakiwa kuwasimamia na sisi tunao wajibu wa kusimamia Maafisa Ugani. Kwa hiyo, sasa hivi hili tutaliweka vizuri ili waweze kutoa mchango mkubwa katika kuhakikisha kwa kweli wanaleta mageuzi makubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini tunapita sheria, tulitamani kabla ya Bunge lako hili halijaisha Sheria ya Kilimo ije hapa Bungeni bahati mbaya mchakato ilianza lakini haikuweza kufikia hatua za mwisho. Nina imani Bunge linalokuja moja ya kitu kitachofanyika ni kupitia Sheria Mpya ya Kilimo pamoja na sera nyingine ambazo zitakuwa zimeletwa. Hata hivyo, nafurahi katika Bunge lako hili tutawasilisha marekebisho ya sheria chache. Tutaleta Sheria ya Kuunganisha TPRA pamoja na PHS waliopo kwenye vituo, Bunge hili litatafakari na tutawashukuru sana mtakapotupitishia sheria hizo. Pia tulitaka tuje na Sheria mpya ya Ushirika, nayo bahati mbaya haikuweza kukamilika katika kipindi hiki, iko kwenye

michakato itaendelea kukamilishwa vizuri ili wadau mbalimbali waweze kutoa maoni yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachotaka kusema sisi tumeweka mkakati wa kutosha, ili kuhakikisha tunawahudumia wakulima huwezi kumhudumia mtu usiyemjua au usiyemtambua. Ndiyo maana tukaweka mkazo kwamba lazima kwanza tutengeneze kanzidata ya kuwasajili wakulima wote ili tuwajue. Tukijua huyu ni mkulima wa korosho, huyu ni mkulima wa kahawa, hawa ni wakulima wa mahindi, hawa ni wakulima wazabibu, hawa ni wakulima wa mchikichi, wapo wangapi, wanalima eneo lenye ukubwa kiasi gani na wanahitaji nini ndiyo tunaweza kuwahudumia. Bila takwimu sahihi hatuwezi kuwahudumia. Hatutaki tuendelee kuimba kwamba kilimo ni uti wa mgongo bila kuwa na sera madhubuti na mikakati na miongozo madhubuti ya kuhakikisha kwa kweli haya yanaonekana kwa vitendo. Nina imani haya yote tutayafanya kazi na tutyaweweka vizuri. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, zipo hoja nyingi, mimi nitajibu kidogo sana. Suala la malipo ya korosho ya kipindi kilichopita Naibu Mawaziri wameshafafanua kidogo. Malipo ya korosho katika mwaka 2018, nashukuru pongezi za Mheshimiwa Nape na wengine wote wa kutoka kwenye korosho, tumehakikisha kwamba mwaka huu hatukupata shida popote. Tumepata shida pale tu ambapo vifungashio vilichelewa na vifungashio kwa sababu vyama vya ushirika vilikuwa vinaagiza vilichelewesha ndiyo tukapata shida ndiyo korosho chache zilizobaki. Wale wa msimu ule ambao Serikali tulinunua ndiyo kidogo bado hatujamala kuwalipa. Nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi Serikali imetoa fedha na wanaendelea kulipwa na kama tulivyojiwekea lengo kwamba kufikia tarehe 30 Juni wote wawe walimelipwa tuwe tumeachana kabisa na matatizo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na mchango wa Mheshimiwa Ngombale kwamba hata wale wasafirishaji wote tumewewe ka kwenye orodha ili ikiwezekana wote

waweze kulipwa tumalizane tuendelee kuchangia katika uchumi wa wa taifa letu. Hili tutalisimamia.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu masoko ya mazao. Kwenye masoko ya mazao na hata katika kipindi hiki cha homa hii ambayo inasababishwa na virusi vya *Corona* tutapata changamoto kidogo, kwa sababu kama hali itaendelea kama hivi maana yake wale wateja ambao walikuwa wanakuja huku kwetu hawaweza kufika. Sasa kama hawataweza tutafanyaje biashara ya mazao yetu. Sisi tunategemea kutumia njia tatu. Njia ya kwanza ni kuuza kwa mtandao, maana yake tutumia soko la bidhaa, tutatangaza *tender* mtu kokote aliko huko duniani kama yupo *lockdown* huko huko aliko ye ye ata-*bid* kwenye mfumo na atatangaza ni kiasi gani anahitaji na sisi tutamhakikishia mzigo wake utafika bila shida yoyote. Hili tumelisimimia na tulishallizindua kwenye Nane Nane kule Simiyu, tunataka tuhakikishe soko la bidhaa lilliozinduliwa na Bunge hili lifanye kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, njia ya pili, tunasema Balozi zetu zilizopo huko nje kwa kushikirikiana na Wizara na Mambo ya Nje lazima sasa watusaidie, waongee na wanunuzi walioko huko wanaohitaji bidhaa, waingie mikataba na watu hao. Sisi tukiona bei ni nzuri hatuhitaji kutangaza *tender*, suala ni kusaini mkataba na kwenda kuwauzia wananchi watapata fedha nzuri na itawasaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini nizungumzie kidogo kuhusu soko la chai na wameshasema Naibu Waziri. Chai yetu ni zao lillioathirika sana baada ya ugonjwa huu kuanza. Tulikuwa tunategemea soko la Mombasa, soko la Mombasa liliopfungwa kwetu hapa hatukuwa na uwezo wa kwenda mahali popote. Namshukuru sana Waziri wa Viwanda na Biashara wametupatia eneo pale Dar es Salaam, tunafanya maandalizi tunataka kuzindua soko letu la kufanya minada ya chai hapa hapa nchi na hiyo itatusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni pamoja na soko la mazao mengine kama ya bustani. Sasa hivi Kenya

wanauzwa maparachichi kwa wingi sana kwa sababu maparachichi ya Tanzania yote tunayasafirisha huku tunayapeleka kwenda kusafirishia Nairobi au Mombasa, hii haiwezeki. Tunazo ndege zetu na watu binafsi lazima masoko yafunguliwe hapa kwetu tuweze kuwa na takwimu sahihi na tuweze kuona manufaa ya haya yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachotaka kusema sisi tumejipanga vizuri na ndiyo maana nimesema kwa kauli moja tu kwamba mwaka ujao sisi kwa kuona hizi fursa zilizopo kwenye kilimo, tunataka nchi sasa izalishe chakula kingi ili sisi tuwe ndiyo *hub* ya kulisha nchi za Afrika Mashariki na nchi za Kusini mwa Afrika. Mazao mengine ya bustani sasa hivi tumeshaingia Soko la Ulaya tunataka tuende Uarabuni na kwenye masoko mengine. Bahati nzuri hata ndege zetu moja imeanza kubeba mizigo, hizi ni jitihada nzuri sana na naipongeza sana Serikali yetu kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunataka kwenye mazao ya biashara tuzalishé zaidi ya tani milioni 5.2 kwa mchanganuo mwingi tu. Kwa mfano, tunataka zao la pamba tufikie tani laki nne. Mheshimiwa Waziri Mkuu amelisimamia sana sisi tunataka tufikie tani laki nne. Mwaka huu tumefika tani laki tatu na hamsini na mbili elfu sasa tunataka tufike tani laki nne. Tunataka Korosho tufike tani zaidi ya laki tatu na hamsini, chai tani elfu arobaini na kahawa tani elfu tisini. Miwa ambapo ardhi tunayo tunapata shida ya sukari wakati kila kitu tunacho na tuna uwezo wa kuzalisha, tunataka tuzalishé miwa zaidi ya tani milioni nne nukta mbili. Hii ni mikakati ambayo tumejiwekea, mazao ya bustani tumeweka mkakati wa kutosha. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, mimi imani yangu ni kwamba naomba wananchi wote wa Tanzania tukubaliane na waelewe kwamba kilimo sasa hivi ni biashara, viwanda, ajira, maisha na ni chakula. Wote tukielewa hivyo tutafanikiwa kusukuma kilimo na kila mmoja wetu humu tena niwapongeze na Wabunge, wote hapa kwa asilimia kubwa ni wakulima. Kama kuna Mbunge halimi atakuwa na matatizo yake binafsi.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini wote ni wakulima nawapongeza, ni wadau wangu, Watanzania wote na wakulima wa nchi hii nawapongeza kwa kazi kubwa, waendelee kuchapa kazi na Mungu atakuwa pamoja nasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuhitimisha hoja yako kwa ufasaha mkubwa kabisa ukisaidiwa na Waheshimiwa Naibu Mawaziri. Kama mlivyosema mwanzo basi mengine yale mtayaafanua kwa maandishi na kututupia kwenye *tablets* zetu kwa ajili ya faida yetu na wapiga kura. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa jukumu langu hapa ni kuwaomba mkubali kuitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kura zangu hapa moja kwa moja zinaonesha kwamba kwa wingi kabisa waliosema 'Ndiyo' wameshinda. (*Makofi*)

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.....Sh.4,925,665,000  
Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika.....Sh.9,608,846,000  
Fungu 43 – Wizara ya Kilimo.....Sh.65,230,973,000

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.....Sh.12,801,180,000  
Fungu 43 – Wizara ya Kilimo.....Sh.137,273,144,000

**SPIKA:** Kwa niaba yenu wote, tukupongeze sana Mheshimiwa Waziri, umejitahidi sana na wasaidizi wako wote; Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wote kabisa mmejitahidi, mmejitahidi, mmejitahidi. (*Makofi*)

Kwa kawaida hii ni Wizara nzito, ngumu kwa sababu ndiyo Wizara ya Watanzania, asilimia kubwa ya Watanzania kilimo ndiyo *occupation* yao. Mmetufikisha hapa tulipofika, tunasema ahsanteni sana lakini safari bado. (*Makofi*)

Kama mlivyoeleza ninyi wenyewe nia na mipango mliyonayo ya kuweza kutupeleka mbele zaidi na sisi tupo nanyi. Tunajua bajeti tuliyowapa si kubwa kiasi hicho lakini hebu kaifanyieni kazi. Huenda Mwenyezi Mungu akijalia tukakutana mwakani inaweza ikawa ni bajeti kubwa zaidi na mka-*cover* maeneo makubwa zaidi.

Kama walivyochangia Waheshimiwa Wabunge, yako maeneo tukiyapa kipaumbele cha kutosha yatatufikisha mbali. Kilimo hata kama hujafanya kingine chochote, soko likiwa zuri tu hilo zao lina *boomyaani* wakulima watalima zao hilo kwa wingi zaidi. Soko likishakuwa zuri la kitu fulani utaona wakulima wana-*move* wanaelekea huko. Kwa hiyo, eneo la masoko lipewe kipaumbele kwa kutafuta masoko yatakayotupatia bei nzuri za wakulima. Hili kiwe ni kipaumbele kikubwa sana kwa sababu soko katika *value chain* inavuta kila kitu kuanzia huku chini. Soko la ufuta lilikuwa limeporomoka na wakulima waliacha kulima ufuta sasa hivi limeanza kuja juu na wakulima tayari wanalima ufuta na mazao mengine ni hivyo hivyo. Soko la kahawa limeshuka chini kidogo watu wanatamani hata kung'oa baadhi ya mikahawa lakini likipanda kila mtu atapanda mikahawa na kadhalika, kwa hiyo soko ni kitu muhimu kweli.

Mengine yote wameyaoeleza Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuna tatizo kubwa sana la mbegu, mbegu zilizopo sokoni kujua *reliability* yake ni mtihani. Vilevile mbegu zilizopo madukani ni ghali sana mkulima wa kawaida hawezu kumudu hasa kama ana shamba kubwa kidogo, sio rahisi.

Upande wa vitendea kazi, matrekta, *power tillers*, majembe ya plau, upande huu kwa kweli tumekwenda vizuri sana. Sasa hivi tuna matrekta mengi zaidi kuliko wakati wowote mwingine na yanazidi kuingia nchini. Tunawashukuru wote ambao wanatuletea matrekta. Sehemu mbalimbali za nchi yetu sasa kilimo kinakwenda mbele na kuwa ni *more mechanized* kuliko ilivyokuwa siku za nyuma jambo ambalo ni zuri sana. Kwa hiyo, maeneo yote haya ya umwagiliaji, viuatilifu na mengine yote ambayo ndiyo yanaongeza tija ni jambo muhimu sana sana.

Kuhusu watumishi wa Wizara ya Kilimo, sasa hapo tunaweza tukawa na *a divided opinion*. Nimewahi kufanya kautafiti kangu kasikokuwa rasmi sana nikagundua wataalam wa kilimo na mifugo *actually* wanasesma sisi ni Maafisa Kilimo na Maafisa Mifugo lakini sisi sio wakulima. Wanaamini hivyo, kuanzia kule *SUA* na kwingine hata Maprofesa wao wanaamini hivyo sisi sio wakulima bwana, Mheshimiwa sisi ni wataalam wa kilimo tunawawezesha wakulima. Ndiyo maana ni mara chache kukuta Afisa Ugani ana shamba zuri. Afisa Kilimo sijui wa Wilaya au Mkoa ana shamba zuri katika nchi yetu sijui kama wapo wachache unaweza ukahesabu kwa mkono. Watu wa Wizara ya Kilimo sijui wakubwa hawa kama wana mashamba, siku moja tukubaliane hebu tutembelee mashamba yao hayo mazuri tuyaone yanafananaje. (*Makofi/Kicheko*)

Ni kwamba wanafanya kazi wameajiriwa kwenye Wizara ya Kilimo lakini *they don't believe in kilimo chenyewe kabisa actively*. Tusipotoka hapo hatuwezi kufika. Wenzetu wote nchi jirani hapa iwe ni Kenya, Uganda ambao ndiyo wenzetu hasa ukiacha wengine wadogo wadogo hawa, Wabunge wao ni wakulima wakubwa, *mechanized agriculture*, mnayofanya ni viongozi. Kweli kabisa, hayo tunayosema mashamba ya mboga mboga, mashamba ya maua kwani ni ya nani kule Kenya? Ni ya mkulima mdogo? Hakuna, ni viongozi. Nenda Uganda nani anasafirisha kahawa nje, nani analima kahawa yaani kwa kiwango kikubwa, nani wafugaji Uganda, mfugaji namba moja

mnamjua na kadhalika. Kenya pale mkulima namba moja mnamjua, mkulima namba mbili mnamjua, mkulima namba tatu mnamjua hata kama ni kahawa au mazao mengine. (*Makofii*)

Sisi Tanzania tulianza kidogo siku za nyuma na ile sera yetu ile kwamba lazima tufanye katika kikundi ndiyo sawa lakini mmoja mmoja siyo sawa sana sasa lazima tutoke huko, hiyo ya kikundi sawa na ya mmoja mmoja sawa. Hii itasaidia kwenda kwa *speed* zaidi, watu wetu washiriki na wawezeshwe katika kilimo. Tusipoanza sisi viongozi tusitarajie mabadiliko yoyote makubwa katika eneo hili. (*Makofii/Vigelegele*)

Mtu anamwambia mtoto wake shauri yako usiposoma utakuwa mkulima wewe. Kwa hiyo, mtoto anakua na *mentality* kwamba kilimo ni kitu cha mwisho. Kumbe kilimo ndiyo utajiri, popote pale duniani *farmerndiyo* anaheshimika. Ukiwa *introduced* kwamba huyu *is a farmer* kila mtu anakupigia *salute* anajua huyu bwana ni tajiri. Sasa sisi hatuwezi kwenda na *peasant agriculture* tukasema tutatoka hapa, watakuwepo hawa wadogo, wa kati na wakubwa na viongozi tukishiriki katika kilimo, tutatoka hapa tulipo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mimi nawapa moyo sana. Tunafurahi sana tunapomuona Waziri wa Fedha anajaribu kwenye kilimo cha zabibu ili na yeze awe anayaona matatizo ya zabibu. Tunaamini kwa utaratibu huo tutatoka hapa. Vilevile na wengine wote ambao mnajishughulisha na kilimo nawapa moyo, msonge mbele, tembeleaneni kwenye mashamba yenu muone nini cha kufanya. (*Makofii*)

Hata zile sera za heka 50 ni za kuziangalia kwamba huwezi kupata zaidi ya heka 50 halafu anakuja mtu wa nje anapata heka 3,000, 5,000, haiwezekani. Yaani wenye nchi heka 50, haiwezekani hiyo lazima iwe heka 10,000 sisi wenyewe, mmoja mmoja, katika vikundi na kadhalika. Hao wakija wakodishe kwetu na kadhalika, tutasonga mbele tukienda hivyo yaani tu *tu-open up* baadhi ya mambo

ambayo tume-*practice* lakini hayajatufikisha tunapotaka kwenda. Kwa hiyo, nawatia moyo sana viongozi na wananchi kwa ujumla tulime na tufuge, tushiriki katika kilimo kweli. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya ushauri huo, nina matangazo mawili. Mheshimiwa Mbarouk Mussa yuko hapa tangu jana amepoteza ufunguo wa gari. Kwa hiyo, anaomba ye yole ambaye amebahati kupa tafadhi funguo hizo awapatie Makatibu hapa mezani au yeye mwenyewe yuko pale. Kama umeona mahali funguo ya gari ambayo siyo ya kwako basi ni vizuri tukampatia Mheshimiwa Mussa Mbarouk.

Mengine tutayatoa katika *press release* kesho kwa hiyo sina sababu ya kusema zaidi hapa. *Otherwise* nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge tunaenda vizuri sana. Bado tuko katika mazungumzo na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu ratiba yetu na tutazidi kushauriana tunavyokwenda tunafanya na itakuwakuwaje.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho kabisa mmekuwa mkipeana taarifa za hesabu ambazo si sahihi kuhusiana na madeni na kadhalika ambayo mmekuwa mkipata ni vizuri mkapata kidogo mwanga mzuri kuhusiana na ulichokipata ili usije ukavunjika moyo kupita kiasi na matokeo yake ukaamua tu kuondoka hapa Bungeni kwa sababu Wagogo wanasema "msina cha kusola" yaani hakuna tija kuendelea kuwepo endapo hesabu zenyewe ndiyo hizo. Kwa hiyo, wengi wenu mme pata hizo hesabu lakini hesabu hizo hazijakaa sawasawa.

Sipendagi tu kusema sana lakini katika watu ambao mahesabu haya yana matatizo makubwa ni katika wasiotaka kuhudhuria humu Bungeni. Yana matatizo makubwa lakini kuna ujanja ujanja mwangi ndani yake. Tutazungumza na Serikali tuone *what to do* siku zijazo na ndiyo maana mnaona hizi vurugu na nini, yaani tabia yetu ya kutokusema wazi inatufanya hampati picha. Mimi ningetamani sana muwe mnapata picha kidogo ya kujua baadhi ya hizi *behaviors* zinakuwa *driven* na *what kind of forces* na *force* mojawapo ni hiyo. Mtu anakuwa amechukua fedha nydingi sana hawezi kuzilipa halafu anadhani kwamba ataliachia Bunge au Serikali madeni hayo na yeye atakuwa amechoropoka. Kwa